EAST AFRICANA COLLECTION

MADA: FANI KATIKA USHAIRI WA HASSAN MWALIMU MBEGA: UHAKIKI WA UPISHO WA UMALENGA NA DAFINA YA UMALENGA

NA: DONALD OMWOYO OSIEMO

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA "MASTER OF ARTS" KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

1997

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146605 1

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

# I K I R A R I

TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE CHOCHOTE

****************************************************************

DONALD OMWOYO OSIEMO

(MTAHINIWA)

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI YETU TUKIWA WASIMAMIZI WA KAZI HII WA CHUO KIKUU

****************************************************************

MWALIMU ZACHARY MUMBO MOSOTI

****************************************************************

MWALIMU LEONARD LISANZA MUAKA

| YALIYOMO | UKURASA |
|---|---|
| IKIRARI | i |
| YALIYOMO | ii |
| TABARUKU | vi |
| SHUKRANI | viii |
| MUHTASARI | x |
| HABARI KUHUSU MWANDISHI | xi |

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI


| | | UKURASA |
|---|---|---|
| 1.0 | UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 | TATIZO LA UTAFITI | 1 |
| 1.2 | MADHUMUNI YA UTAFITI | 1 |
| 1.3 | UPEO NA MIPAKA | 2 |
| 1.4 | SABABU YA KULICHAGUA SOMO | 2 |
| 1.5 | HAIPOTHESIA | 3 |
| 1.6 | YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO | 3 |
| 1.7 | MSINGI WA NADHARIA | 5 |
| 1.8 | NJIA ZA UTAFITI | 7 |
| | TANBIHI | 8 |

SURA YA PILI: MISINGI YA UHAKIKI


| | | |
|---|---|---|
| 2.1 | UTANGULIZI | 9 |
| 2.1.1 | MAANA YA FANI | 9 |
| 2.1.2 | SIFA ZA KIFANI KATIKA USHAIRI | 9 |
| 2.2 | LUGHA | 11 |
| 2.2.1 | MAANA YA LUGHA, UAMILI NA UMUHIMU WAKE | 11 |
| 2.2.2 | MSAMIATI: MAANA, UWEZO NA MAHUSIANO | 16 |
| 2.2.2.1 | UTEUZI WA MSAMIATI | 16 |
| 2.2.2.2 | AINA YA MSAMIATI | 16 |
| 2.2.2.3 | ASILI YA MSAMIATI | 16 |
| 2.2.2.4 | NGUVU/UWEZO WA MSAMIATI | 17 |
| 2.2.2.5 | MOTISHA/KARIHA KATIKA MATUMIZI YA MSAMIATI | 17 |
| 2.2.2.6 | MAZINGIRA AMBAMO MSAMIATI UMETUMIWA | 18 |
| 2.2.2.7 | VIPASHO VYA MSMIATI | 18 |
| 2.2.2.8 | MPANGILIO WA MSAMIATI | 19 |
| 2.2.2.9 | NAMNA MSAMIATI ULIVYOUNDWA | 19 |
| 2.2.2.10 | NJIA ZA UPANUZI MAANA KATIKA MSAMIATI NA ATHARI ZAO KATIKA KAZI | 19 |
| 2.2.2.11 | UANGAVU NA UTATA KATIKA MAANA ZA MSAMIATI | 20 |
| 2.2.2.12 | WIZANI KIMAANA KATIKA MAHUSIANO YA MSAMIATI | 21 |
| 2.2.2.13 | AINA (JINSI) MBALIMBALI ZA MAANA | 21 |
| 2.2.2.14 | TATHMINI YA UHURU WA KISHAIRI | 23 |
| 2.2.3 | HALI YA LUGHA ILIYOTUMIWA (KIWANGO CHAKE) | 23 |
| 2.2.4 | TAMATHALI ZA USEMI | 24 |
| 2.2.5 | MATUMIZI YA LUGHA KIUJUMLA | 38 |
| 2.3 | WAHUSIKA | 38 |
| 2.4 | MTINDO | 40 |
| 2.5 | MANDHARI | 44 |
| 2.6 | PLOTI | 45 |
| 2.7 | WAKATI | 46 |
| 2.8 | TONI | 46 |
| | TANBIHI | 49 |

SURA YA TATU: UPISHO WA UMALENGA


| | | |
|---|---|---|
| 3.1 | UTANGULIZI | 50 |
| 3.2 | LUGHA | 51 |
| 3.2.1 | MSAMIATI: MAANA, UWEZO NA MAHUSIANO | 51 |
| 3.2.1.1 | UTEUZI WA MSAMIATI | 51 |
| 3.2.1.2 | AINA YA MSAMIATI | 52 |
| 3.2.1.3 | ASILI YA MSAMIATI | 56 |
| 3.2.1.4 | NGUVU/UWEZO WA MSAMIATI | 57 |
| 3.2.1.5 | MOTISHA/KARIHA KATIKA MATUMIZI YA MSAMIATI | 58 |
| 3.2.1.6 | MAZINGIRA AMBAMO MSAMIATI UMETUMIWA | 59 |
| 3.2.1.7 | VIPASHO VYA MSAMIATI | 61 |
| 3.2.1.8 | MPANGILIO WA MSAMIATI | 62 |
| 3.2.1.9 | NAMNA MSAMIATI ULIVYOUNDWA | 64 |
| 3.2.1.10 | NJIA ZA UPANUZI MAANA KATIKA MSAMIATI NA ATHARI ZAO KATIKA KAZI | 64 |
| 3.2.1.11 | UANGAVU NA UTATA KATIKA MAANA ZA MSAMIATI | 66 |
| 3.2.1.12 | WIZANI KIMAANA KATIKA MAHUSIANO YA MSAMIATI | 67 |
| 3.2.1.13 | AINA (JINSI) MBALIMBALI ZA MAANA | 67 |
| 3.2.1.14 | TATHMINI YA UHURU WA KISHAIRI | 68 |
| 3.2.3 | HALI YA LUGHA ILIYOTUMIWA (KIWANGO CHAKE) | 69 |
| 3.2.4 | TAMATHALI ZA USEMI | 69 |
| 3.2.5 | MATUMIZI YA LUGHA KIUJUMLA | 83 |
| 3.3. | WAHUSIKA | 84 |
| 3.4 | MTINDO | 86 |
| 3.5 | MANDHARI | 90 |
| 3.6 | WAKATI | 92 |
| 3.7 | PLOTI | 93 |
| 3.8 | TONI | 94 |
| | TANBIHI | 97 |

SURA YA NNE: DAFINA YA UMALENGA


| | | |
|---|---|---|
| 4.1 | UTANGULIZI | 98 |
| 4.2 | LUGHA | 98 |
| 4.2.1 | MSAMIATI: MAANA, UWEZO NA MAHUSIANO | 98 |
| 4.2.1.1 | UTEUZI WA MSAMIATI | 98 |
| 4.2.1.2 | AINA YA MSAMIATI | 99 |
| 4.2.1.3 | ASILI YA MSAMIATI | 101 |
| 4.2.1.4 | NGUVU/UWEZO WA MSAMIATI | 102 |
| 4.2.1.5 | MOTISHA/KARIHA KATIKA MATUMIZI YA MSAMIATI | 103 |
| 4.2.1.6 | MAZINGIRA AMBAMO MSAMIATI UMETUMIWA | 104 |
| 4.2.1.7 | VIPASHO VYA MSAMIATI | 105 |
| 4.2.1.8 | MPANGILIO WA MSAMIATI | 107 |
| 4.2.1.9 | NAMNA MSAMIATI ULIVYOUNDWA | 108 |
| 4.2.1.10 | NJIA ZA UPANUZI MAANA KATIKA MSAMIATI NA ATHARI ZAO KATIKA KAZI | 109 |
| 4.2.1.11 | WIZANI KIMAANA KATIKA MAHUSIANO YA MSAMIATI | 112 |
| 4.2.1.12 | UANGAVU NA UTATA KATIKA MAANA ZA MSAMIATI | 113 |
| 4.2.1.13 | AINA (JINSI) MBALIMBALI ZA MAANA | 114 |
| 4.2.1.14 | TATHMINI YA UHURU WA KISHAIRI | 114 |
| 4.2.3 | KIWANGO YA LUGHA ILIYOTUMIWA (KIWANGO CHAKE) | 115 |
| 4.2.4 | TAMATHALI ZA USEMI | 115 |
| 4.2.5 | MATUMIZI YA LUGHA KIUJUMLA | 130 |
| 4.3 | WAHUSIKA | 132 |
| 4.4. | MTINDO | 134 |
| 4.5 | MANDHARI | 139 |
| 4.6 | PLOTI | 141 |
| 4.7 | WAKATI | 142 |
| 4.8 | TONI | 143 |
| | TANBIHI | 144 |


SURA YA TANO: TATHMINI NA HITIMISHO


| | | |
|---|---|---|
| 5.1 | TATHMINI NA HITIMISHO | 145 |
| 5.2 | MAREJELEO | 148 |

## TABARUKU

Kazi hii nawatabarukia mamangu Jerusha Bonareri, familia ya Bogita na wote wanaotambua, kusema, na kuukubali ukweli pamoja na kuheshimu haki, uhuru wa mawazo na wote wanaoepuka chuki zisizo msingi katika ulimwengu wa kiusomi na maingiliano.

Nawatabarukia pia wote waliozoesha ndimi zao kusema ukweli, mioyo yao kutambua haki na akili zao kuongoza kwenye unyoofu huku kila kiungo katika miili yao kikichangia ujenzi na maendelezo ya msingi imara wa UTU na tangamano. Mwisho ni walio na mioyo salihi ya kuwaauni wenzao kila panapo haja.

## SHUKRANI

Haingekuwa rahisi kwangu kuchukua kozi kama hii ya muda mrefu na gharama kubwa bila msaada wa jamaa na marafiki. Ni kazi iliyokuwa ngumu na kipimo kamili cha mahusiano ya dhati na ya udhaba. Hata hivyo kwa wote hao nawashukuru kwa dhati kwani mchango wao hata kama ni wa kartasi au kalamu ulinifaa na kuniwezesha kuvuta hatua mbele, katika kutekeleza azma niliyokuwa nayo.

Shukrani zangu kwanza ni kwa maulana Muumba wangu ambaye alinikitia kago imara iliyonikingia mawimbi ungama mengi niliyokumbana nayo kutoka mwanzo hadi mwisho wa kozi hii pamoja na kunipa uwezo wa kuvumilia na kustahimili makuruhu mengi na pia kwa kunifungulia njia zangu za ufahamu.

Nawashukuru pia mama Jerusha Bonareri, baba Bogita Isoe, Ndugu zangu Petronilla Nyaboke, Douglas Nyamwamu, Charles Magati, Isoe, Signorah Kerubo, Philip, Enoch & Flora kwa mapenzi yao na msaada wa hali na mali na kwa kunivumilia katika kipindi chote cha masomo yangu mbali na kunifariji kila kulipogunduliwa cheche za kukata tamaa.

Ukarimu uliozidi mahusiano ya kiudugu ulipokelewa kutoka kwa Bi Agnes Mauncho, Bi Sophy Kirorei, Bw. Joseph Kimura, Mabw. Ali Waqo Guyo, Alphonce Franco Mbele, Patrick Gekonge Maraburi, Joel Ndivo, Moore Kirote, Maranga Nyairo, Elias Maranga, Christopher Kinara na wafanyakazi wote wa Taasisi ya K.C.B. ambao walinifadhili kwa mengi - hali iliyonipa nguvu na moyo wa kujihisi imara hadi kutia nukta ya ukomo katika kozi hii.

Wafuatao pia walinifanyia hisani kubwa kwa kuchangia masomo yangu kwa njia moja au nyingine. Nao ni pamoja na Wilson Ondimu Nyagwachi, Simeon Maucho, Gilbert Atika, Esman Nyamongo, Moruri Oburu, David Ruoti, Zablon Moturi, Nyagaka Makori, Michael Oruru, Shem Motuka, Okemwa Mogusu, Samwel Isoe, Elijah Obwang'i, Sunday Mauncho, Stanley Omweri, Nathan Moturi, Nyamweya Matonda, Titus Tong'i, Jeremiah Tanui, Waiyaki Mwaura, Beatrice Wanjala, Jennifer Anyona, R. Kirwa Limo, Susan Njagi, Peter Nguro, Evelyn Kegoko, Bi Rautta, Nkrumah Maucho, Naomi Otwori, Purity Kituma, Peris Nyanchoka, Margaret Ashioya, Anne Kibinda, Jelious Wambui, Susan Oluoch, Gladys Ogeto, Veronica Mbeche, David Matwero, Crispo Njoga, Gentrix Nanjala, Abel Bogeni, Mark Otundo, Ndirangu Njoroge, Samuel Okwoyo, Bw. J.P. Olum na wengine ambao walisaidia kifedha na kiushauri.

Hazina ya shukrani pia ni kwa mlezi wangu wa hii lugha na mshauri mkuu wa dhati na rafiki mwema ambaye ni Hassan Mwalimu Mbega ambaye milango yake ilikuwa wazi kunipokelea lolote kila nilipomwendea katika wakati wowote. Waalimu wangu wa viwango mbalimbali ambao nimefaidi mengi kwao ni pamoja na Prof. Kitsao, Mwenda Mbatiah, Rose Shake, Aggrey Wasike, Gichobi Mungania, Michira Nyachae, Cecilia Thande, Mosoti Mumbo, Lisanza Muaka, Margaret Njuguna, Dr. Nyombe, Dr. Nyaga, Prof. Abdulaziz na wengine wengi. Nawashukuru wote kwa kunikuza na kunipa kariha ya kujifunza lugha hii zaidi.

Wenzangu katika jahazi hili ambao ni Mwailengo kilelu, Omondi Osano, Tom Olali, Anne Waithera, Edith Kathoki, na Hezron Nyamberi wapokee shukrani zangu kwani nilifurahi sana ushirika wao ambao ulikuwa nguzo imara katika mazingira ya kiusomi.

Wengine ni wasimamizi wangu, Ndg. Zachary Mumbo Mosoti na Ndg. Leonard Lisanza Muaka kwa kuniongoza katika mazingira ya udugu na mazuri kiusomi.

Sitamsahau Bi. Mellen Nyanchwa Asiago siyo tu kwa kunipigia taipu kazi hii, bali pia kwa moyo na hamasa kubwa aliyokuwa nayo katika kuifanya mbali na moyo wa ushirikiano aliokuwa nao.

Mwisho nawashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine ambao msaada wao umehifadhika katika kumbukumbu isiyofutika. Sitawasahau wote ambao kwa usitiri au dhahiri vitendo vyao vilinisaidia kutambua sura halisi za watu na thamani kamili inayohusishwa katika neno 'tahadhari' katika maisha ya mtu. Wasamehewa wote ambao kwa kupenda au kujipata, walijaribu kunihujumu na kunikwamisha. Nawashukuru kwa kunipa funzo kubwa, ambalo ni mwongozo azizi katika maisha ya mustakabali.

# MUHTASARI

Tasnifu hii imeshughulikia fani katika ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega. Tumehakiki diwani zake mbili ambazo ni **Upisho wa umalenga (1975)** na **Dafina ya Umalenga (1984)** kwa kutumia nadharia ya urasimu.

Kuna sura tano katika tasnifu. Sura ya kwanza ni ya utangulizi ama pendekezo la utafiti. Ni sura inayohusu somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kulichagua somo, haipothesia, yaliyoandikwa kuhusu somo, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

Sura ya pili ambayo ni ya misingi ya uhakiki inahusu uamili wa lugha ya kishairi katika sanaa, sifa zake, na namna inavyoshirikiana au kutumiwa katika ploti. Tumeangalia umuhimu wa kila mojawapo ya vipengele hivyo na mchango wao katika fani kwa jumla. Baada ya kuangalia mengi ya kifani ambayo ni mwongozo wa sura zinazofuatia, tumezitamzama na kuzihakiki tungo za mwalimu Mbega katika misingi ya yaliyopitiwa katika sura za kwanza na pili. Maswala ya nadharia ya urasimu na mwongozo wake vimezingatiwa katika kuhakiki tungo hizo.

Sura ya tatu inahusu uhakiki kifani wa **upisho wa umalenga**, huku sura ya nne ikishughulikia maswala ya kifani katika diwani ya **Dafina ya Umalenga.**

Sura ya tano ni hitimisho ambapo kwa njia ya muhtasari imethibitisha haipothesia pamoja na kushughulikia maswala mengine ya kifani. Tasnifu hii ina sura tano zinazoshughulikia maswala ya kifani.

Kwa sababu ambazo hatukuweza kuziepuka, alama za kufungia maneno zimetokea zikiangalia upande mmoja. Hii ni kwa sababu, ya aina ya kompiuta iliyotumiwa ambayo haina alama za kufungia. Tunaomba radhi kwa makosa hayo.

## HABARI KUMHUSU MTUNZI

Hassan Mwalimu Mbega alizaliwa tarehe 1/1/1914 alfajiri, siku ya Jumatatu katika kijiji cha Jego, sehemu ya Umba, Wilaya ya Kwale, kilomita chache tu kutoka vanga. Kwa kabila, mshairi ni mdigo. Babake alikuwa mdigo pia.

Babake aliyeitwa Mwalimu Mbega alimwoa Mamake Hassan, ambaye kwa jina ni Munguja binti Kombo (Mshirazi) kutoka kijiji cha Tongoni baina ya 1912-13 akiwa Tanga, akifanya kazi yake ya useremala. Wakati huo hakukuwa na vizuizi vyovyote vya tangamano vya mpakani baina ya Kenya na Tanganyika. Huu ulikuwa wakati wa utawala wa wajerumani huko Tanganyika.

Baina ya 1914 na 1922, Hassan alilelewa Tanga, Tanganyika. Mwaka 1922 alianza masomo yake huko Tanga, kwa sababu wakati huo hakukuwa na shule kwao Jego. Mwaka 1922 alianza masomo yake katika shule ya Tanga Government School. Kwa sababu ya akili yake kama smaku alisoma madarasa mawili katika mwaka 1922, ambapo nusu ya kwanza ya mwaka huo ilimwona katika darasa la kwanza, huku nusu ya pili akiimalizia darasa la pili. Mwaka uliofuata wa 1923, akiwa darasa la tatu, aliomba apatiwe mtihani wa darasa la nne, na baada ya jitihadi kuu alifanikiwa kumshawishi Mwalimu mkuu, Bw. Forster kuridhia ombi lake. Alipatiwa mtihani huo ambao aliupita vizuri sana akiwa wa kwanza katika waliopitishwa kwenda darasa la tano.

Mwaka wa 1924, akiwa katika darasa la tano, aliomba apatiwe mtihani wa darasa la sita, ambao aliupita pia kwa kuongoza (aliwekwa wa kwanza japo walitoshana nguvu na mwanafunzi mwingine, kwa sababu yeye alitoka darasa la chini). Japo mwalimu mkuu hakuelewa nia ya Hassan ya kuruka madarasa ya nne na sita, aliridhia maombi yake, hali ambayo ilimwezesha kuwaruka waalimu wakali sana wa madarasa hayo waliozoea kuwachapachapa wanafunzi.

Mwaka wa 1925, Hassan alikuwa darasa la saba na 1926 alifanya mtihani wa darasa la nane. Baada ya mtihani huo alichaguliwa aendelee na masomo ya sekondari katika shule yiyo hiyo ya Tanga Government School. Mwaka 1927, alijiunga na kidato cha kwanza na 1928 akawa kidato cha pili, na mwaka huo darasa lake lilichaguliwa kufanya kazi za aina tatu, ambazo ni; kufanya kazi, ya telegrafu katika Reli, kupiga taipu (Tabora) na kuchukua mafunzo ya ualimu katika Mpwapwa Teachers Training School. Hassan alikuwa katika kundi hili la kwenda Mpwapwa lakini babake alikataa kata kata, hali ambayo ilimlazimu kuitikia takwa la babake la kujifunza useremala badala ya ualimu.

Kwa sababu hiyo Hassan alilazimika kujiunga na Tanga Technical College tokea 1929 hadi Desemba 1932. Baada ya kupata cheti chake cha useremala alirejea Kenya, ambapo tokea 1933 alikuwa Mombasa akifanya kazi ya kuunda vitu mbalimbali vinavyohusiana na mafunzo yake ya useremala.

Miaka ya 1934 hadi 1972 aliipitisha akifanya kazi na Public Works Department katika Wizara ya Ujenzi. Kipindi kirefu alikipitisha katika kazi wakati wa enzi ya ukoloni, ambapo alifanya kazi Mombasa, Tanganyika, na 1936 (kwa miezi sita), huko Uganda. Alistaafu toka kazi hiyo mwaka 1972.

Mafunzo yake ya kwanza ya kidini aliyapata kutoka kwa Ali wa bwana mkuu. Wakati alipokuwa Vanga kwa mafunzo ya dini ya kiislamu ndipo alipopata nafasi ya kujifunza ushairi toka kwa mzee mmoja msharifu kwa jina Alawi bin Nassir (Alawi kiboga - Mvumba). Mzee huyo alimpa Hassan hazina kubwa sana ya ushairi ambayo kwa maelezo ya mshairi, "Haikupata kupatiwa mtu yeyote na ilikuwa katika hati ya kivumba, ambayo aliitafsiri kwa kiswahili." Mzee kiboga alimfadhili Hassan katika ushairi kuliko mtu mwingine yeyote.

Baadaye alitokea Mohammed Nassir, mjukuu wa Liwali Juya ambaye pia aliiongezea hazina hiyo pale Vanga japo mchango huo haulingani na ule wa Alawi Kiboga.

Wa tatu aliyempa mafunzo ya ushairi ni Bakari wa Shehe. Huyu vile vile, alikuwa mshairi. Wa nne ni Mzee Seif bin Ahmadi (Seif Akida Ahmadi) ambaye alimpa hazina inayohusiana na matumizi ya vina vya Kiarabu na Kiswahili kwa pamoja.

Mwingine aliyemfaa ni Mwalimu Ghulamu Mwabondo pale Msanii alipomtembelea kwake Tanganyika. Hassan asema kuwa hata Shaaban Robert, Mwinyihatibu Mohammed na inasemekana pia Akilimali walijifunza mengi kutoka kwake mwalimu Ghulamu Mwabondo.

Hassan alishirikiana na Shaaban katika mirahano ya kiushairi. Ni katika tungo hizi alichocheka na kuhamasika kuendelea zaidi ambapo 1972 alifanikiwa kutunga **Upisho wa Umalenga**, diwani iliyochapishwa miaka mitatu baadaye, ikitokea miaka kadhaa baada ya mauko ya Shaaban Ufukwe (Robert), ambapo anwani hiyo yamaanisha kuwa Hassan amepishwa tungoni na Shaaban. Kuchapishwa kwa diwani hii kulimpa shime na muhu wa kutunga zaidi. Ndipo akafuatiliza kwa kutunga **Dafina ya Umalenga** (1984), **Utenzi wa Mfalme (1983)** na **Wasia Bora na Hadithi zake (1986)** na vingine ambavyo bado havijachapishwa.

Hassan alikuwa mwanamutribu tokea 1935, hali ambayo ilimpa kariha kubwa ya kutunga mashairi na nyimbo. Mpaka sasa Hassan anaendelea na tungo na mara nyingi nilizomtembelea nyumbani kwake Eastleigh, nimempata akisoma au kutunga mashairi ambapo ni vigumu kwake kubandukana na vitabu na kalamu. Mahaba yake kwa tungo ni makubwa sana, na ni nadra sana siku ipite bila alama yoyote ya maana ya vitu hivyo.

1972 alistaafu toka kazi yake ya ufundi wa useremala na kuhamia Nairobi kutoka Mombasa. Ni katika kipindi hiki ndipo akatunga vitabu hivyo vilivyochapishwa. Tokea 1985 hadi 1989 alifunza katika Raval's Secondary School na baada ya kiwango cha "A" kufutwa akawacha kufundisha. Mbali na Raval's Secondary School, alifunza kwa miezi fulani ya 1984 katika Senior Chief Koinange.

Amewahi kualikwa katika shule za upili nyingi, makongomano ya Fasihi na Lugha, taasisi na vyuo vikuu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na katika Taasisi ya Utawala ya Kenya (K.I.A - Kabete), vyuo vikuu vya Nairobi, Kenyatta na Egerton.

Alikuwa pia mtayarishi wa vipindi vya K.B.C. vya "Asiyesikia la Mkuu" na "Ukicha Mwana Kulia". Mbali na hivyo, kuna vingine kama "Ukumbi wa Kiswahili" na "Lugha Yetu", ambavyo amewahi kushiriki kwavyo na kutoa mchango unaofaa na mkubwa katika matumizi ya lugha hii stahiki.

Amefanya utafiti wa lahaja nyingi, zikiwemo za kimtang'ata, na Kimrima ambazo alifanya kwa kumwongoza marehemu Shihabuddin Chiraghdin (wakati Shihabuddin akishughulika kutafiti kimrima kilichotumiwa katika diwani ya malenga wa mrima) katika miaka ya 1970, hali ambayo imempa ukwasi mkubwa wa lugha. Anasema kuwa kuimarika kwa mtu katika lugha hakutokani tu na kujua lahaja hasa zile alizokulia mtu, bali pia kwa kuzitafiti zingine. Kwa sababu hiyo asema kuwa, yafaa watunzi wasafiri kote kunakotumiwa lugha hii na kukusanya hazina ya leskia zake na namna ya kuzitumia. Ni kwa sababu ya tajriba hizi na uzoevu wake wa miaka mingi katika maswala ya lugha hii, kuwa wengi waliomsikiza na kusoma kazi zake wanamwona kuwa ni mtunzi na mwanalugha shupavu.

Kwa sasa anaishi katika hali ya ukulima huku lokesheni ya Ekalakala, tarafa ya Masinga, Wilaya ya Machakos, ingawa baadhi ya siku anazipitisha katika mtaa wa Eastleigh (Nariobi).

Ameoa na ana watoto kumi (kwa wanawake mbalimbali) na wajukuu. Anapendelea sana habari za ukweli kuhusu maisha yake, ili kutokee unyoofu katika lolote linalotajwa, kusemwa na kuandikwa kumhusu, kinyume kabisa na watunzi wengine wanaopendelea kubana mengi kuwahusu. Tunamshukuru kwa ushirikiano wake wa mara kwa mara kuhusu maswala mbalimbali ya hii lugha. Tunamshukuru pia kwa kuturuhusu kunasa katika kanda mazungumzo tuliyokuwa nayo nyumbani kwake Eastleigh kuhusu hii lugha.

## 1:1 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo letu la utafiti limo katika kipengele cha fasihi, cha fani. Uamili wa fani ni mkubwa sana katika sanaa. Matumizi mazuri ya fani hupendeza na kuvutia katika sanaa. Fani huchukua jukumu la kupitisha ujumbe kama inavyokusudiwa kwa hadhira.

Matumizi ya kihorera ya fani huichakaza kazi na huvyaza uvulivuli[1] katika mawasiliano. Hali hii haivutii katika sanaa na lazima makini na hadhari kubwa vichukuliwe katika kuhakikisha kwamba matokeo ya matumizi ya fani ni upitishwaji ujumbe kwa njia inayopendeza, kurembesha uwasilishaji na kuwasilisha kwa mbinu zinazonasa nadhari. Isiwe ni fani butu[2] na mata[3] ambayo hata kimatilaba (kihemshi) hainasi hisia wala tafakari ya msomaji.

Tatizo letu limo kwenye aina ya fani aliyotumia msanii. Je ni fani iliyokamilika? Ni fani nzuri? Inatekeleza majukumu yake kama inavyopaswa? Ni ya hali ya juu, kadiri au chini? Ni fani changamano au changanuzi? Ni fani iliyoshikamana katika viungo vyake vyote katika kutekeleza majukumu yake au vipi? Kwa hivyo, tatizo letu limo kwenye aina ya fani iliyotumiwa katika diwani hizo mbili za Hassan Mwalimu Mbega.

## 1:2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Nia yetu katika utafiti huu ni kuweka msingi wa uhakiki wa kifasihi wa ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega na kwa kiasi fulani katika ushairi wa kiswahili kwa jumla, kusudi kuwapa kariha na hamasa wahakiki wengine. Tafiti nyingi zilizofanywa ni katika maudhui na kwa kufanya utafiti huu, tunatarajia kuwa kazi hii itawatia shime watafiti wengine katika kuzihakiki tungo zilizobaki za msanii huyu na za wengine kifani.

Pia nia yetu ni kuona kuwa utafiti huu umefanywa kwa njia ambayo yafaa sana katika kupima na kuhakiki mchango wa fani katika kufumbata malengo ya kisanii siyo tu katika diwani za mshairi huyu tu, bali za washairi wengine pia.

Tumeangalia pia viungo vya fani na uamili wao katika kujenga umbo zima na thabiti la fani. Katika kufanya hivyo twatarajia kuwa tutakuwa tumechangia na kuchochea tafiti zaidi za kiuhakiki katika uamili wa fani na umuhimu wake, siyo tu katika ushairi, bali pia katika sanaa kwa jumla.

Uhakiki wa tungo za Hassan Mwalimu Mbega katika diwani hizi mbili umeweka msingi wa utafiti wa kazi zilizobakia na kufungua njia za uhakiki wao kifani na hivyo kuchagiza na kuvutia zaidi uhakiki wa tungo zake zote.

## 1.3 UPEO NA MIPAKA

Utafiti wetu umeangalia matumizi ya fani katika diwani hizo mbili zilizotajwa.

Tumeviangalia viungo mbalimbali vya fani yake katika kiwango cha uamili wao. Uamili huu ndio uliotuwezesha kutathmini thamani ya fani iliyotumiwa. Mchango wa kila kipengele katika kujenga umbo imara na lililotangamana la fani umeangaliwa pamoja na uamili wa fani katika ujumla wake.

Viungo vya fani ambavyo vimeangaliwa ni; lugha, wahusika, mandhari, ploti, mtindo, wakati na toni. Mchango, umuhimu na uamili wa kila kiungo umeangaliwa.

Katika jitihada ya kuhakiki viungo hivyo na kuvifafanua, tumetoa mifano inayowafiki kutoka diwani hizo mbili husika. Pale mifano hiyo ilipokosa kuafiki, mifano kutoka tungo zingine imetumiwa. Kwa kufanya hivi hatukupotoka kwani nia yetu ni kuonyesha kwa njia za mashiko zaidi namna fani ya msanii huyu inavyofanya kazi.

Mawazo, kunga na ushauri wa wataalamu mbalimbali na wahakiki waliochangia katika fani yamezingatiwa kimsingi na kuchangiwa kila ilipofaa katika kutuwezesha kuhakiki tungo za msanii huyu kwa uzuri zaidi. Kama tulivyotaja, nia yetu ni kuziangazia tungo za Hassan Mwalimu Mbega kwa mtazamo mpana zaidi na nafasi ya michango ya mifano iliyo nje ya tungo zake imetumiwa kwa kiwango haba sana, ili tusipotoke na kwenda nje ya utafiti huu.

## 1.4 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO

Tumelichagua somo hili kwa sababu ya uzito wake katika fasihi. Fani ni kipengele muhimu sana katika fasihi, ambacho hutumiwa katika upitishwaji wa maudhui. Kwa sababu ya uzito wa jukumu hili lake, tumelichagua somo hili kumulikia mchango wake ambao unatokana na uamuli wake.

Tafiti nyingi zilizofanywa awali zimo katika kiwango cha maudhui. Fani haijaangaziwa kwa undani na ukamilifu. Hili halikusudiwi tungo za Hassan Mwalimu Mbega zilizowahi kushughulikiwa na Mungai Mutonya (1991), bali pia na za washairi wengine ambazo zimeshughulikiwa na wahakiki mbalimbali. Tunadai hivi, kwa sababu kwa kadiri ya tunavyojua hakuna kazi moja iliyofanywa ya kuhakiki matumizi ya fani katika ujumla wake. Kile kilichofanyika ni kuwa, watafiti huchukua kipengele kimoja, viwili au vitatu na kuacha nje vingine katika uhakiki wao. Kwa kufanya kama tulivyodhamiria, tutakuwa tumefanikiwa katika ulimwengu wa kiusomi katika kuchangia kiuhakiki kwa namna moja au nyingine. Kwa sababu hiyo, twatarajia kuwa huu utakuwa mchango mzuri katika ulimwengu wa kiusomi na kiuhakiki.

Kwa kadiri ya tunavyojua, tungo za Hassan Mwalimu Mbega hazijahakikiwa

kwa undani, ukamilifu na kwa kutosheleza kifani. Waliojaribu kufanya hivyo, wamefanya hivyo katika kiwango cha baadhi tu ya vipengele vyake au kwa mpito tu. Kwa sababu hii, twaona kuwa, tungo za msanii huyu hazijafanyiwa haki katika kuhakikiwa kifani, kwa undani na kwa njia inayoridhisha. Ni kwa sababu hii tumeshawishika na kuhamasika katika kuzihakiki ili kuziba pengo hilo.

Somo hili tumelichagua kwa sababu kazi hizo zina umbo la aina moja. Diwani zote ni mikusanyo ya mashairi mbalimbali huku Utenzi wa mfalme muadilifu ukichukua umbo tofauti. Wasia Bora pia ni tofauti kwani umbo lake ni la kitutumbi. Ni kwa sababu hizo kuwa tumelichagua somo hili.

## 1.5 HAIPOTHESIA

Tumechukulia kuwa fani aliyoitumia msanii huyu si ya kupwaya. Twaelekeza fikira zetu kwenye imani kuwa huenda mshairi huyu ametumia fani kwa njia inayoridhisha sana.

Tumechukulia pia kuwa, kuna umbo changamano au lenye mshikamano wa dhati, ambalo limesilimu[4] viungo vyote vya fani katika diwani hizo.

Tumefikiria kuwa huenda aina ya fani aliyoitumia inafaa katika nyakati zote. Hivi ni kudai kuwa, si fani ya wakati mmoja maalum, bali ni fani inayoweza kuthibitika katika nyakati zote za kuhakikiwa.

Pia twadhani kuwa fani aliyoitumia imefanikiwa kubainisha mkabala[5] wa msanii kwa hadhira yake, ambao kwa uhakiki wa lugha iliyotumiwa, wahusika waliotumiwa, mandhari yaliyoteuliwa na mambo mengine, imefanikiwa kimatilaba[6] kugusa hisia za hadhira yake.

Tumekisia kuwa msanii ametumia fani yenye mwelekeo mzuri na unaofungamana na udhibiti wa dhamira alizozilenga.

Hatima tumechukulia kuwa viungo vyote vya fani vimetumiwa kwa njia nzuri inayomruhusu mhakiki kuvichanganua kila kimoja katika upekee na kutathmini mchango wa kila mojawapo kabla ya kuangalia kimantiki uhusiano baina yao. Twadhani ametumia fani inayoruhusu uwezekano huu.

## 1:6 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kuna kazi nyingi katika Kiswahili na Kiingereza zilizoandikwa ambazo zashughulikia fani siyo tu katika ushairi, bali katika sanaa kwa jumla. Baadhi ya kazi hizo zashughulikia fani katika baadhi ya vipengele vyake tu. Tumezisoma zote na kuchukua vile vipengele vinavyofaa katika kuhakikia tungo za Mwalimu Mbega.

Kwa sababu ya wingi wa kazi hizo, hatukuzitaja zote ila pale ilipolazimu. Zile ambazo zina mwongozo wa moja kwa moja katika somo letu zimeangaziwa katika kutuwezesha kuona siyo upungufu wao tu, bali pia katika kutuwekea wazi pengo tulilokusudia kulijaza. Baadhi ya kazi zilizotufaa katika maelezo na fafanuzi za kifani kwa jumla ni pamoja na zao; Msokile, M,(1993), Kuhenga, C,(1977), kahigi, K, na Mulokozi, M,(1986), Boukheit, A,(1982), Wallah bin Wallah, (1984), Mwinyihatibu, M,(1977), Leech, G,(1969) Levin, S.R,(1962), Shihabuddin, C, na Mnyampala, M,(1977), Farouk, M.T.(1976), Kezilahabi, E,(1976), Khan, M.K,(1981), Syambo, B na Mazrui, A,(1992), Senkoro, F.E.M.K, (1988), Murray, P,(1978), Korg, J,(1959) Spencer, J,(1964), Hough, G,(1969), Medvedev, P.N. et al, (1978), Fowler, R,(1975) Anne, C,(1976), Nowottny, W,(1965),Fokkema, D. W. & Kunne-Ibsch, E,(1989), Davis, R.C & Finke L.F,(1989) Bennett, T, (1979) za wengine nyingi.

Kazi ambazo zahusiana moja kwa moja na somo letu ni Upisho wa umalenga (1975) na Dafina ya umalenga (1984) ambazo ni diwani zake Hassan Mwalimu Mbega. Katika diwani ya kwanza, kuna utangulizi mfupi na maelezo kwa muhtasari, pamoja na mengine kabla na baada ya baadhi ya mashairi ambayo yanaangazia japo kwa ukufi baadhi ya maswala ya fani yaliyotiwa na msanii mwenyewe. Zaidi ni maelezo kuhusu baadhi ya matumizi ya lugha katika kiwango cha msamiati - asili yao na uzito wao. Hata hivyo maelezo hayo yameangazia lugha kwa kiwango finyu huku maswala kadha yakiepukwa, na ambayo ni ya manufaa makubwa katika sanaa.

Katika maelezo ya Hassan Msami na Mohammad Kamal Khan katika Dafina ya Umalenga, kumetolewa mwangaza kidogo kuhusu matumizi ya lugha na mtindo wa msanii, ingawa na maudhui pia yameangaziwa. Maelezo yao hayatoshelezi na yametolewa kwa muhtasari. Kwa sababu hizo na zingine, tunasisitiza kwamba, kazi hizo hazitoshelezi kwa namna zilivyoshughulikiwa. Zina upungufu mwingi kama ulivyoelezewa. Kwanza ni kuwa, wataalamu hao wamezihakiki kazi hizo katika viwango vya lugha na mtindo, na kugusia wahusika kidogo. Na katika kufanya hivyo hawakuzingatia kwa undani na upana sifa zote za vipengele hivyo vya fani.

Pili, upungufu wa kazi hizo umo katika ukosefu wa mwongozo wa nadharia. Wanafasihi hao hawakuongozwa na nadharia yoyote.

Tatu, upungufu wa kazi hizo umo katika yaliyoshughulikiwa. Kwa kweli, yaliyoangaziwa ni ukufi tu wa yaliyopaswa kuangaliwa katika kazi hizo. Ni kwa sababu hiyo, tulitaka kujaza pengo hilo lililopo, la kukosa uhakiki wa kina. Tunatarajia kuwa uhakiki wetu umeangalia kwa kina yote yaliyopuuzwa na kazi hizo. Kwa njia hii tumetoa mwangaza zaidi kuhusu aina ya fani aliyoitumia na namna alivyoitumia.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Nadharia tuliyoitumia katika kazi hii ni ile ya urasimu. Mizizi yake yarejea hadi miaka ya 1880 nchini Urusi. Ilitokea kupitia tapo lililokuja kutambuliwa miaka michache kabla ya mapinduzi ya Oktoba 1917 na mwongo mmoja au zaidi baadaye. Waasisi wake hawakuwa wa shule moja maalum ya kitafakari. Hata neno urasimu halikuwa la uteuzi wao, bali ni la uzulifu[7], walilopachikwa na mahasimu wao nyakati za misukosuko ya kiuhakiki, baada ya mapinduzi.

Baadhi ya waasisi wake maarufu ambao walikuwa na mwelekeo wa mawazo wa aina moja ni pamoja na Victor Shklovsky, Boris Eichenbaum, Jurij Tynyanov na Roman Jacobson. Muungano wa tapo ulitambulishwa na Moscow Lingustic Circle, iliyoanzishwa mjini Moscow, 1915 na kuongozwa na Roman Jacobson na Society for the study of poetic language (Opojaz) iliyoanzishwa mjini Leningrad na kuongozwa na Victor Shklovsky.

Mashirika hayo mawili yalishirikiana katika kuweka misingi ya usomaji fasihi kisayansi, kwa kuunda sayansi kuu[8], katika njia na taratibu zake. Hili lililazimu kimsingi kutambua sifa rasimu na za kiisimu ambazo zasemekana zatofautisha fasihi na ushairi toka maumbo mengine ya usemi wa kawaida na lugha ya kawaida. Namna walivyoyashughulikia haya na kuhitimisha ndiyo iliyowafanya wabandikwe wanaurasimu. Waliamini kuwa umahsusi wa fasihi utaangaliwa kwa kurejelea sifa rasimu za matini za kifasihi.

Walidai kuwa, thamani na uamili wa ala ya kifasihi hutegemea uhusiano wake na zingine katika mfumo wa mahusiano uliojengwa na matini nzima ya kifasihi. Mwaka 1930, urasimu ulivia nchini urusi kwa sababu za kisiasa na maashiki wake kukimbilia prague. Miaka ya mwisho mwisho wa 1920 nadharia ilipokelewa nje ya Urusi. Ilipokelewa huko prague, Uingereza na marekani, ambako iliendelea hadi miaka ya 1960. Katika kipindi cha mwisho mwisho wa 1920, prague ilikuwa maarufu sana katika masomo ya fasihi na lugha, na kwa sababu pia ya baadhi ya wanaurasimu kuhamia hapo au wale waliokuwa na mawazo karibu sawa na yao kuhamia huko. Kuibuka unazi[9] pia kulilazimu wengi kukimbilia Czechoslo-vakia.

Nadhari iliendelezwa katika hawamu tatu ambazo ni urasimu wa kirusi[10], umuundo wa Zeki[11] na usemiotiki wa usovieti[12]. Nje ya Czech nadharia ilipata mashiko, Uingereza na Marekani ambapo ilipata wafuasi na wahakiki wapya kama vile Wimsatt, Beardsley, Schorer, Brooks na wengine. Ilianza kuyumbayumba miaka ya 1960 huku ikiweka misingi ya uvyazaji wa nadharia mpya ya umuundo iliyochipushwa kutoka kwake. Hata hivyo huo haukuwa mwisho wake kama anavyotujulisha Fokkema, D, (1977) ambaye anasema kuwa, "Leo haipothesia na thamani za urasimu wa kirusi vyaonekana hai zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali, na havikuwa na mashiko sana nje ya muungano wa usovieti kama ilivyo leo".

## MWELEKEO

Kuna mambo mengi sana yaliyoshughulikiwa katika nadharia hii. Hatukuyataja yote ila baadhi ambayo yalifaa sana katika kutuongoza na kutuelekeza katika uchunguzi wetu.

Nadharia ya urasimu iliegemea sana utafiti ambao ulifungamana sana na njia na taratibu za kiisimu. Ilijikita zaidi katika utafiti wa kiisimu katika uhakiki wa fasihi. Waasisi wake kama Roman Jacobson na Victor Shklovsky walisisitiza sana uhakiki wa kunga zilizotumiwa kuwasilisha mawazo ya msanii kuliko mawazo yenyewe. Tahakiki nyingi zilizotumiwa na maashiki wa nadharia hii zilishughulikia vina na sauti katika ushairi. Pia walisisitiza uchunguzi wa 'neno' sana katika tungo za sanaa.

Waliamini kuwa, fani ikitumiwa vizuri itaeleweka na hivyo tungo zitakuwa na fasiri moja tu ambayo ni ile aliyoikusudia msanii. Walidai kuwa kazi za fasihi zikiwa na fani isiyoeleweka na zisomwe kipotofu, basi zitaharibiwa kwa kuchipuzwa fasiri nyingi tofauti. Walishikilia kuwa ala au miongozo ya tungo inayofanya matini kuwa kazi ya kisanii ni mambo halisi ya kusomwa katika fasihi.

Jacobson na Eichenbaum waliamini kuwa, baadhi ya elementi au mambo yanawezakuchukuliwa au kutolewa kutoka matini ya kifasihi na kuchunguzwa nje ya matini na muktadha wake. Wote walikubaliana na maoni ya kruchenych kuwa, fani mpya huvyaza maudhui mapya na kuwa maudhui hutegemea kanuni[13] za fani (Jacobson, 1921). Hivi ni kusema kuwa fani mbalimbali huwa na maana mbalimbali. Sinonimia na homonimia ni vighairi[14] vinavyomruhusu mshairi kuvuta nadhari kwa ishara husika[15] za maneno au kama Jacobson (1921), anavyosema, "kufungulia maana za maneno".

Katika sinonimia maana moja huenezwa katika maneno mawili au zaidi, huku homonimia zikiunganisha zaidi ya maana moja katika neno moja. Mshairi anawezakuchezea homonimia na sinonimia kinyume na msingi wa kanuni kuwa, fani mpya lazima iwe na maana mpya, kanuni ambayo hukataza mjadala wa maudhui bila mjadala wa fani. Kwa sababu hiyo kulikuwa na mwelekeo wa kukataa matoleo yoyote toka matini. Wanaurasimu hawakunuia kuharibu matini ya kifasihi au ivyaza upya katika fani hafifu. Walilotaka tu, kwa njia ya busara, ni kutaja kanuni ambazo kwazo imejengwa. Waliziba pengo la uchukuzi[16] na matini peke[17] kwa kuanzisha dhana ya uamili.

Walipenda kuchunguza jinsi kanuni fulani au vipengele vinavyofanya kazi katika matini ya kifasihi na namna vinavyofanya matini kuwa utaratibu mmoja kamili. Baadaye walikubali kuwa elementi mbalimbali za mfumo wa kifasihi zinawezakuungana katika uamili wao. Kwa ufupi ni kuwa nadharia inajaribu kuitathmini fasihi kwa kuchunguza fani yake - namna ilivyojengwa na namna inavyofanya kazi ili kuwa na maana. Maelezo haya ndiyo yaliyotuvutia zaidi kwenye nadharia hii na ndiyo yaliyotuongoza katika kuhakiki diwani hizo mbili.

Msisitizo wa fani katika uhakiki wa fasihi kwa ujumla upo katika matumizi yanayoleta ufahamu wa ruwaza ya undani wa matini au namna inavyofanya kazi na katika utambuzi kuwa fani hutambulisha kazi mahsusi - riwaya, drama, liriki[18] na kadhalika. Urasimu katika mtazamo mpana huiangalia fasihi kama mfumo teti wa fani zinazoweza kutathminiwa kwa kuzihusisha na zingine katika viwango mbalimbali vya ujumuishi - toka umahsusi wa jazanda za ushairi au mshororo hadi kwa jinsia[19]. Inajaribu kuangalia fasihi, siyo kama iliyoundwa na maana asilia[20] ya uigaji wa uyakinifu, bali kama ruwaza husiani[21], ambazo zina maana katika kazi maalum na jinsia.

Kwa ufupi ni kuwa nadharia ililengwa kuondoa maudhui katika uhakiki wa fasihi na kusisitiza kuwa fani lazima iangaliwe kwa njia zilizo sawa na utafiti wa kijarabati[22].

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu ulilengwa kutimia kwa kupitia kazi mbalimbali za maktaba na kwingineko ambazo zimetoa mwongozo bora wa kutazamia, kuchambulia, kutathminia na kuhakikia fani katika ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega.

Pale palipotokea haja, tulimwona msanii mwenyewe kwa ufafanuzi zaidi. Pia wataalamu wengine wa uwanja huu waliendewa kwa ushauri zaidi katika kutatulia utata wowote uliotokea.

Tanbihi

1. Limetumiwa kwa maana ya hali butu katika mawasiliano
2. Ni aina ya fani isiyo na uwezo wa kuwasilisha. Ni fani hafifu sana isiyotekeleza majukumu yake.
3. Ni ile fani inayofaa katika wakati fulani maalum
   Hili huwezekana katika baadhi ya vipengele vyake, kama vile, kile cha lugha, hasa katika kiwango cha msamiati. Mathalani, siku hizi neno 'manyanga' lina mashiko sana katika kuwarejelea wasichana wazuri wazuri. Upo wakati ambapo halitakuwa na uzito huo wa sasa.
4. Limetumiwa kwa maana ya umbo linalovuta na kumeza viungo vyote vya fani. Ni umbo lililokamilishwa kwa kuhusisha vipengele vyote vya fani.
5. Ni neno lililotumiwa kama kisawe cha "attitude"
6. Ni kisawe cha emotively

7. Limetumiwa kufafanua fungu la 'pejorative label'
8. Kisawe cha 'autonomous science'
9. Kisawe cha Nacism
10. Tafsiri ya Russian Formalism.
11. " " Czech structuralism
12. " " Soviet semiotics
13. " " ' content is conditioned by form'
14. Kisawe cha exceptions
15. Tafsiri ya sign character
16. " " abstractions
17. maelezo ya individual text
18. utohozi wa lyric (wimbo hisia)
19. kisawe cha genre
20. " " intrinsic meaning
21. tafsiri ya "related patterning"
22. kisawe cha empiricism

## SURA YA PILI: MISINGI YA UHAKIKI

### 2:1 UTANGULIZI

### 2:1:1 MAANA YA FANI

Kwa sababu twashughulikia somo la kifani linaloongozwa na nadharia ya kifani, kuna haja ya kuelezea maana ya fani, kabla ya kuangalia maana yake katika mkabala wa ushairi, au sifa zake za kiuamili katika ushairi. Tumefanya hivyo kwa kunukuu na kuchukua maoni mbalimbali ya wataalamu tofautitofauti. Maoni hayo yanatoa mwangaza wa sifa za fani na hivyo yanatoa mwongozo wa kuielezea fani.

Kwa maelezo ya Senkoro, F.E.M.K.,(1982:8), "Fani katika fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake. Mambo mbalimbali huweza kuunda ama kubomoa fani ya kazi ya fasihi kutegemea na vile ambavyo msanii kayatumia". Maelezo haya yanafaa sana.

Beckson, K na Ganz, A'(1960), wanatupa maelezo ya aina mbili kuhusu fani. Kwanza, wanasema kuwa, fani ni mpangilio unaolingana wa kimizani kama ule wa tenzi. Pili, wanasema kuwa, fani ni umbo katika kazi ya sanaa. Wanahitimisha kuwa, fani wakati mwingine hupambanuliwa kwa kutofautishwa na maudhui. Maoni yao ya kwanza ni finyu. Yanahusu tu umbo la baadhi ya kazi za sanaa kama Ushairi. Maana ya pili ni pana lakini haitaji vipashio vya fani.

Kutoka Oxford Advanced Learners Dictionary tuna maelezo kuwa, fani ni: "umbo la nje la kitu au mtu; mpangilio mahsusi wa kitu au muundo wa kitu; jinsi kitu kinavyoonekana au kukaa; muundo wa kawaida na mpangilio wa kitu katika zile tungo za kimuziki au zilizoandikwa, kinyume na maudhui yake". Maelezo haya nayo ni sawa na yale ya kina Beckson & Ganz.

Msokile, M(1993) anasema kuwa, "Fani ni, umbo, ufundi, umbo au muundo wa kazi ya sanaa. Mambo kama lugha itumikayo, mtindo, muundo, mandhari na kadhalika." Kwa ufupi ni kuwa, fani ni mbinu za kisanii ambazo hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe au maudhui. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya lugha, mandhari, wakati, wahusika, mtindo na ploti ambavyo huweka wazi mtazamo wa msanii katika kuvyaza toni ya kazi.

### 2:1:2 SIFA ZA KIFANI KATIKA USHAIRI

Ushairi umeelezwa katika kamusi ya Kiswahili sanifu kama. "kazi au namna ya kutunga mashairi". Shairi limeelezwa katika kamusi hiyo kama; "mtungo wa kisanii wenye mpangilio maalum wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo unaoelezea wazo au tukio juu ya maisha na ambao hufuata utaratibu wa urari na muwala maalum unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utunzi wa ushairi unaohusika". Maelezo haya yameangazia fani na maudhui na hivyo yatosheleza kwa kina.

Maelezo hayo yanaenda hatua moja zaidi ya yale ya wanaurasimu ambao waliamini kuwa utunzi unafaa zaidi lau utafuata njia na taratibu zinazothibitika kijarabati[1]. Imani hapa ni kuwa, kazi zikifuata kanuni sawa zitathibitika na kutokea vivyo hivyo nyakati zote zitakapojaribiwa na kuhakikiwa kwa misingi ya njia zile zile. Kwa ufupi basi ni kuwa, mashairi ni, "Tungo za sanaa zenye mdundo maalum katika mpangilio na uteuzi wa msamiati katika lugha, unaofuata taratibu za mishororo na beti katika kuwasilisha ujumbe kwa mitindo mbalimbali ili kutimiza nia maalum".

Baada ya kuangalia maana ya ushairi, kuna haja pia ya kuangalia sifa ambazo huutofautisha na matawi yale ya tamthilia na riwaya. Haya yanafungamana na maelekezo ya wanaurasimu kuwa matumizi ya fani hutambulisha utanzu (genre) wa tungo. Sifa ambazo hutuwezesha kuupambanua ushairi au kuuchanganua toka yale matawi mengine ya kifasihi ni za kifani zaidi kuliko za kimaudhui.

Maudhui ya kisanii ni yale yale - hayabadiliki, na huendelezwa kwa mitindo mbalimbali. Njia hizi mbalimbali za kifani za kuyaelezea maudhui ndizo hutuwezesha kupata mafungu ya kifasihi ya ushairi, tamthilia na riwaya.

Vipengele vya fani kama lugha, mtindo na wahusika husaidia sana katika uainishi wa tanzu za kazi. Kwa mfano, lugha, ambayo ni ya ushairi huwa tofauti na ile katika tamthilia au riwaya. Hili linategemea mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha katika tanzu hizo. Katika ushairi, lugha inatumiwa kwa njia ya mkato na maelezo si ya undani na kina sana kama yalivyo katika riwaya ambapo mshairi hutoa maelezo na maelezo kuhusu jambo kwa mizunguko na njia mbalimbali ili kuwafikia wasomaji wake. katika ushairi na tamthilia hili halitokei. Lugha hutumiwa kwa wekevu mwingi na katika umbo la kibeti kinyume kabisa na la kiaya katika tungo za tutumbi (nathari). Wahusika katika tamthilia na katika ushairi hasa katika ushairi wa Ngonjera na Malumbano hutokea kwa mpangilio ulio sawa kinyume kabisa na ule katika nathari. Kwa mwongozo wao kunatokea uanishi wa tanzu za fasihi.

Mandhari, ploti, wakati na toni hutufaa, katika ufafanuzi wa vipengele hivyo pambanuzi. Katika lugha, huangaliwa mambo kadha katika viwango vya; msamiati, maana, uwezo na mahusiano; urasimu wa lugha iliyotumiwa na matumizi ya tamathali. Katika kiwango cha kwanza, huangaliwa mambo kama; uteuzi wa msamiati, aina ya msamiati; uwezo wa msamiati; kariha na motisha katika matumizi ya msamiati; mazingira ambamo msamiati hutumiwa; mpangilio wa msamiati; jinsi msamiati ulivyoundwa; njia za upanuzi maana katika msamiati na athari yao katika tungo; uangavu na utata wa msamiati, wizani kimaana (Ridhimu kisemantiki); matokeo ya uhuru wa kishairi na jinsi mbalimbali za maana katika maneno.

Kiwango cha pili kina kuangaliwa kwa kiwango cha lugha iliyotumiwa - ni ya urasimu[2] au ni simo[3] au lugha mitaa[4]. Kiwango cha tatu huangalia matumizi ya tamathali za usemi, uamili wao, na umuhimu wao katika tungo. Viwango hivyo hutuwezesha kujua jinsi lugha ilivyotumiwa. Udhibiti wa lugha katika viwango hivyo vyote humpa mamlaka mtunzi kuitumia lugha kwa kujiamini na kwa njia za hakika.

Katika ushairi, lugha ina sifa ya maneno kupangiliwa kibeti na kwa njia isiyofuata kaida za kiisimu kwa sababu ya ule uhuru wa kishairi unaodhihirika kimsingi katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Uhuru huo humruhusu mshairi kughairi mwongozo wa kiisimu katika viwango hivyo vinne lau matumizi hayo yatafaulisha kifani, thamani ya tungo, au ubora wa kazi.

Kwa hivyo, matumizi ya lugha, na mtindo hutuwezesha kuainisha ushairi na yale mawako[5] mengine ya kifasihi. Kwa kiasi fulani, wahusika huchangia katika maumbo ya ngonjera na malumbano ambayo hutofautishwa kwa kigezo cha maudhui. Ngonjera huongea kuhusu maudhui yasiyo mazito na kwa njia isiyo nzito. Malumbano huendeleza maudhui mazito na kwa fani nzito.

Riwaya hutambulishwa na ile sifa ya maendelezo ya msamiati kitutumbi katika maumbo ya aya, japo wakati mwingine, na, kwa uchache hutokea maumbo ya kibeti. Hili hutokea ili kuvunja ule uchovu wa mtindo mmoja wa maelezo. Matumizi haya kwa kiasi fulani huleta msisimko na mvuto kwa hadhira lau yatatokea kwa uzuri katika mazingira na wakati muafaka. Mfano huu kutoka siku ya watenzi wote (1968:102) unatuthibitishia kauli.

> Watu wenye utukufu, katika dunia hii
> Ndiyo wawao dhaifu, fahamu kama hujui
> Na wenye utakatifu, na maarifa na rai
> Ndiyo walao nyamafu, na wakuu wa jinai

Hayo ni mawazo yaliyompitia na kumsisimua Sarah, ambayo yameelezwa kwa njia inayoridhisha, ya mkato na inayoondoa ukinaifu[6] katika maendelezo ya kiaya. Ni mtindo unaofaa kisanii lau msanii ataumudu.

Katika tamthilia, sifa bainifu hutokea katika mpangilio wa wahusika ili kurahisisha kuigizika kwa tungo jukwaani. Maneno hupangiliwa kinathari au kibeti. Sifa hii ya mpangilio wa wahusika hutokea katika ngonjera na malumbano, na sifa zao tambuzi tayari tumeziona. Mengi zaidi kuhusu mitindo ya kishairi yameangaliwa katika sehemu ya mtindo.

## 2:2 LUGHA

### 2:2:1 MAANA YA LUGHA

Wanafasihi na wanalugha wanaelekea kukubaliana kuhusu maana ya lugha. Yafuatayo ni baadhi ya maelezo yao.

Mdee, J.D,(1986) anasema kuwa, "lugha ni chombo kilichoundwa na wanadamu kwa ajili ya matumizi yao". Katika kitabu chake cha Kiswahili: muundo na matumizi, amenukuu maoni ya wataalamu wengine. Kwanza amemnukuu Charles L. Meader katika kamusi ya Encyclopedia Americana ambaye anasema kuwa, lugha

ni njia yoyote ya kuelezea fikira. Pili ni maoni ya Otto Josepersen katika Encyclopedia Brittanica ambaye anasema kuwa, lugha ni njia yoyote ya mawasiliano kati ya viumbe vyenye uhai -- iwapo imekuzwa na kuwa ya hali ya juu sana hujibainisha na binadamu pekee. Tatu, amechukua maelezo kutoka Webster's New International Dictionary ambayo yanasema kuwa lugha ni maneno yaliyotamkwa na yenye kusikika ambayo hufanywa kwa msuguano wa ulimi na ala za sauti zilizo jirani nao -- maneno hupangiliwa kwa namna inayoeleweka kwa jamii ya wazungumzaji. Mwisho, amechukua maoni ya John Hughes, Kutoka The Science of language 1967, ambayo yanasema kuwa, lugha ni mfumo nasibu wa alama za sauti ambao husafirisha fikira kutoka mtu mmoja hadi mwingine.

Mtaalamu mwingine aliyechangia ni Loreto Todd katika kitabu An Introduction to Linguistics ambaye anasema kuwa, lugha ni fungu la ishara ambazo kwazo tunawasiliana.

Naye Senkoro, F.E.M.K,(1982:13), anasema kuwa, "kipengele cha lugha ni muhimu sana kwani ndicho kinachotofautisha fasihi na sanaa zinginezo, kwa mfano za uchoraji ambao kipengele chake muhimu ni kalamu, rangi na kipande cha kartasi au nguo n.K; lugha basi, ndiyo njia aitumiayo msanii wa fasihi kuyaelezea mambo mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya ubunaji na kiusanii".

Hatima ni maelezo ya msokile, M, (1993:85), ambaye anasema kuwa, lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana ambao hutumiwa na watu wa taifa au kabila moja kwa ajili ya kuwasiliana; maneno na matumizi yake; mtindo anaotumia mtu kujieleza. Maelezo haya ni reale kwa ya pili na yale yaliyomo katika kamusi ya kiswahili sanifu.

Kwa kuzingatia maoni ya hao na wengine ambao hatukuwataja tunaweza kuielezea lugha kama, "Zao la jamii linalotumia maneno na sauti kwa utaratibu maalum unaokubalika katika kuleta mawasiliano na lenye uwezo wa kubadilika kiwakati".

Lugha ya ushairi ina sifa kadhaa kama zinavyobainika katika sura hii. Maswali kama lugha ya ushairi ina sifa zipi?, Uamili wake ni upi, na uwezo wake umo kwenye nini?, Inatofautianaje na lugha ya kawaida?, Na mengine yamejibiwa katika sehemu hii.

Lugha hutumiwa na wanajamii katika kupashana habari na kuwasiliana. Matumizi yake huwa mengi yakitegemea mahali na hali ya wanaoitumia. Kila mtu na kundi la wanajamii huitumia kivyake, na hivyo kunatokea aina fulani ya matumizi katika fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia. Ina sifa ya kubadilikabadilika na hivyo ni muhimu kuhakiki mabadiliko hayo na athari zake katika lugha kwa jumla. Mabadiliko mengi ambayo hasa ni ya kileksia na kisemantiki lazima yahakikiwe ili kupima matokeo ya mabadiliko hayo.

Uhakiki wa lugha ni muhimu katika kutupa uamili wake na udhibiti wake wa mawasiliano. Waandishi mbalimbali hutofautiana katika matumizi ya lugha, hili likitegemea makini yao katika utunzi, tajriba zao za kuitumia, na uwezo walio nao wa

kuelezea mambo. Kunga wanazozitumia za lugha na uhusiano wake na vipengele vya fani huimarisha hali ya mawasiliano ya tungo.

Ingawa wanalugha na wasanii hufuata taratibu fulani katika matumizi yao ya lugha, wakati mwingine huzikiuka kwa sababu maalum, kama vile kuwapa wahusika nafasi moja kwa moja kuongea ili tujue ugugumizi wao, ububu, ulevi, ugonjwa, au tuone hali ya lugha iliyo katika udhibiti wao, ambayo yawezakuwa kiswahili safi, sanifu, sheng, Engsh na Engshve[6].

Ingawa watunzi wa fasihi wana uhuru katika matumizi ya lugha, watunzi wa ushairi wana uhuru zaidi, siyo tu katika kuchezea mpangilio wa vipashio vya maneno, bali pia mpangilio mzima wa fungu la maneno au hata mpangilio mzima wa mishororo na hata beti. Uhuru huu katika sintaksia na mofolojia huendelezwa kwa namna ambayo haitatizi fonolojia na uibukaji wa maana katika tungo. Katika mofolojia, maneno hupunguzwa vipashio, huongezwa, na hata hubadilishwa kwa ustadi, makini na ufundi mkubwa kusudi yasipoteze maana na yatamkike kwa urahisi. Kwa sababu hii, mpangilio wa maneno wakati mwingine huonekana kama mkorogo wa maneno unaohitaji makini, hadhari, uzingativu na utulivu ili kupata maana. Ufuatao, ni mfano, wa uhuru wa kishairi katika kiwango cha mofolojia. Neno jehanamu linaweza kubadilishwa na kuchukua maumbo kadha kama Jehanami, Jehana, Jehanama, Jehaanaamu, Jahanamu, Jahanami, Jehanamo, Jehaanamu, Jahaanami, Jahanamo, Jahaanamu, Jehaanaami, na kadhalika ili kupata kina au idadi kamili ya mizani katika mishororo. Uhuru huo wa inkisari, tabdila na mazida haukusudiwi kukoroga ujumbe bali kuuwezesha kuwafikia wasomaji kwa hali bora zaidi isiyosinya.

Swala la lugha limepatiwa uzito mkubwa kwa sababu ya ule uwezo wake wa kuwasilisha mawazo kinyume na vile vipengele vingine vya fani, ambavyo havina uwezo wa kujielezea kama ambavyo lugha hutumiwa kufafanulia maswala yanayoihusu. Lugha ya ushairi sawa na lugha ya sanaa yote kwa jumla ni lugha bunifu, hisishi na inayotekeleza jukumu la kuwasilisha. Kwa sababu hii mwandishi yeyote wa fasihi apaswa kutambua kwamba, jukumu la kazi yake ni kuwasilisha. Hatungi kwa sababu tu kashikwa na muhu[7], bali pia hujali namna atakavyopitisha ujumbe. Nia ni uwafikie wasomaji na lau sivyo huwa kama silaha butu isiyofaa.

Kwa sababu hiyo yampasa kila mtunzi kuhakikisha kwamba hata iwe ni kidhahania, ana picha halisi ya hadhira anayoilenga. Hivyo ala zake za utunzi zapaswa kuzaa mazao bora na ambayo yapaswa kuwafikia waliokusudiwa kwa uwazi na unyoofu. Matumizi mabaya ya lugha, humtenga msanii na hadhira yake, na mawazo yake hata yakiwa mazuri vipi huepukwa kama walivyoepukwa wagonjwa wa Ebola wakati fulani, watu wakihofia kuambukizwa lau watatangamana na wawele. Hili linatuelekeza kwenye ukweli kwamba kinachofaa kwa wasomaji si maisha ya mwandishi bali mawazo yake, na namna yalivyowasilishwa. Akiwa na mawazo mazuri na yawafikie watu kwa njia nzuri, basi hapo jukumu la kazi ya sanaa litakuwa limekamilika.

Lugha ina mamlaka ya kuwasilisha na yeyote asiyeweza kuyadhibiti mamlaka hayo, ataponyokwa na lugha kinyume na matazamio. Kwa sababu hiyo, kuna haja kubwa ya kudhibiti na kumiliki lugha katika fani zake zote ili kuepukana na mawezekano ya mawasiliano butu, ukosefu wa mawasiliano, udhoofu wa mawasiliano, uyumbifu na upungufu wa mawasiliano.

Lugha yoyote hujengwa na maneno ya maumbo mbalimbali. Mpangilio mzuri wa maneno hayo huleta maana iliyokusudiwa. Hata hivyo, hili si jambo la lazima katika ushairi, kwani mpangilio wa maneno si lazima uitikie kanuni za kisarufi.

Mshairi ana uhuru wa kutumia msamiati anaoupenda, lakini apaswa kuwatolea wasomaji maelezo ya msamiati wake ili wapambanukiwe na alichokusudia. Mshairi yeyote anayekosa kufanya hivyo, huwa hajali dhima yake, wajibu wake na hawajali wasomaji wake. Sababu za hili, ni kuwa siyo watu wote wana uwezo sawa wa kuelewa na kufahamu mambo. Si ajabu kuona baadhi wakiyapa mawazo mepesi fasiri nzito nzito kwa sababu yamewasilishwa kwa mafumbo, njia tata au hali isiyotoa mwangaza katika maana za maneno. Lugha hutawala mawasiliano yote kwa namna inayovutia ikiwa msanii atakuwa na uwezo mkubwa wa kuitumia ipasavyo.

Mwandishi Korg J, (1959), anasema kuwa, hali ya ushairi inakaribiana sana na ile ya malighafi yake (lugha). Lugha ni kitu badilifu, elezevu na funizi[8]. Udhaifu wake umo katika kukosa uwazi na udhahiri katika maana na hali linganishi, kubadilika kwake na kutodumu kwake, ugumu na ukosefu wa uelekevu na hali ya kukaidi baadhi ya mambo. Lakini katika ushairi (kama ilivyo katika sanaa zingine) ule udhaifu wa lugha humpa msanii mvuto katika uteuzi wa namna ya kuwasilisha.

Korg amemnukuu Wordsworth akisema kuwa, matumizi sahili sana ya lugha hayahisiki tena kuwa hayafai katika ushairi. Funzo lingine kutoka kwake ambalo pengine ni muhimu ni hisia kuwa, ushairi haupaswi kubanwa kwenye viwango vya lugha asilia na lugha zufu[9], ingawa yawezabadilisha kiwango chake ikitegemea mada na hata tumia msamiati wa viwango mbalimbali vya maana, katika njia sawa na inayowezatumia unasibishi, kukuza na kuimarisha nguvu zake za uelezi.

Kwa upande mwingine inakuwa kawaida sana kwa ushairi wa kisasa kujishughulisha na maswala mazito kwa njia tata. Wakati mwingine toni ya usemi wa mazungumzo huelekea kusema kuwa mshairi hachukui jukumu maalum la utabiri, hajitengi na msomaji wake na badala yake anachukua lengo la kuwasilisha kitu cha kawaida na kilichozoeleka. Wakati wazo la shairi linapotokea kuwa geni, la ajabu na hemshi[10], matokeo yake kwa hekima huongezeka kinyume na jinsi ilivyoelezwa. Hata hivyo sifa fulani za miongozo ya kiisimu hutatiza juhudi za kusoma ushairi. Maana za maneno hazidumu na hubadilikabadilika. Huku kukiwa tatizo mara nyingi kushika kivuli halisi cha maana na unasibishi wa neno fulani katika ushairi wa kisasa, shida hiyo huongezeka katika ushairi wa zamani.

Ni maneno haba sana hudumisha maana zao katika matumizi yao katika kipindi cha mamia ya miaka; kama inavyotokea katika baadhi ya maneno yaliyotumiwa sana katika ushairi wa zamani kama vile, akili, sanaa, tunu hali, utu, wengu (bandama), nyama, tisho na mengine. Mahame hayo ya maana na sifa zingine za hali ya kiisimu,

ni swala linalosomwa kimakini na wasomi wengi. Matokeo ya kazi zao yamewasilishwa kama visaidizi vya msomaji kwa njia ya tanbihi na sherehe ambazo sana huwepo katika ushairi uliochapishwa katika matoleo ya kiusomi na pia kutokea katika makamusi maalum.

Uchangamfu wa kupata mawazo ya watu walioadhimika huchochea ubunifu wa wasomaji katika kubahatisha maana na semi zisizoelezeka. Matini ya ushairi kwa njia ya uchunguzi wa makini wa leksia na sifa za kisintaksia, zikihusisha pia tamathali za usemi na elementi za wizani,-- hujaribu kubadilisha taratibu za kisanii zinazopatikana katika matini kwa njia ya nadharia, wasilisho, uchanganuzi na usarufi wa lugha ya wahakiki.

Maana ashirifu, mapendekezo ziada (overtone) na arki za akili-laza ni muhimu katika ushairi. Washairi wengine katika kupima maneno, huwa makini sana katika taathira zinazowezazaliwa kwa matumizi ya sifa zao batini kama zilivyo katika maana zao za kidhana. Valery, kwa mfano, akifikiria uchunguzi wa mshairi, na wa maneno, aliangazia wana, muundo wa silabi, thamani za sauti na mawezekano ya mizani, na baada ya haya, maana zao na toni.

Fungutenzi huwa la kifasihi ikiwa litawasilisha mada katika zaidi ya kiwango kimoja katika wakati mmoja au kama sehemu moja ya tamko ina uamili zaidi ya mmoja katika umbo lililotumika. Katika elementi za lazima za kufanya tamko kuwa na maana yenye nguvu zaidi ni sintaksia, ambayo hudhibiti ule mpangilio wa upokezi wa ushawishi na kuonyesha ule uhusiano wa fikira na mpangilio wa maneno.

Sintaksia ni muhimu sana kwa mshairi na mhakiki huku ikiathiri sana kwa njia ya sitara. Ni msingi wa sanaa ya mshairi. Elementi mbalimbali kama sintaksia, vina na usemi, hutangamana na kuingiliana zenyewe. Chanzo halisi cha nguvu za usemi na ufahamu katika ushairi, huwa mara nyingi kimesitiriwa sana. Kinachopangilia nguvu za maana katika maneno, kwa kuzikusanya mahali moja toka ambamo zawafiki ni sintaksia.

Kwa mujibu wa Winifred Nowottny, maana na thamani ya ushairi ni zao na utaratibu mzima wa elementi za lugha, zote zikiwa na uwezo mkubwa wa ufasaha, ambao hudhihirika wakati elementi inapopambanuliwa kwa kuihusisha na nyingine; na kwa hili, uhitilafiano kuhusu mahusiano na yawezekana kufululiza madhali mahusiano yanayotumika katika shairi yamo katika mgongano usiokisiwa vizuri na kuelezwa; pia, mijadala hakiki ya ujumla ya hali na umuhimu wa elementi yoyote ya lugha ya ushairi haitazamiwi kuzalisha chochote ila, tu kwa kuangazia mahusiano yaliyo baina ya elementi moja na zingine.

Hali ya kuangalia mawako jenzi ya lugha ya ushairi huchochea hamu ya mchunguzi wa nguvu zilizomo katika maneno ya ushairi. Sintaksia kwa ukariri au msukumo dhibitifu wa makini, huhudumu kama kipangilio kikubwa cha elementi katika ruwaza au msukumo wa shairi. Kwa njia ya muhtasari, tuna viwango zaidi vya uhakiki wa lugha ambavyo tumevifikia kwa kupitia kazi mbalimbali za wanaurasimu na wahakiki wengine.

## 2:2:2 MSAMIATI: MAANA, UWEZO NA MAHUSIANO

### 2:2:2:1 UTEUZI WA MSAMIATI

Hapa kunaangaliwa kama msanii ameteua msamiati vizuri au vibaya. Mshairi ana uhuru wa kutumia msamiati, lakini apaswa kutathmini uwezo wa msamiati wake na kisha kuitolea hadhira yake maelezo kuhusu maana (ikiwa ni ngumu) katika sehemu ya sherehe. Maneno hutumika vizuri kwa njia asilia yakiteuliwa kwa makini.

Hali ya uteuzi wa neno muafaka huzingatiwa sana katika ushairi. Pia kuna ughafi na ubunifu katika hali ya matumizi ya leksia za ushairi. Neno muafaka huwa tu muafaka katika matini au muktadha fulani - ndiyo maana ufaafu wa fungu hauwezi kutegemea tu neno moja. Kuelekeza matokeo ya ufahamu kwenye usemi ambamo nguvu za maneno haya elezi hutokea ni sawa na kuchukulia kuwa shairi lote halikuwa kitu kabla ya neno fulani kutumiwa.

Msanii huitumia lugha kuepuka ule udhaifu wake asilia kwa kutumia malighafi inayofaa. Hufanya hivyo kwa kutumia maneno yaliyo ya kawaida kwa njia maalum. Hili humwezesha kujielezea kwa ufasaha katika maneno aliyoyachagua. Kwa kuwa neno vutifu (pambe) huweza inua athari (matokeo) ya fungu la maneno, mshairi lazima ataabike katika kuhakikisha kwamba neno atakalochagua ni litakalochangia haja hiyo.

Kila neno huwa huria kiasi kwamba lawezatumika kwa njia nyingi. Hali tatizi ya lugha humsukuma mshairi kwenye chaguzi nyingi na teti, na katika hali ambapo neno moja tu lawezakuwa na maana nyingi.

Wasomaji wengi hujiuliza kuwa maneno ya ushairi hupata wapi nguvu zao? Huenda si maneno ya kawaida bali ya ajabu. Ukweli ni kwamba ushairi na sanaa huchota maneno yake kutoka hazina pana ya lugha ya kawaida. Kile ambacho huipa nguvu ni uteuzi mzuri, mpangilio mzuri, uhusiano mwema na mazingira, wahusika na mkatiko wa matukio katika nyakati faafu. Mbinu nzuri za kupangilia maneno hayo hutupa mazao yenye kugusa hisia na kuathiri fikira zetu.

### 2:2:2:2 AINA YA MSAMIATI

Katika kiwango hiki kunaangaliwa kama msamiati uliotumiwa ni wa lahaja au ni wa lugha sanifu. Pia unaangaliwa kama ni wa mafumbo au wazi, hafifu au wenye nguvu. Aina ya msamiati hufaa katika kupambanua maana.

### 2:2:2:3 ASILI YA MSAMIATI

Msamiati una asili katika lugha sanifu, lahaja au hata lugha za kigeni. Hutuwezesha kuondoa hali ya kubahatisha katika maana za maneno.

Tathmini sawa na ya kina yapaswa kuzingatiwa katika kutambua asili ya msamiati, nguvu zake, ulegevu wake, na kwa nini yanapatiwa nafasi.

Matumizi ya msamiati mwingi na wa asili nyingi hutupa aina za kunga za uhamishi wa ndimi, mchanganyo wa ndimi na Tadmini. Ni mbinu ambazo huwa na leksia ambazo hazitokani na kiswahili tu, japo baadhi huswahilishwa kifonolojia, kimofolojia, kisemantiki na baadhi humezwa kiasi kwamba haziwezi kutambuliwa kuwa zina asili ya kigeni.

Asili ya maneno ni muhimu katika kutuwezesha kutambua maana zao asilia. Katika zile jinsi mbili za maana (halisi na nasibishi), hutuwezesha kujua maana asilia za maneno na maana zao nasibishi. Mgao huu wa sifa za kisemantiki katika maneno humaanisha kuwa maneno huelekezwa kwenye kitu au tajriba na aidha hupendekeza hali guso katika kukielekeza kwa mshairi, ambacho hakukusudia kumwathiria msomaji.

Mtazamo wa msamiati wa ushairi kiwakati ni muhimu katika kutuwezesha kutambua kama maana zao asilia zimehifadhika, potea au hata ongezeka. Hili hufaa katika kuona maendeleo yaliyofikiwa kisanii. Kuna msamiati mwingi wa kiasili uliohifadhiwa huku mwingine ukipotea kwa sababu za kihistoria, kiisimu na kadhalika. Msamiati kama mtima, ng'andu, vitimbi na mwingine wa kale hadi sasa wahifadhi maana zao. Msamiati kama sono, nyono, zitono, karaba, tindikano, matelo na mwingine mwingi hautumiki sana ila tu katika lugha ya ushairi zaidi. Inavutia kugundua kwamba baadhi ya msamiati huo kama nyia una maana tofauti na ile asilia. Awali lilitumika kwa maana ya sahani katika wingi (sahani likiwa la asili ya kiarabu). Matumizi yake hivi sasa ni yale ya kiushairi, likitumiwa kama kisawe cha nyimbo (nyiso). Mfano wa matumizi ni kama, nyia za kongozi, kwa maana ya nyimbo za kuukongowea (kuukaribisha) mwaka mpya.

### 2:2:2:4 NGUVU/UWEZO WA MSAMIATI

Hapa kunaangaliwa kama msamiati uliotumiwa unafaa katika kuhimili majukumu ya kishairi. Uwezo wa msamiati katika shairi hutegemea uzito wa maana zao, namna ulivyotumiwa, mahali ulipotumiwa na kadhalika.

Pia kunaangaliwa kama msamiati unajitosheleza na una uwezo wa msukumo wa mawazo kwa namna inayokidhi au vipi? Ni msamiati hafifu usiosaidia kuendeleza mawazo ya mwandishi, kwa njia inayogusa, natisha na nasa nadhari za wasomaji? Una uwezo wa kudhibiti na kutawala mawasiliano kwa namna inayoleta upevu wa lugha na mawazo?

Haya na mengine ndiyo tuliyoyaangalia katika tungo za Hassan Mwalimu Mbega.

### 2:2:2:5 MOTISHA/KARIHA KATIKA MATUMIZI YA MSAMIATI

Msamiati ulioteuliwa lazima uwe ule unaompa msomaji hamu ya kusoma kazi na kudhibiti bila kubandukana na nadhari yake. Lau hili litakosekana, basi ulegevu huo katika matumizi ya msamiati utamtibua moyo msomaji ambaye huenda akakosa hamu ya kuzisoma tungo.

## 2:2:2:6 MAZINGIRA YA MATUMIZI YA MSAMIATI

Mazingira ya matumizi ya leksia yasiwe ya kuruhusu kupwaya kwake na kutojitosheleza. Ni lazima yawe mazingira yanayofaa ambayo yanauwezesha msamiati kuwasilisha vizuri. Tunakusudia kwamba neno lazima liweze kuwasilisha - liwe na uwezo wa kuwasilisha maana hata bila kuhusishwa na mengine.

Mwongozo wa matumizi ya maneno katika mazingira maalum hufaa sana katika kutuongoza kufikia maamuzi ya maneno kwa maana asilia na za kawaida na ni muhimu mazingira ya muktadha kubainika kusudi kupata ile maana yake.

Maneno yenyewe huwa elezevu zaidi nyakati yakitokea katika matini zao au miktadha yao.

Ufanisi wa mshairi haumo katika uteuzi wa neno muafaka, bali katika kulitafutia muktadha ambamo litafaa zaidi. Tatizo la mshairi siyo tu kutafuta neno ambalo litafaa sana katika kutimiza nia yake katika shairi zima, bali pia njia litakavyotumika. Ni muhimu mazingira na miktadha ya matumizi kubainika kusudi kupata ile maana yake katika matumizi hayo. Ndiyo maana neno lolote halipaswi kupuuzwa madhali limetumiwa. Hivyo si kudai kuwa neno hilo lawezaleta athari peke yake bila kuhusishwa na mengine. Lau neno hilo halifahamiki, yale mengine yatasaidia katika kuwaongoza wasomaji kupata angalau mwanya wa mwangaza wa kimaana.

Katika ushairi maneno hunolewa na mengine ili ncha zao za maana ziwe kali zaidi kuliko zilivyo kawaida. Muktadha wawezaligeuza neno kuwa sitiari na panua maana yake hadi mahali papya pa matumizi katika shairi. Jinsi ambavyo sehemu yote ya mstari ni muktadha wa neno fulani na huathiri maana yake, ndivyo basi neno pekee huwa sehemu ya muktadha wa maneno yanayolizunguka na kuwa na athari kwalo. Uhusiano huu dhalili wa sawa baina ya maneno pekee na maana ya usemi mzima hudhihirika katika ushairi.

Wakati mwingine washairi huenda kwa kina sana ili kumfanya msomaji ajue maana kamili aliyonuia nayo. Unoaji na mikazo ya maana huwezekana kwa sababu kila neno lina idadi kubwa ya mawezekano ya maana nyingi. Lakini maneno hayawi tu na maana, bali pia aina tofauti za maana. Itatosha kuzigawa aina hizi za maana kuwa halisi na nasibishi. Ufafanuzi kuhusu aina hizi za maana umeangaliwa katika sehemu ya 2:2:1:13.

## 2:2:2:7 VIPASHIO VYA MSAMIATI

Kwa sababu ya ule uhuru wa kishairi katika kiwango cha fonolojia na mofolojia, baadhi ya maneno hupata vipashio ziada, hupunguzwa au hubadilishwa. Katika kufanya hivyo maana hutanguka katika baadhi lau hilo limefanyika kikaidi bila kujali matokeo. Kwa kuvihakiki vipashio vya leksia, mhakiki hupata maana asilia ya neno.

Baadhi ya vipashio huwa ni vile ambavyo havikutarajiwa na visivyofaa katika matumizi. Vipashio hivi huleta mkorogo, katika mpangilio wa mizani katika neno. Hili hupotosha maana na kulegeza nguvu za neno au hata kulikosesha maana kabisa.

Baadhi ya maneno huwa si rahisi kupata maana zao hata kwa kubahatisha kwa sababu ya uchopekaji wa vipengele ambavyo hutokea kihorera bila ya kutathmini matokeo ya jambo hilo.

Uhakiki huu wa viambajengo ni muhimu sana kwani huwaongoza wahakiki na wasanii siyo tu kutambua vina na idadi ya mizani, bali pia aina za bahari za tungo. Hili ni muhimu sana katika uainishi wa tungo ambazo hulingana kwa sifa zingine. Tungo za tumbuizo na ukawafi hutambulikana kimsingi kwa sababu ya idadi ya silabi na mizani katika kila mshororo. Mashairi kama Gungu na tenzi hutambulikana kwa kuzingatia sifa za idadi ya mizani katika mishororo

### 2:2:2:8 <u>MPANGILIO WA MSAMIATI</u>

Hapa tumeangalia uhusiano baina ya maneno yaliyotumiwa katika tungo. Hili hutokea pale sintaksia inapofanya kazi yake katika kuleta unyoofu wa kisemantiki. Mahusiano haya hufaa katika kuonyesha kuwa neno limetumiwa vizuri au vibaya. Haya ndiyo yaliyoangaliwa katika diwani hizo za Mwalimu Mbega.

### 2:2:2:9 <u>NAMNA MSAMIATI ULIVYOUNDWA</u>

Njia nyingi hutumiwa katika kuundia msamiati. Kipengele hiki kinapatiwa uzito na ile haja ya kutathmini namna msamiati ulivyoundwa ili kumwezesha msomaji kupata maana kamili ya maneno.

Uhuru wa kishairi huwawezesha washairi hata kuunda msamiati nonsi (wa wakati maalum) ili kuwawezesha kukamilisha tungo zao. Kwa kuelewa namna neno lilivyoundwa, msomaji atakuwa katika nafasi nzuri ya kuuelewa msamiati ambao pengine ulimkanganya.

### 2:2:2:10 <u>NJIA ZA UPANUZI WA MAANA KATIKA NENO NA ATHARI ZAO KATIKA KAZI</u>

Tunakusudia hapa njia mbalimbali ambazo hutumiwa kisanii katika kuuongezea msamiati maana na nguvu. Hili huitwa pia upanuzi wa kisemantiki. Njia zenyewe zimetajwa tu na zimeonyeshwa namna zinavyopanua maana katika sura mbili zinazofuata ambapo pia mifano imetolewa, kutoka kazi tulizozishughulikia.

Maneno huongezeka maana pale yanapotumiwa kisitiari. Hapa twakusudia zile sitiari hai, si sitiarififi.

Maneno pia hupanuka kimaana pale yapotumiwa kwa njia ya nidaa.

Mafumbo ni njia nyingine inayoruhusu maneno kupanuka kimaana.

Maneno mengine hupanuka maana yanapotumiwa kwa kuyahamishia maana toka matini asilia. Njia nyingine ni ya kulihamisha neno toka mazingira yake asilia ya matumizi. Matumizi katika mazingira mazuri na yanayofaa pia huliwezesha neno kujivutia maana zaidi au nguvu zaidi.

Sinonimia ni njia nyingine inayoyasaidia maneno kupata nguvu zaidi. Katika hali hii, maneno mawili au zaidi yanayotofautiana kiumbo lakini kupatana kisemantiki hutumiwa pamoja kusudi kumpa msomaji angalau maana hata moja ya neno. Katika mpangilio wao katika tungo, yale fuatilizi katika matumizi hukusudiwa kuyaongezea nguvu yale tangulizi.

Matumizi ya takriri katika vipashio vya viwango mbalimbali katika neno na fungu la maneno huchangia kuyapanulia maneno maana.

Kwa kiasi fulani na ikitegemea aina, tanakali sauti hufaa katika upanuzi wa kisemantiki.

Kupitia njia ya neolojia msamiati uliochakaa hubadilishwa, na mwingine wenye nguvu kutumiwa badala yake. Kwa mfano miaka ya nyuma,neno 'adabu' lilitumika kwa maana ya 'literature' kabla ya neno fasihi kupata nafasi. Isitoshe katika neolojia maneno hujiongezea maana, hupoteza maana na kuibuka na nyingine mpya. Kwa mfano neno miwa awali lilitumiwa kwa maana ya miiba. Leo latumiwa kwa maana ya aina ya mimea inayokamuliwa maji matamu ambayo hukaushwa yakawa sukari. Nalo neno tindikano, lenye asili ya kibantu lilitumiwa miaka ya nyuma kwa maana ya wakati na leo halitumiki.

Kwa ufupi ni kuwa matumizi ya maneno kinasibishi na kitamathali huyapanua maana na kuyaimarisha kisanii.

### 2:2:2:11 UANGAVU NA UTATA KATIKA MAANA ZA MSAMIATI

Msamiati huwa wa uangavu au utata kimaana. Wa uangavu hurahisisha mawasiliano huku wa nyuma ukizungusha fahamu za wasomaji. Hili hutokea wakati washairi waendapo kwa kina ili kumfanya msomaji kuelewa maana kamili ya lugha wanayonuia kuitumia. Unolevu na undani wa maana huwezekana kwa sababu kila neno huwa na hazina kubwa sana ya maana. Maneno pia huwa na maana za jinsi mbili; nasibishi na halisi. Hili limeangaliwa katika 2:2:1:13.

Wakati mwingine maneno huwa na utata. Mhakiki leo William Empson anasema kuwa, wakati mwingine neno au usemi waweza kisemantiki kuwa na zaidi ya maana moja. Korg haioni hali hii kuwa mbaya kisanii. Anasema, "katika nathari, utata wa lugha kwa kawaida ni dalili na chanzo cha mkanganyiko; lakini katika ushairi huwa hususan ni ala stadi ya kutajirisha nguvu elezi za lugha, njia ya werevu ya kusema vitu viwili kwa pamoja".

Washairi hutumia muktadha na nasibishi katika kupanua na kufinya maana za maneno. Kuhusu hali kama ya utata, Aristotle atoa ushauri ufuatao katika kitabu chake cha (Poetics) Taaluma ya ushairi, ambapo asema, "wakati neno likielekea

kukosa mshikamano katika mwelekeo wa kimaana, lazima tuangalie maana zake kadha linaloweza kuwa nazo katika usemi fulani".

Muktadha unafaa sana katika kutanzulia utata wa maana katika maneno. Hali tatizi ya lugha hutokea inayompa msanii chaguzi nyingi na teti, ambapo neno moja lawezakuwa na maana nyingi. Maana hizo nyingi zinazohusishwa na maneno ni za manufaa, kwani kila maana ingetengewa neno maalum basi tungekuwa na maneno mengi na ambapo kila moja lingeishia kimatumizi hapo tu. Ikiwa maneno si maangavu kimaana basi tutawasilianaje nayo? Hilo lawezekana kwa kuangalia muktadha wa matumizi. Umuhimu wa neno hutegemea mazingira. Neno huwa kitu hafifu kinachojipatia umbo kutokana na yale maneno mengine yanayolizunguka.

Neno huwa ni sehemu ya muktadha na mbali na hilo huwa na athari fulani katika huo muktadha. Sifa ya ushairi ni tangamano la maneno na maana zao katika ufahamu wa ushairi.

## 2:2:2:12 WIZANI KIMAANA

Kuna ridhimu fulani kisemantiki inayotokea maneno yanapopangiliwa vizuri. Hili hutokea katika mahusiano ya msamiati.

Kwa ufupi wizani kimaana, ni yale mapigo maalum au mdundo au ridhimu ambayo ni ya kimaana katika kazi, ambayo hutegemea mpangilio mzuri wa maneno. Wengine huiita kunga hii Ridhimu kisemantiki.

Kwa maelezo ya msokile, ni mapigo ya lugha ambayo ni ya asili. Kila lugha ina mapigo yake asili. Katika lugha, ridhimu husaidia kujenga maana na mwendo wakati wa kusema. Huleta mvuto fulani katika usemi. Tumechunguza haya katika diwani hizi tulizozishughulikia. Nia yetu ni kuona kama mpangilio wa msamiati kisemantiki umefanikiwa katika kuibua ridhimu au wizani.

Tayari yabainika kuwa, maana inayokusudiwa hapa siyo ya neno moja, bali ya muungano wa msamiati na mahusiano yao. Hili laturejesha kwenye uteuzi wa makini wa msamiati na kuutumia katika mahusiano yenye mvuto huo wa kimaana.

## 2:2:2:13 AINA MBALIMBALI ZA MAANA

Kwa mujibu wa Korg, J,(1959:36), maana za maneno kimsingi hugawika katika makundi ya maana halisi na maana nasibishi. Maana halisi za maneno ni maana asilia au tambuzi za maneno. Maana nasibishi ni maana kimatilaba. Ni maana inayoongezwa ili kudhihirisha hisia maalum.

Maana halisi ndizo wahakiki wanazozizingatia kama maana asilia au maana za lugha asilia na maana nasibishi kama maana zufu au maana za lugha zufu. Mwongozo wa matumizi ya maneno katika mazingira maalum hufaa katika

kutuongoza kufikia maamuzi ya maneno ya maana asilia na za kawaida, na maana nasibishi. Maana nasibishi hutuelekeza kwenye umuhimu wa tamathali za usemi. Mgao huu wa kisemantiki hauepukiki katika sanaa.

Mgao huu uliozoeleka wa sifa za kisemantiki za maneno humaanisha tu kuwa maneno mengi huashiria (hurejelea) kitu fulani, au tajriba na aidha hupendekeza msimamo hemshi kwenye kitu, katika upande wa msemaji, ambacho kawaida akusudia msikizaji wake awe na hisa. Kwa mfano maana halisi ya 'Kijibwa' ni mbwa mdogo au mchanga lakini neno kelbu shombe (mbwa suriama) ambalo lawezatumiwa na msemaji yuyo huyo kwa mbwa huyu katika muktadha (hali) mwingine hudhihirisha dharau.

Kweli, wakati maneno yanapotumiwa katika ushairi, kwa kawaida hupitia mageuzi ya kistadi na kiajabu; maana yao nasibishi huelekea kutawala ile halisi. Hili wakati mwingine hutokea katika ushairi. Kinyume na mwandishi nathari, ambaye zaidi anashughulikia uwezo wa maana halisi za lugha na kujitwalia maana nasibishi za maneno kwa kiwango tu cha kuzipanga kwa utaratibu, mshairi huchukulia kikawaida maana halisi za maneno anayoyatumia na kushughulikia kupuja (exploit) sifa zao nasibishi.

Maana nasibishi za maneno huwa muhimu sana, kiasi kwamba huelekea kujivutia maana yao yote, na kufuta ukinzano wao au sifa zao halisi (denotative properties).

Maneno yaliyotumiwa kiholela (kwa njia ya ovyo) huzalisha shairi duni.

Washairi lazima waepuke maneno yenye nasibishi zisizofaa, ingawa maneno yenye ufaafu zaidi kinasibishi hayawi hivyo siku zote, au kwa kawaida mazuri zaidi.

Washairi na wasomaji wao pambanufu (pendelevu) hufadhaishwa na matumizi mengi mno ya nasibishi. Ushairi mzuri zaidi huelekea kutumia nasibishi kuboresha uhalisi wa lugha, kuangazia kwa uwazi hisia inazoeleza kuliko inavyowezeshwa kufanya na lugha halisi. Mshairi aweza kufanya nasibishi kumhudumia kwa njia nyingi. Pengine njia ya kawaida zaidi na iliyozoeleka zaidi ni ile, ambayo kwayo sifa nasibishi za maneno husisitiza tu na kuongezea nguvu maana iliyoelezwa.

Ushairi pia wawezatumia maneno kwa njia ambayo yayafanya kubeba nasibishi ambazo kwa kawaida yanazo. Hii ndiyo sifa bainifu zaidi ya ushairi katika matumizi ya maneno. Umuhimu wa nasibishi katika lugha ya ushairi wawezadhihirika zaidi kwa mifano miwili, mmoja ukitumia maneno kwa njia za mapendekezo wazi ya kihemshi na nyingine inayotumia nasibishi kwa ustadi na uficho. Ni njia mojawapo ya ushairi kuepuka upungufu asilia wa lugha.

Washairi waweza pia tumia ala za sitiari zilizojengwa kindani ili kupanua maana za kawaida za maneno. Njia nyingine ya mshairi kutumia nasibishi katika kuongezea malighafi za kawaida za lugha ni kwa kufanya maneno yabebe sauti ndogo

inayoelezea kinyume na maana halisi zao. Kwa hivyo, kwa kusema vitu viwili vinavyokinzana kwa wakati mmoja, shairi hakika huelezea kupitia stihizai, maana ya tatu. Kwa hivyo twaona kuwa mchango wa nasibishi ni mkubwa sana katika kuimarisha nguvu za lugha ya kawaida.

### 2:2:2:14 TATHMINI YA UHURU WA KISHAIRI

Uhuru wa kishairi umeelezwa ifuatavyo katika Mulika nambari 16. Umeelezwa kama, "Uhuru wa mshairi kuweza kutumia miundo, msamiati au mpangilio wa lugha isiyokuwa sanifu bila ya kutoka nje ya msingi wa lugha inayohusika k.m. kutumia 'mbwene' badala ya 'nimeona'. Maelezo haya yamebanwa zaidi kwenye kiwango cha mofolojia, na hivyo hayatoshelezi sana kama inavyopaswa.

Tuna maelezo ya kuridhisha na kutosheleza ambayo yameshughulikia dhana hii kwa upana kutoka kwao, Karl Beckson na Arthur Ganz katika kamusi yao ya A Readers Guide to Literary Terms (1960:169), Wanasema kuwa, uhuru wa kishairi, ni, "uhuru uliofungishwa kwenye ushairi, unaochukuliwa na mshairi katika hali za mpangilio wa maneno, vina, matumizi ya maneno ya kale na tamathali za usemi".

Kutoka maelezo hayo ambayo yanafunika yale tuliyoyazoea katika kiwango cha mofolojia na kuupanua hadi viwango vya fonolojia, vikale, mtindo, sintaksia na semantiki, twafaidi kwa mengi.

Matumizi hayo ya lugha kutokana na huo uhuru hayakusudiwi kuharibu ubora wa tungo bali kuzihami zaidi na kuzipa nguvu. Nia yetu ni kuona namna uhuru huo ulivyotumiwa. Umetumiwa katika kubomoa au kuboresha tungo? Hili ndilo tumeshughulikia kujibu na mengine katika tungo tulizozitafiti.

### 2:2:3 KIWANGO CHA LUGHA ILIYOTUMIWA

Hali nyingine katika lugha ambayo ina umuhimu fulani katika ushairi ni ukweli kuwa maneno huwa na viwango tofauti vya matumizi; huingia katika viwango mbalimbali vya matumizi kama simo, umitaa, urasimu na kadhalika. Viwango hivi havielezwi kwa uwazi sana, kwani maneno mengi yawezaingia katika kiwango chochote, kama vile, mtu, mti, daraja, mkono na kadhalika. Yafaa katika kiwango chochote cha lugha.

Hata hivyo kuna maneno ambayo huleta hali isiyo ya urasimi kwa sababu ni ya simo tu, lahaja au lugha isiyo rasimu kabisa, kwa mfano, matumizi ya maneno kama kijitu, kijana fidhuli na kadhalika.

Katika upande mwingine, maneno mengine hufaa tu katika lugha ya mahusiano rasimu. Mfano wa maneno hayo ni 'ndoa' ambalo hutumika katika miktadha isiyo ya mizahazaha.

Japo viwango vyote ni muhimu, matumizi ya lugha ya kiwango cha urasimi yanasisitizwa sana katika sanaa, ingawa lazima kioane na dhamira. Matumizi ya lugha mitaa na simo hufaa lau yapendeza hadhira husika. Umuhimu wao huangaliwa katika kiwango cha dhamira na mwitikio wa hadhira kwa kazi ile yenye matumizi hayo

## 2:2:4 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi zimeelezwa kama, "fungu la maneno linalogeuza maana yake halisi ili kuwakilisha nyingine katika Mulika nambari 16.

Naye Senkoro, F.E.M.K(1982:13) anazielezea kuwa, ni, "maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Hizi wakati mwingine hutumiwa kuwa njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha".

Tamathali hizi hugawika katika mafungu kadha[9]. Uanishi wao unawekwa katika misingi ya mambo mengi. Kwa mfano kuhenga,(1977), amezigawa kama, tamathali za zinduna, za misisitizo, za vilinge, za mwigo wa sauti, tumbuizi, zindushi, linganishi tabia na kadhalika. Inadaiwa kuwa tamathali zote hufaa sana katika kujenga taswira. Umuhimu wa kila fungu ni mkubwa.

Umuhimu wao kwanza ni kwamba huwawezesha wasanii na watumizi wengine kupitisha ujumbe mkali bila matokeo mabaya papo kwa papo. Hili hutokea zaidi katika tamathali za vilinge kama vile mafumbo, vijembe, vinaya na kadhalika. Tamathali zingine husaidia katika kujenga picha zinazoeleweka ili kuzidi kumpanua msomaji fikira na kumpatia picha kamili ya mazingira na kile kinachoelezwa. Pia ni muhimu katika kudhibiti nafsi za hadhira; kuingilia hisia za ndani za hadhira ili kuishawishi kufikiri au kutenda; kushauri na kuchochea ikitegemea lengo; kuvunja uchakavu na uzoevu wa kawaida wa maneno; kuvuta nadhari za hadhira; kusisitiza na kufupisha masafa ujumi; kuibua mapigo mapya na yenye nguvu katika matumizi ya lugha ya kawaida; kuhimiza na kushawishi matumizi aina aina ya lugha ile ile na kadhalika.

Matumizi ya lugha ya kitamathali huibua hali inayokosa ukawaida fulani katika lugha na hivyo kuimarisha na kuyapa mapigo na msukumo mkubwa mawasilisho ya mawazo. Siyo tamathali zote huwa na nguvu za kuzalisha hali hiyo kwani baadhi huwa hafifu ikitegemea wakati zinapotumiwa, mahali zinapotumiwa na mazingira ambamo zinatumika. Mazingira ya matumizi yao huwa ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kimapenzi, kijamii, kidini, kivuvi na mengineyo. Nia huwa ni nyingi na hutegemea mahali pa matumizi. Mfano ufuatao toka Mtango wa kiswahili 74:2 (uk.74, ub.2). Unathibitisha kauli.

> Ninyi viumbe hasidi, uovu u vifuani
> Ni chafu zenu fuadi, hamna nuru nyayoni
> japo ua la mkadi, nikiwa nalo ni zani
> sasa sitawaamini, mna jicho la husuda.

Kutoka ubeti huu kunatokea tamathali za usemi zipatazo tatu hivi: Kwanza ni ile ya taswira ya vifua vichafu kwa ajili ya uovu uliokithiri. Pili ni Istiara ya nyoyo kuwa na nuru. Kuna sitiari pia, ambapo uzuri wa ua la mkadi walinganishwa na uzuri wa watu ambao hawaaminiki. Madhali tumeona umuhimu wao, lililobaki ni kuangalia aina mbalimbali za tamathali katika mafungu hayo tuliyoyaona. Ufuatao ni ufafanuzi zaidi wa tamathali hizo.

## TAMATHALI ZA VILINGE

Fungu hili lina vijembe, midokezo, kejeli, Dhihaka, Tasifida, Nasiha, Istiara, Ngano, Kharafa, Stihizai (Kinaya), Mafumbo na kadhalika. Ufuatao ni ufafanuzi wao.

### KIJEMBE (KILINGE)

Kuhenga, C,(1977:68), anatupa maelezo yafuatayo ambayo yanaridhisha sana. Anasema kuwa, kijembe ni, "Namna ya msemo wa fumbo au mzunguko, ambao kwao msemaji hutoa mdokezo juu ya jambo fulani kwa kijanja bila ya kutoboa waziwazi ukweli wa mambo. Mtindo huu wa uneni wa mzunguko, pengine waweza kuingilia tafakari ya mtu na kumfanya yeye binafsi kutoa hukumu juu ya jambo analodokezewa kwa maneno ya mafumbo".

Senkoro, (1982:20), naye anachangia kwa maelezo yafuatayo. Anasema, "Tamathali hii hushirikiana na pia hushabihiana sana na kejeli na dhihaka. Hapa yapo maneno yenye maana mbaya iliyofichika".

Msokile, (1993:84) anaielezea tamathali hii kama, "maneno ya kifumbo ya kumsema mtu, maneno ya mzunguko".

Hatima tunatathmini maoni yao. Kimsingi tunachokiona katika mbinu hii ni hali ya kumsema mtu kwa njia isiyo dhahiri na kumwachia mwenyewe nafasi kufasiri kulichokusudiwa. Matokeo yake aghalabu huwa ni kuchoma mtu kwa maneno ambaye ndani kwa ndani hughadhabika kwani hata iwe usemi umewekwa kwa mfuniko, hutoa sifa za mwelekeo wa kilichokusudiwa.

### KEJELI (KINAYA/STIHIZAI)

Kwa maelezo ya kuhenga,C (1977:71), Kejeli ni "Namna ya usemi wa mafumbo,ambao kwao msemaji kwa maneno yake ya kebehi au dharau ya kisirisiri, hutoa wasifu kwa matendo yasiyofaa, ilhali moyoni mwake anafidisha kinyume cha matamko yake, Yumkini ukejeli umwudhi mtu, bali si nia ya mtu atumiaye msemo wa kejeli kumwudhi yeyote. Nia ya lugha ya kejeli ni kumwonya mtu kwa siasa au kichinichini bila ya bughudha".

Msokile, M,(1993:83), anafuatilia na maelezo kuwa, "Hii ni tamathali ya usemi ambayo ina maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa ama kuongelewa. Ni tamathali inayoleta maana iliyo kinyume na ukweli wa mambo ulivyo".

Katika Mulika 16, imeelezwa kama, "Tamathali ya usemi ambayo inakusudia kuleta maana iliyo kinyume cha yale yaliyotamkwa".

Karl Beckson na Arthur Ganz(1960:106) wameielezea Kejeli kama, "Ala ambayo kwayo mwandishi huelezea maana kinyume na iliyotajwa au inayobainika".

Senkoro (1982:19) anasema, "Hii ni tamathali ambayo maneno yake huwa kinyume kabisa na maana yanayotakiwa kutoa. Kejeli huweza kuchanganya tamathali zinginezo kama vile za ubeuzi uliofichika, kinyume, tabaini na msisitizo bayani".

Sifa kuu ya tamathali hii ni kuwasilisha kwa kinyume ambapo linalokusudiwa silo linalotamkwa, na linalotamkwa silo linalokusudiwa.

## DHIHAKA

Imeelezwa na Senkoro,(1982:20), ifuatavyo: "Hii nayo ni aina ya Kejeli. Ni tamathali ambayo ina ubeuzi mkali, jahili unaopenya kweli. Hii pia hutumia mbinu ya kutoa maneno ambayo kijuujuu yanasikilika vizuri sana masikioni wakati ambapo huwa yamekusudiwa yatoe maana iliyo kinyume chayo kabisa".

Msokile, (1993:78), anaiona kama, "maelezo au masimulizi yaliyokusudiwa kubeuawa jambo kisirisiri. Ni maelezo yanayomdunisha mtu kisirisiri".

Casimiri Kuhenga, (1977:73), anasema, "Huu ni mtindo wa uneni ambao kwao mtu kwa makusudi mazima, husema maneno ya kumjukumu na kumdhihaki mwingine kisirisiri".

Nao Karl Beckson na Arthur Ganz, (1960:194), wanaielezea kama, "msemo wa mzaha wa uchungu au ukali, mara nyingi unaohusisha stihizai kama ala, ambapo kinachotajwa ni kinyume cha kile kilichokusudiwa".

Mawazo hayo yanaridhisha. Yanaangazia uwasilishi kisanii ambako kimzaha kunaumiza waliokusudiwa.

## MDOKEZO

Kwa maelezo ya kuhenga, (1977:69), "Huu ni mtindo wa uneni wa fumbo, ambao kwao msemaji hukatiza maneno yake na kumwacha msikilizaji au msomaji ahisi yeye (mwenyewe) binafsi mwisho wa maneno hayo yanafidisha nini. Mtindo huu wa uneni, ambao mara nyingi huonyesha mtanguo wa kauli juu ya jambo fulani, humpa msikilizaji uhuru na fursa ya uchaguzi wa kufanya tendo apendalo kadiri ya matamanio yake".

Senkoro, (1982:18), anasema, "Hiki ni kipengee cha kitamathali ambacho kwacho msomaji au mwandishi hukatiza maneno au huacha kitu fulani bila kukitaja; kitu au maneno ambayo kwa kawaida ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu".

Kwa maelezo ya Karl Beckson na mwenzake Arthur Ganz, (1960:18), mdokezo ni "ukatizwaji kwa wazo ghafula katikati ya sentensi, zaidi kwa sababu ya mkazo wa hemshi".

Katika ushairi, tamathali hii ghalibu hutokea katika mshororo mmoja kabla ya kibwagizo, ambapo msanii hulazimika kukatiza ghafula ule mtiririko au muwala kwa sababu ya zile kaida zinazomwongoza. Mara Nyingi, alama zile zinazotumiwa kama vile za dukuduku katika riwaya au tamthilia hazitumiwi katika ushairi. Inahitaji makini kwa msomaji kutambua kwamba kuna mdokezo au mkatizo wa wazo.

## TASIFIDA

Kwa maelezo ya Senkoro, (1982:18), Tamathali hii hujitokeza kwa utumizi wa neno, msemo, au nahau ambayo hupunguza ukali au matusi badala ya kutumia neno au nahau kali ama ya kimatusi.

Benedict Syambo na mwenzake Alamin Mazrui, (1992:XVI), wanatupa maelezo yafuatayo; "Watu wa kila jumuiya huwa na tabia ya kutaja mambo yanayofikiriwa hayafai kutajwa hadharani kwa kuyafunika kwa maneno tofauti. Au mtu anaweza kumtusi mwenziwe bila ya kutumia neno lolote la matusi katika matamshi yake".

Kuhenga, (1977:74), anasema, "Huu ni msemo wa adabu, ambao kwao mambo yasiyopendeza hutamkwa waziwazi hasa hadharani, hutajwa kwa lugha ya siri, bila kuchukiza au kuchafua moyo, ili kuficha kinyaa au hali mbaya waonayo watu moyoni au mioyoni".

Kunga hii hutumiwa ili kuleta usafidi au utakaso katika misemo ambayo ingechukiza kwa hadhira lau ingewasilishwa moja kwa moja. Mara nyingi hili hutokea pale watu wanapoheshimu mahusiano yao au pale heshima iliyopo baina yao haiwaruhusu kuongea baadhi ya mambo katika ulimi wa moja kwa moja. Kwa nia ya kuepuka misemo mikali, washairi na wasanii wengine hutumia mbinu ya kutakasa ujumbe wao kwa kuteua mtindo usiochukiza, kuchafua au kukosa adabu.

## NASIHA

Kwa maelezo yao Karl Beckson na Arthur Ganz, (1960:60), Nasiha ni, "msemo mfupi wa busara, mzuri kimtindo na wenye mawazo ya werevu".

Kuhenga, (1977:75), anaielezea tamathali hii kama, "Mtindo wa uneni ambao kwao mtu kwa makusudi mazima, husema maneno ya kumjukumu, na kumdhihaki mwingine kisirisiri".

Uchunguzi wetu kuhusu nasiha uligundua kuwa hizi ni aina ya methali. Huwakilisha fungu la baadhi ya methali na nahau. Upambanufu wao umeangaliwa katika tungo tulizozishughulikia.

## ISTIARA

Senkoro,(1982:20), anaielezea ifuatavyo; "Kwa kawaida tamathali hii huwa ni masimulizi yatumiayo ishara ambayo maana yake hujitokeza pia katika masimulizi mengine. Istiara basi, ni aina moja ya tamathali ya stiari ambayo imepanuka zaidi katika matumizi. Hekaya ni mfano mmojawapo wa istiara ila hii iko kwenye kiwango kidogo zaidi kwa vile huwa ni hadithi yenye maana ya kawaida ya kitamathali".

Msokile, (1993:82), anafuatilia kuwa huu ni; "mtindo katika kazi ya sanaa ambao kwao vitu husimamia dhana ama wazo maalum. Hadithi nyingi za kimapokeo ni za aina hii".

Patrick Murray, (1978:1), anasema kuwa, "Istiara aghalabu huelezwa kama sitiari iliyopanuka au tashbiha iliyopanuka, kwa sababu ni uwakilishi unaowasilisha maana mbali na iliyo zaidi ya maana ya kifasihi".

Karl Beckson na Arthur Ganz, (1960:12), wanaielezea kuwa, "Ni masimulizi yaliyopanuliwa yanayobeba maana ya pili pamoja na ile ya kijuujuu ya habari".

Benedict Syambo na Alamin Mazrui, (1992:XVii), wanasema, "Mara nyingine maudhui ya utungo mzima wa fasihi huelezwa kwa kutumia mfano wa kitu kingine. Mtungaji kwa mfano, anaweza kutueleza uzuri wa mwanamke kwa kutumia tufaha linaloning'ia mtini. Utungo wa aina hii huitwa utungo wa istiara".

Maelezo ya kuhenga, (1977:79), ni kuwa, Istiara ni; "Namna ya hadithi ya fumbo ambayo ndaniye kuna mawaidha au mwongozo fulani wa siri katika maisha".

Maelezo hayo ya wataalamu hao wote yanaingiliana katika juhudi za kuifafanua tamathali. Usemi wa istiara huwa wa kifumbo, na ni juu ya msomaji kujaribu kupata fasiri inayofaa kwa msingi wa mwelekeo uliowekwa na usemi.

## MAFUMBO

Mafumbo ni wingi wa fumbo. Katika kamusi ya kiswahili sanifu , fumbo ni "maneno yasiyojulisha maana waziwazi."

Naye Kithaka wa Mberia katika "Ushairi: kunga za utunzi: "anasema kuwa, " wakati mwingine washairi hutumia mafumbo katika mashairi yao. Wanaelezea jambo kwa kuzungumzia jambo jingine tofauti kabisa. Kwa mfano, mshairi anaweza kuelezea maovu ya wanyonyaji kwa kuzungumzia wadudu wanyonya damu kama vile mbung'o, chawa, kunguni, viroboto na mbu". (Maelezo hayo ya Kithaka yamo katika muswada wa kibinafsi ambao haujachapishwa).

Kuna mafumbo mazito, mepesi na ya wastani. Yale mepesi hutumia wahusika, mazingira na toni ambavyo havikanganyi. Katika yale ya kadiri, lugha, mandhari, wahusika na hata ploti hutumiwa kwa njia inayofasirika kwa uyakini fulani. Katika

yale mazito, ala za fani zilizotumiwa hutoa mielekeo mingi ya fasiri, kiasi kwamba huwa si rahisi kujua kakusudia nini msanii. Wasanii hutunga kwa makusudi tungo kama hizi. Wanaweza kutumia wahusika, mandhari, nyakati, ploti na hata lugha inayopotosha kwa makusudi, na lazima msomaji achukue makini kubwa sana ili kupata kilichokusudiwa. Mazingira haya huchochea kile ambacho wanaurasimu kama Wimsatt W. K. na Beardsley wanakiita, "Affective fallacy". Wanasema kuwa tungo zikiandikwa kwa uzuri, zitasomwa kwa mwelekeo ule waliodhamiria wasanii na kwa njia hiyo tungo zitaingia katika "Intentional fallacy". Fasiri nyingi zitaepukwa ikiwa wasanii wataunda mazingira yasiyo na mielekeo mingi au mawezekano mengi ya fasiri, hata kama wanarahana.

Katika fungu hili la semi za vilinge tuna pia ngano, Hekaya na Khurafa. Kwa maelezo ya Kuhenga, Istiara, Hekaya na khurafa ni aina za ngano. Madhali Hekaya na khurafa hazikutumiwa katika tungo tulizozihakiki hakuna haja ya kuzipitia.

## SEMI ZA ZINDUNA

Fungu hili lina ritifaa na njozi. Hata hivyo hatutaangalia maelezo ya ritifaa kwa sababu hayapo katika kazi tulizochunguza.

## NJOZI

Kwa maelezo ya kuhenga, (1977:29), njozi ni; "namna fulani ya msemo wa fasaha, ambao kwao msemaji hueleza tukio maalum (halfa) au mambo yaliyopita zamani au yatakayotukia wakati ujao, kama vile anahisi na kushuhudia binafsi papo hapo wakati anaposimulia. Uneni huu wa mwijio wa halfa, ni namna fulani ya mwotoo wa ndoto au utabiri wa mambo yajayo. Mtindo huu wa uneni wa tanabishi, hutumika sana katika hotuba, barua, na mashairi na nyaraka zingine za kumbukumbu. Visa na hadithi nyingi za kubuni hutungwa kufuatana na mkondo wa mawazo ya njozi".

Wakati hapa ni arki muhimu sana katika upambanukaji wa tamathali hii. Wakati uliopo humpa msanii wakati wa kuvuta na kudhukuru yaliyopita yakawa kama kwamba yanapita sasa. Wakati uliopo vile vile humwezesha kutabiri yatakayotokea kama kwamba anayaona yakitokea sasa. Kuna uthabiti mkubwa wa kindoto-wa kuona tukio.

## TAMATHALI ZA USEMI ZA MWIGO SAUTI

Hapa tuna Tanakali sauti na Tanakali lafudhi. Hata hivyo tumeangalia tu Tanakali sauti kwani imetokea katika tungo za Hassan Mwalimu Mbega.

## TANAKALI SAUTI

Kwa maelezo ya msokile, (1993:95), Tanakali sauti ni; "Mwigo wa sauti katika kazi za sanaa.

Senkoro, (1982:17), anasema, "Tanakali sauti ni maneno au nomino ziundwazo katika sentensi kutokana na sauti zinazofanana. Wakati mwingine mfanano huu huweza kutokana na kurudiwarudiwa kwa neno au maneno yafananayo".

Kwa maelezo ya kuhenga, (1977:83), "Ni namna fulani ya mbinu za ufasaha wa lugha, ambayo mwandishi au mhatibu huitumia kwa makusudi. Ni lugha ya mwigo asili wa vitendo vya viumbe ili kuingilia zaidi mahasa ya msomaji au msikilizaji, vivyo msemo upate kufahamika bora zaidi. Tanakali ya sauti ni jitihada ya kunakili sauti ya milio mbalimbali ya vitu ulimwenguni kwa njia ya maandishi".

Katika baadhi ya Tanakali sauti hutokea unakili ambao unarudia baadhi ya vipashio vya kitenzi. Kwa mfano, kitendo demka huwa na tanakali ya 'dem dem' au 'demka dem dem' katika ukamilifu wake. Baadhi ya tanakali hazionyeshi ukariri huo kama kwa mfano, lia kwinyo! kwinyo! au wika kokoikoo!.

Matumizi yao huipamba lugha mbali na kuleta uzito fulani katika mapigo pokezi ya zilikotumiwa. Tunahitimisha maelezo kuhusu tanakali sauti kwa maelezo yao Karl Beckson na Arthur Ganz, (1960:150), ambao wanasema; "Matumizi ya maneno yenye sauti zinazoelekea kuelezea au kudhabiti (reinforce) maana zao. Katika maana halisi onomatopoeia hutokea tu wakati mwandishi anapoiga sauti".

## SEMI LINGANISHI TABIA

Tamathali za usemi zinazolinganisha tabia huhusisha tashbiha, sitiari, lakabu, Taniaba, Tashihisi, Taashira, Majazi na kadhalika.

## TASHBIHA

Kwa maelezo ya Korg,(1959:8), "Tashbiha ni tamathali ya usemi inayotumia maneno kama, 'kama' na 'sawa na' kuonyesha kuwa ulinganishi unafanywa".

Karl Beckson na Arthur Ganz, (1960:203), wanaielezea tashbiha kuwa, " Ni ulinganishi ulioonyeshwa baina ya vitu viwili visivyofanana, kwa kutumia 'kama' au 'sawa na'".

Patrick Murray, (1978:88), anasema kuwa, "mara nyingi tashbiha huangaliwa kama sura ya sitiari. Kila mojawapo inahusu uhamishaji au kubebwa kwa hali ya kitu hadi kwa kingine. Katika kila mojawapo kulinganisha ni sifa muhimu, lakini katika tashbiha, ulinganishi u wazi, na katika sitiari ulinganishi hudokezwa (kwa sababu umefichika)".

Naye Aristotle katika kitabu chake cha Rhetoric alipendekeza kuwa tashbiha ni "sitiari yenye maelezo".

Syambo, B na Mazrui, A, (1992:Xiv), wanasema, "Tashbiha ni yale maneno yanayofananisha kitu au kitendo kimoja na kingine".

Senkoro, (1982:14), anasema, "katika tamathali hii watu ama vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu ama vitu vingine kwa kutumia maneno kama, mithili, kama kwamba, mfano wa, na mengine ya aina hiyo".

Kwa kuhenga, (1977:4), "Huu ni mtindo wa uneni wa kifani, ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au hufananishwa na kitu au vitu vingine tofauti vilivyo na ufanano au ushabihiano fulani fulani wa hali ya utendaji au maumbile, mathalani, sura, rangi, na jinsi ya kujimudu. Kwa kawaida tashbiha, huonyeshwa kwa kutumia maneno; kama, mfano wa, mithili ya, vile, ja, sawasawa, na maneno mengine yenye kuonyesha mlinganisho kati ya vitu mbalimbali".

Ni wengi waliochangia kuhusu tamathali hii na kimsingi maelezo yao yana ulinganifu fulani. Kwa ufupi ni kuwa, "Tashbiha ni tamathali inayolinganisha kitu au mtu na kingine/vingine, kwa nia ya kukipambanua zaidi kwa msingi wa sifa ya ushabihiano fulani baina yao, huku ikitumia maneno ya kulinganishia ya moja kwa moja".

## SITIARI

Kwa maelezo ya Joab Korg, (1959:9), "Tamathali inayoitwa sitiari hutofautiana na tashbiha tu kwa kuacha neno la kulinganishia. Katika matumizi mojawapo yake sitiari hulinganisha vitu viwili tofauti kwa sababu tu ya kusisitiza sifa moja tu vilivyo nayo".

Msokile, (1993:98), anaielezea sitiari kama, "Tamathali ya usemi inayolinganisha na kuhusisha vitu vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile. Ni tamathali ambayo athari yake hutegemea kuhamishwa kwa maana na hisi kutoka katika kitu kimoja na kwenda katika kitu kingine. Kwa kawaida vitu ama viumbe viwili viliyo tofauti kitabia ama kimaumbile vinahusishwa kwa msingi wa sifa fulani iliyopo katika vyote viwili ama zaidi bila ya kutaja dhahiri sifa yenyewe".

Senkoro, (1982:14), anafuatilia kwa maelezo kuwa ":Tamathali hii, sawa na tashbiha, hulinganisha vitu ama watu lakini bila kutumia viunganishi-linganishi vya mithili ya, mfano wa, sawa na, kama na vinginevyo. Kwa hiyo katika tamathali hii, vitu na watu hulinganishwa na vitu na watu wengine kama kwamba vitu na watu hao ni sawa kabisa".

Beckson, K na Ganz, A,(1960:127), wanasema kuwa "Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo kwayo vitu viwili visivyofanana hulinganishwa kwa utambuzi au kubadilisha kimoja kwa kingine".

Kwa maelezo ya Syambo, B na Mazrui, A,(1992:XV), "mbinu ya sitiara inafanana sana na ile ya tashbiha, kwani zote zinashabihisha sifa ya kitu kimoja na kingine. Tofauti iliyopo ni kwamba katika tashbiha yale mambo mawili yanayoshabihishwa hutokezwa waziwazi, moja linawekwa kando ya mwenziwe, pindi katika sitiari huunganishwa yakawa dhana moja".

Kuhenga, (1977:6), anaielezea kuwa ni, "Tamathali ya usemi ambayo kwayo, matendo au vitu vyenye hulka mbalimbali hulinganishwa na hali sawasawa ya maumbile au jinsi ya utendaji. Katika sitiari maneno ya mlinganisho; kwa mfano, kama vile, na mengineyo hayatumiki. Mlinganisho wa sitiari hufichwa ndani kwa ndani na kufichuliwa kwa hisi tu".

Waandishi wengine kama Murray, wamechangia na maoni yao yanaoana na yale tuliyoyaona tayari. Sifa kuu ya tamathali hii ni kuleta tangamano katika vitu vinavyolinganishwa ambavyo vinakuwa kitu kimoja kwa ajili ya ile sifa inayovileta pamoja. Ghalibu sifa za kitu cha kwanza huhama hadi cha pili. Kwa mfano, pale ujana unaposemwa kuwa ni moshi, sifa za ujana huhama, ambazo humezwa na moshi (au kitu cha pili).

Murray na Korg wameziainisha sitiari katika makundi mengi, kama vile sitiari hai, sitiari fifi, sitiari shehenezi, sitiari dokezwa na kadhalika.

## LAKABU

Kwa maelezo yao Beckson, K na Ganz,(1960:219), lakabu (synaesthesia) ni "Mwingiliano (mchanganyo) wa hisia (maono); kuhisi (kuona), kwa mfano, sauti fulani kupitia rangi au harufu".

Naye Kuhenga, (1977:9), anaielezea kuwa ni, "namna ya msemo wa hisi ambao kwao ubadilishano wa sifa au mhisilisho wa maumbile 1. Sifa au vipawa vya vitu vyenye uhai, na vitu vinavyojimudu kusimuliwa kama vile vilivyo na uhai (2) mahasa na sifa nyinginezo zenye kueleweka kama maono ya ndani tu husimuliwa kama vitu vyenye silika na hulka ya kuonekana".

Wataalamu hao wanatupa maelezo ya kunga ya "Synaesthesia/synesthesia" ambayo imeitwa "Hisia mseto" katika Mulika 16, na kufafanuliwa kuwa ni "matumizi ya msamiati wa hisi moja kwa nyingine, kwa mfano sauti yake ni tamu".

Ufafanuzi wa tapo la wataalamu wa pili ni ule uliotafsiri lakabu kama "Hypallage". Katika tapo hili ni Senkoro, (1982:16), ambaye anasema kuwa, "katika tamathali hii uhusiano wa kawaida wa maneno mawili kisarufi huwekwa kwa kinyume. Kwa mfano mti wa umeme uligonga uso wangu badala ya msemo wa kawaida kwamba, "Niliugonga uso wangu kwenye mti wa umeme". Katika maelezo ya kamusi sanifu ya kiswahili, (1981:142), lakabu ni, "Jina ambalo mtu hujipa au hupewa mbali na jina lake hasa, aghalabu huwa ni la kutania: jina la kupanga; msimbo".

Maelezo yetu ambayo yafungamana na ya TUKI ni kwamba, "lakabu ni sifa au mbinu ambayo kwayo wasanii, na zaidi washairi hujipachika majina ya kisanii kama vile 'ustadh sitara' 'ustadh shuara'na "ustadh mti-mle,' kwa msingi wa sifa zao kimaumbile, kitunzi au kieneo." Kwa mfano ikiwa mshairi atoka bara aweza akajibandika jina la 'malenga wa bara'. Tuna lakabu za malenga wa mvita, mrima, vumba, ziwa kuu na kadhalika.

Hizo ni sifa za kieneo au za mahali wanapotoka watunzi. Tabia hii ya washairi kujipa lakabu ilianza katika karne hii - kutoka miaka sitini hivi iliyopita. Mbali na kuwatambulisha hufaa katika kutimiza kanuni za vina na mizani, ikitegemea mahali ambapo imetumiwa.

## TASHIHISI

Beckson, K na Ganz, A,(1960:162), wanasema kuwa hii ni, "Tamathali ya usemi ambayo kwayo vitu visivyo hai au mawazo dhahania hupatiwa sifa za kibinadamu au matendo".

Syambo, B na Mazrui, A,(1992:XV), wanasema kuwa, "Hii ni mbinu ya lugha ya fasihi inayokipa kitu kisichokuwa na uhai tabia au sifa ya kitu chenye uhai".

Senkoro, (1982:14), asema, "Wakati mwingine tamathali hii huitwa fasili ya binadamu. Kwa tamathali hii, vitu visivyo na sifa walizo nazo watu hupewa sifa hizo".

Kuhenga, (1977:15), anasema, "Katika taaluma ya fasihi ya lugha, tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo kwayo 1. mahasa au maono ya ndani ya binadamu, kama vile dhamiri, choyo, woga, chuki kiburi, njaa, furaha, kifo, mapenzi na fadhila au kasoro zingine za binadamu hutaswirishwa na kupewa fasaha za binadamu au sifa nyinginezo za utu, ili ziweze kueleweka vizuri zaidi. 2. Vitu visivyo na uhai, kama vile udongo, nchi, jua, moto, milima n.k. huvishwa taswira ya utu na husimuliwa kama vile vina uhai na maumbile ya wanyama au binadamu, 3. Vitu vyenye uhai, kama vile miti, wadudu, ndege, na wanyama, hupewa hulka ya binadamu vikavishwa vipawa vya kuigiza mahasa na mwenendo wa binadamu".

Maelezo hayo yaeleweka na hakuna haja ya ufafanuzi zaidi.

## TAASHIRA

Senkoro, (1982:15), anasema kuwa, "Katika tamathali hii jina la sehemu ya kitu kimoja, au la kitu kidogo kinachohusiana na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili".

Beckson, K na Ganz, A,(1960:129), wanaielezea kama, "Tamathali ya usemi ambayo kwayo jina la kitu fulani au wazo hubadilishwa kwa kingine ambacho kwacho kuna uhusiano, kama sababu ya athari yake n.k.".

Syambo, B na Mazrui, A,(1992:XVI), wanasema, "katika tashbiha na sitiara sababu ya kitu kimoja kushabihishwa na kingine huwa iko wazi kabisa. Taashira basi ni ile sanaa ya kubaini maana au hisia si kwa maelezo au mishabaha ya wazi wazi, bali kwa mdokezo unaoletwa na matumizi ya ishara zilizoelezwa. Na msomaji hapa huwa ana uhuru wa kuzifasiri ishara hizi kama vile anavyoziona yeye".

Kuhenga, (1977:18), anaiona taashira kama, "Namna ya fani ya usemi, ambao kwao, kwa sababu ya mwambatano wa ujamii au uhusiano mkubwa uliopo kati ya vitu fulani, ishara, alama, dalili, au neno fulani hutumika kuwakilisha tendo au kitu tupendacho kutaja, badala ya kuelezea waziwazi".

Maelezo hayo yafuatilika kwa urahisi na hakuna haja ya ufafanuzi zaidi.

## TAMATHALI ZA USEMI ZA MSISITIZO

### TAKRIRI

Msokile, M,(1993:38), anasema, "Takriri ni marudiorudio ya neno, sauti, herufi au wazo na kadhalika katika kazi ya sanaa ya kifasihi".

Senkoro, (1982:16), atwambia kuwa, "Katika tamathali hii yanakuwepo marudio kwenye sentensi au kwenye usemi ambayo nia yake ni kusisitiza ijapokuwa kwa kawaida hayahitajiki sana".

Kuhenga, (1977:35), anaielezea takriri kama, "mtindo wa uneni wa fasaha, ambao kwao msemaji kwa makusudi au nia mahsusi hurudia neno, au maneno yale yale ili kutilia mkazo au msisitizo zaidi juu ya jambo asemalo. Mtindo huu wa msemo wa msisitizo, huwa na nia ya kutia nanga jambo fulani ili liweze kumwingia msikizaji moyoni apate kulidhibiti vizuri.

Tuna takriri irabu, konsonanti, vina, mshororo na muundo. Kahigi na mulokozi pamoja na msokile wamezielezea aina hizo kwa undani, nasi tumefuata hayo katika kutuongoza kuona umuhimu wao katika somo tulolitafiti.

### TANAKUZI

Kuhenga, (1977:39), anaielezea akisema, "Huu ni mtindo wa uneni wa fasaha, ambao kwao, maono au mawazo mbalimbali yenye mgongano na uhitilafiano, huunganishwa pamoja katika sentensi au kifungu cha maneno ili kufanya mvutano mkubwa zaidi wa mawazo. Kiini kikubwa cha mtindo huu wa uneni wa fasaha ni kuonyesha kifudifudi au uhitilafiano kati ya mambo mawili yenye kupingana, ili kupata jawabu lenye mtanguo maalum, juu ya jambo fulani".

Kwa maelezo ya msokile, (1993:100), tanakuzi ni, "usemi/uneni unaoonyesha kupingana kwa mawazo". Mbinu hii inakaribiana na tabaini, isipokuwa katika tabaini neno 'si' hutumiwa sana kuonyesha ukinzano.

### TABAINI

Kwa maelezo ya kuhenga, (1977:41), tabaini, "Ni mtindo wa uneni wa fasaha, ambao kwao msemaji husisitiza kauli au ukweli wa jambo fulani kwa kutumia maneno yenye ukinzani, aghalabu neno si".

Naye Senkoro,(1982:16), anasema kuwa, "Hii ni tamathali ya usemi ambayo kwayo maneno au mawazo yanayokinzana sana hutumiwa katika sentensi ili kuleta msisitizo wa wazo ama mawazo yatolewayo".

## NIDAA

Kuhenga, (1977:44), ameielezea kwa ukamilifu kuwa ni, "Namna ya msemo wa msisimuo au sauti ya mshangao atoayo mtu kudhihirisha maono yake ya ndani au kilio cha moyo wakati apatwapo na mgutusho ghafula wa furaha, huzuni, hasira, chuki au mshtuko wowote wa moyo. Nidaa ambacho ni kilio maalum cha moyo, huitwa pia siyahi".

## BALAGHA

Senkoro, (1982:17), anasema kuwa, "Hii ni tamathali ya usemi ambayo kwayo swali linaulizwa huku jibu lake linafahamika waziwazi. Kwa hiyo swali hili huweza kuwa kwa ajili ya msisitizo tu au, wakati mwingine mshangao".

Beckson, K na Ganz, A,(1960:184), wanasema,balagha nig "Swali linaloulizwa, siyo kudhihirisha habari, bali kufikia athari fulani kimtindo. Aghalabu mwandishi au msemaji huongeza msisitizo kwa kiwango cha kuuliza swali".

Kwa maelezo ya kuhenga (1977:48),balagha ni, "Namna ya msemo wa tashtiti, ambao kwao mwandishi au mhatibu kwa mathubuti maalum ya kuingilia mahasa ya ndani au kuchipua maoni ya wasikilizaji, hutia hoja za kusisimua au kuuliza maswali ya kuchoma moyo, ambayo huchochea furaha, huzuni, chuki, au mzinduko wowote wa utendaji, ili kushawishi mtu atende jambo fulani zuri au baya.

Kwa kawaida, mtindo huu wa uneni hutumiwa sana na wanasiasa, mahatibu, na watu wengineo stadi katika usemi wa fasaha, ili mradi kila msemaji huwa na kusudi, la kutimiza nia yake ya kuchochea watu watende jambo kadiri ya matamanio ya wakati ule maadam mtindo huu wa uneni humshawishi mtu kutenda jambo fulani, huweza kuitwa pia msemo wa tashtiti". Inavyoelekea hapa ni kuwa maswali ya balagha ni sawa na tashtiti. Lakini hivyo sivyo ilivyo. Maelezo yafuatayo yanatupambanulia tamathali hizo.

## TASHTITI

Katika Mulika 16. tashtiti ni aina ya fasihi inayomfanya mtu, jambo, jamii au kitu kuwa kidogo kwa kutumia dhihaka au bezo.

Ilivyo ni kwamba kuna tofauti baina ya tashtiti na balagha ingawa Msokile na kuhenga wanaziona kama kitu kimoja.

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

## CHUKU

Kwa maelezo ya Senkoro, (1982:18), "Tamathali hii hutia chumvi kuhusu uwezo wa viumbe, tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha au kusisitiza".

Msokile, (1993:77), anasema chuku ni kutia chumvi sana.

Kuhenga, (1977:60), asema kuwa, "Huu ni mtindo wa uneni wa ziada, ambao kwao msemaji, kwa nia mahsusi hutia chumvi maneno yake 1. akisimulia jambo la kawaida kama vile ni jambo la kustaajabisha 2. jambo dogo hudunishwa kupita kiasi 3. Jambo kubwa hukuzwa kupita kiasi".

Beckson, K na Ganz, A, (1960:88), wanasema kuwa hii ni, "Tamathali ya usemi ambayo kwayo msisitizo hupatikana kwa kuongeza sifa au kutia chumvi kwa makusudi".

## SEMI TUMBUIZI

## MJALIZO

Senkoro, (1982:19), anaielezea ifuatavyo; "katika tamathali hii sentensi huwa ni mfuatano tu wa maneno yasiyo na viungo vyovyote". Maelezo haya yanapatana na yale ya koja aliyoyatoa kuhenga (1977:55) ambapo asema kuwa, koja ni, "Namna ya msemo wa fasaha ambao kwao, mwandishi au mhatibu hufupisha mazungumzo kwa kutumia vabu (kiarifa) mbalimbali tofauti katika kifungu kimoja, badala ya kurudiarudia maneno au matendo mbalimbali. Kuna aina mbili za koja. Mwandishi au mhatibu atumiapo vabu moja kwa obijeto (kiima) mbalimbali badala ya sentensi fupifupi nyingi zenye kutengana. Mtindo huu huitwa msemo wa useja; 2. Mwandishi au mhatibu aunganishapo pamoja vabu kadhaa tofauti katika sentensi moja ndefu au kifungu kimoja cha maneno kwa mkato tu badala ya sentensi nyingi mbalimbali zenye kujitegemea binafsi. Mtindo huu huitwa kijalizo". Maelezo haya ya mfano wa pili ya koja ndiyo yaoana na yale ya Senkoro ya mjalizo.

## MATOKEO YA TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi zikitumiwa kwa uzuri huiimarisha lugha ya kawaida. Ufanisi wa tamathali hutegemea nguvu zao za kuweza kumchagiza kitashtiti au kibalagha msomaji. Pia hutegemea aina za picha zinazopatikana kutokana na matumizi yao mazuri. Baadhi wanaiona taswira/jazanda kama tamathali ya usemi, lakini sisi tunaiangalia kama zao la tamathali za usemi.

## TASWIRA (Jazanda)

Kwa maelezo ya Senkoro,(1982:36), "Taswira ni maneno yanayotumiwa na washairi, ambayo yanaweza kuchora picha kamili ya kitu, hali, wazo, dhana, au uzoefu fulani wa jamii au sehemu ya jamii katika mawazo ya wanaopokea shairi

linalohusika. Matumizi ya picha mara nyingi huambatana na yale ya ishara. Ishara ni dhana au mawazo mbalimbali yanayotumiwa na washairi na wanafasihi mbalimbali katika kazi zao za fasihi kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine".

Jazanda kwa maelezo ya Msokile, (1993:83), ni, "Lugha ya kipicha, lugha ya kitaswira (imagery). Ni lugha ambayo huchora picha ya mahali kwa kutumia tamathali za usemi".

Katika Mulika 16, taswira ni "lugha inayochora picha ya mahali au vitu kwa kutumia tamathali za usemi".

Nao Beckson, K na Ganz, A,(1960:92), wanasema, "Kwa kawaida, istilahi taswira hurejelea matumizi ya lugha kuwakilisha kimaelezo vitu, matendo au hata mawazo dhahania".

Mwisho ni maelezo yao Syambo, B na Mazrui A,(1992:38), ambao wanasema, "Taswira au Jazanda ni ule ubingwa wa lugha, wa mtunzi wa kusimulia au kuchora picha ya kitu kikaonekana dhahiri kabisa; yaani usimulizi wenye kunasa nadhari na hisia za msomaji mpaka kile anachokisoma kikawa kama anayekishuhudia wakati ule. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba taswira ni picha inayochorwa kwa maneno".

Syambo na mwenzake wanasema ni picha inayochorwa na maneno. Katika kutoa maelezo hayo wameepuka lile swala la: Ni lugha ipi yenye uwezo wa kuibua picha? Ni ya kawaida au ya kitamathali? Kwa baadhi ya wataalamu na wale wananadharia ya urasimu, lugha ya kawaida ni hafifu na haiwezi kutuchorea picha kiasi cha kuamsha hisi zetu mpaka kuwezeshwa kuona, kunusa, kugusa au hata kuhisi kile kinachoelezwa. Kwa maoni yetu, "Taswira au jazanda ni picha zinazojengwa kwa maneno ya kisanii ya kinasibishi na kitamathali ambayo yametumiwa kwa ustadi hadi kufikia kiasi cha kuibua hisia zinazomwezesha msomaji kupata fahamu zake zote kuhusu kinachoelezwa". Yote mawili yanatokana na kiarabu. Taswira latokana na neno la kiarabu "Tasur" lenye maana ya picha za michoro huku jazanda likimaanisha picha zinazojengeka fahamuni mwa wasomaji. Hata hivyo wengi huyatumia kama visawe, nasi tumefanya hivyo.

## HITIMISHO

Kuna baadhi ya mbinu za matumizi ya lugha kama Tadmini, Taharuki, Mjadala nafsia, mbinu rejeshi, litifati na zingine ambazo hazingii katika fungu la tamathali za usemi kwa njia wazi. Tadmini si tamathali ya usemi, bali ni mbinu katika matumizi ya lugha ambapo msanii hutumia mchanganyo wa lugha mbili tofauti au zaidi katika kuwasilisha mawazo yake. Maelezo yake ni sawa na ya 'kuchanganya ndimi". Litifati ni mbinu ambayo inaingia katika sehemu ya mtindo, ambapo wasanii hutoa nafasi kwa mtu au vitu vinavyozungumziwa au elezwa kuzungumza vyenyewe. Mbinu rejeshi huingia katika ploti, ambapo tukio lilioelezwa na kuachiwa njiani hurejelewa. Taharuki pia ni mbinu ya kimtindo ambayo ina muundo unaoeleza matukio, ukayaachia njiani na kuyarudia baadaye katika kuyakamilisha.

Ni muhimu mipaka ya tamathali kutambuliwa ili wahakiki wasije wakapotea kwa kutojua mahali mipaka ilipo.

## 2:2:5 MATUMIZI YA LUGHA KIUJUMLA

Hii ni sehemu inayoangalia vipashio mbalimbali vya lugha na namna vilivyotumiwa. Hivyo ndivyo vinavyotupa picha kamili ya lugha iliyotumiwa. Ufanisi wa lugha huangaliwa kwa kutizama aina ya picha zinazojengwa na matokeo kihisia ya matumizi ya lugha.

## 2:3 WAHUSIKA

Wahusika ni watu, vitu au wanyama wanaotumiwa na mtunzi katika utendaji na upitishaji ujumbe. Huwa muhimu sana kwani ndio wasemi na wapitishaji ujumbe wa mwandishi. Hutumiwa kama vinywa vya msanii na hivyo kila mmoja lazima apitishe ujumbe maalum kama alivyokusudia mtunzi.

Kila mhusika hata asawiriwe kidufu vipi ana umuhimu mkubwa sana katika kazi ya sanaa - ushairi ukiwemo. Hakuna mhusika ambaye hupachikwa tu kazini hata iwe kwa kutajwa tu au hata achorwe kama kivuli tu. Kama hakuhusishwa na kazi kukamilisha picha ya mandhari, kuthibitisha kauli au ujumbe, basi kuna makusudio maalum ya msanii anayotekeleza.

Kila mhusika huingizwa kazini kwa makusudi ili kutimiza malengo maalum ya msanii kwani bila hivyo huenda baadhi yao wakaonekana kama waliozuka kifutuhi, kikebehi au hata kiajali, jambo ambalo lapaswa lisiwepo na kuepukwa sana hata iwe nia tu ni kusukuma mbele kazi. Hawatokei tu katika tungo kama za tenzi, ngonjera na malumbano, bali katika ushairi wote kwa ujumla. Huwepo katika kazi yoyote bila kuzingatia umbo lake, na hasa ushairi wa aina yoyote.

Kila mmojawapo hudhihirika kama mwakilishi wa wahusika wengine wenye tabia, mienendo, mawazo na hulka kama zake. Nia ni katika kuonyesha upotofu au uelelezo wa wahusika hao. Kuna wahusika ambao hushirikishwa katika kazi kwa kutajwa tu, huku wenyewe wakikosa nafasi za kuchukua majukumu yao moja kwa moja. Hili hutokea bila wao kupatiwa nafasi za kujisemea au hata kujibu waliyoulizwa na hili hutokea pale msanii anapowauliza wahusika hao maswali wakiwa hawamo hata duniani. Kauli hii inathibitika kwa kutazama mfano ufuatao kutoka <u>Mtango wa Kiswahili</u> (19:76) kutoka shairi "Nawe mpenzi.

ubeti 4 Hali yangu ni thakili, mwili wajaa pujuko
usiku mie silali, mawazo yote yakwako
Fanya hal-kul-hali, uniridhie mwenzako
moyo sina pumziko, mapenzi yamenivaa

Kutoka mfano huo hatupati jawabu la mlengwa.

Baadhi ya wahusika hushirikishwa kwa kupatiwa nafasi ya kutenda, kusema, kujiwasilisha na kujitambulisha kwa hadhira. Kuchorwa kwao hudhihirika kupitia njia aliyoipendelea msanii.

Ikitokea kuwa mwandishi ndiye msimulizi kama inavyotokea katika kazi nyingi, basi humtaja tu mhusika kwa nia ya kumfanya kielelezo cha wema au uzuri kwa hadhira au kama njia mojawapo ya kuthibitisha hoja kuhusu uovu wa jamii na kuonyesha kuwa licha ya uozo wake bado ipo mifano mizuri ya kuigwa.

Wahusika wengine ni wale vivuli - ambao huchukua nafasi za wahusika halisi pale watunzi kwa nia mbalimbali huamua kuwafumba wasomaji wao kwa kuchukua wahusika kama, wanyama, ndege, wadudu, na vitu visivyo hai badala ya watu. Kazi yoyote ya kisanii hulengwa kuwafaidi watu na hivyo matumizi ya wahusika wasio watu hayakusudiwi kufaidi vitu hivyo ila watu. Ili hutokea kwa sababu kadha, kama mazingira kutoruhusu au pale msanii anapohiari kufumba kama mtindo wake. Mara nyingi mazingira maovu ya wanasiasa na wanajamii hulazimu hali hii, ambayo huchukuliwa tu kama aina fulani ya hadithi ya kutumbuiza na kupumbaza tu wala siyo ya kuchochea na kuzindua watu.

Isitoshe, kazi hizo hupata uzito kwa kupitisha ujumbe usiokuwa wa kidhahania, bali halisi - unaohusu mambo yanayoshuhudiwa na jamii kila siku. Japo sifa za kimaumbo za wahusika zitatengana sana, sifa moja ambayo huwaleta pamoja ni uamili wao na ile ya umiliki wa lugha na uwezo wa kuwasiliana - na lugha ni zao la jamii. Kupitia kwa sifa tunaelekezwa kwenye uhai wa kazi hizo na umuhimu wa adinasi kama wahusika. Katika kazi awali, sifa, tabia, matendo na yote ambayo ni ya wanadamu huchukuliwa na hao ambao ni wahusika wasio watu. Wahusika hao hucheka, hulala, hubusu, hulia, hupenda, huchukia, huiba na kuchukua jumla ya matendo yote kama wafanyavyo watu.

Wahusika wakiumbwa vizuri huikuza kazi ya sanaa na wakiumbwa vibaya basi huiumbua hiyo kazi. Sifa zao kadha huzingatiwa pale kazi zinapotathminiwa na uamuzi kutolewa kuhusu upungufu wao au utoshelezevu wao. Katika kazi yoyote ya kifasihi, wakati wa kuihakiki itafaa kuangalia namna wahusika walivyochorwa, namna wanavyodhihirika, namna wanavyotekeleza majukumu yao na sababu za kuwepo kwao.

Katika diwani zenye mikusanyo mingi ya mashairi, huwa ni vigumu sana kupata aina za wahusika zilizozoeleka katika kazi za fasihi na hasa tamthilia na riwaya, ambao huainishwa kuwa nguli, bapa, foili, mviringo na kadhalika. Hili ni kwa sababu beti huwa chache na nyekevu - sifa mojawapo ya ushairi katika matumizi yake ya maneno.

Nyakati zingine washairi wenyewe hushiriki kama wahusika huku wakiuliza wasomaji maswali ya kawaida na ya balagha, wakiwalenga watu maalum ambao wanakusudiwa kuwakilisha jamii au wengine wenye maumbile, sifa na tabia kama zao. Kushiriki kwa wasanii wenyewe huyatilia nguvu mawazo na pale hadhira inapoulizwa maswali, tangamano hutokea la moja kwa moja baina ya mwandishi na msomaji. Ushirika huu ni muhimu kwani humleta msomaji karibu sana na kazi, na hivyo basi kumwezesha msanii kufikia hata hisia za ndani na tafakari za msomaji.

Kwa sababu ya umuhimu wao katika kazi, kuna haja kubwa ya kuwatumia kwa makini. Matumizi mazuri ya wahusika ndiyo tuliyokusudia kuyachunguza katika tungo za Hassan Mwalimu Mbega.

## 2:4 MTINDO

Mtindo umewahi kutolewa maelezo na wanasanaa wengi na wataalamu. Lakini kufikia sasa bado upo mtafaruku wa sifa zake jenzi zinazopaswa kuwepo katika kila kijelezi. Kwa sababu hii, tumewanukuu tu baadhi na kisha kutoa maelezo yetu. Baadhi wanaamini kuwa lugha, wahusika, muundo, mandhari, toni, wakati na ploti vyapaswa kuzingatiwa katika ufafanuzi wa mtindo. Kile ambacho waelekea kukubaliana kwacho ni kuwa mtindo ni kipengele cha fani huku baadhi wakiuona mtindo sawa na fani. Hatukuingilia utata uliopo katika swala hili, ila tu tumewanukuu baadhi ya wanafasihi na kisha kuelezea mtindo kama tunavyoulewa na tulivyouhakiki.

Beckson, K na Ganz, A, wanaulezea mtindo kwa maana mbili. Kwanza wanasema kuwa, mtindo ni sifa au hali isiyobadilika katika baadhi ya waandishi na ambayo inakosekana katika baadhi ya waandishi. Pili wanauelezea mtindo kiuanishi zaidi kuliko kifafanuzi. Wanasema kuwa, kwa mfano, tunaposema mtindo wa kitashtiti, tunakusudia kuainisha mtindo wa mwandishi na wa wengine. Wanaendelea kusema kuwa; "Mhakiki anaweza kosa vutiwa na mtindo fulani au anawezaona kuwa matumizi yake katika mazingira fulani hayafai, lakini kuutambua tu katika mwandishi hufaa katika kuainisha, lakini siyo kumlaumu (kumhukumu) mwandishi. Tathmini ya mtindo wa mwandishi inapoangaliwa kwa undani zaidi huishia kwa mtu mwenyewe. Jumla ya sifa zinazohusishwa na mtindo wa mwandishi hujenga sifa zake za kifasihi na humulikia zile za ushunuzi wake. Mtindo, anasema Buffon, ni mtu".

Msokile, M,(1993), anauelezea kama, "Jinsi au namna ya kufanya kitu kwa kuzingatia misingi fulani. Katika kazi za sanaa, ni jinsi kitu kinavyoelezwa. Kitu kilichoelezwa".

Maelezo ya wataalamu hao wote yanafaa. Hata hivyo tumevutiwa zaidi na ya awali. Kwa maelezo yetu ni kuwa, mtindo ni mbinu ambazo kwazo msanii huwasilisha mawazo yake, ambazo zina upekee fulani wa kumtambulisha. Enkvist anatupa maelezo yafuatayo kuhusu mtindo na ambayo pia kwa kiasi fulani yanatoa mwongozo wa aina fulani. Anasema, "Mtindo ni uwasilishaji ujumbe, unaotokea ghalibu - kuusambaza na kuupitisha katika uyumkinifu wa sifa zake za kiisimu, hasa jinsi zinavyotofautiana na zile za aina hiyo katika lugha nzima. Huku isimu ikishughulikia maelezo ya msimbo, umitindo hushughulikia tofauti katika ujumbe zinazotokea kwa mujibu wa sheria za huo msimbo. Uchanganuzi wa mtindo zaidi unahusisha utambuzi na upimaji wa viwango mbalimbali ambavyo kwavyo ujumbe hutofautiana".

Naye Medvedev, (1978), ametuongoza katika kutupa baadhi ya mambo ya kuzingatiwa katika kutambua mtindo wa mwandishi ambayo ni pamoja na msamiati, mishororo, vina, mpangilio wa msamiati, mizani, beti, namna za kuuliza maswali, maumbo ya beti, matumizi ya wahusika, matumizi ya lugha kwa jumla, mandhari, matumizi ya tamathali za usemi na mengineyo.

Mtindo ni muhimu sana katika kuwaongoza wahakiki kutathmini na kuainisha watunzi na kazi zao kwa misingi ya sifa hizo tulizotaja. Kuna shakhsia au ubinafsi fulani unaotokea katika kazi za sanaa ambao huwafanya watu wazichukie ama wazipende. Kwa mwongozo wa elementi hizo tulizozitaja tumewezeshwa kutambua aina mbalimbali za mashairi.

Aina za mashairi kama Tathnia, Tathilitha, Tarbia, Takhmisa, Tasdisa, Asharia na zingine hudhihirika kama mitindo mbalimbali ya mashairi ambayo hupatikana kupitia kigezo cha mishororo. Baadhi ya mashairi ambayo yana vibwagizo vilivyofupishwa hutuwezesha kuyajua kuwa ni 'misuko' kwa sababu ya muundo wao.

Kupitia kigezo cha vina tunawezeshwa kupata aina mbalimbali za mashairi, kama kasida, Tumbuizo, Ukawafi, Mathnawi, Gungu na Tenzi. Kasida huwa na kina kimoja tu sawa na Tenzi, isipokuwa tofauti baina yao hubainika kwa sababu za maudhui na mizani. Kasida huwa na mizani mingi zaidi katika mishororo yake kuliko Tenzi, ingawa wakati mwingine, idadi ya mizani yawezalingana. Tenzi huwa ndefu na zawezalengwa kufafanua tukio moja tu. Kasida zilizowahi kutokea katika kiswahili si ndefu sana. Hata hivyo kuna haja ya uchunguzi wa kina katika kutafuta sifa bainishi za aina hizi mbili za tungo. Gungu pia huwa na kina kimoja, cha ukwapi tu, lakini mishororo yake huwa mirefu, ya mizani 15. Mathnawi huwa ni ule mgao wa mashairi katika vipande viwili vya vina; ambavyo ni vya ukwapi na utao. Mashairi ambayo yana vipande vitatu, yaani ukwapi, utao na mwandamizi huwa ni ya ukawafi na tumbuizo. Ukawafi huwa na idadi tofauti tofauti katika vina vyake na mizani, huku Tumbuizo ikiwa na mizani 8x8x8. Mkondo wa mizani hufaa katika kutofautisha aina hizo mbili za nyuma za ushairi.

Mifano hiyo ya tungo haitambulishwi tu na aina ya vina, bali pia idadi ya mizani. Kigezo cha mizani ni muhimu sana katika kutupa aina ya bahari tunazopata kwa kuangalia mikondo yao. Mathalani, Gungu huwa na kina cha ukwapi tu na mizani yake ni 15. Ukawafi huwa na mizani chini ya 24. Tumbuizo huwa na mizani 24, katika mkondo wa 8x8x8. Kikai hutambulikana kwa kuwa na mikondo ya mizani isiyotimia 16, ambayo ni kama 8x6, 3x8, 8x4, 5x8 na mingine mingi. Bahari za ukara, ukaraguni na mtiririko ni zingine zinazotambuliwa kwa mwongozo wa vina. Katika ukara kuna vina vya aina moja vya utao katika shairi zima huku ukwapi ukikosa vina vya keketo. Katika ukaraguni kila ubeti una vina vya keketo katika ubeti mmoja huku zingine zikiwa na vina tofauti. Kila ubeti huwa na vina vya aina yake. Katika mtiririko kuna keketo katika utao na ukwapi kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Hili hutokea toka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Ikiwa umbo la ubeti mmoja ni kama hili, basi hukaririwa katika shairi lote.

le za
le za
le za
le za

Matumizi ya msamiati hutuwezesha kupata aina za mashairi kama kikwamba, pindu[10] na, Tauria. Katika kikwamba neno hurudiwarudiwa katika kuanzisha mishororo au beti. Ufuatao ni mfano kutoka Mtango wa Kiswahili (uk. 64:2)

Teso lipi nimekosa, hata niume unyasi
Teso lipi waniasa, uniondoke mkosi
Teso kwangu umetosa, kama upepo wa kusi
Teso hunipi nafasi, teso mbona wanitesa.

Kwawezarudiwa hata fungu la maneno matatu, kama inavyodhihirika kutoka diwani hiyo, U.K.85 na 86:5, katika shairi 'mwende mrudi salama'

Mwende salama mrudi, nakama kuwapungukia
Mwende salama mrudi, tuwapambe kwa maua
Mwende salama mrudi, na nema za kutumia
Mwende salama jamia, ndugu mwendao kuhiji.

Kuna pia umbo lingine linalokaribiana hilo ambalo lina matumizi ya kitakriri ya neno, la umbo moja au vitamkwa vya aina moja, lakini vinavyowasilisha maana mbalimbali. Aina ya tungo inayotumia msamiati kwa njia hii hujulikana kama Tauria (word play). Hapa neno hukaririwa kwa namna fulani ya kimchezo japo laendeleza ujumbe. Katika Mtango wa kiswahili. Uk. 68:1, tuna mfano huu katika shairi 'kisi'

Kisi kisi kisikule, Kisi hakikisi kisi
Kisi sikia si kile, Kikanitusha na isi
Kisi lesso kifungile, chendapo kisi kihisi
Kisi hakikisi kisi, kisi leso kisikule

Bahari ya pindu inabainika kwa sababu ya matumizi ya maneno au fungu la maneno ya mshororo wa mwisho ya ubeti awali katika kuanzishia ubeti mpya. Bahari hii huhusu mshororo wa mwisho wa ubeti, na wa kwanza wa ubeti mpya. Ufuatao ni mfano katika Upisho wa umalenga UK. 1; 2 & 3

Maji yalo kisimani, watu wanapoyateka
Aula pale bombani, kufunga na kufunguka
Maji huwa hayaneni, hayana la kutamka
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

Nambie yasema nini, maji yanapochemka?
Pale yawapo chunguni, unapo kuyateleka
Maji, chungu, kijikoni, na huku moto wawaka
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

Mpangilio wa wahusika kidrama hutuwezesha kupata aina za ushairi za ngonjera na malumbano. Mtindo wa uzungumzi baina wahusika wawili au zaidi, wakijadiliana kuhusu mada fulani hutokea pale nia inapokuwa ni kuyaendeleza katika

jukwaa, kwa wale watakaopendelea hivyo. Kwa sifa za kifani hatutaweza kutoa mwangaza kuhusu tofauti za tungo hizo. Maudhui na fani kwa pamoja hufaa katika kupambanua malumbano na ngonjera. Katika ngonjera aina ya mawazo yanayopitishwa huwa si mazito na hushirikisha yeyote. Si lazima wote wawe wajuzi. Mara nyingi hutokea mpangilio wa mhusika arifu na asiyelewa kitu, ambaye humwuliza mjuzi maswali kadha asiyoyaelewa ili amfafanulie. Lakini katika malumbano mawazo mazito hushughulikiwa kwa njia nzito na wajuzi.

Mtindo wa mpokezano wa wazo na jibu toka ukwapi kwa utao, nao hutuongoza kwenye bahari ya mandhuma. Ufuatao ni mfano toka diwani Malenga wa mrima, Uk. 42: ubeti 1&2.

Mmbeya sidhani, ni mtu wa kando
Unaye nyayoni, kwa domo na mwendo
Au la nyumbani, kwa vyote vitendo
Haumi wa kando, chawa yu nguoni

Yu hapo mbavuni, na yake magando
Muwapo njiani, haonyeshi fundo
Akiwa penuni, hupiga vimondo
Haumi wa kando, chawa yu nguoni

Hizo ndizo aina za mashairi zinazopatikana kwa mwongozo wa vigezo vya kifani. Hata hivyo kuna zingine zinazopatikana kwa mwongozo wa maudhui, ambazo ni pamoja na wajiwaji, Inkishafi, kasida na kadhalika. Zote zalengwa kwa waja walioghafilika na raha za dunia kiasi kwamba hawamjali Mola wao. Ni aina ya tungo zenye mwelekeo wa kitanbihi kwa jamii ya wanadamu waasi, ambao wamemsahau na kumtenga mola wao.

Mshairi hawezi kutengwa na kazi aliyoitunga katika sehemu ya mtindo - ule udhibiti wake wa njia za kujielezea. Kwa ufupi wahakiki huangalia daraja ya mawasiliano baina ya msanii na hadhira. Mpangilio ufuatao, kwa maoni (yetu) unafaa katika kuuelewa mtindo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Malighafi | Mtindo | | |
| Msanii-> | Lugha -> | ploti -> | Toni -> | Hadhira |
| (maudhui) | Wahusika | wakati | | |
| | mandhari | | | |

Baina ya mshairi na hadhira, pana kizuizi kinachowatenga wasanii na wasomaji wa kazi.

Udhibiti wa lugha wa msanii utamwezesha kuwaelezea vizuri wahusika wake, ambao nao watatupa mengi kutoka mandhari walimo, kuhusu mpokezano wa matukio kiwakati na kisha kugusa hisia za hadhira kwa aina ya toni watakayowasilishia. Washairi mbalimbali wana njia kadha za kujielezea na hivyo hadhira ikikumbana na kazi hizo, mara moja hutambua ni nani aliyeziandika hata kabla ya habari kuhusu nani kaziandika.

Kuna aina nyingi za uwasilishaji zinazotumiwa na washairi wengi, ambazo huwa za kitaswira, kitashtiti, kimaswali, kimafumbo na kadhalika. Aina ya taswira huwawezesha wasomaji kupata ujumbe kwa msaada wa picha zinazoashiriwa na lugha au maelezo ya msanii. Mtindo wa kibalagha na tashtiti huchochea hadhira kwa njia ya maswali, yasiyohitaji majibu. Maswali ya kawaida na misisitizo huwa mitindo mingine ya uwasilishaji. Ule wa kimafumbo nao hutumiwa. Uvumbuzi wa yaliyositirika katika mafumbo hutoa nafasi ya fasiri mbalimbali ambazo baadhi huchekesha na baadhi huajabisha. Baadhi hukosa mantiki na huwa si rahisi kuwafikiana kuhusu kilichokusudiwa. Fasiri zote huangaliwa tu kama mazao ya ubahatishi japo zitajaribu sana kushawishi akili kuziamini na kukubaliana nazo. Uwasilishaji mwingine hutokea kwa njia ya masimulizi, ambapo nafsi ya kwanza au tatu hutumiwa sana. Tungo zinazohusisha nafsi ya pili huwa chache sana na hatuelewi kwa nini. Hatima ni mtindo wa kimaelezo au kiufafanuzi ambao hutumiwa sana katika ushairi.

Mtindo ambao ni sehemu tata sana katika fasihi umewashughulisha wataalamu kwa muda mrefu na mpaka sasa si rahisi kukubaliana kuhusu namna ya kuutolea vijelezi muafaka. Licha ya utata huo kuna angalau vipengele vyake vya kuuelezea kama hivyo tulivyovipitia.

## 2:5 MANDHARI

Mandhari katika fasihi, ni mazingira ya kisanii ambayo msanii huyachagua katika kumsaidia kuendeleza kazi yake ili ieleweke vyema zaidi. Kwa sababu ya umuhimu wao, lazima yachorwe na kuelezwa kikamilifu katika kumsaidia msomaji kuishika na kuipata kikamilifu ile picha anayoilenga msanii.

Mazingira hayo huwa ya aina mbalimbali ikitegemea muktadha, mawazo na hali ya wahusika wanaohusishwa nayo. Hivyo yapaswa kushikana kikamilifu na maelezo na ujumbe. Yawezakuwa ya vita, kisiasa, kidini, kimapinduzi, kivuvi, kihistoria, kisayansi, kijiografia, kibunifu, kiuchumi, kifungo, kijamii, kimapenzi na kadhalika. Huhusisha mahali mbalimbali hapa duniani na mbinguni kama vile, paradiso, ahera, sirati, jehanamu, misikitini, shuleni, bungeni, bustanini, misituni, miji, bahari, milima, maofisi, nyumba, magarini, mashambani, mashimoni na penginepo pengi.

Mazingira mengine ni ya kidhahania na ya kubahatisha. Mathalan, mahali kama mbinguni hapajulikani palivyo, bali kinachotokea ni uchoraji unaotegemea ubunifu na mawazo tu ya wasanii. Baadhi ya wasanii hutuchorea picha za vitu dhahania kama urembo, uzuri, mapenzi na kadhalika. Mandhari hutokea dhahiri au hufichika ikitegemea kiwango cha ubunifu cha wasanii. Ikiwa anachoelezea msanii ni mahaba, basi mazingira yanayofaa ni yale ya kibustani yenye maua yaliyochanua vizuri, vilimani au popote panapovuma upepo mwanana, mahali huru pasi vizuizi vyovyote na kadhalika.

Ikiwa ni ya kuabudu, mahali kama mimbari, makanisa, misikiti, milimani na kumbi hufaa. Ikiwa ni ya ubatizo, basi mazingira ya mito na vidimbwi hufaa. Mkusanyiko wa watu wengi katika eneo moja kwa nia moja ya kumwomba Mungu huelezeka na kukubalika popote, kwani Mungu hatengewi eneo au mahali maalum. Itakuwa ajabu tukiona visa vya ulevi makanisani badala ya mabaani, uvuvi jangwani badala ya mitoni, maziwani au baharini, na mashindano ya mashua mabarabarani badala ya majini. Kila wazo huelezeka katika mazingira yanayofaa.

Umuhimu wa mandhari hukamilika panapotokea uhusiano mzuri kati yake na vile vipengele vingine vya fani. Kwa mfano, utokezaji mzuri wa picha kamili ya mandhari unatokana na namna ambavyo msanii ataitumia lugha yake. Akiitumia kwa hadhari, makini, ustadi na kikamilifu, basi ujumbe utafika kama ulivyolengwa na kwa waliolengwa. Tumeyazingatia hayo katika kuhakiki diwani zake Hassan Mwalimu Mbega.

## 2:6 PLOTI

Maoni ya wanaurasimu kupitia uhakiki wa Vladimir Propp(1928:18) ni kuwa, ploti ni, "umbo au muundo peke, wa hadithi simuliwa. Ni zao la mfuatano wa motifu (motif - limetoholewa. Lina maana ya 'kipashio simuliwa kisogawika)."

Beckson, K. na Ganz,(1960:166), wanaielezea ploti kama, "Mpangilio wa matukio katika masimulizi au tamthilia. Katika Taaluma ya Ushairi (poetics). Aristotle asema kuwa, ploti nzuri huwa na mwanzo, kati na mwisho; Aendeleza wazo hilo kuwa, lazima ipangiliwe vizuri ili tukio lisiondolewe na nafasi yake kuchukuliwa na lingine bila kuathiri muumano wa kazi nzima".

Syambo, B & Mazrui, A,(1992), wameilezea ploti kama "ule mfuatano wa matukio yanayoijenga riwaya na sababu zake". Katika ushairi, ni, 'mfuatano wa matukio'. Katika muktadha huu, tunaitazama kama, 'mfuatano (mfululizo) wa matukio yanayosimuliwa au mfuatano wa visa au vitukio katika tukio linaloelezwa". Hili hutokea katika mashairi yote bila kujali maumbo yao na urefu.

Msokile, M,(1993:93), asema kuwa ploti ni "mtiririko ama mfuatano wa matukio yanayosimuliwa kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hali hii huandamana na uchaguzi, mpangilio na ufundi wa kusimulia matukio yaliyoundwa vyema katika kazi ya sanaa ya kubuni itumiayo lugha.

Kwa ufupi ni kuwa maelezo ya wataalamu hao wote yanakubaliana katika kutupa maana ya ploti. Katika ushairi hutokea ploti msago, fululizi au tiririshi, ya taharuki na kadhalika. Ploti msago, fululizi au tiririshi ni ile inayolisimulia au elezea tukio toka mwanzo hadi mwisho. Ya pili huliacha tukio njiani na kulirejelea baadaye. Tumeangalia aina za ploti katika tungo za Mbega na namna zinavyodhihirika.

## 2:7 WAKATI

Wakati ni ule muda unaohusishwa kisanii na matukio yanayoelezwa. Haifai kuutaliki kutoka kazi za sanaa. Kazi yoyote ya kisanii hukosa umuhimu na uzito pale inapoangaliwa nje ya wakati.

Wakati waweza kuwa maalum au wowote. Baadhi ya matukio hutengewa tu wakati mmoja na huwa vigumu tena kuelezeka nje ya wakati ule. Katika wakati huu tulio nao, tungo nyingi zinazoshughulikia madhara ya ukimwi zafaa sana. Kukitokea tungo hizo, wakati ambapo tiba ya ugonjwa huo itakuwa imevumbuliwa, basi matokeo yake huenda yakawa ni kupuuzwa kwa kazi hizo, ingawa baadhi watazithamini katika kudhukuru kipindi kigumu cha utawala wa hofu wa ugonjwa huo.

Wakati ni muhimu katika kuwawezesha wasomaji kujua kama matukio yanayosimuliwa au elezewa yamekwishatokea, yanatokea au yatatokea. Japo kuna baadhi ya kazi ambazo ni za nyakati zote, zingine huwa za nyakati maalum.

Ni kwa sababu hizo, inakuwa ni muhimu wakati kuzingatiwa ili kutokeapo mabadiliko katika mitindo mbalimbali ya fani, basi wasomaji wawe na uwezo wa kuyafuatilia matukio na kujua yalitokea lini, kwa nini na yana umuhimu gani.

Tungo zitapoteza thamani kwa sababu ya kutokea katika nyakati zile ambapo hazitakiwi. Tungo nzuri ni zile zinazotokea wakati ule zinapotakikana zaidi. Zingine nzuri ni zile ambazo siyo za wakati mmoja maalum, ambazo zafaa katika nyakati zote, kama zile, kwa mfano, za William Shakespeare.

Kipengele hiki kitazingatiwa kwa kutizama arki za kifasihi zinazodhibitiwa na wakati au zinavyowiana na wakati katika diwani za Mwalimu Mbega.

## 2:8 TONI

Kuhusu toni, mhakiki Robin Skelton, (1978), ametupa maelezo yafuatayo ambayo tumeyatafsiri. Anasema, "Bila kuzingatia ni shairi gani analolichagua mtu, ni lazima livutie katika sauti peke". Sauti[12] hii hupatiwa sifa zake kwa njia ya matamshi mbalimbali bainifu, athari za kiwizani, hali ya ujazanda, na pia, hali zingine zote za maandishi, na bado inaweza kutambuliwa kama katika upekee."

Maelezo hayo ya Skelton japo kwa njia ya muhtasari, yatupa mwongozo wa namna toni inavyopatikana, na licha ya uhusiano wake na vile vipengele vingine vya fani, bado ina sifa za kipekee za kujitambulishia. Ingawa kwa nje toni yabainika kuwa kipengele cha fani chenye uhusiano na vipengele vile vingine kama ploti, ikichunguzwa kwa undani inadhihirika kuwa ni zao la ushirikiano wa maudhui na fani.

Katika shairi lolote, hujitokeza toni. Toni hizo huwa mbalimbali zikitegemea kinachoelezwa. Hata hivyo kwa ujumla huwa kunajitokeza toni za aina nyingi kama

za huruma, masikitiko, bahati, huzuni, kuchanganyikiwa, furaha, ukatili, masumbuko, wasiwasi, imani, hofu, mshangao, vuguvugu (si ya furaha au huzuni. Haiegemi popote), ukali, upole, urafiki, utononovu, uadui, usononevu, faraja, maliwazo, kariha himizi, uchangamfu, ubaridi, joto, kilio, woga, kicheko, kutarajia, uthamanifu, dhihaka, bezo, heshima, mahaba, ulevi, uchafuzi, ujenzi, majuto, shukrani, kujiamini, maangamizi, kufa moyo, tumaini, ubaguzi, ushauri, upotofu na kadhalika.

Toni, kwa maelezo ya Beckson, K & Ganz, A,(1960:225), ni tokeo la uhusiano wa mwandishi na kazi yake au hadhira yake. Wanasema, "Kwa kawaida, wahakiki hutumia istilahi 'msimamo' kurejelea uhusiano wa mwandishi na kazi yake au kwa hadhira yake au vyote. Misimamo hii kama inavyoonekana katika kazi yenyewe, huvyaza au hufinyanga toni. Msemaji hudhihirisha toni, kupitia mabadiliko ya sauti na hali, lakini mtunzi lazima ategemee ala zake za usemi katika mamlaka yake au udhibiti wake".

Naye Murray, P,(1978:163), anasema kuwa, toni ni, "Usemi wa msemi wa kifasihi kwa, msikilizaji au uhusiano wake kwa msikilizaji au kazi." Kwa hivyo, msimamo na uhusiano ndivyo hutupa toni. Msimamo wa mwandishi na uhusiano wake kwa hadhira na kazi ndivyo huzalisha toni.

Toni ni muhimu sana katika kupimia matokeo ya kazi na ishara zinazojitokeza kwa sababu ya ule mguso wa hisia, athari zake na aina ya taswira zinazojengeka.

Kwa mwongozo wa nidaa na utoshelezevu wa kunga za kifani za kifasihi twawezaona aina ya hisia zinazodhihirika katika wakati fulani na katika mazingira fulani.

Toni huwa za aina nyingi. Huwa za mshangao, furaha, huzuni, masikitiko, uadui, urafiki, inadi, unafiki, na kadhalika. Kwa maoni yetu ni kuwa toni huchipuzwa kupitia ushirika wa kunga zote za kifani na huwa na uzito zaidi pale inapoziba masafa ujumi au kuyafupisha sana, kiasi cha kuwaathiri wasomaji moja kwa moja ikitegemea mtindo wa maelezo au usimulizi.

Toni, basi, huwa ni itikio la ujumbe kupitia nguvu za zile arki za fani. Huwa kama tokeo na zao la mwisho kimazingira na kiwakati.

Nguvu zake zaandamana na athari inayozuliwa au inayozuka. Hutusaidia katika kupima uzito kwa kuangalia athari na aina ya hisia zinazojitokeza baada ya kupitia kazi yoyote ya sanaa na hivyo kuifanya hadhira kuwa na kumbukumbu isiyofutika.

Toni hujitokeza katika kila shairi, na kuna hali ya kuingiliana katika fungu la baadhi ya mashairi. Mathalan, kwawezatokea mashairi manne au zaidi yanayozungumzia mambo tofauti kwa njia tofauti na yakawa na toni ya aina moja kama mshangao kwa mfano.

Tungo nzuri ni zile zinazotupa toni ya aina moja au inayokubaliana na mandhari na wakati na maendelezo ya kiploti. Kunapotokea mseto wa hisia ambazo hutupa toni mbalimbali, huwa si rahisi kuona athari ya toni. Umuhimu wake hudhihirika lau toni ya huzuni itaipisha ya uchangamfu na kupandisha hisia zetu, badala ya kuanzia ukaramfu na kututamatishia maelezo na usimulizi kwa toni ya kilio na huzuni.

Nia yetu ni kutathmini matokeo ya toni katika tungo za Mwalimu Mbega na umuhimu wake kama tulivyofanya.

## Tanbihi

1. Kijarabati ni neno linalosimamia dhana ya Empiricism.
2. Urasimu - Kiwango ambacho katika kiingereza ni 'formal level'
3. Kisawe cha slang
4. Kisawe cha Colloquial
5. Mawako ni kisawe cha maumbo
6. Engshve - Akronimu ya English, swahili, vernacular
7. Muhu ni kisawe cha kariha
8. Funizi - neno tulililiunda toka neno ufunia, ambalo ni kisawe 'Euphony', yaani, muungano wa sauti ambao hupendeza masikio sauti hizo zinapotamkwa. Maelezo hayo yamo katika kamusi ya Isimu na lugha (1990:25), 'funizi' ni kisawe cha 'Euphonious'
9. Lugha zufu, ni neno tulililiunda lenye maana ya artificial language
10. Hemshi ni neno linalotumiwa kama kisawe cha emotions au emotive feelings.
11. Maelezo ya toni ya pekee
12. Kisawe cha toni

## SURA YA TATU: UPISHO WA UMALENGA

## 3:1 UTANGULIZI

Upisho wa Umalenga, (1975), ni diwani ya kwanza kuchapishwa ya Hassan Mwalimu Mbega. Ina mashairi 40. Ina visehemu vya 'utangulizi' na 'muhtasari' vilivyotiwa na mwandishi mwenyewe. Katika mianzo au miisho ya mashairi mengi kuna maelezo yaliyotiwa na mtunzi ambayo yanatoa mwongozo wa kimaudhui na kifani - hasa kuhusu matumizi ya lugha.

Mshairi hakutia sehemu ya sherehe ili kuwaongoza wasomaji wake kupata maana za msamiati alioutumia. Yaelekea hakufanya hivyo kwa sababu ya maelezo aliyoyatoa katika kila mwisho wa baadhi ya mashairi. Pili, huenda aliona kuwa msamiati alioutumia si mgumu. Tatu, huenda alifanya hivyo ili wasomaji wenyewe wafanye bidii ya kuuelewa. Hatima, huenda kusudio lake ni kuukusanya msamiati huo katika diwani za kufuatia hii.

Kwa nini msanii ameipa diwani yake anwani hii? Sababu za kifani zimechangia hili kuliko za kimaudhui; ingawa kwa maoni ya Edward Stankiewicz (1964:74), fani na maudhui havitenganishiki katika ushairi. Hakuna ushahidi kutokana na tungo unaoonyesha anwani yatokana na nini. Hata hivyo kuna mwelekeo kimantiki unaotokana na wakati kazi hii ilipochapishwa. Neno 'upisho' lina maana ya, "kuweka nafasi ili mtu au kitu kipite". Sasa swali linalofuatia ni: nini kinachopishwa na kwa nini? Inavyoelekea ni kwamba kinachopishwa kama anwani inavyosisitiza ni umalenga wenyewe wala si kitu kingine. Hili latokana na hali kwamba msanii ameanza kutunga baada ya vifo vya washairi maarufu kama Shaaban Robert. Kwa sababu ya kukulia katika mazingira na wakati sawa na malenga hao waliotukuka, yaelekea msanii alivutiwa nao na hivyo kazi hii inatokea kama upisho wa umalenga wao, au kama upokezano wa huo umalenga.

Si anwani tu ya diwani hii iliyofumbwa bali pia hata baadhi ya mashairi kama 'maji'. Sababu za matumizi ya aina hii zimeangaliwa katika uhakiki wetu.

Ili kutuwezesha kutoa mifano kwa njia ya kiukevu zaidi, tumetumia utaratibu wa tarakimu kama; 24.2.4.6 ambapo tarakimu za kwanza zinawakilisha ukurasa ambamo kuna ushahidi au mfano, pili ni ubeti, tatu ni mshororo, na nne ni idadi ya neno katika mshororo. Mfano huo hapo juu una maana kuwa ushahidi umetolewa ukurasa wa 24, ubeti wa 2, mshororo wa 3, kutoka neno la sita. Pale ambapo tarakimu hizo ni tatu, ina maana kwamba ni nambari ya idadi ya neno iliyowachwa. Lau ni tarakimu mbili, basi ina maana kwamba ukurasa na ubeti, ndivyo vilivyozingatiwa. Njia hii ni rahisi kufuatilia katika kuepuka kupoteza wakati.

## 3:2 LUGHA

### 3:2:1 MSAMIATI: MAANA, UWEZO & MAHUSIANO

#### 3:2:1:1 UTEUZI WA MSAMIATI

Kimsingi hapa linalozingatiwa ni kwamba uteuzi mbaya wa msamiati utavunja mioyo ya wasomaji na kuvunja mawasiliano pia, ambapo lile daraja la kuwavusha watu kimaana litakuwa limebomolewa. Ule uhimili wa uamili utatoweka pia. Kazi za sanaa husifika kwa sababu ya ule ufundi wa kuwasilisha. Ufundi huu kimsingi unategemea namna msanii anavyochagua maneno yake toka hazina kubwa ya malighafi ya leksia. Hili linatupa mawezekano kwamba, maneno hata sita yaweza kuwakilisha kitu kimoja kimaana. Katika haya, yapo ambayo yatafaa zaidi kwa uzito na msisitizo kuliko mengine katika miktadha, matini na mazingira maalum. Ni kwa sababu hii tunadai kwamba, pale ambapo mshairi atafanikiwa kuteua neno muafaka na kulitumia katika mazingira yanayofaa, na kulipa msisitizo fulani unaolipa uzito fulani katika muktadha fulani, atakuwa amefanikiwa.

Si lazima msamiati uliochaguliwa uwe wa kale, wa wastani, mwepesi au wa Kiswahili tu, ila hata wa lugha zingine madhali wakubali kubadilika kiumbo ili kuoana na mazingira ya lugha pokezi. Kwa kuyapitia mashairi yote humo tumegundua kwamba msanii ameyateua maneno yake kwa makini na hadhari kusudi asitangue mawasiliano.

Ustadh Shuara, kwa kiwango kikubwa amefanya uteuzi wa maneno siyo tu unaofaa na kuoana na mazingira, lakini ambao pia unabeba uzito huku ukichukuana vyema na wahusika, wakati na kushikana na ploti, mbali na kuleta ile toni inayotarajiwa katika mazingira maalum. Hivi si kudai kwamba hakuna mahali ambapo mwandishi amekosea, kwani hayo yametajwa pale yalipogunduliwa. Lile lililopo ni kwamba, kwa kiwango kikubwa uteuzi alioufanya ni mzuri na unachukuana na mandhari aliyoyashuhudia msanii. Kwa mfano, katika shairi 'Bahati' lililo katika ukurasa wa 30, mshairi ameteua takriban msamiati wote kwa makini na kuutumia katika mazingira unamofaa. Mfano huu unathibitisha kauli: 30:3

Bahati haina dawa, hirizi kujitatia
Haina kuaguliwa, na pesa kuilipia
Ukabakia mkiwa, ukaapo ukalia
Yenyewe hukujilia, bahati haina dawa

Kutokana na fungu hilo, kuna tashuhudi tosha kuwa msanii ameteua msamiati kwa makini na hadhari. Karibu maneno yote ameyateua kwa njia nzuri. Yanawafiki katika kuhusiana na katika muktadha. Uzito wake watokana na mtindo wa mshairi wa kumhusisha msomaji moja kwa moja. Haya yanadhihirika katika ushahidi uliopo katika vifungu: "Ukabakia mkiwa", "ukaapo ukalia", "yenyewe hukujia" na vingine ambavyo vyafaa. Vifungu hivyo vyabeba maana nzito sana katika matini vinamowafiki. Pia vyachukuana na hadhi ya wahusika lengwa.

Ushahidi wa uteuzi mzuri wa msamiati watokea pia katika mashairi mengine yaliyomo humo. Karibu katika mashairi yote msanii ameteua maneno yake kwa subira kubwa, werevu, hadhari na makini, hali inayoyafanya kufaa sana.

## 3:2:1:2 AINA YA MSAMIATI

Mbali na kile kiwango cha uzito, wepesi na uwastani wa msamiati, huangaliwa pia viwango vya mofolojia, ukawaida na ukosefu ukawaida katika msamiati. Kutajwa kwa aina ya msamiati kunakusudiwa kuyaainisha na kuyatofautisha maneno. Mathalan, pale tunapotaja aina za watu, tunakusudia jinsi zao, vima vyao, hadhi zao, sura zao, rangi zao, tabia zao na kazi zao katika kuwapambanua. Nia yetu hapa ni kutumia vile vigezo vinavyofikika na kuaminika katika kutambua aina za maneno yaliyotumiwa. Kwa sababu hiyo baadhi ya sifa kama za asili ya msamiati na uamili wake ambazo zingefaa sana katika kufafanulia swala hili zimeangaliwa kama vipengele huru.

Mshairi ametumia msamiati mzito wa asili mbalimbali; wa maeneo mbalimbali ya uswahilini na baadhi yaliyokopwa toka kiarabu na kidigo. Uzito wake unatokea kwa uzuri kwa kuangalia muktadha ambamo umetumiwa. Ifuatayo ni baadhi ya mifano iliyotumiwa kwa uzito katika mazingira ya maneno mengine kama inavyodhihirika hapa:

| | Neno | Muktadha |
|---|---|---|
| 1.4.1.3 | Laini | maji umbole laini, mtu huwezi yashika |
| 1.6.2.3 | Mwandani | Ewe swahiba mwandani, sinache nikasumbuka |
| 15.5.1.6 | Muhali | Ufanifu wa milele, kudumu huwa muhali |
| 17.6.1.3 | Malihi | Sauti yako malihi, kila nikiikumbuka |
| 17.5.1.3 | Mastuhi | Ewe huri mastuhi, mzuri uloumbika |
| 25.6.1.3 | Dar-Madari | Tungo za dar-madari, nyia ziso uchokefu |
| 24.9.1.3 | Kago | Leo nimekita kago, kusubiri zenu kombo |
| 32.6.4.4 | Leba | Ila suhuba ya leba, akuvunjia kadiri |
| 58.1-10.4.1 | Hoshari | Hoshari paka hoshari, kuliwa mimi sitaki |

Mifano hiyo ya maneno na mingine mingi imetumiwa kwa uzito katika mazingira inamofaa. Kuna baadhi ya maneno ambayo uzito wao ni wa asili au watokana na asili zao. Lakini siyo yote yenye asili yana uzito kama anavyosema msanii huyu katika ukurasa wa 4, kuwa, "Na kila ubeti iliyoingia neno la kiasili huwa na uzito kuliko lililokosa neno la asili, ---". Tayari katika hiyo orodha hapo juu kuna maneno kama malihi, mastuhi, dar-madari na mengine ambayo asili yao ni kiarabu, lakini yametumiwa hapo kwa uzito.

Uasili wa neno siyo tu ushahidi wa uzito wake, na siyo maneno yote ya asili ya kiswahili ambayo yana uzito huo. Matumizi, kwa mfano ya, dar-madari, ya kinahau na kisitiari ni ya uzito, japo ni la asili ya kiarabu. Uzito huo watokana pia na muktadha. Dar-madari ni neno la kusifia ubora wa kitu na limewafiki katika

matini ambamo limetumiwa. Twaona pia kuwa mpangilio na mahusiano ya maneno unayapa baadhi uzito kama inavyoonekana bado katika mifano hiyo tuliyoitoa. Hapa tunakusudia kufuatwa kwa taratibu za sintaksia katika kuleta maana iliyokusudiwa.

Hivyo ushirika wa sintaksia na semantiki una sehemu muhimu hapa katika kuleta uzito au wepesi katika shairi. Usemi wetu haukusudiwi kupuuza kabisa mazingira ambamo maneno hayo hupata nguvu,na uzito. Hii ni kwa sababu uzuri wa kitu umo kwenye utendaji kazi wake wala siyo katika umbo lake. Mazingira ya matumizi ya maneno hutegemea kaida za sintaksia katika kupata unyoofu wa kisemantiki. Mifano hii miwili ya beti mbili mbili kutoka upisho wa umalenga 19:1 & 5 na kutoka Malenga wa Mrima 81:1 & 7 yatuthibitishia kauli hii kwamba kaida za kisemantiki na kisintaksia zina mchango fulani wa kuleta uzito katika maneno yaliyotumiwa.

19.1 & 5

Achani maneno hayo, tena achani kabisa
1 Achani muyanenayo, kudhani pendo ni pesa
Si pendo hilo ni payo, si pendo ni payo hasa
Viwili katika moyo, kuviweka vyanitasa

5 Viwili katika moyo, kuviweka vyanitasa
Pendo lenye jakamoyo, na tamaa ya mapesa
Pendo la namna hiyo, ni wapi liliko hasa?
Viwili katika moyo, kuviweka vyanitasa

81.1 & 7

Maji lipi kosa langu, nijuzeni hilo kosa
Mtendwavyo walimwengu, kiasi mmetendesa
1 Yu wapi mwamuzi wangu, Vingine havitapasa
Maji lipi langu kosa, nahiliki walimwengu

7 Kutanani makuhani, Mzipekue kurasa
Mdidimie kwa ndani, pasi mwenzi kunifyosa
Muamue kwa wizani, taabuni napupusa
Maji lipi langu kosa, nahiliki walimwengu.

Kwa kulinganisha beti hizo mbilimbili za mashairi 'pendo' na 'maji', katika vipengele vya msamiati asilia, uzito wake na uzito wa beti ambamo umetumiwa, twagundua kwamba katika la awali, uwasilishi ni wa moja kwa moja ambapo mpangilio wa msamiati unachukuana kwa wizani fulani kinyume na ilivyo katika baadhi ya mafungu ya maneno katika la pili, japo kimrima kimetumiwa katika yote. Ni kwa sababu hiyo twadai kuwa ughairi wa kaida za kisintaksia na kisemantiki watokea kwa kiwango kidogo sana katika tungo za Ustadh Shuara. Hivi si kudai kuwa shairi 'maji' halina uzito. Lina uzito ambao unatokana zaidi na matumizi ya

msamiati kama 'maji' kitamathali na kwa kufumba. 'Maji' ni neno lepesi na la kawaida, lakini ambalo limetumiwa kwa njia nzito kulingana na mazingira ambamo limetumiwa na jinsi ambavyo limetumiwa. Halina uangavu kimaana huku ikidhihirika kwamba ile ya kawaida siyo aliyoikusudia msanii. Yameuhishwa na kuingizwa katika mazingira ya kiadinasi, ambapo yaulizwa maswali, na twajua kuwa toka zama za zama maji hayajawahi kuongea au kuzungumza. Kwa njia hiyo matumizi hayo yana uzito fulani kisemantiki.

Tulitaja pia kuwa kuna msamiati wa kadiri na mwepesi. Kufikia hapa, twaainisha tu msamiati bila ya kutoa mwangaza kwa upana kuhusu kinachotuongoza kufikia maamuzi hayo. Tunapotaja uzito wa msamiati, neno uzito hujumuisha mambo mengi. Nayo ni pamoja na asili ya neno, matini linamotumika, nguvu za maana linayowakilisha kimapigo, uangavu na usitiri wa maana katika mawasiliano, uwezo wake wa kuweza kuathiri msimamo wa msomaji, uwezo wa kufanikiwa kuathiri msimamo wa msomaji na nadhari yake, uwezo wa kuweza kutawala nadhari ya msomaji na ile akili-laza yake, ufaaji wake katika muktadha,uhusiano mzuri na mengine, uwezo wake wa kuhamisha sifa hasa za kimaana (kisemantiki), mawezekano yake ya kuweza kutumika katika miktadha mingi, uwezo wake wa kuwakilisha maana nyingi na pana, uwezo wake wa kuweza kuleta wizani katika maana na kadhalika.

Uwastani au ukadiri wa lugha hutokana na hali ya usanifishaji, ambapo msamiati huwa si mwepesi na si mzito. Msamiati wa lugha wastani husahilishwa kusudi kuleta mawazo ya moja kwa moja katika mawasiliano. Katika viwango vya uwastani na wepesi, msamiati uliotumiwa hauna athari kubwa kwa wasomaji, na umezoeleka sana na matumizi yake japo yawasilisha kwa urahisi sana bila vizuizi, haupatiwi uzito wowote. Wengi huuona msamiati wa aina hiyo kama uliochakaa, na ambao hutumika katika mazingira ya kawaida yaliyozoeleka sana. Pia pale unapokosa kupamba ujumbe, ujumbe ule huchukiza kwa haraka kwa sababu ya matumizi mabaya ya msamiati ambao haukuteuliwa kwa makini na kupimwa kama wafaa katika mazingira au matini ambamo umetumiwa. Hata hivyo ukawaida wa maneno hutoweka yanapoingizwa katika mizani nzuri ya kisintaksia. Ufuatao ni mfano wa ubeti ambao una mchanganyo wa maneno mazito na mepesi na ambao umeendelezwa vyema kisintaksia, kutoka diwani ya Upisho...

61.9

Na pindi ovu lijapo, lijaribu kulipima
Lijuwe litokeapo, ulichunguwe hatima
Si togo aula tepo, Si kite wala kuvuma
Jazaye mema ni wema, uovu sio malipo

Vifuatavyo ni vifungu vya maneno mepesi kutoka diwani, lakini ambavyo vina nguvu sana kwa kutegemea jinsi sintaksia inavyofanya kazi.

| | | |
|---|---|---|
| 1 | 72.1-8.4 | Penye wazuri halisi, wajisifuje uzuri? |
| 2 | 40-41:1-10.4 | Mawazo nakupa pole, pole sana ndugu yangu |
| 3 | 42-43:1-10.4 | Mama wa kambo si mama, halei mwana wa mume |
| 4 | 17.4.3 | Mwandani wangu furahi, zungumza na kucheka |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | 17.5.1 | Ewe huri mastuhi, Mzuri uloumbika |
| 6. | 17.6.1 | Sauti yako malihi, kila nikiikumbuka |
| 7 | 46-47.1-10.4 | Ni msumari wa jito, Mwana wa mke si wako |

Mifano hiyo na mingine ambayo hatukuitaja inaleta mapigo yenye nguvu kimaana kwa njia ya kitamathali katika baadhi. Mfano wa kwanza una uzito katika mpangilio wa maneno na swali la balagha lililouzwa. Wa pili una uzito unaotokana na mpangilio mzuri wa msamiati, toni ya liwazo pamoja na msisitizo wa ukaririfu katika neno 'pole'. Wa tatu wapata nguvu toka mpangilio mzuri wa kisintaksia na ukanushi uliokakatiwa[1] vizuri. Wa tano wategemea uteuzi mzuri wa maneno, yanayochukuana kwa uzuri na visifa vinavyofaa. Wa nne wategemea mpangilio mzuri wa kijalizo[2] (kikoja) na nguvu za kimilikilishi 'wangu'. Kimilikishi yako pia kinaleta mvutio na uzito katika mfano wa sita, ambao pia unaimarishwa na mpangilio mzuri wa kisintaksia wa msamiati ulioteuliwa kwa uzuri.

Wa saba wapata nguvu kwa sababu ya mpangilio mzuri wa kisintaksia, uundaji upya ambao umeingizwa katika hali kuzwa, hasa wa neno 'jito' (ukubwa wa moto) na ukanushi unaowafiki. Maneno hayo mengi ni ya wastani na mengine ni yale ambayo yanaonekana ya kawaida, lakini namna yalivyopangiliwa kisintaksia yanaimarishiwa nguvu zao za kisemantiki.

Katika kuhakiki aina ya msamiati uliotumiwa tumeangalia uainishi wao katika makundi ya nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, viarifa, viunganishi, vionyeshi, vimilikishi na kadhalika. Kwa kuchukua mifano miwili na kwa kuiangalia kwa undani, tumegundua kwamba kila mojawapo wa leksia zake huwa na uamili mkubwa sana usiopuuzika na hasa katika sanaa. Katika usemi wa kawaida, watu hulenga tu kuwasiliana. Lakini katika fasihi hulenga kuwasilisha kwa mvuto zaidi na uzito. Hapa wasanii hujali sana wanavyowasilisha. Hivyo nafasi kubwa sana ipo ya vivumishi, vielezi, vimilikishi na viunganishi, kinyume na ilivyo katika matumizi ya kawaida ya lugha ambapo lugha hutumiwa kwa ukavu mwingi bila kujali matokeo ya namna ujumbe ulivyofikishwa. Mifano ifuatayo imetusaidia kuangazia swala hili.

| | |
|---|---|
| 11.3.1 | Usipitishe ahadi, kwa yeyote ukimpa |
| 35.11.1 | Tama nimalizialo, moyo umche wahabu |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Usipitishe | ahadi | kwa | yeyote | ukimpa |
| | I | I | I | I | I |
| | kitenzi | nomino | kielekezi cha mpokea kitendo | kivumishi kionyeshi | kitenzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Tama | nimalizialo | moyo | umche | wahabu |
| | I | I | I | I | I |
| | nomino | kitenzi | nomino | kitenzi | nomino |

Kutoka mifano hiyo twaona jinsi kila kundi la maneno lilivyo na uamili wa kuwasilisha kwa uzuri na mvuto. Maneno yanafuatana katika mpangilio unaofaa.

Vielezi na vivumishi vimetumiwa kwa uzuri na husaidia kupamba ujumbe kisanii. Hili lafungamana na ufundi mkubwa wa msanii katika uteuzi mzuri wa msamiati, na mpangilio wake mzuri ambao unashikana katika kuleta maana.

Katika ushairi, ni muhimu kuangalia pia urefu wa msamiati. Katika ushairi wa kimapokeo unaoongozwa na kaida za mizani, urefu na ufupi wa msamiati wafaa sana kuzingatiwa. Neno likitokea kuwa fupi na mshairi ataka kulirefusha, atafanya hivyo kwa njia nyingi zikiwemo za kulikariri au kuliongezea vipashio vya kitanakali sauti. Hata katika diwani, maneno yaliyo marefu ni yale yaliyorefushwa kwa njia za takriri. Mifano hiyo ni ya maneno kama 'kuututusatutusa'-(uk.20) mizani nane, kusongomasongoma (uk.22) - mizani saba na mingine mingi. Maneno mengi ni yale ya mizani sita. Pia yapo ya mizani moja. Hata hivyo ufupi na urefu wa msamiati haupunguzi uzito wake. Kinachofaa katika msamiati ni vipashio vyao, uamili wao na ufaaji wao vilimotumiwa.

3:2:1:3 ASILI YA MSAMIATI

Umuhimu wa kuliangalia swala hili watokana na hali kwamba neno moja linaweza kutumiwa kwa maana tofautitofauti ikitegemea eneo na lahaja. Tofauti katika lahaja huleta tofauti katika namna ya kuyatamka maneno na kuyaendeleza kihijai. Kwa mfano, neno mtu huendelezwa kama mchu, muchu, mru na mengine katika baadhi ya lahaja. Neno pete huendelezwa kama peche, mtoto huendelezwa kama mroro au mchocho, vita kama zita, dhicha na kadhalika.

Tofauti hizo mbalimbali za kifolojia na kimofolojia huenda zikatatiza maana kwa msomaji ambaye hajapitia kazi au lahaja hizo. Baadhi ya maneno hukopwa toka lugha za kiafrika na kigeni, na kisha kuswahilishwa kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki. Ni kwa sababu hizo inakuwa ni muhimu kujua asili ya neno kama njia mojawapo ya kumwezesha mtu kupata maana yake. Isitoshe, baadhi ya maneno kama yale ya dini ya kiislamu huchotwa moja kwa moja toka kurani tukufu, kusudi kutoyapanguzia uzito katika kuyatafsiri.

Kwa muhtasari ni kuwa msanii ametumia msamiati mwingi wenye asili katika kiswahili, lahaja zake, lugha za kibantu na baadhi uliotoholewa toka kiarabu, na ambao umeshikana vizuri kisemantiki, kifonolojia na kimofolojia na ule wa asili ya kibantu na lugha za kiafrika.

Mshairi ametumia msamiati kutoka lahaja za maeneo ya uswahilini kama vile, kimrima (kilichotumiwa sana kwa wingi), kipate, kimvita, kisiu na kimtang'ata. Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya maneno na asili zao

| **Neno** | **Maana yake** | **Asili yake** |
|---|---|---|
| zizee | zilizaa | kisiu |
| kago | kinga | kimrima |
| maimbo | matuta au wadudu wanaochezea samadi | " |
| leba | udanganyifu, hadaa | " |

| | | |
|---|---|---|
| umshome | umdunge | " |
| aoneto | akiona | kiamu/kipate |
| Hoshari | Niache peke yangu (leave me alone) | kimtang'ata |
| mogo | siku saba za juma | kidigo |
| muhambo | mtego | " |
| kidhaba | mwongo | kiarabu |
| jisadi | kiwiliwili, mwili | " |
| katabtu | naandika | " |
| dar-madari | juu kwa juu (bora) | " |
| vitome vitome | vipande vipande, machanechane | Kimvita |
| Tumetume | woga woga | " |
| Azaujati | mke wangu | Kiarabu |

Asili ya neno inasisitizwa sana kusudi kupata ile hakika ya maana inayobebwa na maneno hayo. Ndiyo maana mshairi huyu katika Dafina ya umalenga 2.8.2 asema, "Neno lijuwe asili, maani lisipotele". Tukirejelea upisho wa umalenga ni kwamba takriban msamiati wote wajulikana asili yake.

## 3:2:1:4 UWEZO/NGUVU ZA MSAMIATI

Mada hii ndogo imekusudiwa kuonyesha chanzo cha uzito au nguvu katika maneno. Hili limesaidia katika kutathmini aina ya msamiati uliotumiwa.

Ni wenye nguvu au la! Kwa kulitazama swala hili, tumetambua kuwa mambo kadha huchangia katika kuimarisha maneno ya ushairi.

Kwanza hilo hutokea kwa sababu za kisemantiki. Hili limejadiliwa tayari na hata kutolewa mifano katika sehemu inayotangulia hii. Pili ni uteuzi aliali wa msamiati. Hili pia limeangaliwa na kuthibitishwa katika sehemu takadamu. Pia kuwepo na matumizi ya msamiati katika mazingira afiki huchangia, na hili limekwishaangaliwa. Itifaki katika uhusiano wa maneno ni hali nyingine changizi. Misisitizo ya ukariri, tanakali sauti na vivumishi vionyeshi pia huyapa maneno nguvu.

Mpangilio mzuri wa kimofolojia nao huchangia. Kwa mfano katika diwani hii kumetumiwa neno 'mastuhi' kwa njia ya kiantomasia[3], ambayo kwayo limebadilishwa vipashio, na kuongezewa vyenye nguvu. Badala ya mstahi, msanii ametumia mastuhi, neno ambalo lina sifa ya uzito kuliko mstahi, na hili ni kwa sababu ya ule mpangilio wa vipashio vyake kimofolojia na kifonolojia ambapo latamkika kwa uzuri fulani kuliko la awali.

Kuzoeleka kwa msamiati huleta uchakavu katika neno na hilo huenda limechangia katika kupunguza nguvu za neno mstahi. Aina nyingine ya uongezeaji nguvu hutokea kwa njia za uambishaji na mnyambuliko wa vitenzi ambavyo huwasilisha maana mbalimbali. Mifano michache ifuatayo yathibitisha kauli.

2.7.1 Sinifanye baahuni, ukawa kunikoweka
3.2.2 Nataka hizi tatizi, sitatuke tatu-tatu
8.9.3 Hii dunia si ndehu, na vituvye vilivyoko
13.3.3 Kule sambe ni sahali, sijeishia kusonya

katika mifano hiyo msamiati wawezeshwa kuwasilisha kwa uzuri kwa sababu ya mpangilio wao mzuri wa kisintaksia. Pili ni ukariri wa baadhi ya vipashio katika baadhi yao, kama vile 'tatu-tatu'. Ukariri huu unasisitiza maana ya neno na kuleta uzito siyo tu katika hilo neno, bali pia katika mshororo mzima. Yategemea pia mtindo wa uwasilishaji unaoendelezwa katika nafsi ya kwanza.

Asili za maneno hayo, mpangilio wao mzuri na uwezo wa kutumiwa katika mazingira yasiyo ya kiasilia vimeyaongezea nguvu. Msanii ameepuka matumizi ya msamiati ya kihorera (ya mpangilio ovyo). Mwandishi John Donne katika shairi lake 'Kifo usijifaharishe' (Death be not proud) alidai kuwa, ikiwa usingizi ambao ni mwigo wa kifo, ni mtamu, basi kifo ambacho ni halisi, ni kitamu zaidi. Uzito wa maneno ya mwandishi huyu unategemea sintaksia katika utendaji kazi wake au mtindo wa uwasilishi. Maneno yaliyotumiwa hapa ni ya kawaida, na katika mazingira ya kawaida, lakini katika njia isiyo ya kawaida. Utamu si neno la kuhusishwa na kifo.

Tukirejelea msanii wetu ni kuwa, uwezo wa msamiati alioutumia wategemea kutozoeleka kwake katika maeneo fulani. Pia wategemea jinsi maneno yalivyotumiwa hata yawe ya kawaida. Watokana pia na mkazo katika matumizi ya baadhi ya maneno. Hilo hutokea kwa kulirudia neno au kulitumia kwa njia fulani ya mkazo. Uhamishi wa sifa za baadhi ya maneno hata yawe ya kawaida hufaa katika kuyaongezea uzito. Upanuzi wa maana katika miktadha fulani fulani, uteuzi muafaka, matumizi mazuri katika mazingira bora, uhusiano na mpangilio faafu unaozaa wizani fulani unaovuta nadhari, minasibisho na tamathali za usemi, ni miongoni mwa yale yanayoongeza uwezo katika jinsi msanii alivyotumia lugha katika diwani yake. Mambo hayo hulipua toni ya aina fulani, ambayo nayo huongezea nguvu mawasiliano ikitegemea namna inavyotokea. Hayo na mengine hufaa katika kuyapa uzito maneno ya kisanii ya ushairi.

## 3:2:1:5 MOTISHA/KARIHA KATIKA MATUMIZI YA MSAMIATI

Matumizi mazuri ya msamiati na lugha kwa ujumla huwavutia wasomaji. Katika diwani ya Upisho wa Umalenga, msamiati umetumiwa kwa namna inayompa moyo msomaji na msukumo unaovutia.

Mitindo mbalimbali ya kuyapangilia maneno, misisitizo, takriri, tanakali sauti, minasibisho, na tamathali kadhaa za usemi, vimesaidia kuvunja mtindo wa uwasilishi wa aina moja. Kuyapangilia maneno upya na kugeuza mpangilio wao katika mishororo awali kupitia mtindo wa pindu, kunavunja uchakavu na ukosefuhamu (ukinaifu) katika tungo.

Mifano miwili ifuatayo yathibitisha kauli

19.3

Hasikizi anenwayo, japo watu wamfyosa
Hadhuriwi sumbuliyo, tukano wala kunyusa
Afanywe yote yawayo, ni kama wamtakasa
Viwili katika moyo, kuviweka vyanitasa

58.3

Mchana kutwa sitoki, kuicha yako hatari
Usiku humakiniki, kucha ni kuvinjari
Uonywapo huonyeki, kisha wazidi kiburi
Hoshari paka koshari, kuliwa mimi sitaki

Mpangilio wa maneno katika beti hizo wavutia na kumpa ushawishi msomaji na hamu ya kutaka kuendelea kusoma zaidi. Mifano hiyo toka mashairi pendo na Hoshari yatuthibitishia kwamba msamiati alioutumia msanii unampa motisha msomaji na hilo laonyesha ule ufaafu wake. Hili latokana na sababu kadha. Nazo ni matumizi ya msamiati mzuri, katika mazingira mazuri, mahusiano mazuri na mbinu za uwasilishi za aina nyingi ambazo hutoa njia mbalimbali zinazovutia katika maelezo. Katika mfano wa kwanza, maneno yamepangiliwa vizuri kisemantiki kwa namna inayofaa, huku yakibeba uyakinifu wa yanayoelezwa. Ni mambo yanayoaminika. Uyakinifu ni kipengele mojawapo katika vile vilivyoshughulikiwa na wanaurasimu. Mfano wa pili pia umepangiliwa vizuri kisintaksia na mtindo huo hauchoshi. Kwa ufupi msamiati umepangiliwa kwa namna isiyomfisha moyo msomaji.

## 3:2:1:6 MAZINGIRA AMBAMO MSAMIATI UMETUMIWA

Mapitio yetu katika tungo zote yametudhihirishia kwamba mazingira yaliyotumiwa ni ya kijamii - yakihusisha vitendo mbalimbali vya wanajamii. Ni mazingira yanayoaminika na kufaa sana aina ya msamiati uliotumiwa humo. Kwa mfano, maneno katika ubeti huu yanawafiki aina ya mandhari ya kijamii ambayo kwayo yametumiwa.

33.7

Enyi mlo mahabuba, kafa nawapa habari,
Imani sasa ni haba, nyuso hazitahayari,
Hakuna mpiga toba, wabakio majusuri,
Iwapo ndio suhuba, yafaa kutahadhari.

Kuna ukweli wa ujumbe huu katika hali ya kisuhuba. Kwa mfano huu, twaona mazingira yanayofaa katika aina ya msamiati uliotumiwa humo.

Katika baadhi ya maneno twaona matumizi ya maneno katika mazingira ya kweli, lakini kwa namna inayoyafanya kufikiriwa upya. Ni matumizi yasiyo ya kawaida, kama inavyobainika katika mfano huu.

1.5

Niliyaona zamani, hakaa kuyapulika,
Hayasikia kwa ndani, yasema huku yacheka,
Haona ni kuu shani, au mijuza kutuka,
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

Kutoka mfano huo, twaona matumizi yasiyoaminika nje ya sanaa ya neno 'maji'ambalo limehusishwa na sifa za kiadinasi za kusema, kucheka na mengine. Nje ya fasihi hayaaminiki. Katika fasihi, yaaminika kwa sababu mtindo wa aina hii wa kimafumbo umezoeleka, ambapo vitu vyatuikwa sifa zisizo zao kabisa, na ambazo hatimaye huwarejelea wanajamii. Neno hilo limetumiwa katika mazingira ya kijamii, ambapo lawakilisha 'msichana' mwenye sifa hizo kinyume na alivyomdhania msanii.

Nyakati zingine maneno huzuka katika mazingira ambayo si yao asilia. Hili hutokea neno linapohamishwa toka mazingira asilia na kutumiwa katika mazingira mageni ambapo huzalisha sifa tofauti na za awali. Katika kufanya hivi wasanii siyo tu huhamisha sifa ya neno au sifa ya matumizi ya neno kutoka eneo moja la matumizi hadi lingine, bali pia hujenga picha mpya, pamoja na sifa mpya. Kunatokea pia upanuzi wa mazingira ya matumizi ya neno. Kwa sababu hii kunatokea uzito fulani katika matumizi ya maneno hayo. Mfano ufuatao wathibitisha kauli.

54.1

Alivyo mwana Adamu, mwepesi wa kuzowea
Iwapo wamkirimu, siku zitateketea
Madhali kila daimu, huwa wamsogezea
Cha bure hakiwi tamu, ila wambiwe sogea

Katika ubeti huo, matumizi ya neno 'teketea' hayatokei katika mazingira yake asilia japo kuna uzito fulani na picha inayojengeka na kujitokeza kwa kulitumia neno hilo. Kuteketea kumetumiwa kuonyesha ile kasi ya kuisha na kutoweka kwa siku alizokirimiwa mja. Kwa sababu hiyo picha inayoibuka hapa ni ile ya kutoweka haraka na kabisa. Twaona kuteketea kukihusishwa na wakati badala ya moto.

Mfano mwingine uliohamishiwa mazingira ni ule wa neno 'sinzia'. Neno hili katika matumizi yake ya mazingira halisi hutumiwa kwa maana ya "shikwa" na usingizi mwepesi au taka kulala kwa kufumbafumba macho na kusinukia. Neno hilo limetumika hapa nje ya muktadha huo japo limehifadhi maana yake.

30.5

Wambwe katafute njiwa, lete na shilingi mia
Bila shaka utapowa, bila kutwa kutimia
Mambo yote yatakuwa, wala hayatasinzia
Sishike la kusikia, bahati haina dawa

Katika ubeti huo twaona hali fulani ya uhamishi wa sifa za wasifu. Twaona jinsi mambo yalivyovishwa wasifu wa kusinzia, sifa ambayo yatengewa tu wanyama, ndege na watu. Kunajitokeza hali ya msepetuko na kuyumbayumba katika mambo. Matumizi hayo yanaleta uzito fulani katika ujumbe.

Mfano wa mwisho unaohusu neno kukoweka umo katika 2.7 na unaendelezwa hivi:

Sinifanye baahuni, ukawa kunikoweka
Kunitupa mvunguni, pamwe na kunifinika
Mwenzio ni taabani, sasa umetimu mwaka
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

Kukoweka ni neno zito sana linalotumiwa kwa maana ya 'shika mwari ili asichukuliwe na somo mwingine au shika kitu kwa kingoe'. Katika kukoeka, mkoekwa hana hiari wala uhuru, na hili ndilo linalobainika ambapo msanii kwa muda wa mwaka mmoja aona kachezewa shere kubwa na kufanywa bwege. Pia kwajitokeza picha mzuri ya hilo.

Kwa muhtasari ni kuwa, mwandishi ameyajengea maneno yake mazingira mazuri ya matumizi ambamo mbali na kuafiki, yanafaa sana katika kuzalisha picha fulani zinazoleta uzito katika maendelezo ya ujumbe.

## 3:2:1:7 VIPASHIO VYA MSAMIATI

Kila neno hujengwa na mofimu mbalimbali ambazo zina umuhimu fulani katika uamili wao. Vipashio vingi vya maneno vi sawa katika ushairi kama vilivyo katika isimu. Licha ya uhuru wa kishairi wa kuchezea maumbo ya maneno, mabadiliko hayo hayaathiri maana za kimsingi za maneno. Pia kuchomekwa kwa mizani katika maneno hakupotoshi maana asilia za maneno.

Kupachikwa kihorera kwa vipashio hukwamiza, huzuia au huathiri nguvu za mawasiliano ya neno. Isitoshe, huchukiza yanapotamkwa. Kwa kupitia mashairi yote katika diwani hii, tumegundua kwamba, maneno yote yamejengwa kwa vipashio vizuri vinavyowezesha mawasiliano kutokea. Mifano ifuatayo yatuonyesha kuwa maneno mengi ni yale ambayo yamejengwa kwa vipashio sawa na vya lazima kwao kusudi yawasilishe maana. Nayo ni; hakuna, swabahi, ulimwenguni, haziko, dunia, liwavyo, kujiminginya, utapenyapenya, usifumwe, utwanzi, bahati, enyi, mlo, suhuba, kiri, dhara, moyo, maovu, fitina, maarufu, sayu, mbuyu na mengine.

Twaona kuwa zile mofimu huru kama maji, moyo, siri, hiari, dafu, macho na zingine zimetumiwa kwa wingi. Kuna pia mifano kadha ya mofimu tegemezi ambazo huhitaji kuambishwa vipashio zaidi ili kuleta maana. Mifano ya maneno hayo ni pamoja na; ujionapo, huioni, huihisi, useagiwa, uoneto, kuniletea, zimepituka, vikitashawari, hadhaminiki na mengine mengi. Kwa kulihakiki neno hili la mwisho, twagundua kwamba lina mofimu nne, na mizani tano.

| ha | dhamin | ik | i |
|---|---|---|---|
| I | I | I | I |
| Mofimu ya ukanushi | Mzizi | Kiambishi cha uwezekano wa kutendeka kitenzi | Kimalizio |

Mfano huo watuelekeza kwenye hali kwamba, ile misingi ya kiisimu ya uhakiki wa vipashio vya maneno haiepukiki hata katika ushairi na sanaa, kwani uamili wa kila kipashio hauepukiki katika kupata maana kamili ya neno. Uwezekano tu uliopo katika fasihi ni wa uingizaji wa vipashio visivyotarajiwa katika neno, ambavyo uamili wao hupatikana kwa kuvihusisha na vile vingine vinavyojulikana katika neno. Na matumizi haya zaidi hutokea katika maneno ya kilahaja kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

| | Neno | Muktadha |
|---|---|---|
| 17.6.3.5 | ’hashituka’ | kabla kucha sabahi, nakuona hashituka |
| 34.5.3.3 | ’halidumisha’ | Wala likuridhishalo, halidumisha muhibu |

Maneno ’hashituka’ na ’halidumisha’ yana kipashio ’ha’ ambacho kina uamili mkubwa katika kuleta maana. Ni kipashio kinachotumika badala ya ’na’. Kwa hivyo, vipashio vya maneno vilivyotumiwa humo kwa kiasi kikubwa vyasaidia maneno mengine katika kuwasilisha maana zao, japo kuna baadhi ambayo yanatatiza kidogo na ambayo kwa idili kidogo yatavumbuliwa yameundwa na viambajengo vipi. Kwa kiwango ridhishi, kuna matumizi mazuri ya vipashio vya leksia ambavyo havikuleta mkwamo wowote katika namna vilivyotumiwa ingawa baadhi vyavunja ule usafi wa semantiki kama inavyobainika katika mfano huu.

38.5.2 Ukaipanda mtama, mahindi na mabamia.

Tatizo lipo katika kipashio ’i’ cha neno mtama, lililopaswa kuwa mitama. Pengine ni kwa sababu za uchapishaji. Baadhi ya maneno yamekosa vipashio vyote lakini yamefanikiwa kuwasilisha. Mfano ni neno ’miujiza’ ambalo limeendelezwa kama ’mijuza’ katika 1.5.3.6. Kwa ufupi ni kuwa vipashio vimetumiwa vizuri bila kutatiza ujenzi wa maneno vilimotumiwa na uwezo wao wa kuwasilisha.

## 3:2:1:8 MPANGILIO WA MSAMIATI

Hapa tunamaanisha jinsi au namna maneno yalivyopangwa na kuunganishwa kisintaksia katika kuendeleza na kuleta maana pana ya tungo ambamo yametumiwa. Ni utaratibu wa kuyaweka maneno katika mpango maalum ambao unayawezesha kuwasilisha kama yalivyokusudiwa. Hili hufanywa kusudi ili kuyaepushia mkwamo

katika mawasiliano, ambayo ndiyo nia kuu ya kazi yoyote ya fasihi.

Ghalibu wahakiki wengi huangalia kama mpangilio wa maneno yaliyotumiwa umefuata kaida za kisarufi au la. Hili zaidi ni kwa wanasarufi, lakini katika ushairi, si lazima kaida hizo kufuatwa, madhali mpangilio wao uwasilishe. Ni kwa sababu hiyo hatuwezi kufungika tu kwenye umbo la neno, kuwa ndiko pekee mshairi ana uhuru wa kishairi. Uhuru huo huanzia kwenye kuchezea umbo la neno na kupanuka hadi kuchezea mpangilio wa maneno, yaani wa neno kwa neno au mahusiano ya maneno. Katika lugha isiyo ya ushairi ambamo kanuni za lugha hutawala, mpangilio wa maneno lazima ufuate taratibu maalum na pale zinapokiukwa, basi kasoro fulani hutokea za kisemantiki na hata kisintaksia. Lakini hilo linapotokea katika ushairi, huwa kama pambo. Hapa kunasisitizwa mawasiliano kwa ufundi mkubwa unaovutia, lakini mpangilio sio sana.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba, mpangilio mzuri wa maneno huvyaza wepesi katika mawasiliano. Kwa kurejelea diwani, kuna mifano kadhaa inayoonyesha kwamba msanii amewasilisha kwa kuyapangilia vizuri maneno yake. Hata hivyo kuna baadhi ya mifano yenye makosa ambayo pengine ni ya kiuchapishaji, au yanayotokea kimakusudi kwa sababu ya tabdilla na zile kaida za vina.

3.3.1 si kale si siku hizi, hili lanenwa ni watu.

Mpangilio wa maneno ni mzuri, isipokuwa tu katika kiunganishi 'ni' kilichotumiwa kimakosa. kilipaswa kuwa 'na'.

3.5.3 kaja kifa cha shangazi, hakutowa pesa tatu.

Kwa namna fulani neno tatu halikutumiwa mahali pake. Linajitenga sana na mengine likiharibu ule wizani, japo lawasilisha.

3.5.2 kuna kingine kikozi, asengenywa mwanagutu.

Kivumishi "kingine", chapaswa kisarufi kutokea baada ya nomino 'kikozi' ili kuleta msisitizo. Lakini hata namna kilivyotumiwa inakubalika. Kuna tabdilla ya 'kikosi' lililoendelezwa kama 'kikozi'. Mifano hiyo ni kama imelazimishwa ili kupata kina cha aina moja. Mifano ifuatayo ni ile ya mpangilio mzuri wa maneno.

| | |
|---|---|
| 15.5.1 | Ufanifu wa milele, kudumu huwa muhali |
| 29.5.1 | Uvumilizi ni ngome, kukuepushia chimbo |
| 56.4.1 | Shibe ya nguo kilemba, wa kale walivyonena |
| 79.10.1 | Udugu nyama ya tako, wanenavyo wa mwambao. |

Katika mifano hiyo yote kuna mpangilio mzuri sana wa kisemantiki, ambapo kila neno limeingia mahali pake. Hatuoni neno lolote lililotumiwa kimakosa. Yote yanafuatana kwa utaratibu usiovunja muwala. Mifano hiyo yatuthibitishia kuwa mpangilio wa maneno katika mashairi yaliyomo humo ni mzuri, unaofaa, kuleta maana na usiovunja mawasiliano.

## 3:2:1:9 NAMNA MSAMIATI ULIVYOUNDWA

Tumeiingiza mada hii kwa sababu ya ule uwezekano wa matumizi ya maneno mengi ya sanaa yaliyobadilishwa maumbo hasa kwa kuzingatia utendaji kazi wa uhuru wa kisanii. Hatukuangalia kwa kina njia zilizotumiwa katika kuunda msamiati uliotumiwa humo. Kimsingi ni kwamba maneno yote katika lugha yalibuniwa kwa misingi mbalimbali.

Tumeishughulikia mada hii katika njia inayofuata.

| Neno | Linakopatikana | Namna lilivyoundwa |
|---|---|---|
| Mafunda futu futu | 52.5.2.2-3 | Kwa njia ya tanakali sauti |
| Akatia vuyu vuyu | 51.7.2.4-5 | " " " " " |
| kuutukusatukusa | 21.9.3.3 | Takriri |
| Kuchupachupa | 11.2.24 | " |
| Chonde | 15.1.3.5 | Ufufuzi au uhafidhina |
| Nyia | 25.6.1.4 | " " " |
| Chajiyo | 20.9.3.3 | Akronimu |
| Mwinzako | 47.7.2.4 | Tabdilla |
| Hasimuyo | 19.4.3.2 | Inkisari |
| Dar-madari | 25.6.1.3 | utohozi |
| Sabaa | 38.4.1.6 | Mazida |
| Azaujati | 75.9.3.3 | Utohozi, uambishaji na unyambuaji |
| Jimbo-nambo | 24.9.3.4 | Uunganishaji |
| Nyingawanya | 13.5.1.5 | " |
| Jakamoyo | 19.5.2.3 | " |
| Mogo | 23.1.4.1 | Ukopaji toka kidigo |
| muhambo | 23.1.4.6 | " " " |
| Kidhaba | 32.3.4.3 | mkopo toka kiarabu na utohozi |
| Jisadi | 32.5.3.4. | " " " " " |

Msamiati uliotumiwa humo ni mwangavu licha ya hizo njia mbalimbali zilizotumiwa katika kuunda. Uundaji umechukua hadhari nyingi na hivyo haupotoshi maana na mawasiliano.

## 3:2:1:10 NJIA ZA UPANUZI MAANA KATIKA MSAMIATI NA ATHARI ZAO KATIKA TUNGO

Upanuzi wa maana katika msamiati ni usemi unaomaanisha kuongezeka kwa maana katika maneno. Hali hii huitwa na wengine upanuzi wa kisemantiki, na hutokea kwa sababu kadhaa. Kwanza hutokea pale ambapo maneno mawili au zaidi yanayotofautiana kimofolojia (kiumbo) na kufanana kimaana (kisemantiki) yanapotumiwa kwa pamoja katika mazingira sawa katika kupitisha ujumbe wa aina moja. Maneno fuatilizi katika matumizi hayo hukusudiwa kuyaongezea nguvu yale yaliyotangulia. Ifuatayo ni mifano.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 15.1.3 | Nilivyo ni pole pole, na chonde na tafadhali |
| 2. | 26.9.2 | Wasio ghera na ari, kuuondoa ukosefu |
| 3. | 36.1.3 | Ikakufika nanzaa, mwishowe ufedheheke |
| 4. | 6.1.3 | Na mengine ya karaha, ya vioja na vituko |
| 5. | 70.3.1 | Kasoro kama upofu, kukosa macho mawili |

Kwa muhtasari kuna matumizi ya maneno na visawe katika maneno hayo. Nayo ni: chonde na tafadhali, ghera na ari, nanzaa na ufedheheke, vioja na vituko, kasoro kama upofu na kukosa macho mawili. Visawe hivyo vimetokea kufafanua na kupimia uwezo wa maneno yanayovitanguliwa yenye ulingano navyo kisemantiki.

Upanuzi wa kisemantiki hutokea pia pale ambapo neno lililozoeleka katika matini fulani huondolewa pale na kutumiwa kuendeleza ujumbe katika matini mpya na tofauti kabisa na ile iliyozoeleka na hili hutokea sana katika sanaa. Ifuatayo ni mifano ya kuthibitisha usemi.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 34.6.1 | Huna moja ushikalo, likawa kwako ni twibu |
| 2. | 45.10.2 | Lilinitosha zamani, nyama kumla nyamawe |
| 3. | 64.4.2 | Kwa hilo usihadaiwe, ukachambachamba moto. |

Twibu ni msamiati wa kimatibabu na katika matumizi yake hapa, kuna uhamishi wa matumizi yake toka muktadha wa matibabu hadi wa mapenzi.

Nyama limetumiwa katika muktadha wa kutenda badala ya kutendwa. Nyama huliwa, lakini hapa twaiona ikila. Imepatiwa sifa za uwezo wa kutenda. Inavyochukuliwa ni kuwa sifa za neno zinapohamishwa toka matini moja hadi nyingine kuna upanuzi wake wa maana, ambapo matumizi yake hupanuka toka mazingira ya aina moja hadi nyingine.

Neno kuchamba hutumiwa kwa maana ya, 'osha utupu baada ya kwenda chooni' au 'tukana' au 'toa maneno mabaya', lakini katika muktadha huu lina maana ya kusafidi au kutakasa uovu wowote uliotokea.

Takriri inapotokea huwa kuna urudiaji wa kitendo ambapo badala ya kitendo kufanyika mara moja, huingia katika hali ya kutokea mara nyingi. Kupitia njia hii kuna upanuzi wa maana katika neno. Wakati mwingine hata ile maana huwa tofauti. Kwa mfano maana ya neno pole na polepole ni tofauti. Kutoka diwani tuna mifano hii

| | |
|---|---|
| 15.5.3 | Pale pale - ni tofauti na pale kimaana |
| 46.1.1 | akizaa zaa wako - ni tofauti na akizaa. |

Pale ni kivumishi cha umbali ulioko baina ya kitu na kingine, huku likipanuka kwa ukariri na kuwa palepale ambalo ni la msisitizo wa mahali na wakati. Kuzaazaa kunaonyesha namna ambavyo kuna dharau ya aina fulani katika maana pamoja na kuonyesha kuendelea kwa kitenzi chicho hicho - pana hali ya kufanya hivyo bila mpango. Ile heshima ya kuzaa inatoweka. Kwa hivyo takriri huchangia katika upanuzi wa kisemantiki wa maneno yaliyotumiwa.

Tanakali sauti ni mojawapo ya njia za upanuzi wa maana katika maneno. Upanuzi huo kimaana hutokea kwa sababu ya msisitizo unaotokea ambao hukosekana katika neno asilia au awali. Kwa mfano, neno bingiria na bingiria bingiri bingiri hayana uzito sawa kimaana, kwani mwigo huo wa kitendo unaotokea katika neno la nyuma huliongezea nguvu la awali. Yafuatayo ni matumizi ya aina hiyo.

27.6.2 Na kujifutuwa futu, kujitapa usikiwe
50.3.3 Hutia ugonganifu, wema huyayuka yayu

Vifungu vile vilivyokaririwa vyaonyesha namna kitendo kinavyofanyika. Pia vyasisitiza ujumbe. Vimetumiwa pia kutimiza kanuni za vina. Futu na yayu yatimiza kanuni za vina pale yalimotumiwa. Mifano kama hii ni mingi katika diwani huku ikitimiza kazi nzuri sana.

Matumizi ya maneno ya kawaida kwa njia zisizo za kawaida hupanua maana zao. Hapa neno huhamishwa toka muktadha wa kawaida hadi mwingine. Ufuatao ni mfano.
20.9.3 Hilo ni pendo chajiyo, halifai lapupusa.

Hapa, mbali na kulinganisha pendo na chajiyo, na kulipa sifa za kupeperuka, tumesawiriwa mazingira ya mawezekano ya maneno kutumiwa kisanii katika matini nyingi huku yakitumiwa kwa maana nyingi, badala ya kuwa na neno moja maalum katika kila matini. Hili latuelekeza kwenya ile sifa ya uekevu katika matumizi ya maneno. Hizo na njia zingine ndizo zilizotumiwa humo katika kupanulia maneno maana. Kuna kuingiliana kwa mada hizi ndogo, na hivyo baadhi ya njia za upanuzi kimaana zimeangaliwa katika sehemu za uwezo wa msamiati na baadhi katika aina ya msamiati.

## 3:2:1:11 UANGAVU NA UTATA KATIKA MAANA ZA MSAMIATI

Uangavu ni hali ambayo inamwezesha msomaji kupata maana halisi ya neno au mwelekeo wa uhakika wa kupata maana iliyokusudiwa. Kinyume chake ni utata, ambapo maneno hutumiwa kwa njia isiyo rahisi kupata maana iliyokusudiwa. Hili hutokea pale neno lenye maana nyingi linapotumiwa katika mazingira ya kiujumla au mchanganyiko na inakuwa si rahisi kupata hata mwelekeo wa kilichokusudiwa. Kwa hivyo, utata hutokea pale msanii anapotumia msamiati wenye maana nyingi katika muktadha usiofahamika au katika mazingira yasiyopambanua maana ya msamiati uliotumiwa. Pia inatokea msanii anapotumia msamiati wa kawaida kimafumbo mpaka inakuwa si rahisi kutambua alichokusudia na hivyo kunajitokeza fasiri nyingi. Hili hutokea pale wasanii wasipotaka kutaja vitu kwa uwazi ambao utakera, udhi au chukiza.

Msamiati mwingi uliotumiwa ni wenye uangavu kimaana. Ni mifano haba sana inayokanganya kimaana kama huu ufuatao. Neno mogo lina maana ya siku saba za juma (fungate) na muhambo ni mtego, lakini katika matumizi haya: "Mogo utajuwa mogo, mogo ujuwe muhambo" ni nini kilichokusudiwa? Neno hilo limetumiwa kwa njia ya fumbo tata na kwa msomi wa chini au kadiri itakuwa shida sana kupata

kilichokusudiwa. Mifano ya aina hii si mingi.

Msanii ametumia maneno ya utata lakini katika mazingira ambamo kupata maana zao inakuwa ni rahisi ama ambapo kuna mwelekeo wa kupata maana zao. Kwa sababu hii, hakutokei ugumu wa kupata maana maalum zilizokusudiwa katika tungo na hili ndilo linalosisitizwa sana na nadharia ya urasimu, kwamba tungo zisiwe na utata unaowafanya wasomaji kujitokeza na fasiri mbalimbali zilizo kinyume, na alivyonuia msanii.

### 3:2:1:12 WIZANI KIMAANA

Hapa tunamaanisha yale mapigo yanayotokea katika muungano au mahusiano ya maana za maneno yaliyopangiliwa vyema. Ni mapigo yaliyo matokeo ya mpangilio mzuri wa maneno kisintaksia. Hili hutokea pale panaposhuhudiwa upokezano wa maana kwa njia inayoleta mapigo fulani katika mahusiano ya maneno yaliyotumiwa katika tungo. Mfano ufuatao unathibitisha haya.

42.1

Halei mwana wa mume, mama wa kambo si mama
Moyo'we ni gumegume, wivu unavyomchoma
Amkalia kinyume, ingawa mwanayatima
Mama wa kambo si mama, halei mwana wa mume

Katika mfano huu kuna upokezano wa kisemantiki unaofuata utaratibu huu. Halei mwana wa mume -> mama wa kambao si mama -> moyo wake una dharau inayosababishwa na wivu -> Anamtaabisha mwanayatima -> kwa hivyo mama wa kambo si mama -> halei mwana wa mume. Upokezano wa mawazo unatokea kwa namna fulani yenye wizani (ridhimu) kwa sababu ya mpangilio mzuri.

### 3:2:1:13 JINSI(AINA) MBALIMBALI ZA MAANA

Kimsingi kuna aina mbili za maana - zile halisi (asilia, tambuzi) na zile nasibishi. Wanafasihi wengi husisitiza matumizi ya minasibisho mingi kisanii katika kuziboresha tungo na katika kuimarisha lugha ya kisanii. Katika kiwango hiki, maneno huhamishiwa sifa zao tambuzi na kuchukua sifa mpya. Sifa hizi huwa za maana wala si za kifonojia na mofolojia. Kwa hivyo hali hii inajitokeza katika kiwango cha kisemantiki. Viwango vyote vyadhihirika katika diwani. Ifuatayo ni mifano ya kiwango cha maana halisi.

| | | |
|---|---|---|
| 1, | 15.1.2 | Ndiyo yangu maumbile, yasiyogeuka hali |
| 2. | 15.4.1 | Watu hufumba kisiri, maneno ya kusanifu |
| 3. | 33.7.2 | Imani sasa ni haba, nyuso hazitahayari |
| 4. | 70.2.1 | Kasoro ni uumbufu, kuumbuka uasili |

Mifano hiyo na mingine yatuthibitisha kuwepo kwa maana halisi[4] katika msamiati. Ifuatayo ni mifano ya maana nasibishi.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 36.3.1 | Ukijipamba tamaa, yakuhimizi utake |
| 2. | 36.5.1 | Ikithiripo tamaa, maarifa hwenda zake |
| 3. | 63.8.3 | Sitie moyo fikicho, ukajipa usalile |
| 4. | 64.4.2 | Kwa hilo usihadawe, ukachambachamba moto |

Mfano wa kwanza watupa sifa tofauti za tamaa - sifa ya kuvaliwa kama kwamba i pambo. Wa pili, watupa sifa za maarifa kumiliki na, kwenda zake tamaa inapozidi. Wa tatu twaona moyo ukififikichwa kama macho, kama kwamba wafikika kwa mikono. Wa nne watupa picha ya moto kuchamba. Nasibishi zina uwezo mkubwa sana kihemshi (emotionally) kama inavyobainika katika mifano hiyo. Mifano hiyo yatudhihirishia mchango wa minasibisho katika sanaa ambapo husaidia katika uwasilishaji mzuri, hupamba maana, huongezea ladha maana zilizozoeleka ambazo ni tambuzi na kujenga picha fulani zinazofurahisha na kuleta uchangamfu fulani katika tafakari za wasomaji. Minasibisho zaidi hujitokeza kwa njia ya vitendawili, nahau, mafumbo na methali.

## 3:2:1:14 TATHMINI YA UHURU WA KISHAIRI

Uhuru wa kishairi umetumiwa vizuri katika viwango vyote. Katika kiwango cha kutumia msamiati wa kale, msanii amefanya hivyo bila ya kupotosha au kuyatumia visivyo maneno aliyoyafufua kimatumizi. Mifano miwili ifuatayo imetufaa sana.

| | |
|---|---|
| 25.6.1.4 | Tungo za dar-madari, nyia ziso uchokefu |
| 15.1.3.5 | Nilivyo ni polepole, na chonde na tafadhali |

Katika mifano hiyo kumetumiwa maneno 'nyia' na 'chonde' ambayo ni ya kizamani, kwa namna inayoyaingiza kiutendaji vizuri na mengine, ambapo huenda hata baadhi ya wasomaji wasitambue kwamba maneno haya ni ya kale. Hili latuthibitishia kuwa kuna, matumizi mazuri ya msamiati wa kale bila ya kukoroga ule mvuto wa tungo.

Uhuru huo hupanuka hadi matumizi mazuri ya tamathali za usemi. Kuna ushahidi tayari kwamba msanii ametumia tamathali kadha za usemi kwa viwango mbalimbali. Kwa sababu hili limeshughulikiwa kama kipengele huru katika sehemu ya 3.2.4, hapa tumetoa tu mfano mmoja, na kisha kuonyesha namna ulivyotokea.

| | |
|---|---|
| 15.5.1 | ufanifu wa milele, kudumu huwa muhali. |
| 15.6.3 | Dunia ni magaule, mchana huwa laili. |

Hayo ni matumizi ya tamathali ya tanakuzi ambayo yanatokea kwa uzuri, katika kuboresha na kuimarisha nguvu za lugha ya kawaida.

Uhuru huo pia unatokea katika kiwango cha kisemantiki, ambapo msanii aruhusiwa kwa njia ya kinasibishi au kitamathali kulipanulia neno maana kama ilivyokwishaangaliwa katika mada ndogo za nyuma. Uhuru huo umetumiwa kwa uzuri.

Uhuru katika kiwango cha sintaksia nao umetokea kwa uzuri, ambapo kama tulivyoona msamiati umepangiliwa vizuri kwa namna isiyoghairi kaida za kisintaksia.

Msanii pia ametumia vizuri uhuru wa kutumia vina apendavyo, ambapo katika diwani hii ametumia zaidi ya vina 53 tofauti tofauti na kwa njia inayoridhisha.

Katika kiwango cha mofolojia, uhuru wa tabdilla, Inkisari na mazidadi wabainika kama inavyodhihirika katika mifano hii.

| | |
|---|---|
| 17.1.1.1 | Mwinzio badala ya mwenzio - tabdilla |
| 17.1.3.2 | 'mekujuruhi - elishia[5] -> ya amekujeruhi. Pia kuna tabdilla - ambapo badala ya mekujeruhi tuna 'mekujuruhi.<br>- Kuna pia inkisari ambapo limekatwa kama alama hiyo ya ritifaa inavyoonyesha. |
| 66.4.3.1 | Maadhali - Badala ya madhali. Hii ni mazida |

Kwa ufupi ni kuwa uhuru wa kishairi katika kiwango cha mofolojia umetumiwa vizuri kwa njia ambayo haipotoshi. Kwa sababu hizo twahitimisha kwa usemi kuwa, uhuru wa kishairi umetumiwa humo kwa njia ya kuboresha tungo kama ilivyobainika na kabisa haukupotosha hata kidogo. Wasanii wote wapaswa kufanya hivyo ili kuwaondolea mkwamo unaowabana sana kwa sababu ya kufuata kaida kali.

## 3:2:3 KIWANGO CHA LUGHA ILIYOTUMIWA

Kuna viwango vipatavyo vitatu hivi vya matumizi ya lugha, ambavyo ni vya urasimu[6], umitaa[7] na usimo[8]. Kwa kupitia tungo zote humo, tumetambua tu matumizi ya urasimu ambapo msamiati wa viwango hivyo vingine umeepukwa japo wadhihirika katika mifano hii haba ifuatayo.

| | |
|---|---|
| 25.2.2 | mtunzi hawi hodari, atungae mbovu wafu |
| 41.8.1 | Vimalenga vya kikungu, acha vipige kelele |
| 43.9.2 | Humvalisha viteme, viguo vichamachama |
| 59.7.3 | Mbali hiyo mishikaki, na manyama ya kidari |

Kwa madhihirisho haya, msamiati mwingi uliotumiwa ni ule wa kiwango cha urasimu.

## 3:2:4 TAMATHALI ZA USEMI

## TAMATHALI ZA USEMI ZA ZINDUNA

### NJOZI

Kumetumiwa tamathali hii kwa wingi kwa njia ambazo zinaridhisha na kuweka wazi ujumbe katika nia ya kuufanya ueleweke bila vizuizi. Beti zifuatazo zatupa matumizi ya tamathali hii.

17.3

Katu sijakusafihi, neno ovu kutamka
Wala sijakukebehi, hadhi yako kupunguka
Daima nakustahi, na kwa hilo sitachoka
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

Mfano huo wamdhukurisha msanii kuhusu yaliyotokea katika uhusiano wao ambapo aona maono ya kidhana yaliyotokea, yanayofaa kufutwa. Pia kwa kuyaangalia kwa uzuri yampa msukumo wa kumwahidi na kumhakikishia kuwa, lau kuna kosa lililotokea, basi halitatokea kamwe. Hakikisho hilo analitoa kwa kinjozi katika ubeti wa nne, ambao umeendelezwa hivi:

17.4

Nakuapia wallahi, sitatenda yote miaka
Kitendo wala shabihi, kabisa hakitafika
Mwandani wangu furahi, zungumza na kucheka
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

Ubeti huo unathibitisha maono ya msanii ya mahusiano shadidi katika wakati wa mustakabali. Wa tano wafuatilia kwa hakikisho hilo hilo. Asema hivi katika wa tano.

17.5

Ewe huri mastuhi, mzuri uloumbika
Ndiwe yangu iftahi, mwingine hatopatika
Iwapo hutanabahi, tambua nitadhurika
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

Kuna mawazo na maono ya kinjozi kwamba hatopatikana mwingine kama huyo mpenzi wake. Mbinu hii hutoa chembechembe za kiutabiri ambazo ni muhimu katika kumpa msomaji mwelekeo wa yanayotazamiwa kutokea katika kipindi kijacho. Kuna mifano mingi ya aina hiyo, lakini huo tulioutoa watupa mwangaza wa aina za tamathali za kinjozi zilizotumiwa na msanii.

## TAMATHALI ZA USEMI ZA MWIGO SAUTI
## TANAKALI SAUTI

Mshairi ametumia tanakali sauti katika diwani hii kwa wingi na kwa njia ambayo kisanii inavutia kama baadhi ya mifano inavyothibitisha. Ifuatayo ni mifano.

3.2.2. Nataka hizi tatizi, sitatuke tatu-tatu
26.8.1 Iwe kakara kikiri, kama mende na siafu
27.8.1 Na kujifutuwa futu, kujitapa usikiwe
50.3.3 Hutia ugonganifu, wema huyavuka vavu
51.7.2 Hulitwaa neno ng'wafu, akatia vuvu vuvu

| | |
|---|---|
| 52.5.2 | Na mafunda futu futu, hajibu hata utajo |
| 52.6.1 | Moyo hufyatuka fyatu, ukaogopa mfujo |
| 76.5.2 | Kwa mikono hujikinga, kwenda bingiri bingiri |

Tanakali hizo zimetumiwa kwa uzuri sana ambapo zinaleta ridhimu fulani kimapigo. Pia zatupa picha ya kufanyika kitendo; ni kama kuonyesha unyoofu fulani katika kufanyika kwa kitendo. Kwa mfano, kuyayuka yayu, fyatuka fyatu na mifano mingine yatupa picha ya namna vitendo vinavyotokea. Pia imetumika kutimiza vina. Mifano ya aina hiyo ni; hufyatuka fyatu, tia vuyu vuyu, mafunda futufutu na kadhalika. Mifano hiyo pia inaleta mapigo imara katika mahusiano ya kisemantiki. Matumizi yao huwawezesha wasanii kujiundia vina zaidi wanavyovitaka badala ya kutegemea tu kuchota msamiati wao wote toka lugha ya kawaida.

## TAMATHALI ZA USEMI ZINAZOLINGANISHA TABIA
## TASHBIHA

Kuna matumizi ya tashbiha nyingi katika miktadha na matini tofautitofauti. Licha ya kutumiwa kuwasilisha mawazo tofautitofauti, takriban zote zimetumiwa kama inavyopaswa.

Mifano ya aina hii imo katika, 2.11.2, 3.6.2, 9.2.1, 9.2.2, 9.6.2, 13.6.1, 15.1-9.4, 19.3.3, 22.9.2, 22.10.2, 22.10.4, 25.4.2, 27.4.1, 32.3.1, 32.6.1, 44.1.3, 44.3.2, 49.8.2, 54.6.2, 60.4.2, 60.6.2, 66.3.1, 50.4.1, 66.4.2, 66.5.1, 70.3.1, 72.2.2, 72.3.1, 72.5.1, 76.4.2, 76.6.3, 76.5.3, 77.7.4, 77.9.1, 77.9.2. Ile ambayo tumeiangalia katika kutathmini nafasi yao katika kuboresha tungo ni ifuatayo.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 17.6.2 | Hunijia kama rihi, pepo za kupambazuka |
| 2. | 22.10.2 | Nasimama kama mbogo, pembe naziweka wima |
| 3. | 32.3.1 | Suhuba kama mkoba, cha ndani kukisitiri |
| 4. | 29.4.3 | Majuto hayana mume, kama mshipi na chambo |
| 5. | 26.8.1 | Iwe kikiri kakara, kama mende na siafu |
| 6. | 41.4.3 | Mtazame mtazame, sura yake kama kima |
| 7. | 72.5.2 | Upanukao sadiri, matiti kama turusi |

Baadhi ya tashbiha hizi zinafafanua vitenzi kwa kutoa picha nzuri za namna vinavyotokea. Picha ambayo inajengeka katika mfano wa kwanza yamfanya msomaji kunusa ile harufu nzuri ya pepo za kupambazuka. Kuna picha ya mbogo na pembe zake zilizotegwa - ikiashiria zile nguvu zake na hatari za mishomo ya pembe zake. Twaona sifa za mapenzi za kuficha kabisa mambo yake kama mkoba unavyositiri kilichomo. Kwa ufupi ni kuwa, mbali na kutuwezesha kupata picha za vitenzi kwa uzuri, huwawezesha wasanii kutimiza kaida za vina. Kuna upambanufu wa vitenzi ambavyo vyaelezwa kwa njia inayomwezesha msomaji kupata picha kamili ya kinachoelezewa. Huleta madoido fulani katika matumizi ya lugha kama inavyodhihirika katika mfano huu wa: "Upanukao sadiri, matiti kama turusi". Hata pale kitu cha kulinganishwa na kingine kisipofahamika, kuna maneno yanayompa

msomaji mwelekeo. Kwa mfano, hata iwe msomaji hajui turusi ni nini, upanufu wa sadiri unaohusisha matiti, unampa mwelekeo wa kinachokusudiwa. Kwa ufupi ni kuwa, msanii ametumia tashbiha zenye uzito na zinazowafiki katika matini ambamo zimetumiwa.

## SITIARI

Msanii ametumia sitiari hai nyingi ambazo zina uwezo mkubwa sana wa kuwasilisha. Ameepuka sana kwa kiasi kikubwa sitiari fifi.

Matumizi yake yamo katika, 11-12.1-7.4, 15.5.2, 27.6.1, 29.6.1, 29.6.2, 40.5.2, 46-47.1-10.4, 46.2.1, 48.2.1, 50.1.1, 52.1.1, 57.9.1, 57.9.2, 62.4.3, 64.5.3, 21.4.2, 72.5.1, na kadhalika. Ifuatayo ndiyo mifano tuliyoiangalia katika jitihada ya kutathmini matumizi yao.

| | |
|---|---|
| 24.7.2 | Jino la fisi ni sago, la gwase ni msirimbo |
| 29.5.1 | Uvumilizi ni ngome, kukuepushia chimbo |
| 40.2.1 | Naswi twaona uchungu, kuwa ngao ipotele |
| 43.10.3 | Mama wa kambo ni ndeme, mwenzenu yalinikoma |
| 77.7.4 | Miguu kama mzinga, vidole ni misumari |

Mifano hiyo yatuwezesha kuona kwa uzuri picha za tunayoelezwa. Nomino na vitenzi vyapambanuka vizuri kiasi cha kutuwezesha kuhisi, na kuona yanayoelezwa. Pia imetumiwa vizuri kutekeleza kanuni za vina. Ni maelezo yenye nguvu, yanayopiga hatua ya kina kuliko yale ya lugha ya kawaida. Msanii ameitumia kwa mvuto wa ajabu katika baadhi ya mashairi, kama inavyodhirika katika mifano hiyo hapo juu.

## LAKABU

Mifano ya lakabu katika diwani hii si mingi, na hiyo michache iliyotumiwa yatokea vizuri. Ufuatao ni mfano 40.5

Shuara na kazi yangu, natambaa pole pole
Anga limetanda wingu, na silaha pale pale
Nitawatia kizungu, wasijuwane makele
Mawazo nakupa pole, pole sana ndugu yangu.

Lakabu huwa muhimu katika kuwatambulisha wasanii hasa washairi. Katika ushairi, majina ya lakabu huchangia katika utimizwaji wa kanuni za vina na mizani kwa wanamapokeo. Kutoka mfano huo twaona kuwa 'shuara' lina mizani tatu na lau angetumia mojawapo la majina yake moja kwa moja, mizani ingepungua ama kuongezeka.

Msanii amejipa lakabu ya 'Ustadh Shuara' ambayo ina maana ya mshairi anayelenga kufikia kileleta cha utunzi, kiwango cha juu kabisa cha tungo zake. Hii ni sifa ya kitunzi. Swali ni je, lakabu yiyo hiyo yamulikika katika kazi? Ina uhusiano wa moja kwa moja na tungo? Jibu ni kuwa kuna ushahidi wa ubora wa tungo kama

inavyotuashiria lakabu. Kuna uhusiano wa moja kwa moja na tungo, ambapo twaona tungo nzuri na zenye mvuto, ingawa hili hubainika kwa uzuri zaidi katika mazingira ya ulinganishi. Mshairi ayafungisha matumizi yake ya lakabu kwa yale mambo anayoyashughulikia - yaani utunzi na nia za kiutunzi.

## TASHIHISI

Tashihisi zilizotumiwa humo sio nyingi sana. Zote hizo zimetumiwa kwa mwelekeo wa aina moja katika mkondo ambao ni wa aina moja. Wa aina moja kwa sababu wahusika husishwa wamevishwa sifa za uhai zisizo zao kabisa. Ifuatayo ni mifano, ambayo imo katika, 60.6.2, 45.10.1, 4.7.2, 1.1-12.4, 1.5.2, 25.5.3. Ifuatayo ni mifano zaidi.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 26.7.1 | Kweli ina msumari, yauma ndani ya pafu |
| 2. | 36.2.1 | Tamaa ina hadaa, yakwacha usitosheke |
| 3. | 30.5.3 | Mambo yote yatakuwa, wala hayatasinzia |

Sifa ya kuvipatia vitu wasifu usio wao kama ilivyo hapa hufaa katika upanuzi wa kisemantiki, (pana matumizi zaidi nje ya mipaka asilia), ambapo sifa zisizo zao huhusishwa navyo, hali inayoviwezesha kuingia katika matini na miktadha isiyo yao asilia. Matumizi haya kisanii hufaa sana katika kuleta hali isiyohalisi (defamiliarization), sifa ambayo inawawezesha wasomaji kuitazama kazi ya sanaa kwa jicho tofauti na la kawaida, ambapo sasa inatazamwa kwa uzingativu zaidi. Inapokelewa kwa nadhari na uzito. Kwa mfano, katika mfano wa kwanza, twaona na kuaminishwa kuwa kweli, ukweli una uwezo wa kumiliki na kuwa na msumari na pia kuuma pafu kama kwamba una meno ya kuyang'wafulia mapafu.

Katika mfano wa pili, twaona na kuvutwa kwa picha ya tamaa kudanganya, na katika wa tatu kuna picha ya usinzivu wa mambo. Matumizi haya ambayo ni ya kuuhuisha vitendo au vitu kwa sifa ziso zao huleta uimarifu fulani kisemantiki. Kuna picha zinazojengeka na za nguvu. Kwa mfano picha ile ya mambo kusinzia yatokea kwa uzuri. Kuna upanuzi kimaana katika neno usinzivu ambalo latumiwa nje ya muktadha wake halisi na hii ndiyo sifa mojawapo ya kisanii ya kuiondolea lugha ya kawaida upungufu. Ni mbinu iliyotimia kimatumizi katika diwani hii ambapo mbali na kutupa mawezekano ya sifa hizo, yatuaminisha kuwa zipo au zatokea kupitia uhaishaji huo.

## TAASHIRA

Kuna mifano ya matumizi ya mbinu hii katika diwani. Katika ukurasa wa kwanza, kuna ishara mbili za maji zinazotegemea mazingira ambamo yamo. Ya kwanza ni ya utulivu, yanapokuwa kisimani au bombani, na ya pili ni ya kutokota yanapokuwa katika sufuria au chungu kilichoinjikwa mekoni juu ya moto, hali ambayo inaashiria kuwa yamefikia kiwango cha kuweza kupikiwa. Fasiri ya maji yahamishika hadi mazingira ya mahaba, ambamo tabia ya msichana hubadilika katika nyakati mbalimbali na katika mazingira mbalimbali. Kwa mfano, pale avunjapo ungo, huchukulika kuwa sasa aweza kuolewa. Inaashiria kupevuka na kukomaa na hivyo si vibaya kuolewa baada ya hapo.

Katika shairi "moyo" mshairi autumia kitasihimu (kama sehemu ya mwili - ukiwakilisha mwili wote) katika kuonyea mwili mzima, unaoashiria uwakilishi wa watu. Moyo umetumiwa kuashiria watu, na pale unapotajwa tu, ishara za jisadi (kiwiliwili) cha mtu hujitokeza na matendo yake.

Taashira hufaa sana katika kuleta karibu mawazo ya wasomaji ambao huenda wakatafakari sana vitu wasivyovielewa vinapotumiwa. Aina ya wahusika aliowatumia kiishara msanii wanaaminika, na si wageni katika mazingira ya hadhira aliyoikusudia na hili linachangia katika kuziwezesha tungo zenye matumizi hayo kueleweka kwa njia nzuri zaidi.

## TAMATHALI ZA USEMI ZA MSISITIZO

### TAKRIRI

Mifano ya takriri irabu na konsonanti

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 9.2.1 | Wambapo yule yu ovyo, ovyo-ovyo kama kumbi -> kumekaririwa o, vy - ukariri huu ni muhimu katika uhakiki wa vipashio vya kimofolojia ambavyo ni muhimu katika kuleta uzito katika mapigo ya kisemantiki, kama inavyodhihirika katika neno ovyo. Kuna msisitizo wa kisemantiki, wa ukosaji manufaa kabisa katika huyo mhusika twezwa. |
| 2. | 9.6.1 | Dunia ni vivyo hivyo, mfano dau na wimbi |
| 3, | 42.6.1 | Mwana heshi tumetume, hujiweka nyumanyuma |

Mfano wa pili unasisitiza mkao na hali ya dunia huku wa tatu ukisisitiza hali ya kutumwatumwa kwa mwana wa mume na mama wa kambo. Urudiaji huo wa vipashio vya irabu na konsonanti huleta msisitizo fulani wa kisemantiki katika mazingira ambamo hutokea.

Takriri Neno

Mifano ifuatayo ni ya ukariri wa neno

| | |
|---|---|
| 13.6.2.7 | Na kuno kuna cha pili, wamba utapenyapenya |
| 15.5.3.3 | Yakawa ya pale pale, hadithi na taawili |
| 59.7.1.6 | Chakula hiki na hiki, tena kizuri kizuri |

Urudiaji wa maneno pale, hiki, penya na kizuri unaleta msukumo wenye nguvu kisemantiki, ambapo kunatokea msisitizo wenye nguvu za kisemantiki. kunajengeka kwa mfano picha isiyoisha kama pale tunapoambiwa kizuri. Kuna uzito katika urudiaji huo ambapo uzito wa kizuri ni pungufu ukilinganishwa na wa 'kizurizuri'.

Takriri ya Kitenzi kwa kitenzi

Mifano

| | |
|---|---|
| 1.2.2 | Aula pale bombani. Kufunga na kufunguka |
| 63.7.1 | Shikilia ushikacho, sipapatishe kelele |
| 63.7.2 | Kipende kikupendacho, ulicho nacho kiole |

Katika mfano wa kwanza kuna kitendo katika ukamilifu wake - katika kufanyika kwake na kinyume chake. Takriri hiyo inasisitiza kitendo katika hali zote - kwamba maji yatakapokuwa bombani yakifungiwa au yakifunguliwa hali itakuwa sawa - yatabaki tulivu. Mfano wa pili ni wa takriri himizi, ambayo inamwuliza mtu kuendelea kudhibiti alichowahi kushika. Wa tatu unakariri upokevu na upokezi wa kitendo chicho hicho, hivyo kuna aina fulani ya msisitizo.

Takriri ya Nomino na kitenzi

Mifano

| | |
|---|---|
| 21.3.1 | Kaufanya mchanjago. Mchama wa chamachama |
| 44.6.1 | Mgumba huwafitini, mzazi na uzaziwe |
| 58.3.3 | Uonywapo huonyeki, kisha wazidi kiburi |

Ukariri katika mfano wa kwanza umetokea kuonyesha ukosefu wa usitaji katika kitendo, huku wa pili ukiiweka nomino katika utendaji kazi wake na katika mazingira yake halisi. Wa tatu watupa picha ya kukosa usitaji katika kitendo licha ya juhudi za kufanya hivyo. Kuna usisitizaji katika uendeaji wa kitenzi. Kwa kiasi fulani, matendo ya nomino yamewekewa mipaka, ambapo kinachoashiriwa tu, ni kile kinachofungamana na mtenda au nomino tenda. Hapa kitenzi kinasisitiza yanayotendwa na nomino.

Takriri ya kitenzi na Nomino

Mifano

| | |
|---|---|
| 1.6.1 | Sinambie kwa kudhani, dhana haina hakika |
| 15.3.2 | Usitake awe vile, kumithilisha mithali |
| 25.6.3 | Ndizo tungo za khatri, zikinyowa nyonyo pofu |
| 36.1.1 | Itamaushe tamaa, mpaka itamauke |
| 40.1.3 | Jamii ya walimwengu, hapatasaa kisale |

Mifano yote hiyo, inaonyesha kuwa nomino ndiyo inayopokea kitendo - ndiyo inayotendwa na hapa twapata sifa dhahanifu zilizochorwa kama zilizo za kweli. Hapa msisitizo huko kwenye kitenzi, kinyume na mifano awali ambapo msisitizo ulikuwa katika nomino.

Takriri Mshororo

Mifano

| | |
|---|---|
| 15.1&2.4&1 | Akili ni kama nywele, hakuna aso akili |
| 19.4&5.4&1 | Viwili katika moyo, kuviweka vyanitasa |
| 23.2&3.4&1 | Mogo utajuwa mogo, mogo ujuwe muhambo |
| 54.1&2.4&1 | Cha bure hakiwi tamu, ila wambiwe sogea |
| 62.1&2.4&1 | Muiza kiwi hanacho, na chema kimpotele |
| 64.2&3.4&1 | Kikande nyumbaye mawe, aliepake mzito. |

Mishororo hiyo imekaririwa ili kuondoa ule mkwamo katika mtiririko wa ujumbe husika katika muktadha huu. Pili umetokea ili kusisitiza ujumbe kwa kuupokeza kutoka ubeti mmoja hadi mwingine kwa maneno yale yale. Tatu, matumizi hayo yametokea, kama inavyoelekea, pale mwandishi alipokosa uteuzi muafaka zaidi wa maneno ya kuanzishia ubeti mpya bila kukoroga ile ridhimu ya muwala wa habari.

Takriri kibwagizo

Kuna mifano zaidi ya 30 ya aina hii, nasi tumechagua tu mitatu kutathminia matumizi yake katika diwani.

| | |
|---|---|
| 3&4.1-9.4 | Baina utu na kitu, kipi bora waamuzi |
| 17-18.1-7.4 | Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi |
| 29.1-6.4 | Juta kabla ya jambo, usije juta kinyume |

Ukariri wao umetokea, kwanza katika kuonyesha kuwa msanii anazungumzia maudhui ya aina moja. Pili, ni kusisitiza ujumbe na kuonyesha kuwa kibwagizo ndicho chahimili maana kuu ya tungo.

Takriri Muundo

Kumekaririwa muundo wa tarbia katika beti zote na mashairi yote. Pia umbo la kimathnawi la ukwapi na utao limekaririwa katika mashairi yote. Mkondo wa 8x8 umekaririwa katika tungo zote. Umuhimu wa ukariri huu wa muundo ni kuonyesha kuwa, msanii ana uwezo kisanii wa kuweza kudumisha umbo moja, na ambalo ni rahisi kukaririka katika kujikumbusha ujumbe.

Takriri Vina

Katika mashairi mengi diwanini, vina vya ubeti wa kwanza hukaririwa hadi wa mwisho. Baadhi ya vina vilivyokaririwa ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30.1 | 32.1 | 34.1 | Maumbo haya yote |
| wa ia | ba ri | lo bu | yamekaririwa toka |
| wa ia | ba ri | lo bu | ubeti wa kwanza hadi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| wa ia | ba ri | lo bu | wa mwisho pale yanapotokea |
| wa ia | ba ri | bu lo | |

Ni katika shairi irabu tatu tu, ambapo ukariri umetokea katika baadhi ya beti tu!

Ukariri wa vina katika tungo kama ulivyotokea waonyesha tu kimsingi kwamba msanii amejimudu kisanii kwa kudumisha kina kile kile. Kuna baadhi ya watunzi ambao hukaukwa na msamiati utakaowapa aina ile ya kina walichonacho. Ukariri huu ni ishara ya msanii kuimudu lugha siyo kileksia tu, bali katika matumizi yake yote kama ilivyokwishadhihirishwa na mifano kwingineko.

## TANAKUZI

Tamathali hii imetumiwa katika 8.7.1, 9.2.3, 9.5.1, 15.6.3, 21.4.2, 62.6.1 na mingine. Ifuatayo ndiyo tumeihakiki.

| | |
|---|---|
| 7.2.1 | Mazuri yenye furaha, ni yale ya maudhiko |
| 15.5.1 | Ufanifu wa milele, kudumu huwa muhali |
| 8.8.1-3 | Mwema atakudhabihu, akitwae kilichoko |
| | Akuache majuruhu, akajisifu endako |
| | Na mbele ya madhabahu, akakane hakuwako |

Msanii ameitumia mbinu hii kwa njia ambayo inasisitiza ujumbe kwa mawezekano ya ukweli au yanayokuja kwa kinyume au mkinzano fulani. Kwa mfano, pale anapotuambia kwamba yale mazuri yanayofurahisha ndiyo yanayoudhi, anatupa mawezekano kwamba hali haiwi moja tu. Kwa ufupi ni mbinu inayotupa msisitizo kwa kutoa ukinzano. Katika mfano wa tatu, atupa mawezekano ya maovu ya mwema na kutupa picha ya kuwa kila jambo lina kinyume chake, na halina sifa tu ya aina moja. Matumizi hayo yametokea katika mazingira ambayo yanaongezea uzito lugha iliyotumiwa.

## TABAINI

Matumizi ya kunga hii si mengi sana na yale machache yanayotokea, yanatokea kwa namna inaonyesha kuwa, msanii ameyamudu. Baadhi ya mifano iko katika 15.4.2, 40.1.1, 52.4.3. Ifuatayo ni ile tuliyoiangalia.

| | |
|---|---|
| 3.3.1 | Si kale si siku hizi, hili lanenwa ni watu |
| 47.7.1 | Si wako baba si wako, mwana wa mke yu moto |
| 54.6.1 | Cha bure katu si tamu, si tamu kukunyegea |
| 76.2.1 | Si uchawi si uganga, Vitabu wala tunguri |
| 25.1.3 | Si miski si ambari, si wardi ah si afu |

Kuna mvuto katika ukanushi huo uliosisitizwa ambao waonyesha msisitizo ulio kinyume na matarajio ya wahusika lengwa. Msanii ameitumia vizuri.

## NIDAA

Mwandishi ameitumia mbinu hii kwa wingi kwa namna inayoonyesha kuwa ameimudu katika kuwasilisha kama alivyonuia. Baadhi ya mifano imo katika, 9-10.1-7.4, 78.4.2, 35.7.4, 35.8.1. Ifuatayo ni ile tuliyoihakiki.

2.9.1 Kigamba wangoja nini, wakati waatilika!
1.4.3 Vipi yaweza baini, neno la kutamkika!
11.5.3 Hili deni la ahadi, vipi utalilipa?

Katika mifano yote hiyo kuna hali ya kumakia yaliyotokea. Kuna mshangao wa namna matukio hayo yanavyotokea. Pia kuna hali ya kuajabia matokeo yake. Kwa mfano, katika mfano wa kwanza, msanii amakia yaliyomsibu kigamba, na ambaye bado hajaamua kufanya lolote. Mfano wa pili waonyesha mshangao wa jinsi maji yanavyoweza kuvumbua neno la kutamkwa, ilhali wa tatu, watupa kimako cha mbinu za kulipia deni la ahadi.

Nidaa ni muhimu sana katika sanaa kwani humpa msomaji mwelekeo wa kupata toni ya habari inayozungumziwa, hali ambayo pia inagusa hisia zake kuhusu tukio linalowasilishwa.

## BALAGHA

Kunga hii imetumiwa kwa wingi na kwa njia ya upevu na ukomavu mkubwa kisanii. Imetumiwa katika 5.1-10.4, 1.1-12.4, 5.3.3, 19.6.1, 31.7-2, 35.8.1, 56.5.1, 56.6.2, 56.6.2, 66.6.1-2, na 9.6.3. Ifuatayo ni ile ambayo tumeitathmini.

19.5.4 Pendo la namna hiyo, ni wapi liliko hasa?
19.6.3 Vipi mtu yuyo huyo, apende mtu na pesa?
72-73.1-8.4 Penye wazuri halisi, wajisifuje uzuri?

Katika mifano hiyo mitatu, twaona jinsi ujumbe unavyosisitizwa kwa kuuliza maswali, ambayo majibu yake yafahamika. Katika swali la kwanza, pendo hilo halikai popote wala halipo. Katika wa pili, mapenzi yamo kwenye pesa na katika wa tatu ni dhihaka tupu kujisifu uzuri, na wazuri wenyewe wapo. Maswali hayo yametumiwa kisanii kwa njia inayosisitiza ujumbe.

## CHUKU

Ufuatao ni mfano toka 46.2

Mwana wa mke si wako, ni msumari wa jito
Mlee kwa kilichoko, na kumpamba kwa vito
Kisha mpende kuliko, mwana wa mke mzito
Ni msumari wa jito, mwana wa mke si wako

Msanii ameongezea chumvi mno ubaya au uovu wa mwanaharamu wa mkewe katika kusisitiza ujumbe wake. Kuna ukuzaji wa uyakinifu na ambapo lililosisitizwa latupa picha iliyopanuliwa na kutufanya kuona hali halisi vinginevyo.

## MISISITIZO YA VIVUMISHI VIONYESHI

Misisitizo imetumiwa kwa kiasi - si haba wala si mingi.

Mifano

19.6.3 Vipi mtu yuyo yuyo, apende mtu na pesa?
20.8.3 Ni yayo yao ni yayo, ni yayo kujimamasa

Vivumishi hivyo vimetumiwa kwa mvuto na tashtiti, hali ambayo inampa msomaji hisia kali kuhusu ujumbe unaozungumziwa.

Kwa ufupi ni kuwa, vivumishi vionyeshi hutumiwa kutilia uzito kwa njia ya msisitizo, ule uwasilishi wa mawazo ya msanii, kama ilivyotokea humo.

## TAMATHALI ZA SEMI TUMBUIZI MJALIZO

Matumizi ya mbinu hii ni ya kiasi na yote yatokea kwa namna fulani inayoonyesha kuwa kuna unyoofu katika namna ilivyotumiwa.

Mifano

21.2.1 Katunga kutaka togo, asambwe yupo nyuma
78.3.1 Usingie hangaiko, hupatana wagombao
74.5.1 Majumbani mna feli, tafadhali zingatia
70.5.3 Nawe japo kinadhifu, bure hakiwi jamali

Katika tungo hizo ujumbe umeendelezwa kwa njia ya mkato inayoepuka viunganishi na kuwasilisha kwa uzuri. Kuna uekevu katika matumizi ya msamiati kama inavyodhihirika katika mifano hiyo, ambapo ujumbe wafika kwa maneno haba sana. Ni sifa mojawapo nzuri katika matumizi ya msamiati katika tungo za ushairi.

## TAMATHALI ZA USEMI WA VILINGE MDOKEZO

Mwandishi hakuitumia kwa wingi isipokuwa tu katika mifano haba.
Kuna mfano wa tamathali hii katika 46.2.3 ambapo umeendelezwa hivi:
Kisha mpende kuliko, mwana wa mke mzito.

Katika mfano huo, msanii kwa makusudi auvunja ujumbe katika kipande cha ukwapi, cha mshororo huo ambapo ametupa wazo ambalo hakulikamilisha. Hata hivyo ametupa mwelekeo na mwangaza wa namna ya kujaza wazo alilotudokezea.

Ulinganishi anaotaka kutupa ni ule wa watoto wake halisi, na wanaharamu wa mke wake. Imetokea kwa uzuri kwa namna isiyotatiza ujumbe. Kwa hivyo, msanii ameitumia kwa uzuri. Kuna mkazo fulani wa kihemshi unaotokea katika mfano huo.

**DHIHAKA**

Tamathali hii imetumiwa katika mazingira na matini chache sana, lakini kwa njia ambazo zinavutia. Mifano tuliyoitumia yawakilisha usemi wetu.

Mifano

75.8.2-3 Si vyote vyenye akili, vijike viruka njia
Kukiowa siku mbili, pesa utazijutia
73.8.3 Mbona unayo dosari, huioni huihisi?

Katika mfano wa kwanza, mshairi adhihaki wanaopendelea wanawari badala ya wake wakuu. Wa pili wahusu wale wanaodhani kwamba wamekamilika katika maumbile yao. Awadhihaki pia kwamba wako na vithibitisho vipi kwamba wametasawarika. Ni mifano inayofaa na iliyotumiwa inapofaa.

**TASIFIDA**

Mwandishi ameitumia kwa uchache na kwa namna inayopendeza kama inavyothibitishwa na mifano tuliyoitoa.

Ifuatayo ni mifano

40.2.2 Naswi twaona uchungu, kuwa ngao ipotele

"Ngao ipotele' ni kifungu kinachotaja kwa njia ya upole isiyo ukali kifo kilichotokea, na hili halina athari kubwa kama ile inayotokea kwa kuwapa faraja waliofiwa kwa kuwambia 'pole kwa kifo cha---'.

36.5.1 Ikithiripo tamaa, maarifa hwenda zake.

Watu wasioongozwa na maarifa huchoreka kama wapumbavu au washenzi na ukali na uzito wa usemi huu ndio umesitirika katika mfano huo wa 'maarifa hwenda zake'.

**NASIHA**

Kuna matumizi mengi ya kunga hii ambayo yanapendeza sana katika njia za uwasilishaji wa mawazo. Zinatoa picha ya upevu katika matumizi ya maneno.

Mifano

13.1.4 Mwana mwangaza mbili, lile moja humponya
56.4.1 Shibe ya nguo kilemba, wa kale walivyonena

| | |
|---|---|
| 56.4.2 | Shibe ya kande kujamba, vimbizi la mla jana |
| 60.4.1 | Shikana ushikwapo, majambo mbele na nyuma |
| 62.1.3 | Akatanga kimlacho, kinguonimwe vile vile |
| 69.8.2 | Pole pole ndio mwendo, akiba ulimbikizi |
| 69.8.3 | Sio chururu ndondondo, kiwekwacho hakiozi. |

Mifano hiyo ya busara imetumiwa kwa uzuri kwa njia inayomfanya msomaji kuyatafakari kwa undani mawazo ya mwandishi. Imetumiwa mahali pake, katika matini zinazofaa.

## NAHAU

Kuna matumizi mengi sana ya nahau, ambazo nyingi si za kawaida ama zilizozoeleka. Hata hivyo zimetumiwa kwa namna isiyozuia mawasiliano.

Kuna mifano mingi ya aina hii katika, 3.2.3, 3.4.2, 3.5.1, 3.6.1, 6.10.2, 7.4.1, 12.7.1, 13.5.3, 29.6.3, 46.2.3, 47.10.2, 54.4.3, 52,6.3, 56.4.2, 57.9.2, 77.8.2, 78.1.1, 40.2.1, na kadhalika.

Ifuatayo ni ile tuliyoiangalia

| | |
|---|---|
| 36.3.2 | Iwe watu kuwavaa, kwa magumi na mateke |
| 64.2.3 | Hilo lisikusumbuwe, kuutia moyo joto |
| 79.10.1 | Udugu nyama ya tako, wanenavyo wa mwambao |

Nahau hizo zimetumiwa kwa njia isiyokoroga mawasiliano. Zina hekima na uzito wa kipekee katika namna zinavyotokea, ambayo inaziwezesha kutupa picha za yale yanayoelezwa. Wa kwanza watupa picha ya uvamizi kwa watu kwa njia ya magumi na mateke. Ya pili ni ya kutuna. Hatima ni picha ya uhusiano usioepukika wa damu na kihemshi.

## MAFUMBO

Aina ya mawazo yaliyoendelezwa katika mashairi maji, bubu, mogo, moma na mengine ni ya kifumbo. Ifuatayo ni baadhi ya mifano.

Kile anachokisemea katika shairi maji, chawezatafsiriwa kwa njia nyingi na katika miktadha mingi, ya kinyumba na kisiasa. Matumizi haya hayakusudiwi kutatiza msomaji bali kumwingiza katika bahari teti ya sanaa ili mwenyewe atambue kwa maarifa yake mwenyewe anakoelekezwa na mshairi.

Ni mbinu inayohitaji busara, utulivu na subira kubwa katika kutafakari ili kubahatisha kimantiki alichokusudia mshairi bila kuteleza. Fumbo hilo lililotumiwa ni la hali ya juu na si rahisi kufumbuliwa bila makini ya kutosha. Limetumiwa kwa njia nzuri ili kuburudisha maashiki wa ushairi katika kujaribu kupata na kupima uwezo wa bongo zao katika kufumbua mawazo ya kisanii yaliyositirika sana.

## KEJELI/KINAYA/STIHIZAI

Mifano ya aina hii ipo katika 43.9, 55.9, 41.8.1, 73.7.3, 73.8.3, 72-73.1-8.4 ingawa haitokei kwa nguvu sana.

Hata hivyo ufuatao wafaa sana.

50.1.1-2 Fitina mtu nadhifu, mrembo kushinda kuyu
umuonapo latwifu, hana payayu payayu

Maelezo ya msanii kumhusu fatani ni kinyume kabisa na yanavyopaswa kuwa. Amempa sifa ambazo si zake kabisa. Msanii awaonya watu kuhusu mafatani kwa kuwachora kinyume kabisa na walivyo ili wasomaji wapate picha zilizolengwa kwa kuzama kidogo katika bahari ya luja ili kung'amua ukweli huo.

## KIJEMBE

Ifuatayo ni mifano

23.5.1-2 Leo pana mvurugo, wa borohoa na pombo
Tena pana mchanjago, wa manyama na utumbo
2.7.1-2 Sinifanye baahuni, ukawa kunikoweka
Kunitupa mvunguni, pamwe na kunifinika
41.9.1-3 Kila mcheza na fungu, hatavuka maji male
Tutamzamisha nungu, na kibaazi cha chole
Hapa shungi la utangu, hapatawali muwele

Katika mifano yote hiyo, msanii azungumzia mambo tofauti kabisa na yale yanayojitokeza hapa. Kiini hasa cha maneno tunayoyaona kimesitirika sana. Njia ya kipekee ya kupata mwangaza na kupambanukiwa ukweli wa hayo ni kwa kusoma tungo toka mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano, katika wa tatu aongea kuhusu watunzi ambao hawajakomaa. Hapa bahari limetumiwa kwa maana ya mazingira ya utunzi. Nungu hawaingia katika mazingira ya bahari, ila limetumiwa kisitiari kusimamia nafasi ya watunzi wapotofu. Kwa ufupi, msanii ametumia vijembe vya uzito sana na vinavyofumbuliwa kwa kukaa kimakini na kupata muktadha.

## ISTIARA

Mfano

21.6 Mtwanzi penye upwago, kuliza pwande lazima
Kwa madaha na mikogo, kunyaka na kusukuma
Utwanzi wa mtitigo, si mwema huo si mwema
Fundi tueleze vema, ushogo na hiyo shogo

Msanii hapa atupa mawasilisho ya mawazo katika muktadha tofauti na asilia. Anazungumzia utunzi ambao auona sawa na utwanzi. Si utwanzi tu bali utwanzi wa bidii ya bure, kwani utunzi huo unakosa kuwasilisha kwa kuharibu mambo. Kwa

ufupi ni kuwa ni utunzi muovu usiowasilisha. Hivyo vitendo vya kunyaka na kusukuma ni sifa za utunzi mbaya. Mfano huu watupa picha ya usanii wa mkorogo usio na thamani yoyote.

## MATOKEO YA TAMATHALI ZA USEMI
## TASWIRA

Kuna mifano mingi ya aina hii. Yapatikana katika kurasa za 32.3, 29-5, 25.2, 38-39,-2-10, 40.5-8, 42-43, 44-45, 46-47, 48-49, 50-51, 52-53, 54-55, 56-57, 59-59, 64-65, 70-71, 72-73, 74-75, 78-79, na ifuatayo ni ile tuliyoitathmini.

18.7

Tamati hadi asubuhi, machozi yanipukutika
Nilacho chanikirihi, na moyo kunichafuka
Ndani naona riyahi, ghafula nikatapika
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

Hapa kunatokea vizuri picha ya msimulizi anayemshtakia mwenzake hali aliyonayo. Ili latokana na nguvu za maneno yaliyotumiwa pamoja na mpangilio wao mzuri.

19.3

Hasikizi anenwayo, japo watu wamfyosa
Hadhuriwi sumbuliyo, tukano wala kunyusa
Afanywe yote yawayo, ni kama wamtakasa
Viwili katika moyo, kuviweka vyanitasa

Hapa kunajengeka picha wazi inayotufanya kumwona kwa uzuri mhusika katika usugu wake.

24.7.1-3

Zizi lisilo mifugo, ndani hulala maimbo
Jino la fisi ni sago, la gwase ni msirimbo
Nyungu bila ya kirugo, umbole mavimbovimbo

Fungu hili latupa picha za aina tatu kwa pamoja. Kuna ile ya zizi la maimbo liso mifugo. Pili ni ya jino la fisi, na tatu ni ya nyungu bila kirugo. Picha hizo humwezesha msomaji kuhisi, kugusa, kunusa, kuonja na kuona yanayoelezwa. Ni matokeo ya matumizi mazuri ya tamathali za usemi.

## 3:2:5 MATUMIZI YA LUGHA KIUJUMLA

Msanii ametumia pia Tadmini. Matumizi ya mchanganyo wa ndimi au lugha yanatokea katika Upisho kama inavyofafanuka kwa kuangalia mifano ifuatayo.

8.9.1 Allahu Rabbi Allahu, Mola usie mwinzako
25.1.1 Katabtu l'hakiri, si kwa maneno machafu
25.6.1 Tungo za dar-madari, nyia ziso uchokefu

Katika mifano hiyo kuna mchanganyiko wa kiarabu na kiswahili, na hali hii hutatiza mawasiliano kwa wasiovielewa vipashio kopwa. Baadhi vyafasirika kama vile vya mfano wa pili ambao wawezatafsirika kama "Naandika kwa unyonge, si kwa maneno machafu".

Kwa kuhitimisha ni kuwa, mwandishi ametumia lugha kwa njia nzuri katika viwango vyote (vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki) katika kuyaendeleza mawazo yake na kuyawasilisha kwa njia nzuri. Ameitilia nguvu kwa minasibisho na tamathali kadha za usemi. Ni lugha tamu isiyovunja mawasiliano wala kukera wasomaji. Ni lugha ambayo zaidi inaegemea kiwango cha urasimi (formal) - hivyo matumizi yake hata japo ni ya kisanii hayatiliwi shaka.

Ina uhusiano mzuri na vipengele vingine vya fani ambavyo ni wakati, ploti, toni, mazingira, mtindo na wahusika. Kwa ufupi ni kuwa kuna matumizi mazuri ya lugha.

## 3:3 WAHUSIKA

Msanii ametumia wahusika wa aina mbalimbali. Nao ni pamoja na Mungu, watu, vitu, mahali, wanyama na kadhalika. Wakati mwingine yeye mwenyewe ni mhusika, na wakati mwingine anawahusisha wasomaji wake moja kwa moja kwa njia ya maswali, balagha na kadhalika.

Wahusika hao amewapa sifa mbalimbali za maumbo na utendaji au utendwaji. Katika kuwasawiri, mshairi ametupa picha za kutuongoza kuwaona kiutendaji au kiumbo. Kwa mfano, pale anapotaja mhusika Mungu, hamtaji bure bila kutupa sifa zake hata kwa ukufi. Anasema hivi katika 8.9.1 Allahu Rabbi Allahu, mola usie mwenzako. Hapa anatupa sifa za ualimu za mola pamoja na kutupa ile picha kwamba hana mwingine kamwe wa kumlinganisha naye katika sifa hiyo na zingine. Yale mazito yanayotukera huwa mepesi sana kwa Mungu, na huu ni ushahidi wa heshima aliyonayo msanii kwa muumba wake.

Kuhusu mhusika mgumba msanii atupa sifa zake za utendaji na hasa za ulezi. Anatupa sifa chungu nzima za mgumba ambazo ni pamoja na za ukatili uliopita mipaka, uhasidi, ulimi mkali, uhaini, ufyosi, kukosa mwandani ila mgumba mwenzake, mbomoaji wa mahusiano baina ya baba na wanawe, vichinichini, undani, kukosa hisani, mwenye roho mbaya na kadhalika. Amemsawiri katika ukamilifu wake na kwa njia hii twapata picha kamili ya mhusika huyu ambaye ni sawa na hayawani, na hata pale msanii anapomfananisha na jini, afanya hivyo kihaki, kwani si matendo ya kiutu aliyonayo. Mwenzake kwa sifa katika diwani ni mama wa kambo ambaye pia matendo yake ni maovu. Jukumu la ulezi wa wana wa mume alitekeleza kama mhusika mgumba. Naye pia ni jemadari wa mateso na afanana na mtakadamuye kwa njia zote. Naye amesawiriwa kwa ukamilifu.

Mhusika mwingine katika uovu ni mwana muwi ambaye hata akilelewa kwa uzuri vipi, bado ataendelea na tabia zake mbaya. Naye amechorwa kwa ukamilifu. Kufikia hapa swali tunalojiuliza ni je, msanii amewasawirije wahusika wake? Je wanasaidiaje katika kuendeleza ujumbe? Ni upi umuhimu wao katika tungo?

Tunayajibu maswali hayo kwa kusema kuwa, mshairi amewasawiri vizuri na kikamilifu wahusika wake katika kuchukuana vyema na majukumu ya kisanii aliyowaumbia. Hakuna wahusika wanaojitokeza kiajali, na hao wanaoelekea kujitokeza hivyo husaidia kwa njia moja au nyingine. Kwa mfano, kuna wale wanaotokea katika mazingira ambamo majina yao yameishia kwa kina au vina vile vilivyoendelezwa katika shairi. Wahusika wake wote amewataja kiusimulizi au kimaelezo au hakuwapa nafasi kujisemea - hivyo basi hakuna ushahidi wa matumizi ya mbinu ya litifati[9]. Wengine wamehusishwa kwa kutajwa tu. Kwa mfano, katika beti zifuatazo, wahusika wametajwa tu, huku wakiulizwa kuchangia katika maswali waliyoulizwa, au kuitikia wito wake.

48.1-3 Ewe swahibu Azizi, usilimatie katu
Hatibu na jinamizi, pia obo mtukutu
Kizere ivunje kazi, ngome iwe na upatu

2.8.1-3 Nanyi mlo mitaani, siachi kuwakumbuka
Jinamizi usihuni, ukawa utatoweka
Moto ingia kundini, tupate kuongezeka

2.9.1-3 Kigamba wangoja nini, wakati waatilika!
Obo uko pembe gani, jua limekwishatoka
Saidi nuru unani? Mbona umeadimika?

Katika mfano wa kwanza na wa tatu mhusika Obo atajwa tu, japo akusudiwa kujiunga na wenzake katika kujibu maswali waliyoulizwa. Katika baadhi ya mashairi kama 'pole', 'maji' na mengine atuchorea wahusika maalum japo wanawakilisha jamii kwa jumla. Katika shairi pole, ubeti 1, mshairi asema;

Pole ewe ndugu yangu, msiba ukupatile
Kifo ni kazi ya mungu, si ya huyu si ya yule
Jamii ya walimwengu, hapatasaa kisale
Mawazo nakupa pole, pole sana ndugu yangu

Hapa amkusudia mawazo. Katika shairi 'maji' ubeti 1, atueleza yafuatayo kuhusu sitara.

Sitara usinihini, kwako ninalolitaka
Najua toka zamani, mrembo usie shaka
Hakika mwangu moyoni, hilo lanipa mashaka
Maji yanapochemka, nambie yasema nini?

Wahusika wengine amewapa majina ya kuwabandika. Kwa mfano, amwona mwana wa mke kama msumari wa moto mkubwa. Hivyo amwita msumari. Kwa kweli, wahusika waliomo humo ni wengi, wenye tabia na sifa mbalimbali. Wametokea katika mandhari mazuri yanayolingana na sifa zao na kuchukua majukumu yao kwa uzuri. Kwa hivyo kuna matumizi ya wahusika kwa njia inayotosheleza kisanii.

## 3:4 MTINDO

### MUUNDO WA MASHAIRI

Mashairi yote yaliyomo humo ni ya tarbia ya mkondo wa 8x8 na pale panapatokea kasoro katika mkondo kimizani, basi hayo hayakutokea kwa makusudi bali ni kwa sababu za uchapishaji.

Jumla ya mashairi ni 40 yenye beti zipatazo 359. Mashairi hayo yanatofautiana kwa idadi ya beti. Lile fupi zaidi kwa upande wa beti ni majuto, ambalo lina beti sita. Kuna mashairi kumi na moja yenye beti saba ambayo ni, Huruma, Deni, Muangaza mbili, Lambalo, Bahati, Suhuba, Mwakijo, Kikande, Dhamana, Fitina na Kasoro. Yenye beti 8 ni mawili, ambayo ni; tamaa na uzuri. Kuna mashairi 6 ya beti tisa ambayo ni; utu na kitu, Irabu tatu, Akili, Pendo, Mogo, na kingine. Ya beti 10 ndiyo mengi zaidi ambayo ni; Bubu, Moma, Utenzi, Mgogoro, Pole, Mama wa kambo, Mgumba, Msumari, Mwana muwi, cha Bure, Hoshari, Jaza, Muiza kiwi, Uzazi, Mke mkuu na Tega. Mashairi 'tungo' na 'moyo' ni ya beti 11. Marefu zaidi ni mawili ambayo yana beti 12, nayo ni; maji, na Mpigwa kwao.

Mgao wa vipande ni wa mathnawi, yaani wa ukwapi na utao, huku kila kipande kikiwa cha mizani 8. Jumla ya mizani katika kila mshororo ni 16. Kuna maumbo mbalimbali ya vina, nayo yamejadiliwa ifuatavyo. Kwanza ni mifano ya vina. Kuna vile vilivyopangiliwa katika mtindo tuliouita wa pindu, ambapo kina cha mshororo wa mwisho katika ukwapi chatumiwa katika mishororo mitatu ya kwanza ya utao, huku kile cha mishororo mitatu ya kwanza ya ukwapi kikihitimisha katika utao. Mifano

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 - 2 | 3 - 4 | 5 - 6 | 9 - 10 | 11 - 12 | 17 - 18 |
| ni ka | zi tu | bu wi | vyo mbi | di pa | hi ka |
| ni ka | zi tu | bu wi | vyo mbi | di pa | hi ka |
| ni ka | zi tu | bu wi | vyo mbi | di pa | hi ka |
| ka ni | tu zi | wi bu | mbi vyo | pa di | ka hi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 21-22 | 25-26 | 29 | 30-31 | 34 - 35 | 36 - 37 |
| go ma | ri fu | me mbo | wa ia | lo bu | aa ke |
| go ma | ri fu | me mbo | wa ia | lo bu | aa ke |
| go ma | ri fu | me mbo | wa ia | lo bu | aa ke |
| ma go | fu ri | mbo me | ia wa | bu lo | ke aa |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 38-39 | 40-41 | 42-43 | 46-47 | 48-49 | 50-51 | 52-53 |
| ro wa | ngu le | me ma | ko to | zi ki | fu yu | tu jo |
| ro wa | ngu le | me ma | ko to | zi ki | fu yu | tu jo |
| ro wa | ngu le | me ma | ko to | zi ki | fu yu | tu jo |
| wa ro | le ngu | ma me | to ko | ki zi | yu fu | jo tu |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 58-59 | 60-61 | 68-69 | 70-71 | 72-73 | 78-79 |
| ki ri | po ma | ndo zi | fu li | ri si | ko ao |
| ki ri | po ma | ndo zi | fu li | ri si | ko ao |
| ki ri | po ma | ndo zi | fu li | ri si | ko ao |
| ri ki | ma po | zi ndo | li fu | si ri | ao ko |

Mtindo huo wa kina pindu hutokea ili kuvunja ukinaifu (uchoshi) unaotokana na maendelezo ya aina moja na hivyo ndivyo ilivyotokea katika diwani hii.

Mtindo mwingine ni ule wa kina sawia (cha mtiririko) ambapo kwao vina vya ukwapi na utao huwa vya aina moja katika mishororo yote, na umbo hilo hukaririwa katika shairi zima. Ifuatayo ni mifano.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 13-14 | 15-16 | 19-20 | 23-24 | 32-33 | 56-57 | 62-63 |
| li nya | le li | yo sa | go mbo | ba ri | mba na | cho le |
| li nya | le li | yo sa | go mbo | ba ri | mba na | cho le |
| li nya | le li | yo sa | go mbo | ba ri | mba na | cho le |
| li nya | le li | yo sa | go mbo | ba ri | mba na | cho le |

| | |
|---|---|
| 74-75 | 76-77 |
| li ia | nga ri |
| li ia | nga ri |
| li ia | nga ri |
| li ia | nga ri |

Pia kuna mtindo wa kipoto, ambapo vina vya utao huwa vya mtiririko, huku vile vya ukwapi vikibadilika toka ubeti mmoja hadi mwingine. Ifuatayo ni mifano

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7-8:1-3 | 7-8:4-7 | 7-8:8-9 | 44-45 |
| ha ko | hi ko | hu ko | ni we |
| ha ko | hi ko | hu ko | ni we |
| ha ko | hi ko | hu ko | ni we |
| Ha ko | Ha ko | Ha ko | ae we |

Hatima ni ule mtindo ambao tumeuita wa kipotoukara ambapo hutokea kina tofauti katika mshororo wa nne wa ukwapi na utao. Ufuatao ni mfano

27 - 29
tu we
tu we
tu we
we nzi

Mitindo hii yavunja ule ufishihamu[10] unaotokea kwa kutumia tu aina moja ya mtindo. Hili ni dhihirisho la ukwasi wa hazina kuu ya leksia aliyonayo msanii na udhibiti mkubwa wa hazina ya leksia ya lugha. Nia yetu kwa kufanya hivyo siyo kusifu pasipostahili. Uchunguzi wetu umegundua kwamba mshairi ametumia zaidi ya vina 53 katika tungo hizi, katika mitindo minne tofauti.

Kuna ukariri wa kibwagizo katika mashairi yapatayo 30 hivi ambayo ni pamoja na maji, deni, huruma, akili, lambalo na mengine.

Mashairi nane ambayo ni moma, tungo, utenzi, moyo, suhuba, tamaa, mgogoro na tega hayana kibwagizo kilichokaririwa katika beti zote.

Kupitia kwa mpangilio wa msamiati, mishororo na vina, kumetambuliwa aina au bahari kadhaa.

## AINA ZA MASHAIRI

Kwa kuzingatia kigezo cha msamiati na mpangilio wao tunapata bahari za kikwamba na pindu. Ifuatayo ndiyo mifano ya kikwamba: 27.1-9.1 - matumizi ya neno utenzi, 39.2-10.1 - matumizi ya mgogoro/gogoro, 44-45.1-10.1 - kurudiwa kwa neno 'mgumba'.

Kuna mifano ya pindu katika 1.2.4 -> 1.3.1, 9.3.4 -> 9.4.1, 25.1.4 -> 25.2.1, 34.2.4 -> 34.3.1, 36.1.4 ->46.2.1, 52.1.4 - 52.2.1, 70.1.4 -> 70.2.1, 78.3.4 ->78.4.1.

Ifuatayo ni baadhi ya mifano hiyo

| | |
|---|---|
| 30.2.4 -> 30.3.1 | Rabbi akimjalia, bahati haina dawa<br>Bahati haina dawa, hirizi kujitatia |
| 26.4.4 -> 36.5.1 | Fikira zikuepuke, kwa kukithiri tamaa<br>Ikithiripo tamaa, maarifa hwenda zake |
| 58.1.4 -> 58.2.1 | Hoshari paka hoshari, kuliwa mimi sitaki<br>Mimi kuliwa sitaki, Hoshari paka hoshari |

Kupitia mifano hiyo, zadhihirika aina tofauti za pindu. Kuna ile ya ukwapi na utao kubadilishana nafasi moja kwa moja bila ya mabadiliko katika mpangilio wa maneno. Kuna ile ya kipande cha utao kutumiwa kama kilivyo huku cha ukwapi kikibadilishwa maneno. Tatu ni kule kupangiliwa upya kwa maneno ya utao yaliyoazimwa katika ukwapi wa mshororo wa ubeti mpya. Mifano hiyo ya pindu haijitokezi katika shairi zima ila tu katika baadhi ya beti na zaidi katika beti mbili tu za mashairi husika.

Kupitia kigezo cha vina, tunapata bahari za ukara na mtiririko. Katika ukara, kunatumiwa kina cha keketo katika utao, katika shairi zima, huku vya ukwapi vikiwa tofautitofauti. Mfano ni wa shairi 'Irabu Tatu'.

Katika mtiririko kuna vina vya keketo katika ukwapi na utao. Ni aina ile ya vina tulivyoviita sawia. Mifano ya aina hii yadhihirika katika mashairi tisa, ambayo ni; Muangaza mbili, Akili, pendo, mogo, suhuba, kingine, muiza kiwi, mke mkuu na mpigwa kwao.

Aina ya mwisho iliyomo ya bahari ni ile ya tarbia inayopatikana kupitia kigezo cha mishororo. Mashairi yote arobaini katika diwani hii ni ya tarbia.

## MITINDO YA UWASILISHAJI

Msanii ametumia mitindo ya usimulizi na kimaelezi katika kuwasilisha. Katika mashairi mengi nafsi ya kwanza ndiyo imetumiwa na hili huzua uzito fulani katika kutoa tashuhudi kuwa yanayozungumziwa ni ya kweli, yamewahi kutokea na sio uzushi. Hili huifanya hadhira kuyaamini na kuyatathmini. Ifuatayo ni mifano

1.5.1-3

Niliyaona zamani, hakaa kuyapulika
Hayasikia kwa ndani, yasema huku yacheka
Haona ni kuu shani, au mijuza kutuka

Uzito hapa umo kwenye kuwaaminisha wasomaji kwamba hayo yanayosimuliwa katika nafsi ya kwanza kweli yalitokea. Mbali na usimulizi huo kupitia nafsi ya kwanza, mshairi pia alitumia nafsi ya tatu na ufuatao ni mfano.

21.1.1-4

Mtunzi katunga mwigo, utungo umesawama
Tena umengia zogo, wakana kutojisema
Manenoye legolego, hayapatani kalima
Kamba kaliona moma, kadhani la kuni gogo

Mitindo hiyo ya usimulizi imetumiwa kwa njia nzuri inayovuta nadhari za wasomaji kwa njia ekevu. Tulitaja kuwa mwandishi ametumia mtindo wa kimaelezo ambao unaandamana na kuulizwa maswali ya kawaida na ya balagha kama ifuatavyo katika mifano hii.

75.9

Hebu tizama mithali, haya ninayokwambia
Tena bila mushkeli, mtume katangulia
Khadija kamratili, azaujati sikia
Huowi humkubali, kwa chuki au tabia

70.1

Kasoro ni upungufu, wa kisokuwa kamili
Ema kilicho hafifu, kisotimia mithali
Na ambacho kidhaifu, kwa kubadilika hali
Lazima kina muhali, kasoro ni uumbufu

Huu ni mfano wa mtindo wa maelezo. Kuna pia mtindo wa ushawishi kitashtiti kama unavyodhihirika katika mfano huu.

17.1-2

Mwinzio nakunasihi, mpenzi wangu ridhika
1 Lilo kuudhi aswahi, natambuwa pasi shaka
Najua 'mekujuruhi, nimekosa kwa hakika
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

2 Usione ikirahi, ni mengi mambo hutuka
Nikwambialo sahihi, kwa ajali limetoka
Toka mbele sijawahi, kutenda usilotaka
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

Kutoka mfano huo twaona jinsi msanii anavyomshawishi mpenzi wake kufuta doa katika mahusiano yao, ambalo limetokea kiajali. Hiyo ni ithibati ya ushawishi wa kitashtiti.

Kwa ujumla, mwandishi ametumia mtindo vizuri huku ukichukuana vizuri na mandhari, wakati, matukio, na vipengele vingine vya fani.

3:5 MANDHARI

Mshairi ametuumbia mandhari mbalimbali kwa nia ya kumwezesha kuwasilisha mawazo anayotaka ambayo yanaoana na wakati. Kwa mfano, kuna mandhari mbalimbali ya kijamii yanayojitokeza kama yale ya mapenzi, ndoa, maombolezo, ulezi na tabia (mahusiano). Pia ametupa mandhari ya kitaalamu kama vile ya utunzi.

Mandhari yote yamesawiriwa kwa njia inayodhihirika kwa uwazi. Kwa mfano, katika mandhari ya ulezi twaona namna wagumba na mama wa kambo walivyo wakatili, waovu na wenye unyanya mwingi kwa wana ambao si wao. Wahusika wa aina hii na majukumu yao yanadhihirika vizuri kwa njia inayomfanya msomaji kuyaona kwa uwazi matatizo yanayowasibu wana wanaolelewa katika mazingira ya udhibiti wa wagumba na mama wa kambo. Pia katika mazingira yayo hayo ya ulezi, twaona namna wana waovu walivyo wagumu na sugu katika kuleleka kwa njia za uadilifu. Twaona usumbufu wao mwingi kwa walezi wao. Ndiyo maana mshairi awaona kama misumari ya moto hasa wale waliokuja na hao mama wa kambo.

Katika mandhari ya mapenzi twaona namna yanavyotaabisha wahusika wake pale yanapotangua kidogo ile misingi yao ya mashiko. Madhali hakuna mwalimu wa mapenzi, athari zinazojitokeza kwa maashiki wake zinaaminika na zatokea katika mazingira zinamowafiki. Kwa mfano, katika shairi lambalo kunatokea hisia kali za mapenzi, hali ambayo inamfanya msanii kuomba radhi katika kurejesha ule uhai katika uhusiano wao. Ni shairi lenye nguvu Kitoni, ambapo twaona masikitiko makubwa aliyonayo kwa yaliyotokea na kuharibu uhusiano wao mzuri wa kimapenzi. Hatutambui kama ni ya dhati kwa sababu huyo anayezungumziwa hakupatiwa nafasi ya kutoa hisia zake. Beti mbili zifuatazo za shairi zatupa picha ya hali ya msanii kuhusu uhusiano wao

17.2&7

2. Usione ikirahi, ni mengi mambo hutuka
Nikwambialo sahihi, kwa ajali limetoka
Toka mbele sijawahi, kutenda usilotaka
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

7. Tama hadi asubuhi, machozi yapukutika
Nilacho chanikirihi, na moyo kunichafuka
Ndani naona riyahi, ghafula nikatapika
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

Katika shairi hilo msamiati ulioteuliwa unafaa kidhati katika mazingira hayo. Ni mazingira ya kimahaba na hayawezi kuangaliwa vingine, kama vile kisiasa. Wahusika aliowatumia wanafaa kabisa katika mandhari hayo, kiasi kwamba mbali na kutuwezesha kupata taswira ya hali hiyo, hisia zetu zaguswa na aina ya toni inayojitokeza katika kazi hiyo. Hapa mandhari yanatokea vizuri katika kuendeleza aina hiyo ya mawazo.

Kuhusu mandhari ya kiutunzi kunajitokeza vizuri picha anayoitaka msanii. Lazima yawe mandhari ya tungo bora, yanayotumia lugha ya heshima na yasiyoruhusu hali ya kujifaragua na kujibodowa kuwa ndiwe msanii stadi, wengine kamwe si kama wewe na kadhalika. Mandhari haya nayo yatokea vizuri siyo tu katika shairi 'tungo' bali pia katika mashairi mengine yanayoshughulikia maudhui ya aina hiyo.

Kwa hivyo, kila aina ya mandhari imetokea kwa jinsi nzuri na inayofahamika. Hakutokei mandhari ya kulazimishwa au yanayokinzana na aina ya mawazo yaliyonuiwa kuendelezwa kwayo. Yametokea katika mpango mzuri unaoruhusu wahusika wanaofaa kuendeleza na kutekeleza majukumu yao humo kama yalivyonuiwa. Hayatokei kwa namna inayotatiza ploti na mtiririko wa mawazo ya mwandishi. Ni uteuzi kidhifu kwa mujibu wa kilicholazimu yaumbwe na kutumiwa.

## 3.6 WAKATI

Kwa hakika si rahisi kutaliki wakati katika sanaa. Kawaida hujitokeza nyakati mbili muhimu; zilizopita na zilizomo, ambazo husaidia katika kutupa mwelekeo wa wakati ujao. Kila wakati huhusishwa na matukio yake. Namna wakati unavyotokea katika tungo husaidia katika kutupa taharuki na njozi. Mathalan, pale msanii anapotupeleka mbele na nyuma katika usimulizi wa matukio, hudhihirika matumizi ya taharuki. Isitoshe pale msanii huyo atakapotupa matokeo ya yaliyotokea na yanayotokea, atatupa pia chembechembe za kutabiria au kubashiria kitakachotokea kwa njia ya njozi. Japo taharuki pia hutokea katika ploti, hutokea pia katika kipengele cha wakati. Kuna ushahidi wa kutosha kuwa mbinu hizo zote zimetumiwa katika Upisho wa Umalenga. Njozi tayari imeangaliwa chini ya kipengele cha tamathali za usemi.

Taharuki ni mbinu ya kisanii ambayo kwayo mwandishi huelezea tukio, akaliacha kutulia huku akipisha maelezo kuhusu tukio lingine kabla ya kurejelea lile la awali kulikamilisha. Hili hutokea katika ule mtindo wa kuyapangilia matukio, kutokea kwa mvuto zaidi kama anavyotaka mshairi. Katika Upisho--, tuna mifano kadhaa, lakini huu mmoja katika shairi maji utatosheleza maelezo yetu. Katika ubeti wa kwanza, mshairi atuelezea mengi kuhusu mhusika sitara, na kuanzia ubeti wa sita hadi saba aturejesha tena kwa sitara akimshauri juu ya jawabu analotarajia na namna anavyolitarajia. Ni mtindo ulioendelezwa vizuri na haukwamishi mawasiliano.

Kwa ushahidi uliomo diwanini, msanii hakuwasilisha matukio yake katika wakati usiofaa. Ameyapatia ya awali nafasi kabla ya kuyaingiza mapya yaliyofuatia au yanayofuatia kusudi amwezeshe msomaji wake kutotatizika katika yale anayoyasoma. Udhibiti mzuri wa wakati huwezesha matukio kutokea wakati nafasi yao inapotokea na hili hutimia lau mshairi atayapatia yale makuu wakati kwanza ndipo yale mengine yafuatie. Na hivyo ndivyo alivyofanya Ustadh Shuara.

Hayo yote yaonyesha mamlaka aliyonayo msanii kupima vizuri na kukadiria nyakati za kuwasilisha tukio na kwa mpangilio usiotatiza. Hili laleta karibu uhusiano baina ya ploti na wakati, na ushirikiano kwa njia njema.

Mshairi hakuyanyima matukio muhimu nyakati muafaka kabla ya kuyapisha mengine. Kwa kufuatilia yaliyomo humo, tumegundua kwamba nyakati za matukio yote zatokea vizuri na hivyo hakutokei nafasi ya maswali kama; Haya yalitokea lini" Ifuatayo ni mifano ya matukio ya miaka ya nyuma au nyakati zilizopita.

25.5&6

Zitazameni dahari, za watunzi wale wafu
Tungo zao za fakhari, zisizo na hitilafu
Zapenya kwenye suduri, husomi zikakukifu
Ziacheni tungo chafu, watunzi wa mashairi

Tungo za dar-madari, nyia ziso uchokefu
Njema zisizo dosari, kuimbwa panapo safu
Ndizo tungo za khatri, zikinyowa nyonyo pofu
Ziacheni tungo chafu, watunzi wa mashairi

Katika mfano huo wakati unapambanuka vyema, nao ni ule uliopita, na matokeo yanayosimuliwa ni yale yaliyopita na yaliyokwishatokea. Madhihiriko mengine ni ya wakati uliopo na mifano ni kama ifuatavyo;

17.1

Mwinzio nakunasihi, mpenzi wangu ridhika
Lilokuudhi aswahi, natambuwa pasi shaka
Najua mekururuhi, nimekosa kwa hakika
Lambalo limekoseka, mpenzi nakunasihi

56.3

Umekuwa wajichimba, hivi sana nakuona
unaposema watamba, wajifutuwa upana
Upitapo wajigamba, ya kwamba umenibana
Baada ya kukupa nyumba, kingine sikupi tena

Katika mifano hiyo kunadhihihirika nyakati maalum kulipotokea matukio yanayoelezwa. Uliopita unapisha uliopo katika kutupa mwelekeo wa yatakayofuatia. Kwa kuhitimisha ni kuwa, matukio yanayosimuliwa katika tungo yaliyotokea katika nyakati mbalimbali zilizopita na zilizopo hushirikiana katika kutupa mwelekeo, mdokezo, au ubashiri wa yatakayotokea.

Kwa hivyo kipengele hiki kimeshughulikiwa vizuri na kila tukio angalau limehusishwa na wakati wake, na hili lashuhudika katika diwani yote.

## 3.7 PLOTI

Kuna mitindo ya ploti ipatayo mitatu hivi ambayo inatumika katika sanaa, ukiwemo ushairi. Wa kwanza ni ule wa msago au mfululizo ambao hulielezea tukio toka mwanzo hadi mwisho. Wa pili ni ule unaojenga taharuki na wa mwisho ni ule jumuishi. Aina hizo tatu za mitindo ya ploti zashuhudiwa pia katika tungo hizi tulizozihakiki.

Ustadh Shuara ametumia ploti fululizi au msago katika mashairi mengi ambayo ni pamoja na bubu, deni, lambalo, pendo, tungo, utenzi, mama wa kambo na mengine mengi. Kwa mfano katika shairi mama wa kambo, msanii anayasimulia maovu ya mama huyo tokea mwanzo hadi mwisho. Anaanzia uovu wake wa kuwatesa wana wa mumewe kwa kuwasukuma na kuwazulia maovu. Pili ni ule ukatili wake wa

kuwapiga hadi kuwatia alama. Tatu ni kuwachoma kwa kinga. Nne ni kuwatemea mate. Tano ni kuwaombea kila aina ya maovu na mikosi kuwapata. Sita ni kuwavalisha matambara. Maovu hayo yote yanasimuliwa na kutokea kwa muwala, na hivyo kunadhihirika matumizi ya ploti fululizi.

Mfano wa ploti inayoendelezwa kwa njia ya taharuki unajitokeza katika shairi maji, ambapo ubeti wa kwanza unaelezea mengi kuhusu mhusika sitara. Kutoka ubeti wa pili hadi wa tano mshairi aelezea kuhusu maji na yalivyomwajabisha katika aliyoyaona. Ubeti wa sita na saba wamrejelea tena sitara kwa kumshauri juu ya atakavyomjibu mshairi kuhusu swali alilomuuliza na kuliendelezea vidokezo kutoka ubeti wa pili hadi wa tano. Hata bila beti zile zingine za shairi, mfano huu wa taharuki utakuwa umedhihirika kufikia hapa.

Mtindo changamano (jumuishi) unajitokeza katika baadhi ya mashairi lakini mfano ufuatoa wa shairi 'pole' umefaa sana katika kutuongoza. Katika shairi hilo, beti nne za kwanza ni za maliwazo kwa mawazo kwa msiba uliomsibu. Kutoka ubeti wa tano hadi wa mwisho, mshairi anaongea kuhusu mambo tofauti kabisa yasiyohusiana moja kwa moja na yale yaliyotokea katika beti awali. Kile kinachodhihirika ni maendelezo ya mambo mawili tofauti yanayoletwa pamoja na kichwa kimoja na kibwagizo kimoja kilichokaririwa. Hata hivyo, kutokea kwa masimulizi kuhusu ustadi wa msanii huyu na maonyo yake kuhusu watunzi wapotofu watokea baada ya kukamilisha maelezo kuhusu tukio la awali, la faraja kwa mhusika mawazo aliyefiwa.

Uchunguzi wetu wa ploti uligundua kuwa matukio yanatokea kwa utaratibu maalum, unaoruhusu yale ya awali kutokea vizuri kama yalivyokusudiwa kabla ya kutokea mapya. Ni kipengele kimojawapo kilichoimarisha fani katika kuendeleza maudhui kwa njia nzuri.

## 3.8 TONI

Katika diwani hii, kuna mseto wa hisia na mikabala, hali ambayo inatupa mseto wa toni.

Kunadhihirika humo aina nyingi za toni ambazo kimsingi zategemea aina ya mawazo anayoyawasilisha msanii na namna alivyoyawasilisha. Mifano imetolewa kuthibitisha kuwa toni fulani imetumiwa na imetumiwaje. Aina ya kwanza ya toni tunayoiona ni ile inayotokana na sifa za kusisimua na kuajabisha katika baadhi ya wahusika wanaohusishwa na matukio fulani fulani. Toni za msisimko, mshangao na kuajabisha zabainika katika mashairi kama maji, Bubu, Mpigwa kwao na mengine. Katika shairi maji, tunaona sifa za kusisimua, kuajabisha na kushangaza za maji ambayo yamepatiwa sifa za kusema na kucheka. Katika shairi Bubu, kuna hali hiyo pia ambapo mhusika bubu ana sifa za uziwi, ilhali kiziwi anakosa sifa za ububu. Hili linamshangaza msanii hadi kumfikisha katika hali ya kuuliza swali ili kujua yaliyomsibu Bubu. Toni ya mshangao yatokea katika shairi mpigwa kwao ambapo ashangaa kuhusu mahali pa usalama ambapo mhusika huyu atakimbilia.

Hali ya kutojali ambayo yadhihirika katika baadhi ya mashairi kama **Irabu Tatu** yatupa toni ya kutojali iliyopo katika adinasi wengine ambao kabisa hawawajali wenzao ila ubinafsi wao. Hili huleta maudhi na mahusiano mabaya kama inavyobainika katika toni ya maudhi katika shairi "utu na kitu".

Toni ya huruma kwa wahusika wanaopokea matendo maovu na ya ukatili kutoka kwa wenzao, yabainika katika baadhi ya mashairi kama **Huruma, mama wa kambo, mgumba** na mengine. Twaona jinsi watoto wanaolelewa na wagumba na mama wa kambo wanavyotaabika katika mikono ya walezi hao katili. Kuna hisia zinazochipuza huruma na toni ya huruma kwa watoto hao wanaopokea vitendo hivyo viovu na malezi hayo ya uchungu. Toni hiyo ya huruma yadhihirika katika shairi **Huruma** ambapo kuna wahusika wanaopuuzwa na kudharauliwa kwa misingi ya maumbo yao, hali ambayo inasikitisha na kuudhi na kuzua hisia za huruma, kwa wale wanaofumwa na hali hiyo. Hali hii yatokea pia katika shairi **kasoro.**

Mshairi hakuepuka jukumu la kuishauri hadhira yake kwa kuipa mawaidha kuhusu mambo mbalimbali ya kijamii kama inavyodhihirika katika mashairi kama; **Suhuba, utenzi, bahati, moyo, Tamaa, Mwakijo, Fitina, cha bure, Mgogoro, Jaza, Muiza kiwi, Kikande, Dhamana, Majuto** na mengine. Katika fungu hili la mashairi, kuna kuchipushwa kwa toni ya ushauri.

Malezi ya unafiki mkubwa kutoka kwa walezi kama mgumba, ambayo yadhihirika katika shairi **uzazi,** yatuwezesha kupata toni ya unafiki.

Tungo za sanaa chafu zashtumiwa na msanii kama inavyobainika katika mashairi **moma na mogo.** Toni ya kashifa kwa tungo yathibitika hapa na badala yake mshairi ashauri watunzi kutunga tungo nyoofu na zinazovutia. Himizo hili ndilo latokea katika shairi **Tungo,** hali ambayo yatupa toni ya shime kwa tungo nzuri.

Furaha na uchangamfu katika kuvumbua vitendawili vilivyotegwa pia inashuhudika katika shairi **Tega.** Hapa toni ya uvumbuzi inabainika.

Kuna hali ya ukataaji kata kata na kwa ukali pamoja na dharau kwa maovu ya aina zote. Hali hii yatupa toni ya kukataa na dharau kama inavyotokea katika mashairi kama **Hoshari na Kingine.**

Matendo maovu ya kubomoa chochote kizima katika jamii na mahusiano ya kijamii kwa sababu ya fitina yawasilishwa kwetu kupitia shairi **Fitina,** hali ambayo yatuwekea wazi toni ya ubomovu.

Kuna hali ya kejeli kwa wale waja waliosahau kuwa utasawarifu kamwe si sifa ya kuelekezwa kwao, ila tu kwa mwenyezi Mungu. Kwa sababu hiyo kuna toni ya kejeli kwa wale wanaodhani ni wazuri na kamili kama inavyotokea katika shairi **uzuri.**

Katika mahusiano ya mahaba na unyumba msanii awasilisha mawazo ya kuwathamini sana wake wakuu. Mawazo haya yatupa toni ya uthaminifu kimahaba kwa wake wakuu kama inavyodhihirika katika shairi **mke mkuu.**

Ni kawaida kwa wanadamu kuwaliwaza wenzao waliofikwa na msiba wowote, kama ule wa kufiwa. Hali hii huwawezesha kuonyeshwa mapenzi na kufarijika katika wakati huo mgumu. Naye mshairi kupitia mashairi **pole na lambalo** awashauri wahusika wawili tofauti walio katika mazingira tofauti na hali tofauti. Kwanza ni mhusika mawazo ambaye aliwazwa kwa kumpoteza jamaa yake kwa njia ya kifo. Wa pili anayefarijiwa kwa njia ya kurairai ni mpenzi wake msanii. Kuna hali ya kutanguka uhusiano wao na mshairi ajaribu kumbembeleza warejeane kwa kumhakikishia kuwa makosa yaliyotokea hayatarudiwa. Katika mashairi haya kuna toni ya liwazo.

Msisitizo wa mahaba ya dhati watokea siyo tu katika shairi **lambalo** bali pia katika shairi **pendo.** Mshairi ashauri mshikamano wa dhati katika mahaba, hali ambayo yatupa toni ya mahaba. Ashtumu maendelezo ya uayari mwingi katika mahaba kama inavyotokea katika shairi **pendo** ambapo kuna toni ya uchati na uayari katika mapenzi yanayodhibitiwa na alivyonavyo mtu, bali si alivyo mtu (ya damu).

Toni ya kujiamini katika utunzi na usanii yajitokeza katika mashairi mengi likiwemo lile la pole.

Hali ya masumbuko kwa sababu ya tamaa kithiri inatokea katika mashairi **moyo na Tamaa.** Mshairi akataa mwongozo wowote ulio katika udhibiti na mamlaka ya tamaa zisiso na mipaka - hali ambayo yatupa toni ya masumbuko kwa wale wanaoathirika na tamaa zilizokiuka mipaka.

Toni ya mateso inayovyazwa na malezi ya taabu yabainika pale mlezi anapowalea watoto sugu wasiosikia ushauri wowote kama inavyotokea katika mashairi **msumari na mwana muwi.**

Kwa ufupi basi ni kuwa msanii amezitumia kunga zake za fani vizuri kwa njia ambayo inatuwezesha kupata toni za mashairi yake mbalimbali katika diwani hii. Mwandishi ameziandalia vyema toni, ambazo zatokea wazi katika mazingira aliyoyateua kwa namna ambayo inagusa hisia za wasomaji moja kwa moja na kuathiri upokeaji wao wa mawazo yake. Huu ni ufanisi mkubwa katika mwandishi.

## Tanbihi

1. Uliopangiwa vizuri mahali unapofaa zaidi
2. Wa mfuatano tu wa viarifa au vitenzi bila viungo kama viunganishsi, n.k.
3. limetumiwa katika kamusi ya Isimu na lugha kwa maana ya kivumishi kinachochukua nafasi ya nomino.
4. Kisawe cha "denotative meaning"
5. Ina maana ya kutumia alama kama ya ritifaa badala ya kitamkwa kilichodondoshwa
6. Urasimu - Kisawe cha "formal"
7. Kisawe cha "colloquial"
8. Kisawe cha "slang"

## SURA YA NNE: DAFINA YA UMALENGA

## UTANGULIZI

Dafina ya umalenga ni diwani ya pili ya Hassan Mwalimu Mbega. Ilichapishwa 1984 na shirika la longman. Ina utangulizi ulioandikwa na Mohamed Kamal Khan na Hassan Msami, unaomulikia fani na maudhui. Utangulizi huo una historia ya maisha ya mwandishi wa diwani hii.

Katika utangulizi, kumeshughulikiwa pia aina ya tungo zilizomo. Kuna pia sehemu ya sherehe ambayo ina baadhi ya maelezo ya kimaana ya msamiati uliotumiwa. Maelezo hayo yanafaa sana, katika kumwongoza msomaji kupata maana za msamiati uliotumiwa.

Kwa nini diwani hii yaitwa 'Dafina ya Umalenga'? Dafina ni neno lenye maana tatu. Kwanza, ni hazina iliyozikwa. Pili, ni vitu vya thamani vilivyozikwa au fichwa katika ardhi. Tatu lina maana ya tunu au zawadi iliyopatikana bila ya kutarajiwa. Katika muktadha huu twalichukulia tu kwa maana ya hazina. Nalo neno umalenga lina maana ya utunzi stadi wa mashairi na nyimbo. Tukiyaunganisha pamoja basi, twaifasiri anwani hii kama "Hazina ya utunzi stadi wa mashairi na nyimbo."

### 4.2 LUGHA

### 4.2.1 MSAMIATI : MAANA, UWEZO NA MAHUSIANO

### 4.2.1.1. UTEUZI WA MSAMIATI

Mifano ifuatayo inafaa katika kutuwezesha kutambua kama msamiati umeteuliwa vizuri au kihorera.

50.11 Huja nyuma tafakuri, za wale walokusapa
Waliokuwa ayari, wakakuganda na kwapa
Wakawa kukuhasiri, kwa takirima za chupa
Uzee wa kifakiri, ni jambo la kuogopa

37.8&12 Tenda wema utoshao, mwingi usio dimamu
Wape vyote viwe vyao, vikamilike kutimu
8 Kabisa haiwi ngao, ya kukulinda dawamu
Umekuwa marehemu, wema umekuwa mwao

12. Wema umekwenda kwao, hauko tena fahamu
Umebaki ole wao, si wema ni kula sumu
Kila usiku uchao, mtenzi ndiye dhalimu
Umekuwa marehemu, wema umekuwa mwao

Mifano hiyo michache inaonyesha kuwa msamiati uliotumiwa humo una uhusiano mzuri na umepangiliwa kwa namna inayoibusha maana zao kwa urahisi, hali ambayo inathibitisha kauli kuwa msanii amefanya uteuzi mzuri wa leksia alizozitumia. Mshairi amefanikiwa kuteua msamiati mzuri na kuutumia mahali unapofaa zaidi.

## 4:2:1;2 AINA YA MSAMIATI

Kama tulivyotaja awali katika sura ya tatu, msamiati hugawika katika viwango vya uzito, ukadiri na wepesi. Katika kuvichanganua, inafaa kuzingatia mwongozo kuwa, viwango hivyo vyote hubainishwa kwa uzuri zaidi kwa kutumia kipengele cha muktadha wa matumizi. Katika muktadha, hata neno ambalo wengi huliona la kawaida na kulipuuza hujipatia nguvu. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya msamiati mzito, ingawa huwa si rahisi kuweko mipaka ya kuvipambanua viwango hivi, kwani mengi bado yapo katika kiwango cha ujarabati. Kuna yale maneno ambayo tokea asilia yana uzito, na kuna yale yanayopatiwa uzito na muktadha. Mifano

| | | |
|---|---|---|
| 6.3.1 | Ndundu | Ni nini nakitambulwe, kilicho ndani ya ndundu? |
| 10.14.3 | Wambeja | Wambeja hukitapiya, watongo huuma zanda |

Mifano hiyo ya maneno ndundu na wambeja imejipatia uzito kwa njia zote mbili. Tokea asili zao yana nguvu na muktadha pia umeziongezea zaidi. Ufuatao umepata nguvu kwa mageuzi ya kimofolojia na uambishaji wa vipashio vyenye nguvu.

31.10. Maguvuguvu si mema maguvuguvu, mambo yatwae mpango

Neno hilo maguvuguvu lina uzito unaotokana na sababu tulizotoa pamoja na ukariri wa kipashio cha mzizi. Hali hii inatupa picha fulani isiyo nzuri ya kutekeleza mambo.

Ifuatayo ni mifano ya maneno ya wastani yaliyotumiwa.

48.11 Usijifunge na shari, zinduka mja zinduka
Shetani anakughuri, maovu akubandika
Utakuja tahayari, usipotubu hakika
Siku ya kuazirika, mwanaadamu fikiri

20.4 Ndugu asiye imani, ingawa ya vuguvugu
Chake usikitamani, pataingia vurugu
Mtoleane undani, utamani funga bugu
Ukitumai cha ndugu, wafa uli maskini.

Beti hizo mbili zina mchanganyiko wa msamiati mzito na mwepesi. Msamiati wake ni wa wastani.

Kuna pia mafungu ya leksia mepesi sana yaliyotumiwa kwa njia nyepesi na katika mazingira yasiyoyapa uzito. Ifuatayo ni mifano.

69.3 Vyakula maguniani, kila aina mnacho
Kila anayetamani, atumia apendacho
Atakaye simuhini, naatwae atwaacho
Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani?

69.4 Asubuhi na jioni, hakuna mkikosacho
Na nguo masandukuni, zimejaa kochokocho
Pambo za utamaduni, mpaka wanja wa macho
Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani?

Idadi kubwa ya msamiati katika beti hizo ni mwepesi na umetumiwa kwa njia nyepesi. Kuna msamiati japo haba uliotumiwa kwa uzito. Mwingi ni mwepesi.

Maelezo ya kiujumla ni kuwa msamiati mwingi ni ule mzito na mgumu kueleweka. Ni msamiati unaohitaji makini kubwa na kuuelewa muktadha wa matumizi vizuri ili kupambanukiwa kimaana.

Kiwango kingine cha kutazamia aina za maneno ni kile cha mofolojia, ambapo vipashio vyao huchanganuliwa na umuhimu wao kuangaliwa. Hivyo urefu wa maneno huangaliwa. Kuna yale marefu, ya wastani na mafupi. Hata hivyo, hili si muhimu. Kwani kinachofaa ni ule uwezo wao wa kuhimili maana na kuwa na uwezo wa kuiwasilisha vizuri. Ndiyo maana ule urefu huangaliwa kama ni wa kawaida au ni uliozuliwa kwa sababu ya uhuru wa kishairi ili kutumiwa kama msamiati nonsi (wa wakati na muktadha maalum tu).

Tulichogundua ni kuwa maumbo ya leksia zilizomo yakifuatiliwa kwa undani na makini hayatatizi, japo kiwango cha lugha cha msomaji ni muhimu kuzingatiwa katika kufanya maamuzi ya aina hii. Njia ya upambanuzi hutuwezesha kuyaainisha maneno katika makundi ya nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na kadhalika. Hili hutuwezesha kupata ule uamili wao, umuhimu wao, na ile nafasi yao katika mpangilio. Kwa uzito kimwelekeo, maneno yanayotokea kisanaa kabla na baada ya nomino husaidia sana katika kuifinyanga maana kuu ambamo nomino imetumiwa. Kile kinachovutia humo ni kuwa nafasi ya vivumishi ni kubwa sana katika kupamba utendaji na uamili wa nomino iliyotumiwa. Kwa mfano, katika 38.5, nomino kuu kisanii ni mzazi na twapata maendelezo haya;

Mlezi hajitulizi, penye waganga atamba
Akaigea palizi, na vyote vilivyo shamba
Waganga huja vikozi, na mijikoba mitumba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mlezi

Twaona namna mlezi anavyokosa utulivu, akikimbia kwa waganga huku akikosa hata wakati wa kupalilia mimea yake. Yote kwa sababu ya mwana kuugua. Picha hiyo inawasilishwa vizuri na vitenzi visaidizi, vimilikishi, nomino zingine, viunganishi, vitenzi na ule mpangilio wao mzuri wa kisemantiki.

Mshairi pia ametumia msamiati wa kiantomasia (wa kivumishi kuwakilisha nomino) kama inavyotokea katika mfano huu.

16.3.2 Anachokupa Ghafuru, 'ngawa sicho lako pendo.

Katika mfano huo, sifa ya Mola ya kutoa ghofira (msamaha) imetumiwa kimsingi katika kutupa nomino ya Ghafuru. Matumizi haya ni kama yanaleta mahadhi fulani katika fonolojia yenye mvuto yanapotamkwa.

Tuligundua kuwa aina ya leksia zilizotumiwa humo licha ya tofauti zao kiumbo na kiasili zinaleta mapigo ya uzito kimaana siyo tu katika kiwango cha neno moja bali pia katika mfululizo mzima wa shairi husika, hali ambayo inavutia kisanii na kihemshi.

### 4:2:1:3 ASILI YA MSAMIATI

Mshairi amechota msamiati wake toka lahaja mbalimbali, za upwa wa Afrika mashariki, kidigo na Kiarabu.

| Asili | Mifano |
|---|---|
| Kidigo | gwavya |
| Kiarabu | Athama, thuma, Qahari, Rabuka, Ghafuru |
| Kifunzi/chichifundi | magovya, uchimvya, chimvya, kukukwavya kuchavya, kurorwa, chavya |
| Kimvita | Kuwanwa, hukuchi, kanwa, mtambuzwa |
| Kivumba | Voro, uchadarwa, lavurwavurwa, kutinvya |
| Kiamu | awanywa, kuwanwa, zanda |
| Kingazija | Mororo |
| Kisiu | Kimezo |
| Kimrima | Kuovya, kutaramvya, kuchumbuvya, marovyarovya, kukurumvya, kigovya, marovya, kayana, maimuro, kerwa, si wamwe, vingaja, utamwe, simwe, sianie, mashemwe, usikimwe, kimwe kimwe, ushomwe, ashaja, tomwe tomwe, kiseja, kijibwe, kipwipwi, tende, kumwe n.k. |

Licha ya kuchukuliwa kutoka maeneo mbalimbali, maneno hayo yana mchango mkubwa sana hasa katika kumwezesha msanii kupata kina alichokitaka pamoja na idadi sawa ya mizani. Mengine hata hayaonyeshi kuwa yatoka maeneo mbalimbali kama inavyoonekana kutoka mifano ya msamiati wa kidigo, kifunzi na kimrima uliotumiwa katika shairi 'Sifa'. Hata hivyo namna yalivyotumiwa yanashikana kwa dhati katika uamili wao ambapo ule uasili wao haumpitii msomaji akilini mpaka pale pengine atakapopata neno asilolielewa lilivyotumiwa.

## 4:2:1:4 NGUVU/UWEZO WA MSAMIATI

Kwanza, muktadha ambao huandaliwa na matumizi au mpangilio mzuri wa sintaksia katika kuupa msamiati uwezo wa kuwasilisha, hufaa sana katika kipengele hiki. Ufuatao ni mfano, wa beti mbili za shairi 'ukiwa'

41.3 Utakuliza ukiwa, likupatapo sumbuko
Wakati umeemewa, sipo kitendeni pako
Huna unayemjuwa, mbali na kwenu uliko
Hapo utaona mwako, utakuliza ukiwa

41.5 Ukiwa ukiuguwa, pekeyo nyumbani mwako
Huna wa kukuaguwa, wala mganga hayuko
Hupajui penye dawa, wala uji wa bambiko
Na huo nao ni mwako, utakuliza ukiwa

Mpangilio mzuri wa maneno hayo kisintaksia unayawezesha kupata nguvu kisemantiki. Hayo yatokana na muktadha unaofaa wa matumizi ulioandaliwa na mpangilio mzuri wa maneno kisintaksia.

Pili, jinsi maneno yalivyotumiwa hufaa katika kuyapa uwezo kisanii. Yakitumiwa kwa mfano, kwa njia ya kukariri sauti au kipashio na kunakili sauti, ile maana asilia ya neno inapata uwezo zaidi. Mfano ufutao wa takriri unatupa picha ya kauli tuliyoitoa.

35.5.1 Iwe ni mwendo mwendao, upendezao kaumu

Katika mfano huo kuna ukariri wa 'mwendo mwendao' wa nomino na kitenzi. Matumizi haya yanawezesha neno hili kutumiwa kwa uwezo zaidi. Hili pia linaandamana na uteuzi mzuri wa msamiati ulioumiwa kabla na baada ya msamiati uliokaririwa.

Hili linaonyesha kwa njia wazi sana kwamba matumizi ya tamathali za usemi za aina mbalimbali huuwezesha msamiati uliotumiwa kutumiwa ukawa na nguvu na mapigo ya kisanii. Hata hivyo mengi kuhusu matumizi ya tamathali yameangaliwa katika sehemu ya 4.2.1.14.

Matumizi ya minasibisho huchangia katika uongezeaji nguvu msamiati. Kimsingi tunachukulia kuwa kuna tofauti baina ya tamathali za usemi na minasibisho. Ingawa kuna mwingiliano, kuna tofauti, ambapo tamathali hutokea kama njia na matokeo, huku minasibisho ikitokea zaidi kama matokeo ya matumizi ya maana katika kiwango kimoja tu - kile kinachohusishwa na maana zao wala si cha uasilia.

Maendelezo yao kimofolojia huyapa uwezo fulani wa kiuamili katika sanaa. Kwa mfano, neno maguvuguvu lina uzito sana ambao watokana na vipashio vyake pamoja na kutumia katika mazingira yanayofaa na katika muktadha mzuri.

Msamiati uliotumiwa unafaa na umefaulu kutekeleza majukumu ya kisanii. Mfano huu unafaa katika kuithibitisha kauli hiyo.

16.1 Sililie haidhuru, moyo kuusonga fundo
Ukipatacho shukuru, polepole ndio mwendo
Na wala usikufuru, ukajipaka uvundo
Chururu siyo ndondondo, na ndondondo si chururu

Msamiati uliotumiwa hapa una uwezo wa kuwasilisha tena vizuri sana. Sintaksia imefanya kazi vizuri, ambapo maneno yamefuatana kwa utaratibu unaofaa sana. Hakuna neno lililoingia hapo kiajali na lisilo na uwezo wa kushirikiana na mengine katika kutekeleza jukumu la uwasilishaji kwa ufundi.

Ni msamiati unaojitosheleza - unaojitosheleza kwa sababu hakuna ulegevu katika mahusiano yao, unaohitaji maongezeo ili kuziba ufa huo wa ulegevu. Kwa hivyo ni msamiati wenye uwezo wa kuendeleza mawazo kwa namna inayokidhi. Ni msamiati unaotawala mawasiliano kwa namna inayoonyesha upevu katika sifa siyo tu katika uteuzi wake bali pia katika matumizi yake.

Tukienda kwa undani kidogo tumegundua kwamba kabla ya kuangalia uhusiano baina ya neno na neno, kuna haja ya kuhakiki vipashio vya neno - ambavyo kwa kuangalia maneno katika mfano huo hapo juu vimetimia na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Ni kwa sababu hii tunahitimisha kuwa, matumizi mazuri ya msamiati katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki unafaa sana katika kuuwezesha kutimiza majukumu yake kwa njia inayofaa.

### 4.2.1.5 <u>MOTISHA/KARIHA KATIKA MATUMIZI YA MSAMIATI</u>

Idadi kubwa ya msamiati imetumiwa kwa namna isiyomfisha moyo msomaji. Mvutio huo unatokana na msamiati unaofaa kwa kuteuliwa vizuri, kutumiwa unapofaa na kuhusiana na msamiati mwingine katika muktadha kwa njia nzuri. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuthibitishia kauli.

20.1 Wafa uli maskini, utumaipo cha ndugu
Na chanda kuwa menoni, moyo ukafanya tungu
Kisikufae dhikini, kikawa juu ya dungu
Ukitumai cha ndugu, wafa uli maskini

30.1 Utendewapo uovu, wa kupituka kiwango
Moyo siutie chevu, ukautapisha nyongo
Na kujipa maumivu, ya fikira na maungo
Kipitacho kipe chongo, kitendo hakina kovu

47.1 Ewe mja tafakuri, ujuwe ulikotoka
Baadaye jifikiri, wapi mwisho utafika
Jawabu lilo dhahiri, mwisho ni kufa kumbuka
Witwapo ukaitika, mwanaadamu fikiri

Mafungu hayo yatuonyesha kuwa msamiati uliotumiwa unampa kariha msomaji na kumvutia kuisoma hadi mwisho. Mvutio huo watokana na sababu nyingi. Baadhi ni kama zile tulizozitaja mwanzoni mwa sehemu hii. Zingine zatokana na uhamishi wa maana toka ile halisi hadi ile ya minasibisho kama inavyobainika katika vifungu vya maneno kama 'moyo siutie chevu', 'moyo ukafanya tungu', 'kipitacho kipe chongo' na vingine. Matumizi ya tamathali za usemi kama njozi kwa mfano, katika ubeti wa mwisho pia hayafishi moyo msomaji. Hata hivyo kiwango cha elimu kinafaa sana, hasa cha taaluma ya ushairi. Kwa waliolelewa katika eneo la uswahilini (eneo lote la matumizi yake) na kufanya juhudi ya kukielewa kiswahili kwa mapana na marefu yake watafurahia tungo kama hizi moja kwa moja japo kila mmoja ana ladha yake.

## 4:2:1:6 MAZINGIRA YA MATUMIZI YA MSAMIATI

Haya hutegemea dhamira ya msanii. Mazingira kimsingi hutegemea eneo, mahali, hali au lile jambo linaloendelezwa kwayo. Kwa mfano kuhusu unyumba, kuna maneno ambayo hufaa zaidi kuliko mengine japo ni mengi yanayoweza kutumiwa katika mazingira yale. Ifuatayo ni mifano

64.1 Wangajitia vingaja, vya kumweka mwe! mwe! mwe!
Na furushi la makoja, umuonapo utamwe
Uzuri huo si hoja, wengine si wake kamwe
Wangawa ni kundi moja, lakini wake si wamwe

66.6 Lilipokuwa li sawa, pendo limetangamana
Lilikuwa limetuwa, tena mkisikizana
Madhali limepunguwa, haliji japo pindana
Moyo hupendezi tena, shukuru kama wenzio

68.11 Ni kheri mke muole, wa kwachwa na kuolewa
Avijuwa vipengele, kuficha na kufichuwa
Litajisiri jambole, ajichungie muruwa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa

70.14 Mimi ni wenu mwendani, sina nibadilishacho
Ni nyinyi mwangu moyoni, sina tena niwazacho
Sifikiri asilani, wala kinighilibucho
Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani?

Msamiati huo bila tashwishi yoyote unamwelekeza mtu kwenye unyumba na mapenzi moja kwa moja. Katika ubeti wa kwanza twatahadharishwa kwamba licha ya uzuri wao kiumbo na kimavazi, kitabia hawasemeki - ni waovu wa mwisho. Wa pili wazungumziwa hali halisi ya mapenzi kukatika - na ashauri kuwa watu wasijiumize wanapokosa kupendwa - kwani likiisha halilingani na hakuna haja ya kulifikiria sana. Kwa hivyo neno mke katika ubeti wa kwanza na pendo katika wa pili yatuelekeza moja kwa moja hadi mazingira ya mapenzi na ndoa.

Mfano wa tatu wazungumzia faida ya mke muole ambaye kwa mambo mengi amshinda mwanamwali. Wa nne, ambapo awahakikisha wake wake kuwa bado 'Yu mwandani' wao pia watufanya kuamini kuwa mazingira ni ya mahaba. Swali ni je msamiati huo wafaa? Kwa kweli wafaa. Haya ndiyo mazingira yake afiki. Ni dalili ya jinsi msanii alivyotumia msamiati katika mazingira ambamo unafaa sana. Mifano ifuatayo pia yafaa katika kutuongoza kutambua mazingira ya matumizi.

38.2 Kulea nako ni kazi, japo i ndani ya nyumba
Mwana awapo mlizi, wakesha kucha kuimba
Akupaza usingizi, wagotea na kuyumba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mezi

48.9 Huna kimoja kiburi, ni bure wadanganyika
Upesi tia nadhari, rudi kwa mola haraka
Sijifanye kutokiri, uchao waharibika
Moliwa wamuepuka, mwanaadamu fikiri

25.3 Ni kama asiyetenda, mtenda jambo asishe
Lawa mapandamapanda, hatendi alinyooshe
Hutililia ja kanda, na pia asilipashe
Mtenda jambo asishe, ni kama asiyetenda

Msamiati wa mfano wa kwanza umetumiwa katika muktadha wa ulezi na unawafiki sana hapo. Wa pili wazungumzia mahusiano mazuri na Mola. Nao wafaa katika muktadha wa kidini. Wa tatu wahusu utendaji kazi, ambapo kuna himizo la ukamilifu wa linalotendwa ndipo uzuri na ubaya wake ubainike. Mafungu ya maneno kama "kulea nako ni kazi," "rudi kwa mola", "Ni kama asiyetenda, mtenda jambo asishe" na mengine yatuonyesha kuwa yametumiwa katika mazingira ambamo yanahitajika na yanafaa.

Katika diwani yote idadi kubwa ya msamiati ni ile ambayo imetumiwa katika mazingira ambamo inafaa zaidi.

## 4:2:1:7 VIPASHIO VYA MSAMIATI

Msamiati mwingi ni ule uliojengwa kwa vipashio ambavyo vinawakilisha nomino, maana, wakati, hali, mtenda, mtendwa, mzizi na kadhalika. Kila mofimu iliyotumiwa ina kazi inayofanya katika neno kusudi isitangue ile maana ya neno au kulipotosha. Licha ya kutumiwa kwa uhuru wa kishairi katika kuongeza, kupunguza, au kubadili baadhi ya mofimu au vipashio vya maneno, maana zimehifadhika.

Maneno kama umma, mtima, kumi, dunia, maimuro, mkole, chole, winde, na mengine yamewasilika kama mofimu huru zisizohitaji mofimu zingine ili kuwa na maana. Nazo zaidi ni za nomino.

Kuna zile tegemezi ambazo zaidi hudhihirika katika vitenzi, vitenzi ambishwa na nyambuliwa, ambapo kila mofimu huwa na utendaji kazi wake. Kile ambacho wengi

hukipuuza ni uhakiki wa vipashio vya maneno katika sanaa, kwa msingi kuwa hayo yampasa mwanasarufi, lakini madai hayo hayafai kwani bila uhakiki wao, maana halisi ya neno na uwezo wake si rahisi kupatikana. Naye mshairi Mbega japo ametumia baadhi ya nomino, vitenzi na vivumishi vyenye vipashio vya kikale, havikwamishi maana.

Katika maneno hayo baadhi ya vipashio hutoa mwongozo wa maana ambapo kwa kupanua matumizi na kuangalia mahali lilimotumiwa, msomaji atapata kisawe na maana kamili. Mfano

72.3 Hii dunia tambale, na mabonde
Wala si nzuri umbole, i mavunde
Haidumu vile vile, si kitende
Likasaki jambo tule, lisenende

Maneno tambale, umbole, i, mavunde, tule, kitende, na lisenende yatupa mambo mengi ya kuelezea. Tambale ni neno lililobadilishwa umbo, kwani umbo lake kamili na lenye maana inayobainika moja kwa moja ni 'tambarare.' Umbole ni neno lililoundwa toka maneno mawili:umbo + lake ambapo kipashio le kimeongezwa kwenye neno umbo kikiwakilisha 'lake' kimaana. Kimsingi, 'le' ni kipashio kilichofupishwa toka mofimu mbili na kuwa moja iliyoshindiliwa uwezo wote wa kisemantiki wa neno asilia 'lake'. Kitende limetumiwa kwa maana kuwa si maskani, au makao. 'i' ni kiunganishi na kiwakilishi ashirifu cha uvundo au mavunde kama linavyotokea humo. Katika neno mavunde, 'ma, ni mofimu ya kuonyesha wingi wa kitu, ambapo katika muktadha huu ni wingi wa uvundo. Uvundo umebadilishwa vipashio na kuwa mavunde badala ya mavundo kwa sababu za kisanii za kutaka kupata kina 'nde' katika shairi 'Dunia' ambamo limetumiwa. Tule pia limefupishwa. Katika ukamilifu wake ni tulivu. Lisenende limetumiwa kwa maana ya lisiende.

Sababu za kutaka kina sawa, mizani toshelevu na utimizwaji wa kaida za kisintaksia na za kisemantiki zilimlazimu msanii kupangilia maneno kama alivyofanya katika ubeti huo.

Kuna baadhi ya maneno yaliyohifadhi vipashio vya kikale na ifuatayo ni mifano

69.5.1 Kila kizuri dukani, muda <u>ha</u>kipasha jicho
34.3.1 Chuchu nifumbatiapo, si<u>oli</u> nyuma
23.7.1-2 Ulimwengu guzo, mamboye <u>vitimbi</u>
<u>Uwelee</u> chanzo, kutendea dhambi

Vipashio ha, na li, ni vya kale. Uwelee badala ya umekuwa ni neno la kikale au lililoendelezwa kikale. Neno vitimbi limetumiwa kwa miaka mingi kama lilivyo kwa maana yiyo hiyo. Hata hivyo vipashio hivyo havizuii mawasiliano.

Vipashio vingine katika maneno vimekaririwa kwa nia ya kusisitiza maana yao. Katika maneno kama songasonga, maguvuguvu, mtengotengo na mengine, kuna

ushahidi wa kukaririwa kwa baadhi ya vipashio vyao ambavyo vimepigiliwa vistari, hali ambayo inatupa vitendo vinavyorudiwa.

Hali za uambishaji na mnyambuliko zimeendelezwa kwa namna isiyokingama mawasiliano. Maneno kama Kuzuzuwana, Kutoonana, Kuozeana, Kusimangana, Umefaiti,asiyangoje, na mengine yameongezewa vipashio kwa njia ya uambishaji na mnyambuliko kama ilivyoonyeshwa kwa vistari, na bado yawasilisha vizuri kwa uangavu mwingi.

Kwa ufupi, ni kuwa, vipashio vilivyotumiwa, vimetumiwa vizuri huku vikitekeleza majukumu muhimu vilikotumiwa. Kuna ukamilifu katika mpangilio na utendaji kazi wa vipashio, hali ambayo imeimarisha uwezo wa maneno vilimotumiwa. Hata hivyo kuna baadhi ya maneno japo haba yaliyoendelezwa vibaya kwa sababu ya kufuata kaida za ushairi. Ufuatao ni mfano.

71.15.4 "Ya ukewenza ya'cheni, pasiwe na kigombwacho," ambapo neno 'Kigombwacho ' limeendelezwa vibaya. Lilipaswa kuwa 'Kigombewacho' ambapo kwa sababu ya mizani limeendelezwa hivyo, japo kimaana halipotoshi.

## 4:2:1:8 MPANGILIO WA MSAMIATI

Hapa tumeangalia ule utaratibu wa maneno kufuatana kwa mpangilio mzuri usiotatiza na kuvunja urari katika mtiririko wa ujumbe. Mifano ifuatayo inafaa katika kuthibitisha kauli.

34.1 Pale chuchu nishikapo, natabasama
Mkono nipelekapo, kwa taadhima
Kwa pendo lilinganapo, nikaterema

59.5 Hapunguzi machachari, kipwipwi ajishiriki
Hakai akadhukuri, muovu hasalimiki
Walau kuwa kadari, kiumbe haiepuki
Imeumbiwa bashari, jumuiya makhuluki
Lakini kutahadhari, kimlimwengu hachoki

Katika mfano wa kwanza, mpangilio wa sintaksia wa mshororo wa kwanza unaanza na kivumishi kionyeshi, unafuatwa na nomino, kisha kitenzi, kituo na hatima kitenzi. Mpangilio huo wa maneno wafaa na kabisa hakutokei mkwamo. Hili linaangazika katika mishororo yote ya beti hizo mbili. Katika ubeti huo wa pili hapo juu, mpangilio umetokea kwa njia ya koja - ya mjalizo, ambapo maneno yafuatana kwa uzuri bila ya haja ya viunganishi.

Kupitia kwa mifano hiyo, twaona kuwa kuna ushahidi wa mpangilio mzuri wa msamiati, hali ambayo inauimarishia uamilifu wake kisanaa na kuifanya kazi kuvutia.

## 4:2:1:9 NAMNA MSAMIATI ULIVYOUNDWA

Njia ya kwanza inayodhihirika ni ile ya kuunganisha maneno mawili tofauti yenye maana mbalimbali katika kuunda neno jipya lenye maana ya kipekee na tofauti na zile za maneno yaliyoliunda. Ifuatayo ni mifano

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 29.4.2.1 | Mtaka'che | kutoka | Mtaka | + | chake |
| | ! | | ! | | ! |
| | Nomino | | Nomino | | Kimilikishi |
| 29.4.1.2 | Kisa'che | " | kisa | + | chake |
| | ! | | ! | | ! |
| | Nomino | | Nomino | | Kimilikishi |
| 27.2.3-3 | Ukomo'we | " | ukomo | + | wake |
| | ! | | ! | | ! |
| | Nomino | | Nomino | | Kimilikishi |
| 27.4.2.3 | Kizingamwewe | " | kizinga | + | mwewe |
| | ! | | ! | | ! |
| | Nomino | | Kitenzi | | Nomino |
| 55.7.2.5 | Walolafuka | " | walio | + | lafuka |
| | ! | | ! | | ! |
| | Kitenzi | | kirejeshi cha kitenzi | | kitenzi **kisaidizi** |

Pamoja na hayo, mwandishi amechota maneno ambayo yamo katika lahaja ambayo mengine yaelekea yaliundwa kwa njia ya ubunifu. Mifano ni ya maneno kama biri kutoka lahaja za kimvita, kipwipwi kutoka kimrima, na mengine mengi.

Maneno mengine yaliyotumiwa ni yale yaliyoundwa kwa njia ya uambishaji, na mifano ni kama; uliegeshe, namuolea, aukwatushe, naamtimbe, wagwavya, naicha, na mengine.

Mengine yameundwa kwa njia ya mnyambuliko na ifuatayo ni mifano; kusukumana, kusimangana, kudanganyana, kunywewa, kugongomewa, huchongewa, lipwekeshe, avigharikishe, huchongewa, kutenzwa, hufunzwa, waloarifiwa na mengine mengi.

Kwa njia ya neolojia, neno jipya au maana mpya inayopatiwa neno la kale huangaliwa kama njia nyingine ya uundaji wa msamiati. Huangaliwa kama njia ya uundaji upya kwa sababu ya ule ufinyanzi wake upya wa maaana ya neno. Mfano ni wa neo 'ihtiramu' kwa maana ya hadhi. Neolojia pia huwezesha neno kopwa kuchukua nafasi ya neno lililopo tayari katika lugha, na mfano huo tulioutoa wafaa.

Kuna njia ya ufufuzi wa maneno yaliyokuwa yakitumiwa awali katika lugha. Baadhi ya wanafasihi huiita njia hii ya kihafidhina. Ustadh Shuara hakuiepuka na baadhi ya maneno yaliyotumiwa kwa njia hii, ni pamoja na; chondechonde, ng'andu, ngemo, togo, atenzileo, ukema, embetele, uwelee, hapata na mengine.

Pamoja na hizo ni ile ya uhuru wa kishairi ambapo maneno hupatiwa maumbo mapya kwa njia za tabdbila, mazida, na inkisari kama inavyodhihirika katika maneno 'kikozi' badala ya 'kikosi', 'mwanaadamu' badala ya 'mwanadamu' na 'melimatiya' lililoendelezwa kielishia badala ya 'nimelimatiya'. Haya ni katika tu kiwango cha mofolojia. Haya hutokea siyo kwa sababu ya kimtindo tu bali kwa nia ya kufuata kaida za utunzi mashairi.

Kipengele hiki cha uundaji msamiati ni muhimu sana katika kumwezesha mhakiki wa ushairi na hata mwanasarufi katika kuangalia uamili wa maneno katika mawasiliano unaofungamana na uhakiki wa vipashio vya maneno yaliyotumiwa. Kwa ufupi ni kuwa, jinsi msamiati ulivyoundwa hauvunji nguvu zao katika kuwasilisha.

## 4:2:1:10 NJIA ZA UPANUZI MAANA KATIKA MSAMIATI

Kwa njia ya tanakali sauti, maana za maneno hupanuka. Katika mfano ufuatao, twaona jinsi maneno yanavyopanuka kimaana kupitia njia ya tanakali sauti. Mifano.

64.1.1 "Wangajitia vingaja, vya kumweka mwe! mwe! mwe!

Katika mfano huo, neno kumweka limepanuka kupitia picha inayosawiriwa na mwe! mwe! mwe! Tunapata sura ya kitendo hicho kupitia kwa unakili wa vipashio hivyo.

Takriri ni njia nyingine inayowezesha maneno kupanuka kimaana. Ufuatao ni mfano.

64.4.3 "Wenende huku ukija, uone kumwe na kumwe"

Takriri hiyo ya kumwe na kumwe kwa maana ya huku na huku yatupa dhana ya kuangalia kila mahali bila kubagua. Lau matumizi yangekuwa ya kumwe tu, basi maana ya huku tu ingedhihirika, hali ambayo yaweka mipaka fulani ya mahali panapoangaliwa.

Maneno pia hupanuka kimaana kupitia kwa njia ya uhamishi wa maana za maneno yaliyo tayari katika lugha. Kwa mfano neno nyanya tayari lipo katika lugha, na lina maana ambazo ni za kinomino. Lakini katika diwani hii limetumiwa kwa maana ya kujimudu, neno ambalo ni kitenzi. Hivi ndivyo lilivyotumiwa katika diwani;

59.2.3 "Kabisa hajisairi, hajinyanyi hajishiki," ambapo limetumiwa kwa maana ya hajimudu au hajiwezi.

Uhamishi wa mandhari na matini yanamotumiwa maneno hupanua maana zao. Ifuatayo ni mifano.

58.1.1 Nilipa na mimi n'onje, kwamba fadhila zalipwa

71.15.2 Roho zenu zituzeni, mjijuwe kiumacho

9.2.1-3 Si kule nimesongeya, na kule nali hionda
Hionda kipembejeya, maovu nikiyapinda
Hipishana na thureya, manzili yasiotunda

Kutoka mifano hiyo maneno kuonja, kuuma, kupinda na kupishana yametumiwa katika matini na matendo au mazingira yasiyo yao ya kawaida au asilia. Yamehusishwa na matendo au vitu ambavyo havikuzoeleka. Twaona fadhila zikionjwa, roho zikiumwa, thureya zikipishwa na maovu yakipindwa. Hayo yote ni mahamisho toka matini asilia ambamo maneno hayo hutumiwa, na kwa njia hiyo yanapanuliwa maana zao au yamepata mawezekano ya maana ziada.

Maneno ya kawaida yakitumiwa kinahau, zile maana zao hupanuka. Haya yathibitika kwa kuangalia mfano ufuatao

49.1 "Kafa nawapa habari, mkanye yenu mishipa"

Mishipa katika muktadha huu imehuishwa na inatarajiwa kuonyeka au kukanyika kama kwamba ina masikio na fahamu. Matumizi haya yamepanua maana ya neno 'mishipa'.

Mafumbo hufaa nayo katika upanuzi wa maneno yaliyotumiwa hata yawe ni ya kawaida. Ufuatao ni mfano

6.3 Ni nini nakitambulwe, kilicho ndani ya ndundu?
Na ambacho kifungilwe, kina sabaa vidundu
Na kila kimwe kitilwe, sabaa saba chachandu
Kilicho ndani ya ndundu, ni nini nakitambulwe?

Katika matumizi ya kawaida neno ndundu hutengewa matumizi katika muktadha wa mambo ya wanawake ambayo hayapaswi kuwafikia wanaume. Lakini katika muktadha huu limetumiwa kwa mwelekeo wenye mawezekano mengi. Hapa matumizi yake ni ya uhifadhi wa siri, katika mazingira yoyote yale.

Matumizi ya maneno katika mandhari yanayofaa au matini nzuri huyawezesha kujiongezea uzito au uwezo wa kimaana. Hii ni mifano

9.5.2 Iwe ni kuchuchumiya, wale wenye vimo Shinda

9.6.1 Kwa zitunu wataliya, nyoyo, ndani zitadunda

Matumizi ya 'vimo shinda' na 'zitunu' yamepata uzito na hivyo kupanuka kimaana kwa sababu ya kutumiwa katika mandhari nzuri na matini nzuri.

Kwa njia ya neolojia, maneno hupanuliwa kimaana. Neolojia ni njia ambayo kwayo neno hujipatia kisawe kipya au neno ambalo tayari lipo katika lugha, hupata maana mpya. Huu ni mfano.

9.6.2 Zitatunza kama mwiya, uputao ovu donda.

Kutoka mfano huo, neno mwiya limetumiwa kwa maana ya mwiba. Neno hilo tayari lipo katika lugha kwa maana ya mdai na muda. Pia neno uputao latokea kama kisawe cha upigao. Matumizi ya maneno haya mawili kwa njia ya neolojia, yameyawezesha kupanuka kimaana.

Uambishaji wa vipashio kwenye maneno fulani huyawezesha kujipatia maana za ziada. Huyapa sura za ukuzaji zaidi. Hili hutokea katika matumizi ya maneno kama matiko, maguvuguvu na mengine ambayo hutupa picha ya ukuzaji zaidi wa kitenzi au nomino. Ufuatao ni mfano

10.5.2 Mifuo nivugutiya, matiko nikiyakunda

Hapa kiambishi ma - kimeleta uzito fulani kimaana.

Matumizi ya tashbiha pia huyapanulia maneno maana. Mfano huu kutoka 14.3.3 usemao " Haiva mnyinyiriko, mweusi kama mpingo." Watuthibitishia kuwa kutokana na matumizi haya, neno mweusi limepanuka maana, ambapo weusi unaotokea si ule wa kawaida, bali ni ule wa mpingo.

Kwa njia ya sitiari, maneno hupanuka kimaana. Mfano huu kutoka 49.2.1, watuthibitishia jinsi neno dunia lilivyopanuka kupitia sifa za kisitiari. Mfano huo umeendelezwa hivi "Thuma tieni nadhari, hii dunia ni fupa". Picha inayojitokeza hapa ni ya dunia ngumu, isiyo rahisi kuchezewa. Dunia ni ngumu si ya kuchezea.

Kwa sinonimi[1] maneno hujipatia maana zaidi. Kwa mfano matumizi ya neno baliya badala ya balaa yanaleta uzito na upanuzi wa maana katika la awali. Katika ukurasa 47 msanii ametumia maneno: Qahari, Rabuka, Muniri, Mola, Moliwa na Mungu katika kumrejelea Mungu. Baadhi yao yanahusishwa na sifa za mwenyezi Mungu, na hivyo aina hiyo ya matumizi inasaidia sana katika upanuzi wa maana ya neno 'Allah' au 'Mungu'.

Homonimia[2] ni njia nyingine ambayo kwayo kuna upanuzi wa maana. Matini pamoja na mazingira hufaa pia katika kuchanganua aina ya maana inayowasilishwa pale ambamo imetumiwa. Mfano

57.1-7.4 "Haya na usalitivu"

Neno haya lina maana nyingi. Kwanza hutumiwa kama kivumishi kionyeshi cha kurejelea vitu au mambo yaliyo karibu. Katika kamusi sanifu ya kiswahili kuna maana nyingi za neno hilo. Ya kwanza ni ile ya 'hali ya mtu kuogopa maovu au aibu yake isijulikane na watu." Pili, ni ya "fedheha, soni". Tatu, ni "hali ya kusitasita kusema au kufanya jambo kwa sababu ya kumheshimu mtu mwingine." Nne na mwisho, ni, "hali ya kutoweza kuangalia mtu machoni." Tukirejelea Dafina ya Umalenga, tunagundua kwamba limetumiwa kwa maana ya fedheha au aibu. Kwa hivyo hapa muktadha umetufaa katika kulipambanua kimaana.

Ule uhuru wa kishairi katika kiwango cha mofolojia husaidia katika upanuzi wa maana ambayo sasa hutamkika upya kwa njia ambayo kisaikolojia inampa mvuto msomaji. Kwa mfano katika 52.5.3.5, tuna neno 'kikozi' badala ya 'kikosi' lililopatikana kitabdila ambapo mizani na fonimu 'zi' ina nguvu sana kuliko 'si' tunapoangalia sifa za kifonetiki za vitamkwa hivyo.

Tunahitimisha kuwa maneno hupanuka kimaana kupitia tamathali za usemi na matumizi ya minasibisho, kwani njia hizo zote tulizoziangalia zatuelekeza hapo. Ni chache zisizoingia hapa.

## :2:1:11 WIZANI (RIDHIMU) KIMAANA KATIKA MAHUSIANO YA MSAMIATI

Mahusiano ya msamiati yanayoleta mapigo fulani katika sanaa hudhihirika sintaksia inapofanya kazi yake vizuri. Ridhimu kimaana hutokea katika kiwango cha fungu la maneno ambalo limepangiliwa kwa namna ambayo lapokea ujumbe na kuupokeza kwa njia ambayo inaleta mapigo hayo ya kisemantiki. Ifuatayo ni mifano

55.2.1-3 Wafile waficha siri, wenye nyoyo za mivungu, si waume hata wake
Wamo ndani ya kaburi, wako wewe hata wangu, hupati kifupa chake
Na wala usijasiri, watu wa leo mavungu, wana la kinyume teke

Kisintaksia,"Kifupa chao" ndiyo maendelezo sahihi badala ya "hupati kifupa chake"

64.2 Waume siwo wamoja, na wake nao si wamwe
Wengine wao mafuja, si wake ni wake simwe
Wana chungu ya miuja, wala lao lisisemwe
Wangawa ni kundi moja, lakini wake si wamwe

Upokezano wa maana toka kipande cha ukwapi kwa utao na mwandamizi na kutoka mshororo wa mwanzo wa ubeti hadi mwisho kama inavyoonyeshwa kwa mifano hiyo, waendelezwa kwa namna inayojenga wizani fulani kimaana. Hapa maana za maneno katika kiwango cha umoja inapotea na maana ya kiujumla ya fungu inadhihirika. Kwa mfano ubeti wa kwanza wahusu maana ya siri na msamiati wote uliotumiwa hapo umeshirikiana katika kutupa aina fulani ya ridhimu ya kisemantiki. Katika mfano wa pili, maana kuu ni kuwa 'wanawake si wamoja', wanatofautiana - wapo wazuri na wabaya na maana ya 'wanawake si wamoja', ndiyo inayoendelezwa katika ubeti huo kwa namna inayovutia kimapigo.

Mifano hiyo yatupa wizani kimaana unaowezekana kwa sababu ya mpangilio wa msamiati ulioteuliwa kwa njia nzuri. Ingawa kila neno lawakilisha maana ya kiupekee, mpangilio wao unayapa tangamano katika uamili wao, hali ambayo inayawezesha kuendeleza maana kuu (wazo kuu) kwa wizani fulani. Wakati mwingine matumizi ya maneno mengi yanayowakilisha maana moja hufaa katika kuleta wizani wa kisemantiki. Huu ni mfano

55.2 Sili naapa mwenyezi, jina la mola, Rabuka
Kwamba'ye ndie mwokozi, mtenzi vikatendeka
Atanoweza moyozi, sitokula kisolika
Nileje tokoro hizi?

Katika ubeti huo, maneno mwenyezi, mwokozi, mola na Rabuka yana uhusiano wa karibu na hivyo yanaleta wizani kimaana kwa jinsi yalivyopangiliwa. Wizani kimaana huleta mvuto katika tungo za sanaa kama inavyodhihirika kupitia mifano hiyo.

## 4:2:1:12 UANGAVU/UTATA WA MSAMIATI

Idadi kubwa ya msamiati uliotumiwa ni ile yenye uangavu kimaana. Mifano hii miwili inayofuata inafaa katika ufafanuzi wa kauli.

1.6 Kisu kisicho makali, si kisu si ukengele
Fugutu ni jisu hili, lisonyoa hata nywele
Mpoto awe wakili, ni kudanganya wavyele
Potofu wa kiswahili, mzowevu wa songole

46.8 Kila neno lina jibu, usitafute kwa nini
mambo yenda taratibu, pupa jingi lafaani?
Akopeshae zabibu, atalipwa zaituni
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu

Maneno yaliyotumiwa katika beti hizo yana uangavu wa moja kwa moja. Ni maneno mengi yaliyotumiwa kwa njia hiyo. Msamiati ambao unakosa uangavu huo wadhihirika zaidi katika shairi 'sifa'. Ni msamiati unaoishia kwa kina "vya" na wenye vipashio visivyoeleweka kwa mtu ambaye hakukipata kiswahili cha lahaja nyingi. Wote umechukuliwa kutoka maeneo mbalimbali ya uswahili na yana ugumu kueleweka. Sherehe iliyotiwa nyuma ya diwani pamoja na muktadha vyafaa katika kuiondoa hali hiyo teti ya ukosefu mwangaza kimaana. Ni hali ambayo ina chembe cha utata na ukosefu wa ukawaida, ikitegemea elimu ya msomaji, hali yake na wakati anapoipitia kazi hii. Inahitaji akili stakiri, utulivu na umakinifu katika vitivo vyote vya fahamu.

Kwa ufupi ni kuwa utata watokea kwa kiwango kidogo sana. Hali hiyo hapo juu twachelea kuiita utata kwa sababu moja. Utata unapotokea, hutokea kwa sababu ya wingi maana na matumizi katika muktadha usioeleweka. Lakini katika shairi sifa, baadhi ya msamiati wake si ule wa maana nyingi, na japo muktadha wa matumizi waeleweka, namna ulivyotumiwa na vipashio vyao yatupa mkwamo mkubwa kimaana.

4:2:1:13 **JINSI (AINA) ZA MAANA**

Kuna viwango viwili vya maana katika tungo zilizomo kwenye diwani hii. Maana tambuzi, halisi au asilia na maana nasibishi au husishwa zabainika kama inavyodhihirika katika mifano hii.

30.1.1 Utendewapo uovu, wa kupituka kiwango

45.6 Utendapo la thawabu, jema lenye ihsani
Adui au sahibu, hasimu au mwandani
Iwa yake matulubu, au umelitamani
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu

Hiyo ni mifano ambayo yawasilisha maana halisi za msamiati uliotumiwa humo. Ifuatayo ni mifano ambayo kwayo kwadhihirika maana nasibishi.

30.1.2 Moyo siutie chevu, ukautapisha nyongo

20.5.3 Na izara mitaani, moyo ukautapisha nyongo

4.5.2 Iwe ni kuchuchumiya, wale wenye vimo shinda

Maana za kutapisha moyo nyongo, moyo kufanya nzigu na vimo shinda ni za kunasibishwa. Siyo maana zao asilia - asilia kwa sababu moyo hautapiki, haufanyi nzigu na kadhalika.

4:2:1:14 **TATHMINI YA UHURU WA KISHAIRI**

Tukizingatia maana pana yake, tumegundua kwamba msanii ameutumia vizuri kwa njia inayoridhisha katika kuongezea nguvu fani aliyoitumia kuendeleza mawazo yake.

Uhuru huo katika kiwango cha mofolojia ambapo tabdila, mazida na inkisari hutumiwa, umetumiwa vizuri katika diwani hii.

Mshairi pia ametumia tamathali za usemi nyingi kwa namna inayoridhisha. Mengi yameangaliwa katika kipengele cha tamathali za usemi. Matumizi yao yanaiimarisha fani katika kuwasilisha.

Ufufuzi wa maneno ya kale pia umetumiwa pamoja na msamiati wa karne hii kwa namna inayoridhisha. Yametumiwa mahali ambamo hayakanganyi na katika matini inayosaidia kuleta uangavu wao kimaana. Baadhi ya matumizi hayo ni haya:

21.2.3.1 Maozi asifumbuwe, hasumbi wala hatweti

34.2.1.3 Hasa chuchu nisondapo, hujisukuma

34.3.1.3 Chuchu nifumbatiapo, sioli nyuma

Hiyo ni mifano ya matumizi wa msamiati wa kale. Uhuru huo umetumiwa kwa uzuri.

Na katika kiwango cha sintaksia ambapo mpangilio wa msamiati huangaliwa, msanii ameutumia vizuri ambapo maneno yanahusiana kwa kutumiwa kwa njia inayoyaamilisha[3] kubeba majukumu yao vizuri. Ufuatao ni mfano wa mpangilio mzuri wa msamiati.

35.3 Tata zikipinda, hazinyooki
Zinapokutanda, hazibanduki
unayempenda, hakusadiki

Kwa mfano huo, twaona mpangilio mzuri wa maneno. Hata hivyo kuna baadhi ya maendelezo ambayo ni ya kimakosa na ambayo twachukulia yametokea kimakosa katika uchapishaji. Kwa mfano katika 55.2.3 neno 'kisolika' limeendelezwa kama 'kisokila'. Kwa vyovyote hakuna ushahidi wa kuhusisha usipuna[4] katika hali hii. Hakuna ushahidi wa matumizi ya makusudi katika hali hii.

Katika kiwango cha vina, tumegundua kwamba mshairi ameutumia uhuru huo kwa ukamilifu. Ametumia vina tofauti tofauti vipatavyo 63 katika diwani hii. Ni kwa sababu hii tunahitimisha kuwa mshairi ameutumia uhuru wa kishairi kwa njia ya kuridhisha. Hatumuoni akipotoka mahali popote. Uhuru huo hausaidii kupotosha malengo ya kisanii. Na hiyo ndiyo maana uhuru huo ukatolewa.

### 4:2:3 KIWANGO CHA LUGHA ILIYOTUMIWA

Kiwango kinachodhihirika ni kile cha urasimi. Mwandishi ameepuka sana matumizi ya lugha mitaa na simo. Viwango hivyo vya umitaa na simo husababisha kushuka kwa hadhi ya tungo katika mtazamo pana wa wakati. Hatukupata matumizi yoyote ya viwango hivyo yaliyotumiwa kama ushahidi wa kuwepo kwa viwango hivyo.

Fungu lolote la maneno litakalochukuliwa bila mapendeleo yoyote litathibitisha kuwa mwandishi amejikita sana katika kiwango cha urasimi. Mara nyingi matumizi haya yanathaminiwa huku yale ya umitaa na simo yakizaa lugha mata[5]. Tunahitimisha tukitumia ugunduzi huu kama ishara ya ukomavu wa msanii kilugha na kifani.

### 4:2:4 TAMATHALI ZA USEMI

Kuna tamathali nyingi za usemi katika diwani hii. Kila aina ya tamathali iliyotumiwa humo ina sifa zake na uamili. Hata hivyo zote zashirikiana katika kuipa nguvu lugha ya kawaida (isiyo ya kisanii)

## TAMATHALI ZA USEMI ZA MSISITIZO

### TAKRIRI

### TAKRIRI IRABU

75.6.1 "utaingia kasoro, kwa kutakurwatakurwa" ambapo ambapo irabu 'a' imekaririwa, kwa namna ambayo hatuwezi kudai ina uzito sana.

### TAKRIRI KONSONANTI

75.4.2 "Ikawa kinyang'anyiro, kinyang'a kunyang'anyirwa" ambapo konsonanti 'k', 'n,' 'g' na 'y' zimekaririwa. Umuhimu wao kama ilivyo irabu 'a' ya mfano awali ni vipashio vya lazima katika maana iliyokusudiwa ya msamiati.

### TAKRIRI MIZANI (SILABI)

7.1.2 "Ah! hii niambavyo, si kwamba nimependezwa" ambapo 'mba' imekaririwa, na yafaa katika kuleta ridhimu fulani kimapigo

75.3.2 "Vijishoroba vyororo, vya kuseserwaseserwa", ambapo 'se', 'ro' na 'rwa' zimekaririwa. Silabi hizo zimekaririwa kwa namna inayoibua ridhimu fulani siyo tu katika kiwango cha fonetiki bali pia cha mofolojia.

### TAKRIRI YA NOMINO + KITENZI

3.5.3 Siwe mnuka kutuzi, unukae pombe

2.12.3 Lingaliwapo usuli, wajuwi huli juvile

3.2.1 Domo watu hubarizi, walumbi walumbe.

Katika mfano wa kwanza, maana ya nomino mnuka imepanuliwa na kusisitizwa na kitenzi unukae. Ili linatokea pia katika mfano wa pili wa nomino wajuvi na kitenzi wajuvile. Wa tatu pia watokea vivyo hivyo.

### TAKRIRI YA KITENZI + KITENZI

3.3.1 Domo la ushangamzi, waambao wambe

66.7.2 Lipende likupendalo, liwalo mwapendezana

34.5.2 Wakati niishibapo, hushiba vyema

34.7.1 Mara chuchu nikomapo, nimeshakoma

Ukariri huu wa vitenzi au vipashio kama mizizi yao wafaa sana katika kusisitizia maana za vile vinavyotokea mbeleni ili kupata uzito zaidi katika kazi. Hivyo wambe lasisitiza waambao, ukupendalo lasisitiza lipende na mwapendazana lakariri upokezano wa 'kupenda', hushiba lasisitiza niishibapo na kadhalika. Matumizi haya yameendelezwa vizuri.

## TAKRIRI NENO

13.5.1 sili! sili! sili! ish! vimbizi likanshika.

Mfano huo waonyesha msisitizo mkali wa ukataaji kata kata wa kula hicho asichokitaka msanii. Si mtindo unaochukiza. Una mvutio fulani, ambapo katika kila kidato cha ukariri kuna msisitizo wa maana - hali ambayo inapanua neno kisemantiki - inalipa msisitizo unaolipa nguvu zaidi.

## TAKRIRI VINA

Kuna ukariri wa vina katika mashairi mengi na umbo la mpangilio wao limekaririwa katika mashairi mengi. Ufuatao ni mfano

35.-7 nda ki umbo hili la vina limekaririwa
nda ki katika shairi lote
nda ki

Mshairi ametumia umbo la aina hii katika mashairi mengi, hali ambayo inafaa sana katika kumtambua msanii huyu kimtindo.

## TAKRIRI KIBWAGIZO

Mifano hii ni mingi sana na ufuatao utafaa sana katika kutuwezesha kutambua namna ulivyotumiwa.

36-37:1-12 "umekuwa marehemu, wema umekwenda kwao"

Mshairi amefanya hivyo pale maana kuwa inapoelekea kubebwa katika kibwagizo. Pia husaidia katika kuonyesha kuwa bado shairi ni lile lile. Kuna nyakati ambapo washairi huzungumzia mambo hata matatu tofauti katika shairi moja. Kile kinacholeta ushikamano wa yote hayo katika shairi moja ni ukariri wa kibwagizo, na hivyo ndivyo ilivyotokea humo.

## TAKRIRI UMBO/MUUNDO

Muundo wa beti umekaririwa katika shairi zima. Kila shairi lina muundo wake wa beti na miundo miwili mikuu yatambulika, kwanza ni ule wa mishororo inayotoshana kiubeti. Pili ni muundo ule wenye msuko katika kibwagizo. Ifuatayo ni mifano inayoonyesha maumbo hayo

| | | |
|---|---|---|
| 66.1-7 | ro na<br>ro na<br>ro na<br>na do | Hapa kuna vina vya mishororo minne Inayotoshana kimizani. Muundo huu umekaririwa katika shairi zima. |
| 79.1-7 | mbi mba<br>mbi mba<br>mbi mba<br>mba | Hili ni umbo la mishororo mitatu ya kwanza kutoshana huku wa nne ukisukwa (ukifupishwa). Umbo hili limekaririwa katika shairi zima. Hilo ni umbo ambalo latokana na mishororo. |

Maumbo hayo ni kwa kigezo cha mishororo. Kwa kigezo cha vina twapata maumbo kama haya:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 54.1-7 | nda ngu ma<br>nda ngu ma<br>nda ngu ma | 72. | le nde<br>le nde<br>le nde<br>le nde |

Mfano wa kwanza ni wa vina vitatu na huku wa pili ukiwa wa vina viwili. Kimsingi hayo ndiyo maumbo ya vina yaliyokaririwa. Kwa jumla takriri imetumiwa vizuri katika kupamba, kusisitiza, na kupanua matumizi ya leksia katika sanaa.

## TANAKUZI

Mifano

53.2.8 Katu siingie ghururi, la tamu lina uchungu, mwema ana ovu lake
27.7.3 Usivumbuke ukowe, pawe ndipo wala sipo.

Kuna ukinzano kimaana katika mafungu ya maneno "La tamu lina uchungu", "mwema ana ovu lake" na "pawe ndipo wala sipo". Kwa matumizi haya, twaonakuwa, hii ni mbinu inayosisitiza kwa kutumia mpangilio unaofaa wa kisintaksia wa maneno unaokinzana. Kwa mfano, katika fungu la kwanza twasisitiziwa mawezekano ya uchungu katika utamu na hivyo tusidanganyike tukadhani ni utamu tu mpaka mwisho.

Tamathali hii imetumiwa kwa uzuri katika kuwasilisha kwa uzuri kama ilivyofunuka katika mifano hiyo.

## TABAINI

Tamathali hii ina sura mbalimbali lakini sifa inayoziunganisha ni ile ya ukanushi wa kutumia si na njia zingine za ukanushi. Inadhihirika katika 6.1.1,

36.6.1, 53.2.1, na 6.4.2. Ifuatayo ni ile tuliyoipitia kuhakikia matumizi ya tamathali hii.

21.3.1 Yalobaki atendewe, h'enuki wala haketi

36.7 Wema hauna kikao, hauna ihtiramu
Si rafiki si mwanao, si nduguzo bin amu
Hata wake na wa kwao, hakuna anaezumu
Umekuwa marehemu, wema umekuwa mwao

38.1 Japokuwa si mzazi, wa uzito wala mimba
Si wa kite na pumzi, na chaliyani kufumba
Si kwa siku wala myezi, hajazaapo mgumba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mlezi

Katika usemi huu, kuna msisitizo wa hali halisi kwa ukanushi. Kwa mfano katika mfano wa kwanza mshairi asisitiza ukosefu satuwa wa maiti-kwamba hana uwezo wa kutenda lolote - kuinuka au hata kuketi. Anasisitiza hali halisi ya mambo. Katika wa pili asisitiza kwa ukanushi wa wanajamii wengi kwamba, hawana wema hata iwe wana uhusiano wa kidamu. Katika wa tatu asisitiza kwamba hata mlezi awe si mzazi, ana matatizo mengi yanayoandamana na jukumu hilo. Ni tamathali iliyotumiwa vizuri katika kusisitiza ujumbe kama tulivyoona.

## NIDAA

Tamathali hii inapotumiwa kwa werevu humwezesha msomaji kupata toni ya uwasilishaji papo hapo. Imetumiwa katika diwani hii kwa wingi na mifano michache ifuatayo imetuwezesha kuthibitisha matumizi yake na namna yanavyotokea.

7.1.1 Ah! siambile ovyo, sambi ah!kupuuzwa
13.5.1 sili! sili! sili! ish! vimbizi likanishika
13.10.4 Ndipo nikasema ish!
29.5.3 Leo kauchocha ndole, wambaje! Atabukuka?

47.7.3 Hivi leo wajibari, wapitukia mipaka!
52.7.4 kwani upishi si kazi?
53.2.5 wengi wao ni ayari, kwa upitu na majungu, Allah! siponzeke
75.6.4 Kisha uambiwe: "voro!"

Matumizi hayo yanatupa sura mbalimbali za tamathali hiyo. Mfano wa kwanza ni wa kuguna, wa pili ni wa ukataaji kata kata, wa tatu ni uvuguvugu (haudhihirishi hisia maalum). Wa nne ni wa ulizo linaloandamana na arki fulani za mshangao. Wa tano ni mshangao, wa sita ni ulizo lenye mshangao na kadhalika. Kumetokea toni mbalimbali kutegemea ule mpangilio wa maneno na matini ambamo zimetumiwa. Kwa ufupi ni kuwa, nidaa imetumiwa humo kwa namna inayoibusha hisia fulani na isiyokera msomaji.

## BALAGHA

Maswali haya yametambuliwa katika; 10.10.1, 10.8.1, 36.1.1, 36.2.1,

48.12.1, 48.13.1, 48.14.1, 49.3.2, 53.1.1, 54.2.1, 54.3.1, 54.4.1, 54.5.1, 54.6.1, 54.7.1. Ile tuliyoiangalia ni:

27.4.1 Nazi yavunjaje jiwe, ikasaa papo hapo?
36.1.2 Ni upi uutendao, hata usiwe laumu?
19.9.1 Wangapi walalamika, mateso na unguliko?

Majibu ya maswali hayo yajulikana moja kwa moja, ila ameutumia mtindo huo katika kuwahusisha wasomaji wake moja kwa moja ili wayajibu kwa kuyatafakari kwa undani. Ajua vema kuamba kwa vyovyote nazi haitavunja jiwe nayo ibaki. Ni jiwe livunje nazi, siyo nazi kuvunja jiwe. Pia ajua kwamba kwa adinasi, wema hauwi wema bali uovu. Ajua kuwa ni wengi wanaolalamika kwa mateso na ungaliko. Msomaji anapoyasoma maswali haya mbali na kuyafikiria majibu yao, kuna picha fulani anayoijenga akilini mwake kuhusu namna ya kuyajibu maswali hayo. Kuna hali ya kuyaelekeza moja kwa moja kwa mazingira lengwa.

Kwa hivyo matumizi ya aina hii huingilia mahasa ya ndani ya msomaji huku yakimwathiri kwa njia moja au nyingine. Yanamshirikisha msomaji katika maamuzi na kuufunua ufahamu wake wa kinachozungumziwa. Yanamsaidia pia katika kumchochea kutenda yanayofaa, ikitegemea matini ambamo yametumiwa.

Msanii ameitumia tamathali hii kwa uzuri huku akiwashirikisha wasomaji wake kwa njia ya tashtiti. Kwa jumla ni matumizi ambayo yanafaa katika mazingira yalimotumiwa. Yanafaa pia aina ya ujumbe unaoendelezwa. Pia yanapanua uwezo wa msomaji wa kuyaangalia mambo yanayoendelezwa.

## TASHTITI

Matumizi haya huangaliwa kama sehemu ya maswali ya balagha, lakini mtindo huu unahusisha zaidi ya hayo.

Ni mtindo unaotumia njia mbalimbali katika kumshawishi kwa toni inayoziba masafa ujumi na kuathiri moja kwa moja hisia za msomaji. Si mara zote maswali ya balagha yatafanikiwa kihemshi kuingilia hisia za ndani za msomaji. Siyo yote yana uwezo huo. Sifa kuu ya tashtiti ni kuingilia mahasa ya ndani ya msomaji na kutawala maamuzi yake kuhusu jambo linalozungumziwa. Mifano hii japo haina nguvu sana, yatuwezesha kuona matumizi ya mbinu hii.

72.1 Hii dunia potole, siipende
Nenda nayo polepole, sijipinde
Itakuzushia gole, likushinde
Utabakie uole, usitende

7.2 Hii dunia salale, ni udende
Imetambaza wavyele, pundepunde
Hebu tiani makele, msiponde
Ni kuu mno shimole, sijifyande

9.3 Hii dunia kiwele, siigande
Wala haijai tele, ja umande
Ndio yake maumbile, usikonde
Pata tambaa uvale, ujikunde

61.4 Ya nini kusonywa, ukilacho hakiliki
Kisichoawanywa, elewa hakiwanyiki
sitake kuminywa, ulihali kujidhiki

Mifano hiyo ina ushawishi wa moja kwa moja kwa msomaji. Inamwonya na kumshauri pamoja na kumtahadharisha kuhusu uovu wa dunia. Toni katika beti tatu za kwanza ni ya upole, huku ikiwa na ukali mwingi wa kuingilia hisia za ndani za msomaji katika ubetiwa nne.

## CHUKU

Katika mfano ufuatao twaona chuku kubwa ya usawiri wa wanawali.

67.1 Iwapo mambo ni yale, niyaonayo wakawa
Ya daima makelele, na kwingi kujibodowa
Ni radhi naenda mbele, nepukane na shokowa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa

67.3 Kwanza hawana makele, ya mambo ya sawa sawa
Ila ringo na potole, tepo na kujishauwa
Huo unyumba ni ndwele, ya kujuta kuzaliwa!
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa

67.4 Asikiapo kengele, hatangoja kugutiwa
Kwa hovu la kwenda kule, ajiona akawiwa
Atelekeza michele, na nyama ikaunguwa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa

Kuna chuku kubwa hapo katika usawiri wa mke muole na wanawali. Amewasawiri wanawali kama wasio utulivu, wakosa uaminifu na wasioyaweza majukumu ya unyumba. Kwa maelezo yake wanaofaa na kuaminika ni wake waole. Lakini ukweli ni kuwa siyo wanawali wote ni waovu na wala siyo wake waole wote ni wazuri. Kwa hivyo kuna chuku katika usawiri wao.

70.14 Mimi ni wenu mwendani, sina nibadilishacho
Ni nyingi mwangu moyoni,sina tena niwazacho
Sifikiri asilani, wala kinighilibucho
Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani?

Mfano huu wa pili kutoka 70.14 watupa ukuzaji zaidi wa ukweli wa hali ya mambo. Mshairi atupa maelezo yenye chumvi nyingi kuhusu wakewenza wake. Asema hafikirii kabisa chochote (lolote). Hilo lawezekana kweli katika ulimwengu huu tulio nao hata kwa sekunde moja! kwa hivyo kifungu cha 'sifikiri asilani' kimekuzwa sana nje ya mipaka halisi ya uaminifu.

## MISISITIZO YA VIVUMISHI VIONYESHI

Vivumishi vionyeshi ni vipashio vya kisanii vinavyoweka wazi au elekeza umbali uliopo baina ya kitu na kingine au baina ya kitendo na kingine au sifa yoyote inayoangaliwa. Ifuatayo ni mifano.

| | | |
|---|---|---|
| 1 | 67.5.1 | Kutwa ni huyu na yule, wajao kumchukua |
| 2 | 15.8.2 | Ila ni huku na huko, mlango hadi mlango |
| 3 | 29.5.1 | Uchu ni wa tangu ule, ule wa myaka na myaka |
| 4 | 29.6.1 | Kikumbu kumbuka yale, yale yaliyotendeka |
| 5 | 29.8.1 | Hukungojea papale, uaniapo kushika |
| 6 | 2.8.3 | Ulitambuwe feeli, kwa fani hizi na zile |
| 7 | 27.4.1 | Nazi yavunjaje jiwe, ikasaa papo hapo? |

Kwa ufupi ni kuwa matumizi haya yasisitiza ujumbe kwa mvuto wa aina yake ikitegemea jinsi yanavyotokea. Mfano wa mwisho, watokea kwa namna ya swali la balagha, hali ambayo inauongezea nguvu msisitizo huo.

## TAMATHALI ZA USEMI AINA YA ZINDUNA

### NJOZI

Ifuatayo ni mifano

66.4 Muhibu umtajae, kwa usiku na mchana
Akikuapa babae, huwa hakutaki sana
Mpende akupendae, pendo mnaependana
Moyo hupendezi tena, shukuru kama wenzio

66.6 Lilipokuwa li sawa, pendo limetangamana
Lilikuwa limetuwa, tena mkisikizana
Madhali limepunguwa, haliji japo pindana
Moyo hupendezi tena, shukuru kama wenzio

Toni ya beti hizo mbili yatuelekeza kwenye uhusiano wa mahaba uliofika daraja la kuvunjika kabisa. Ni kweli kama inavyotajwa katika ubeti wa kwanza kwamba mpenzi akifikia kiwango cha kukuona kama babake, staha hiyo haimpi nafasi ya ingiliano la kimahaba. Ikiwa anakuheshimu kama babake, vipi pendo litawezekana, huku ikizingatiwa kwamba mahaba ni mahusiano ya mambo mengi ya sitara? Utabiri wa uhusiano huu ni wa kuisha - hakuna arki yoyote ya kuliokoa jahazi hilo. Mfano ufuatao nao watupa ubashiri wa mahaba yasiyowezekana.

68.8 Watakujia wavyele, na jamvi kutandikiwa
Kisha wambiwe kefule, huyu hukumnunuwa
Tulijuwa tangu kale, lakini tulighumiwa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa

68.10 Wataliziba kosa'le, wapate kukuumbuwa
Ili kusudi wakule, na maovu kutendewa
Mwana wao atawale, ubaki huna satuwa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa.

Hapa pia pana toni yenye mwelekeo wa uhusiano usiowezekana - kwa sababu ya tabia mbaya za wanawali na wavyele wao, ambapo inakuwa si rahisi kukubali vituko vyao. Kinjozi kwatabiriwa mwisho wa mahusiano ya kimahaba katika mifano hiyo miwili. Mshairi ameitumia mbinu hiyo vizuri kwa namna isiyokanganya wasomaji wake, katika diwani yote.

## TAMATHALI ZA USEMI ZA MWIGO SAUTI

### TANAKALI SAUTI

Mifano

4.5.2 Usije piga kelele, "kwinyo! kwinyo!" kama jimbi
16.1.4 Chururu siyo ndondondo, na ndondondo si chururu
21.3.2 Aoshwe akafiniwe, atitikwe titititi
64.1.1 Wangajitia vingaja, vya kumweka mwe! mwe! mwe!

Katika mfano wa kwanza tunaona tanakali ambayo haiwezi kufungiwa mazingira maalum. Kwinyo! kwinyo! ni tanakali ambayo haiwezi kupambanuka vizuri mpaka kutolewe mwangaza zaidi. Ina mawezekeno ya kutumiwa katika mazingira yasiyo ya aina moja. Hata hivyo kifungu cha 'kama jimbi' chatupa mazingira yake ya matumizi na ambayo yawafiki bila tashwishi yoyote. Mfano wa tanakali katika chururu na ndondondo watokea katika muktadha wa utekaji maji au utiririkaji maji. Japo imetumiwa kisitiari, imetumiwa katika mazingira inamofaa. Haihitaji vifungu zaidi vya kuelekezea matumizi yake.

Wa tatu kidogo ungetatanisha. Unafanana na ule wa kufananishia weusi, ambapo weusi husemwa ni wa tititi. Hata hivyo neno vyazi[6] ambalo ni 'titika' laondoa utatanishi huo ambao ungetokea. Ukariri wa kipashio mwe! mwe! mwe! katika mfano wa mwisho, umesisitiza maana ya neno mweka, ambapo mwe ni kiambajengo kimojawapo chake.

Kwa hivyo matumizi hayo yametokea kwa mvuto na kutumiwa mahali ambapo yanafaa kisintaksia, hali ambayo inakuza ile toni ya uwasilishaji, ambayo sasa yatokea vizuri.

## TAMATHALI ZA USEMI ZINAZOLINGANISHA TABIA

### TASHBIHA

Baadhi ya mifano imo katika 10.11.1, 13.10.2, na 64.6.1 ifuatayo ni tuliyoihakiki.

5.10.1 Uwe ja paka muwele, hata nzi hakurambi
14.3.3. Haiva mnyinyiriko, mweusi kama mpingo
53.1.3 Niwe kama punda, pasipo fungu, wala kima.

Katika wa kwanza twaona picha ya kufananishwa na paka mgonjwa ambaye hata nzi hamfiki karibu. Ni ufananishi unaofaa kwani unaibusha taswira mara moja ya kile mtu anachofananishwa nacho. Hivyo ujumbe umefika vizuri na kuingia katika fahamu ya hadhira. Wa pili wapambanuka kwa kupata picha ya weusi wa mpingo. Wa tatu pia wapambanuka vizuri kwa kuujua ushenzi na upumbavu wa punda, wa kufanya kazi nzito bila tija. Umetokea kisitiari na wafaa sana katika ulinganishi huo.

Mifano hiyo imetumiwa inamofaa na yawiana na ujumbe inaouendeleza. Inatuwezesha kupata picha ya virejelewa katika matumizi hayo. Hili linapanua kile kiwango cha upambanuzi wa wahusika tajwa. Kwa mfano, katika tashbiha ya kwanza inayomrejelea msomaji yeyote, twaona picha inayosikitisha ya mhusika huyo, kuwa kama paka mgonjwa asiyekaribiwa na hata nzi - wanaovutiwa na hali hiyo, kwa sababu ya pengine harufu ya jasho la homa na kadhalika.

## SITIARI

Kwa ufupi ni kuwa, mwandishi ametumia mbinu hii kwa wingi kwa namna isiyotatiza mawasiliano.

Imetumiwa katika 23.2.1, 23.4.1, 23.5.1, 23.7.1, 49.2.1 na ifuatayo ni mifano iliyohakikiwa.

18.1.4 Mume ukuni wa koko, usipowaka wafuka
23.1.1. ulimwengu jifa, la kusimangamana
23.3.1 Ulimwengu gofu, la kuozeana
23.6.1 ulimwengu zuzu, wa kuzuzuwana

Katika mfano wa kwanza, mume amechorwa kuwa sawa na ukuni wa koko ambao huwaka na ukikosa hufuka. Wa pili waonyesha dunia kuwa ni sawa na ovu. Wa tatu waudhihirisha kama gofu huku wa nne ukiutoa kama uwanja wa kuzuzuwana.

Matumizi ya tamathali hii yafungamanisha vitu viwili vinavyolinganishwa, ambapo cha awali chabatizwa kwa kuacha sifa zake awali na kupokea za kitu cha pili. Kwa mfano, sifa za uume na ubinadamu zatoweka, na badalaye kunaibuka picha za ukuni koko wa kuwaka na kufuka. Matumizi haya yanajenga muumano na tangamano la dhati linalosisitizwa kwa ule ushabihiano wa sifa katika vitu viwili au zaidi. Yametokea kwa uzuri na yanafaa sana katika kupambanua na kujenga picha mbalimbali za vitu husika. Msanii hakuitumia tamathali hii kwa namna ya kupotosha au isiyoaminika kisanii. Kwa mfano ile picha ya uovu wa kusimangana yaaminika, kwani watu na masimango hawawezekani.

## LAKABU

Kuna matumizi haba sana ya tamathali hii katika diwani hii. Mbali na mfano huo, kuna ule wa sitara katika shairi kondoo. Hata hivyo lakabu zote zimetumiwa vizuri.

Mifano

28.1 Pulikizani wapule, shuara nikitamka
Msambe napiga kele, kudhani nina mzuka
Vuani mato muole, miuja iliyotuka
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika

Katika mfano huo twaona msanii akijipa lakabu ya 'shuara' yenye maana ya 'mlenga juu kwenye tungo bora'. Imetokea vizuri kisintaksia na kisemantiki kama kiwakilishi cha nafsi ya msanii. Ni matumizi ambayo moja kwa moja yatuelekeza kwa 'msanii'. Mazingira ya neno shuara nikitamka yamesaidia katika kupambanua anachokusudia msanii. Baada ya kupata mwangaza huo awahusisha moja kwa moja wasomaji wake katika tungo ili kuona miujiza iliyotokea. Ni mfano unaowasilika vizuri.

## TASHIHISI

Matumizi yake siyo mengi na yote yanachangia ubora wa tungo kifani

Ifuatayo ni mifano

14.1.1 Niliko ndiko ujako, peku lamwambia ungo
37.12.1 Wema umekwenda kwao, hauko tena fahamu
48.14.3 Imewatwaa safari, muda'wo ulipofika

Kutoka mifano hiyo twaona vitu kama peku, ungo, wema na safari kuwa na uwezo wa kutenda mambo ya kibinadamu kama kujua, kuambia, kwenda au kwondoka na kutwaa. Katika ulimwengu halisi, hayo hayawezekani. Yawezekana tu katika ulimwengu wa usanii - wala siyo ulimwengu halisi.

Katika matumizi ya mbinu hii, picha inayotokea ni sawa au halisi kama kile hasa kilichopewa sifa hizo. Kwa mfano, picha ya uhaishaji wa peku ni halisi kama peku lenyewe. mifano hiyo imejenga picha ambazo kisanii zina wizani unaowafanya wasomaji kuziamini. Tashihisi hizo zimetumiwa vizuri na zinamofaa.

## TAASHIRA

Haikutumiwa kwa wingi, japo yatokea vizuri. Baadhi ya mifano ni:

34.4 Sondoki chuchu ilipo, 'nganisukuma
Sikomi unambiapo, ya kwamba koma
Huilinganisha pepo, yenye huruma

66.5 Moyo sijitie kero, kujipinda kukazana
Pendo liwapo kasoro, halina tena namna
Wewe wajipa kihoro, kwa pendo lisolingana
Moyo hupendezi tena, shukuru kama wenzio

Chuchu inaashiria moja kwa moja msichana au mwanamke huku moyo ukiwakilisha jisadi au mtu. Ni matumizi ambayo yanaashiria moja kwa moja vile vitu vinavyowakilishwa. Ameitumia vizuri kwa namna isiyotatiza,siyo tu katika mifano hiyo,bali pia katika diwani nzima.

## TAMATHALI TUMBUIZI ZA USEMI

Tamathali hii imetokea vizuri japo matumizi yake siyo mengi katika diwani.

### MJALIZO

Mifano

| | | |
|---|---|---|
| 1 | 8.9.4 | Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa |
| 2 | 12.3.1 | Sili kwamba hakiwashi, sili nikafurahika |
| 3 | 18.6.1 | Ya nini kubeheneka, kitanga kila wendako |
| 4 | 33.1.4 | Nawanene wanenalo, atendaye hachi kwambwa |
| 5 | 59.2.3 | Kabisa hajisairi, hajinyanyi hajishiki |

Katika mfano wa kwanza twaona mfuatano wa viarifa (vitenzi) katika mshororo vinavyojengeka vizuri na kuwasilisha kikamilifu bila kuhitaji msaada wa viunganishi na vipashio vingine. Hilo laangazika katika mfano wa pili. Katika wa tatu viarifa kubeheneka na kitanga vimefuatana vizuri bila msaada wa viunganishi. Katika wa nne, msururu wote wa maneno ni wa vitenzi. Katika wa tano 'najisairi, hajinyanyi na hajishiki' ni vitenzi vilivyoendelezwa kwa njia ya mjalizo. Ni matumizi ya wekevu[7] katika msamiati. Imeendelezwa kwa ufanisi na kuwasilisha vizuri pasipo kuhitaji vipashio zaidi wala kukongoa mawasiliano.

## TAMATHALI ZA USEMI ZA VILINGE

Mbinu hii japo yatokea vizuri katika diwani, haikutumiwa kwa wingi.

### MDOKEZO

1 69.5 Kila kizuri dukani, muda hakipasha jicho
Kilicho kubwa thamani, ndicho niwaleteacho
Tena natuza makini, nikachagua ambacho - mdokezo
Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani

2 28.1.1-2 Pulikizani wapule, shuara nikitamka
Msambe napiga kele, kudhani nina mzuka - mdokezo

3 73.7.1-3 Hii dunia salale, ni udende
Imetambaza wavyele, pundepunde
Hebu tiani makele, msipondeke

4 54.2.3. lipi liso inda, kwa walimwengu, na lazima?
Liwe la kuonda, kukupa Mungu, lisokwama
Laiti si winda, enyi nduzangu, lau kama mdokezo

Katika mfano wa kwanza twaona kuwa msanii alikusudia kuwa "nikachagua ambacho chawafaa" lakini kwa sababu za kaida za utunzi akalazimika kutua hapo. Twaona pia kuwa alama za dukuduku hazikutumiwa lakini mfuatilio wa matukio na kisintaksia watupa mwelekeo. Katika mfano wa pili twaona kuwa alikusudia kuwa "msambe napiga kelele" na sio kele kama alivyofanya sababu ya mizani na kina. Katika wa tatu, pia kwa sababu hizo hizo, amelazimika kukata neno 'msipondeke' na kuliendeleza kama 'msiponde'. Katika wa nne, msomaji aweza kuukamilisha kwa maneno kama "mngejua, mwajua n.k.", kwa kuangalia muktadha na kupata mwelekeo.

Ni mbinu yenye manufaa ikitumiwa kwa hadhari, kwani matumizi mabaya huvunja muwala na kupotosha kimofolojia kwani huenda baadhi ya wasomaji wakachukulia kuwa maneno hayo yameendelezwa katika ukamilifu wao, na kumbe kuna vipashio vilivyofungiwa nje. Lakini Shuara hakuitumia hivyo.

**TASIFIDA**

Imetumiwa kwa kiwango haba sana. Hata hivyo imetumiwa vizuri

Imetumiwa ifuatavyo.

31.9.2 Wa kuiga si werevu, mbele hauna utungo
48.14.3 Imewatwaa safari, muda'wo ulipofika

Mfano wa kwanza warejelea upambavu na kwa sababu ya makuruhu ya matumizi ya neno hilo, limeepukwa. Limerejelewa kwa kinyume kwa njia inayotakasa toni ya usemi. Wa pili wakusudiwa kifo, lakini umetolewa kwa usafidi na hali ambayo inaondoa ile hofu, woga na ukali wa toni ya moja kwa moja. Badala yake twaona mawazo ya safari yenye uwezo wa kuwatwaa watu. Safari huleta hisia za furaha na uchangamfu. Hisia kama hizi ndizo zinazotokea japo katika kiwango kidogo kwa usemi huo wa usafidi. Mifano yote miwili imetoka vizuri kwa namna inayoondoa kero na ukali katika usemi wa kurejelea vitenzi na matokeo mabaya ya moja kwa moja.

**ISTIARA**

Matumizi yake si mengi japo hayatokei kwa udhahiri, katika diwani nzima. Wakati mwingine yahusisha hata nafaka.

9.7 Kwa umbo uchangaliya, na mwendo vile wachenda
wamepishana mikiya, na pembe juu ya anda
Na milio wakiliya, malishoni wakishinda
Ng'ombe, kondoo na punda, wote walishe pamoja

Katika mfano huu uliowasilishwa kwa njia ya fumbo, na katika muktadha wa kufumba, kuna wanyama tofautitofauti malishoni ambao wanashauriwa walishe pamoja. Muktadha halisi wa tukio hili, ni wa utunzi ambapo watunzi wa sifa mbali mbali na uwezo washauriwa wavumiliane na kushirikiana katika utunzi. Ni fumbo lililotumiwa vizuri na kwa njia ambayo haimchanganyi msomaji.

**MAFUMBO**

Kuna mafumbo yapatayo manane hivi katika tungo. Mengi yao ni rahisi kufumbiliwa. Baadhi ni magumu, kama vile ndundu, sipandi na kadhalika.

Mifano

1 6.6 Tama ndundu ipangilwe, haitaki nyandunyandu
Na umbole iumbilwe, uzuriwe kama pandu
Yanifanya nisikolwe, wala sifanyi usindu
Kilicho ndani ya ndundu, ni nini nakitambulwe?

2 51.1 Sipandi kisichokwenda, majira yanapojiri
Sipandi kinachovunda, pepo za alfajiri
Sipandi kinganipenda, katwaani sijasiri
Hakihimili safari, ndipo hashindwa kupanda

Mifano hiyo yatuonyesha jinsi mafumbo hayo yanavyotuchorea picha ambazo ni juu yetu kuzitafutia mandhari. Uzuri wa mafumbo ni kuwa humpa msomaji uhuru wa kutoa fasiri aionayo yafaa na kuthibitika. Hili humkuza msomaji kwani makini yake lazima izame kwenye matini ili kulifumbua shairi. Ndiyo maana mafumbo mara nyingi hukusudiwa waliobobea katika misingi ya lugha na tungo. Hata hivyo kuna viwango viwili au zaidi vya mafumbo. Kuna yale mazito kama yaliyomo katika mashairi ndundu, na sipandi, ya wastani kama yaliyo katika mashairi sili, nderemo, na mepesi kama yaliyo katika shairi peku na kondoo.

Yale mazito hutoa mazingira ya mawezekano mengi ya fasiri, huku fasiri zikipungua kwa yale mepesi. Kwa ufupi ni kuwa, mafumbo yaliyotumiwa yanawafaa wasomaji wa viwango mbalimbali na angalau kuna mwanya wa mwangaza unaoleta uangavu unaowaelekeza wasomaji kwa kiashiriwa. Tukirejelea mifano hiyo, twaona kuwa wa kwanza watupa siri na namna zinavyopaswa kuwekwa. Wa pili wahusu kutenda jambo ambalo halinyooki katika wakati wake. Azungumzia vitu viwili tofauti kama inavyodhihirika katika mishororo miwili ya kwanza.

## NAHAU

Matumizi ya nahau ni mengi, na mifano ifuatayo imetufaa katika kuhakiki uamili wao na umuhimu wao kisanii. Ifuatayo ni ile mizito

| | |
|---|---|
| | Zifuatazo ni Zile Nzito |
| 20.5.3 | Na izara mitaani, moyo ukafanya nzigu |
| 20.1.2-3 | Na chanda kuwa menoni, moyo ukafanya tungu |
| | Kisikufae dhikini, kikawa juu ya dungu |
| 43.3.2 | Wasemi wakutanapo, maji ya ndugu kurashwa |
| | Zifuatazo ni zile za kadiri |
| 40.6.2 | Majuto hupija, kondo'ye kinyuma, pale wishapo |
| 57.7.1 | Pato halina sakata, kupata si kwa mabavu |
| | Zile nyepesi zimo katika mifano hii |
| 1.4.1 | Katu haiwi halali, lugha kutiwa vidole |
| 70.11.3 | Na wajapo wakanyeni, dhahiri kimacho macho |

Tumetumia kigezo cha kuzoeleka, muktadha na mpangilio wa kisintaksia katika uainishi huo. Matumizi hayo yanafaa sana katika kupokea na kuendeleza ujumbe kwa namna inayomvutia msomaji. Lakini haya yanategemea aina ya nahau iliyotumiwa. Baadhi ya zile nyepesi ni zile zilizozoeleka huku za wastani zikiwa ngeni au zikitumiwa katika miktadha isiyo yao asilia, na hivyo humfanya msomaji kuyatafakari zaidi mambo yanayorejelewa kwa matumizi yazo. Nzito hutumiwa katika miktadha isiyozoeleka au kwa namna ambayo kisintaksia inaimarisha semantiki kwa kuibusha maana nasibishi katika msamiati.

## METHALI

Katika kamusi ya kiswahili sanifu imeelezwa kuwa ni; "kifungu cha maneno yaliyotumiwa pamoja kisanii kwa njia ya kufumba au kupigia mfano na ambacho kinachukua maana ndefu na pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa; muhtasari wa maneno ya kisanii wenye maana pana".

Kwa sababu ya kufuata kanuni za utunzi wa ushairi, methali hupunguzwa au huongezwa baadhi ya vipashio katika maumbo yao na hufanywa hivyo kisanii kusudi zisije zikapoteza maana zao asilia. Ifuatayo ni mifano.

| | |
|---|---|
| 12.8.3 | Shikana ushikwapo, majuto mbele hayaji |
| 16-17.1-9.4 | Mume ukuni wa koko, usipowaka wafuka |
| 20.1-6.4 | Ukitumai cha ndugu, wafa uli maskini |
| 21-22.1-7.4 | Mwenda somea maiti, huondoka na ujakawe |
| 29.10.3 | Mchezea maji male, hazami akaibuka |
| 71.15.1 | Nawambia fahamuni, ki nguoni kiwalacho |

Methali hizo zimetumiwa zinamofaa na zinawasilisha ujumbe kwa njia ya busara. Baadhi zimegeuzwa maumbo kwa njia ambazo zazipa uwezo zaidi kuliko ule wa kawaida uliozoeleka. Baadhi ni zile ambazo zatumiwa katika maeneo fulani fulani ya uswahilini. Kwa ufupi ni kuwa, japo zimetumiwa kitanakali, kisitiari, kimafumbo na kinahau, zawasilisha kiuangavu na vizuri, pote zilipotumiwa katika diwani.

## MATOKEO YA TAMATHALI ZA USEMI

### TASWIRA

Matumizi ya lugha na vipengele vingine vya fani yamesaidia kutujengea taswira nyingi sana, ambazo si ngumu kueleweka.

Mifano

66.6 Lilipokuwa li sawa, pendo limetangamana
Lilikuwa limetuwa, tena mkisikizana
Madhali limepunguwa, haliji japo pindana
Moyo hupendezi tena, shukuru kama wenzio

Hapa twapata picha ya pendo lililoshikana ambalo sasa limevunjika na hakuna bidii itakayoliunga likatengenea.

23.3 Ulimwengu gofu, la kuozeana
Una udhaifu, wa kutatizana
Huzidi machafu, hisabu hayana
Na waaminifu, kwa kukosekana

Hapa pia twachorewa picha ya ulimwengu wenye uozo juu ya uozo na ambapo matokeo yake ni udhaifu unaotatiza pamoja na machafu mengi, kiasi kwamba waaminifu hawapo.

Japo mifano hiyo yajenga fikirani mwa wasomaji picha za dhahania, yawawezesha kuona, kuhisi na kutafakari. Kuna ile yenye nguvu sana inayotokea katika baadhi ya beti kama, 36.1, 36.6, 37.12, 33.1 ambayo kwa matumizi ya tamathali kadha yaibusha hisia za moja kwa moja ambazo zagusa fahamu za wasomaji.

## 4.2.5 MATUMIZI YA LUGHA KWA JUMLA

Kwa kiasi kikubwa lugha imetumiwa vizuri katika fani zake zote. Hakuna makosa katika viwango vya fonolojia na mofolojia yanayotatiza maana na mawasiliano. Hata hivyo kuna baadhi ya vipashio vya mofolojia ambavyo siyo rahisi kuchanganuka siyo tu katika kiwango cha maana, bali pia cha kuwasilisha. Vinahitaji makini na kuelewa muktadha ili kuelewa maana zao. Kwa mfano katika shairi si wamwe, 64.4.2, kuna matumizi ya "Jifanye babu mjaja, kila mahali utumwe".

Fikira za kwanza zitakazompitia msomaji ni kuwa, kifungu "babu mjaja" kimeendelezwa vibaya. Kitachukuliwa kumaanisha babu mjanja, na kumbe ni jina la mtu. Makini ni muhimu kupatiwa uzito katika kusoma vifungu kama hivi. Hata hivyo mafungu ya maneno yenye mielekeo kama hii si mengi.

Baadhi ya makosa yaliyotambuliwa yapo katika, kwanza, matumizi ya baadhi ya tamathali za usemi kama vile tanakali sauti. Kwa mfano, katika ukurasa wa 4.5.2 ametumia tanakali ya 'kwinyo! kwinyo! kuashiria kushindwa kwa jogoo, lakini katika muktadha tanakali hiyo inawakilisha ushindi. Inatuelekeza zaidi kwenye ushindi kuliko kushindwa.

Katika matumizi ya msamiati, kumetumiwa baadhi ambao hauna nafasi kubwa, na wakati mwingine unatatiza muwala wa kutiririka habari. Kwa mfano katika 66.5.3.1, mshairi ametumia neno 'wewe' kama msisitizo na halileti nguvu hizo zinazotarajiwa. Badala yake matumizi yake yanashukiwa. Hivi ndivyo alivyolitumia "wewe wajipa kihoro, kwa pendo lisolingana" kungekuwa na nguvu kama kungekuwa na maendelezo kama; "Nawe wajipa kihoro, kwa pendo lisolingana."

Kuna pia maendelezo mabaya ya kisintaksia katika mfano huu:

53.1.9 Wengi watu si wazuri, nyoyo zao zina wingu, uovu hulala kwake.

Tatizo limo kwenye neno'kwake' ambalo lilipaswa kuwa 'kwao'. Hata hivyo japo tutalihukumu kama kosa, ni zao halali la matumizi ya uhuru wa kishairi, katika kiwango cha mofolojia na mpangilio wa maneno (kisintaksia).

Katika 73.7.1 kuna mfano huu:

"Hii dunia salale, ni udende."

Mfano huo umekosa kuandamana na uakifishi wake, na hivyo hautoki kwa nguvu. Kwa mfano, kama kungetokea alama kama ya nidaa au mshangao neno salale lingetoka kwa nguvu.

Hata hivyo makosa yanayotokea humo kama hayo tuliyoyaangalia si mengi na hayakwamishi mawasiliano ambalo ndilo lengo kuu la msanii yeyote. Amefanya hivyo kwa ufundi unaotufanya kuona udhibiti wake wa hazina hii kuu ya mawasiliano.

Kuna matumizi mengi ya msamiati wa lahaja ya kimrima na wa ukale, ambao japo waidhinishwa kwa uhuru wa kishairi, watatiza sana kwa wale ambao ndio wanainukia katika kuulewa ushairi. Ni maendelezo yanayofaa wasomi na waliojifunza lisani ya kimrima na lahaja za uswahilini zote.

Kuna pia matumizi ya kuchanganya ndimi (za lahaja na lugha). Kuna matumizi ya msamiati wa kiswahili na kiarabu. Hata hivyo ule wa kiarabu sio kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya maneno yaliyotumiwa ya kiarabu ni pamoja na Ihtiramu, athama, thuma, Qahari, Ghafuru, Rabuka na mengine. Yametumiwa kwa njia nzuri.

Ni kwa sababu hizo twahitimisha kuwa msanii ameitumia lugha vizuri kama inavyompasa msanii yeyote anayetaka kuwasilisha kwa ufundi mzuri kwa wasomaji wake.

## 4.3 WAHUSIKA

Msanii ametusawiria wahusika mbalimbali ambao ni pamoja na Mungu, wanadamu, wanyama, miti, vitu na hata mahali. Wote watokea kwa utaratibu unaomwezesha msomaji kuona namna walivyotumiwa. Ingawa hatukuwapitia wote kwa undani, tumeangalia baadhi yao.

Vifungu vifuatavyo vilituongoza katika kuona jinsi Mungu alivyosawiriwa.

| | |
|---|---|
| 23.6.4 | Bado hujafuzu, mwombe Rabbana |
| 47.2.1 | Amekuumba Qahari, kwa umbo la kupambika |
| 47.3.1 | Tizama ya mungu siri, kukuumba'we hakika |
| 47.5.4 | Kwa rehemaze Rabuka, mwanaadamu fikiri |
| 47.8.2 | Mikononi mwa Muniri, kukutia akitaka |
| 47.7.4 | Ya mola kutoyashika, mwanaadamu fikiri |
| 30.3.2 | Mcha Mungu si mtovu, kwalo sijitie pengo |
| 48.9.4 | Moliwa wamuepuka, mwanaadamu fikiri |
| 53.1.6 | lilo baya ama zuri, yote ni ne'ma ya Mungu, lakini yasitirike. |
| 54.2.2 | Liwe la kuonda, kukupa Mungu, lisokwama |
| 55.2.1-2 | Sili naapa mwenyezi, Jina la mola Rabuka<br>Kwamba'ye ndie mwokozi, mtenzi vikatendeka |

Mifano hiyo yatuelekeza kwenye baadhi ya sifa za Mungu katika sifa nyingi alizonazo. Yeye ndiye muumba na mtoa vyote vilivyomo humo duniani. Kwa hivyo milki yote hiyo aliyotupa kutuendeshea maisha yatupasa kutufanya kumwona kama mfadhili mwema ambaye yafaa tujenge uhusiano mzuri naye. Badala yake twaona namna mwanadamu alivyo mwepesi katika kumsahau Mungu. Japo hatukunukuu vifungu vyote ambavyo vyamrejelea Mungu, kuna mahali ambapo twahimizwa kutubu, kwani yeye ni mwingi katika kutoa toba. Sifa ambazo amesawiriwa nazo diwanini ni zake na msanii hakupotoka katika kumsawiri jinsi alivyo. Hata mahusiano baina ya waja na Mola wao ameyajenga kwa njia nzuri. Maneno mbalimbali aliyoyatumia kumrejelea Mungu ni ya sifa zake na hivyo hayapotoshi. Kwa hivyo, msanii amemsawiri Mungu vizuri na kumhusisha na sifa na matendo yaliyo yake.

Kuhusu wahusika watu, kuna msanii mwenyewe, wasomaji, wahusika maalum,

Kuhusu wahusika watu, kuna msanii mwenyewe, wasomaji, wahusika maalum, washairi, watumizi wa lugha, wazee, vijana, walezi, wapotofu, wanawake, wanaume, ndugu, wafanya kazi na wengine. Hao wote amewachora kwa namna inayowapa nafasi tukawaona pamoja na ule umuhimu wao. Tumefafanua baadhi ya sifa za aina hizo za wahusika alizotuchorea.

Katika baadhi ya mashairi, mshairi mwenyewe ahusika katika kutusimulia na kutuelezea anayoyataka. Katika kufanya hivyo nafsi ya kwanza na tatu zatumiwa na moja kwa moja awashirikisha wasomaji wake kwa njia ya maswali au awahusisha kitashtiti. Mifano hii miwili yafaa katika kuthibitishia kauli

20.4 Ndugu asiye imani, ingawa ya vuguvugu
Chake usikitamani, pataingia vurugu
Mtoleane undani, utamani funga bugu
Ukitumai cha ndugu, wafa uli masikini

4.4 Nawakongoa wa kole,wenye kunge na sombombi
Nikawapasua mbale, kwa nzumari na firimbi
Sembuse wewe bungule, taa usiye utambi
Kila mtunzi potole, hajakomaa ulumbi

Mifano hiyo yatuonyesha nafsi ya masimulizi au maelezo. Umuhimu wa matumizi haya ni kuwa yanatuwezesha kuamini tungo ambazo sasa hatuzioni kama zilizo mbali na maisha halisi. Kwa uhusika wa msanii na wasomaji, japo hawamjibu moja kwa moja watokea kwa ukamilifu unaotufanya kuziamini.

Mwandishi pia atuchorea wahusika watu wenye silika mbalimbali. Kuna wale waovu na wapotofu wasioshauriwa wakashaurika. Amewaelezea kwa undani katika mashairi kipwipwi na mnenwa. Wengine ni makafiri waliomtenga Mungu wao ambao wameangaziwa katika shairi tafakuri. Kuna wale waliotopewa na mzigo wa ulezi ambao wameangaziwa katika mashairi mlezi na uhunzi. Wengine ni wanawake wa hadhi mbalimbali. Kuna wakewenza wanaopigania mapenzi ya mume. Kuna na wale wenye tabia mbaya hasa za ubadhirifu ambao wamesawiriwa katika shairi 'si wamwe'. Kwa jumla ni kuwa msanii amewatumia wahusika katika mandhari yao na wanawasilisha ya wajibu.

Wengine ni wazee na vijana ambao wamesawiriwa kisitiari kama peku, na ungo. Tunaona uhusiano wao na jinsi vijana walivyoghilibika na maungo yao ya ujana wakidhani hawatazeeka. Pia msanii atuchorea uzee wa kifakiri akitahadharisha kuwa mali itafutwe wakati wa ujana.

Kuhusu watunzi wapotofu awaonya na kuwashauri kuzama zaidi kabla ya kufikiria utunzi. Atetea hadhi ya lugha na tungo akihimiza na kushauri matumizi mazuri. Kuhusu ndugu ashauri wajitegemee kusije kukatokea aibu. Mahusiano ya kutumia cha ndugu ayapiga marufuku kupitia usawiri wa uhusiano mbaya pale kutegemea kunapotokea.

Wengine ni wahusika maalum ambao amewataja kwa majina, na ambao baadhi ni washairi wenzake kama vile sitara, ambaye atuelezea kuwa si mnene hivyo ashtumu unene usio wa kufidiya na thamani inayohusishwa na maumbo ya watu. Kila moja ni binadamu na licha ya umbo hakuna haja kudharau na kupuuza watu kwa ajili ya maumbo yao.

Kwingineko ametumia wahusika ndege, mimea, na wanyama. Kwa mfano, kwa njia ya mafumbo awashauri kondoo, mbuzi, ng'ombe na punda walishe pamoja akikusudia watunzi wa viwango mbalimbali. Twaona kwamba wahusika hao wote waendeleza ujumbe wa aina fulani japo ni wanyama, mimea, na ndege. Kuna shairi "Nazi" ambalo lashtumu na kudhihaki ujinga wa nazi, ambapo matumizi haya ya kisitiari yamrejelea mhusika ambaye ana manufaa mengi yasiyomfaidi kwa sababu ya ushenzi wake.

Kwa ufupi ni kwamba amewasawiri wahusika wake kwa uzuri na ukamilifu. Hata wale aliowasawiri kimafumbo na kisitiari hakuwapa sifa za ajabu zisizoweza kuaminika na kufasirika na kutumiwa katika mazingira ya adinasi. Wote amewapa sifa zinazohimilika na zilizo zao. Amewatumia katika mazingira ambamo wanafaa.

## 4.4 MTINDO

Hapa tumeangalia maumbo ya tungo zilizomo na hatimaye jinsi msanii alivyowasilisha mawazo yake. Diwani hii ina mashairi 56 yenye beti 461. Shairi fupi zaidi kwa idadi ya beti ni 'siri', ambalo lina beti 2 huku lile refu zaidi lenye beti 16 ni uke wenza.

Shairi moja ni la beti nne, manne ya beti 6, sita ya beti 12, mawili ya beti 13, moja la beti 16, moja la beti 11, matatu ya beti 10, kumi ya beti 9, mawili ya beti 8, kumi na nane ya beti saba, mawili ya beti 15, na moja la beti 14.

Wahariri wa diwani hii ambao ni Mohamed Kamal Khan na Hassan Msami wanasema hivi; "Mwalimu Mbega ametumia bahari tisa na mikondo kadha wa kadha. Bahari zenyewe ni za Tathlitha, Tarbia, Takhmisa, Tasdisa, Ukawafi, Msuko, kikwamba, Tumbuizo na Mandhuma".

Tuligundua kwamba bahari ya Tasdisa haimo katika diwani hii kama wanavyotudokezea wahariri hawa. Kwa hivyo bahari walizozitambua na kuzielezea ni nane, tukiondoa hiyo ya Tasdisa. Hata hivyo kwa kuzingatia vigezo mbalimbali tuligundua kwamba msanii ametumia bahari zipatazo kumi na nne. Zile walizoziacha wahariri hao ni za Asharia, Kikai, Upindu, Ukara, Mtiririko, na sakarani. Ushahidi wa sakarani watokana na kutambuliwa kwa bahari zaidi ya moja katika shairi kwa kutumia vigezo mbalimbali.

Kwa kutumia kigezo cha mwongozo wa mishororo tunapata bahari za Tathlitha, Tarbia, Takhmisa, Ashara na Msuko. Tungo nyingi zaidi ni zile za mtindo wa Tarbia. Katika Tathlitha kuna mashairi, Domo, Chuchu, Tata, Malimwengu,

Ndundu, Ah, Kondoo, Nderemo, Peku, Chururu, Ukuni wa koko, Tumaini, Ujaka, Ulimwengu, Nazi, mtenda jambo Asishe, Hila, Mpewa Sumu hafile, uvumilivu, uhunzi, utendi, Wema, Mlezi, ukiwa, Mwosha, Sifa, Malifi, Tafakuri, Uzee, Sipandi, Fadhili, Si wamwe, Moyo, Ni kheri mke muole, uke wenza, Dunia na Msopeko.

Bahari ya Takhmisa imetumiwa katika mashairi kipwipwi na upasi.

Nayo bahari ya msuko yadhihirika katika mashairi, sili, upishi, Nileje?, Masimango, Biri, Voro, na kujigamba.

Bahari ya Ashara (Ukumi) imetumiwa katika shairi 'siri'.

Kwa kufuata kigezo cha mizani tunapata bahari za kikai, ukawafi, na Tumbuizo, ingawa hizo mbili za nyuma pia zatambulika kwa sababu ya mwongozo wa vina. Bahari ya kikai yabainika katika shairi ulimwengu la Tarbia ya mkondo wa 6x6 na pia katika 'Nazi' ambalo pia limeendelezwa katika mkondo wa mizani 6x6. Kikai ni bahari ambayo ina mishororo minne na mizani isiyotimia 16. Ina mikondo mingi kama ya 8x4, 8x6, 8x3, 6x6, 8x6 na kadhalika. Mifano ni mingi lakini hiyo miwili inatosheleza.

Bahari yenye mizani mingi zaidi ni ya Tumbuizo, ambayo ina mizani 24 katika mkondo wa 8x8x8 katika kila mshororo. Ile ya ukawafi huwa na idadi sawa ya vina (yaani vitatu) lakini vyenye mizani isiyotimia 24 vya mikondo kama ya 8x6x5, 6x6x5 na kadhalika. Mizani katika ukawafi huwa si mingi kama inavyodhihirika katika mashairi malimwengu lenye mizani ya mkondo wa 6x5x4 na 'upasi' lenye mizani ya mkondo wa 6x6x5.

Kwa kuongozwa na kigezo cha vina, tunapata maumbo ya vina viwili (mathnawi) na vina vitatu kama inavyodhihirika katika bahari za ukawafi na Tumbuizo. Kina cha kwanza ni cha ukwapi, cha pili ni utao, na cha tatu ni cha mwandamizi. Kina cha nne ambacho ni ukingo hakimo katika tungo hizi. Mashairi mengi ni ya mgao wa mathnawi, yaani wa ukwapi na utao. Ni mashairi matatu tu yenye mgao wa vina wa utatu, ambayo ni, malimwengu, upasi na Siri. Pia katika mashairi mengi vina vimekaririwa. Hivi vyatupa ushahidi wa bahari ya mtiririko ambayo huwa na vina vya keketo (irabu moja) toka ubeti wa mwanzo hadi wa mwisho, katika ukwapi na utao.

Kuna ushahidi pia wa bahari ya ukara katika mashairi kama chururu, Peku, Tumaini, na mengine ambapo kina cha utao kimekaririwa au umbo la kina hicho limekaririwa katika shairi zima.

Kuna kile ambacho tumekiita **'kipotoukara'** ambapo kina cha ukwapi chabadilika toka ubeti mmoja hadi mwingine huku cha utao kikitiririka. Bahari hii yathibitika katika shairi 'ulimwengu' ambapo kuna vina vipatavyo saba vya ukwapi huku cha utao kikiwa kimoja tu.

Kigezo cha msamiati kinatuongoza katika kupata bahari ya kikwamba ambayo imetumiwa katika mashairi, "nileje?", 'malimwengu', 'sifa', 'sipandi', 'Fadhili', 'upasi', 'Wema' (baadhi ya beti), 'Sili', 'Ah', 'Domo', 'Sikutaki', na 'Dunia'. Bahari hii hutambulika kwa kuwa na neno au fungu la maneno mwanzoni mwa kila ubeti au mshororo ambalo linarudiwarudiwa katika kuanzishia mishororo mipya au beti mpya. Hata hivyo kuna mtindo mwingine wa bahari hii wa kukariri neno moja au fungu la maneno katika sehemu ya kipande cha utao, au mwandamizi. Kwa mfano, katika shairi malimwengu, neno malimwengu limekaririwa katika mishororo yote ya kina cha utao, huku vipande vya ukwapi na mwandamizi vikiwa vya maneno yanayobadilikabadilika.

Mtindo wa upangaji mawazo na mishororo unatuongoza katika kupata bahari za mandhuma na upindu. Katika mandhuma kuna mpangilio wa ukwapi kutoa wazo na utao kutoa jibu. Mtindo huu washuhudika katika mashairi, Tata, Sikutaki, Dunia na mengine. Mtindo wa upindu wa kuchukua kibwagizo cha mshororo wa ubeti awali au fungu la kibwagizo awali kuanzishia ubeti mpya pia watambuliwa humo. Baadhi ya mashairi yaliyoendelezwa hivi ni, Tumaini, Mtenda jambo asishe, msopeko, Chururu na mengine. Ufuatao ni mfano

16.2.4 -> 16.3.1

Chururu siyo ndondondo, na ndondondo si chururu
Na ndondondo si chururu, boko hushindwa na wando

Twaona hapo aina ya pindu inayotokea, na inatokea katika beti hizo mbili tu za shairi.

Katika mandhuma, kuna mtindo wa ukwapi kutoa wazo na utao jibu na baadhi ya mifano, ni mashairi, Tata, Sikutaki, Dunia na mengine.

Mshairi ametumia vina vipatavyo 63 katika maumbo tofautitofauti yapatayo manne hivi. Umbo la kwanza ni lile fululizi au tiririshi ambalo ladhihirika ifuatavyo

| 1-2:1-14 | 3:1-8 | 4-5:1-13 | 7-9:1-9 | 24:1-7 | 28-29:1-10 |
|---|---|---|---|---|---|
| li le | zi mbe | le mbi | vyo zwa | zi wa | le ka |
| li le | zi mbe | le mbi | vyo zwa | zi wa | le ka |
| li le | zi mbe | le mbi | vyo zwa | zi wa | le ka |
| li le | zi mbe | le mbi | vyo zwa | zi wa | le ka |

| 34.1-7 | 35:1-7 | 40:1-6 | 44:1-6 | 49-50:1-12 | 52:1-7 |
|---|---|---|---|---|---|
| po ma | nda ki | ja ma po | eo vya | ri pa | sa zi |
| po ma | nda ki | ja ma po | eo vya | ri pa | sa zi |
| po ma | nda ki | ja ma po | eo vya | ri pa | sa zi |
| | | ja ma po | eo vya | ri pa | zi |
| | | ja ma po | | | |

| 53:1-12 | 54:1-7 | 57:1-7 | 59:1-4 | 60:1-7 |
|---|---|---|---|---|
| ri ngu ke | nda ngu ma | ta vu | ri ki | zi ri |
| ri ngu ke | nda ngu ma | ta vu | ri ki | zi ri |
| ri ngu ke | nda ngu ma | ta vu | ri ki | zi ri |
| ri ngu ke | | vu | ri ki | ri |
| ri ngu ke | 61:1-7 | 62-63:1-13 | 64-65:1-8 | 74:1-7 |
| ri ngu ke | nywa ki | ki aa | ja mwe | mi ma |
| ri ngu ke | nywa ki | ki aa | ja mwe | mi ma |
| ri ngu ke | nywa ki | ki aa | ja mwe | mi ma |
| ri ngu ke | | | | |
| ri ngu ke | | | | |

| 67-68:1-12 | 72-73:1-9 | 79:1-7 |
|---|---|---|
| la wa | le nde | mbi mba |
| le wa | le nde | mbi mba |
| le wa | le nde | mbi mba |
| le wa | le nde | mba |

umbo la pili ni lile la upindu na ladhihirika kama ifuatavyo

| 6:1-7 | 9-10:1-15 | 11-12:1-9 | 14-15:1-10 | 16-17:1-9 | 18-19:1-12 |
|---|---|---|---|---|---|
| lwe ndu | ya nda | po ji | ko ngo | ru ndo | ka ko |
| lwe ndu | ya nda | po ji | ko ngo | ru ndo | ka ko |
| lwe ndu | ya nda | po ji | ko ngo | ru ndo | ka ko |
| ndu lwe | nda ya | ji po | ngo ko | ndo ru | ko ka |

| 20:1-6 | 21-22:1-7 | 25-26:1-12 | 27-28:1-9 | 30-31:1-11 | 32:1-7 | 33:1-7 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ni gu | we ti | nda she | we po | vu ngo | wa mbe | mbwa lo |
| ni gu | we ti | nda she | we po | vu ngo | wa mbe | mbwa lo |
| ni gu | we ti | nda she | we po | vu ngo | wa mbe | mbwa lo |
| gu ni | ti we | she nda | po we | ngo vu | mbe wa | lo mbwa |

| 36-37:1-12 | 38-39:1-9 | 41-42:1-9 | 43:1-6 | 45-46:1-9 | 47-48:1-15 | 51:1-7 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ao mu | zi mba | wa ko | po wa | bu ni | ri ka | nda ri |
| ao mu | zi mba | wa ko | po wa | bu ni | ri ka | nda ri |
| ao mu | zi mba | wa ko | po wa | bu ni | ri ka | nda ri |
| mu ao | mba zi | ko wa | wa po | ni bu | ka ri | ri nda |

| 69-71:1-16 | 77-78:1-9 | 58:1-7 |
|---|---|---|
| ni cho | ko kwa | nje pwa |
| ni cho | ko kwa | nje pwa |

| | | |
|---|---|---|
| ni cho | ko kwa | nje pwa |
| cho ni | kwa ko | pwa nje |

Umbo la tatu ni lile la kipotoukara ambapo vina vya ukwapi vyabadilika toka ubeti mmoja hadi mwingine huku vya utao vikibaki hivyo hivyo. Ufuatao ni mfano, 23: 1-7,

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 fa na | 2 fi na | 3 fu na | 4 za na | 5 zi na | 6 zu na | 7 zo na |
| fa na | fi na | fu na | za na | zi na | zu na | zo na |
| fa na | fi na | fu na | za na | zi na | zu na | zo na |
| fa na | fi na | fu na | za na | zi na | zu na | zo na |

Aina ya nne ni ile ya ukarapokevu[8]. Aina hii yadhihirika ifuatavyo.

| 55-56:1-12 | 75-76;1-9 |
|---|---|
| zi ka | ro rwa |
| zi ka | ro rwa |
| zi ka | ro rwa |
| zi | ro |

Umbo la tano ni lile Tabdilifu[9] ambalo labainika katika mifano miwili ifuatayo.

| 12-13:1-10 | 66:1-7 | |
|---|---|---|
| shi ka | ro na | maelezo kuhusu aina hizi |
| shi ka | ro na | mbili za vina yametolewa |
| shi ka | ro na | katika sehemu ya tanbihi. |
| Ish | na io | |

Wa sita na mwisho ni ule wa msuko. Ni mtindo wenye vina haba katika ukwapi, na zaidi katika vya utao. Ufuatao ni mfano

| 57:1-7 | mwingine ni 79:1-7 |
|---|---|
| ta vu | |
| ta vu | mbi mba |
| ta vu | mbi mba |
| vu | mbi mba |
| | mba |

Katika mifano yote utao una vina vinne, huku ukwapi ukiwa na vitatu.

## MITINDO YA UWASILISHAJI

Mwandishi ametumia mitindo ya usimulizi, maelezo, na uulizi maswali. Amefanya hivyo kwa namna inayofaa, kwani haja kubwa ya kazi hizo ni kuwasilisha,

na siyo kuwasilisha tu, bali kuwasilisha kwa uzuri. Mitindo hiyo haichoshi na ameitumia vizuri.

Kwa ufupi ni kuwa mwandishi ametumia mitindo inayofaa na kufahamika katika tungo zake. Hata pale anapotumia minasibisho, tamathali, balagha, mafumbo, na hata sitiari, amefanya hivyo kwa namna inayompa hamu msomaji kusoma kazi yake. Kwa jumla ametumia mtindo unaofaa kisanii. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya mitindo hiyo.

56.10 Sili hajipa simazi, hataka kuazirika
Na kupata umbulizi, ya nini kuja umbuka?
Heri kiliwe na njuzi, au fungo au paka
Nileje tokoro hizi?

Katika ubeti huo kuna mtindo wa uulizi maswali ya balagha na ya kawaida kama inavyodhihirika katika mshororo wa pili na katika kibwagizo.

16.2 Mola aloamuru, huwa halina mavundo
Ungapapa na kukuru, ni kuumiza maondo
Na akili kukuduru, mawazo yakenda kando
Chururu siyo ndondondo, na ndondondo si chururu.

Hapa mtindo wa maelezo wadhihirika na umetokea vizuri. Mtindo wa usimulizi umetumiwa katika mfano ufuatao.

20.6 Niliyaona zamani, pande hizo za kiwegu
Ukazuka ukakani, Ba mwarizo na mwadegu
Ikawa yani ni yani, kisa kuombana mbegu
ukitumai cha ndugu, wafa uli maskini.

Ufuatao ni mfano wenye mseto wa tashtiti, kuuliza maswali, na ushawishi japo hautokei kwa nguvu, pamoja na usafidi wa aina fulani.

48.14 Wawapi watu wa kheri, mitume ilotukuka
Pamoja na answari, na swahaba kadhalika
Imewatwaa safari, muda'wo ulipofika
Sembuse wewe kitaka, mwanaadamu fikiri

Kwa ufupi hiyo ndiyo baadhi ya mifano iliyotuwezesha kuona mitindo aliyoitumia msanii katika uwasilishi wake wa mawazo.

## 4.5 MANDHARI

Mshairi ametengea tungo zake, mandhari mbalimbali, yakiwemo ya utunzi, unyonyaji, unyumba, mapenzi, ulezi, mahusiano ya kijamii, utendaji kazi, majumbani, mapishini, kilimoni, kidini, kimalishoni na kadhalika.

Yote ameyapa sifa zinazofaa na kuoana nayo. Kwa mfano katika shairi mwosha twapatiwa sifa za mwosha, mazingira ya kufanyia kazi hiyo, na jinsi maiti wanavyolazwa kuoshwa na kisha kuzikwa. Ni shairi linalotupa picha ya umauti, namna maiti anavyokaa na mengineyo. Yote hayo yanatokea kwa namna inayowafiki mazingira yaliyoteuliwa.

Kuhusu mandhari ya ulezi twajengewa picha nzuri ya mahali unapotekelezewa na namna unavyotekelezwa. Aina ya picha tunazozipata kwa maelezo zafaa na zaaminika. Hata msamiati aliouchagua kuendeleza ujenzi huo wa mandhari wafaa. Wahusika aliowatumia ni wale wanaofaa katika mazingira hayo. Ni mandhari yanayohusisha mashairi kama uhunzi linalorejelea ulezi kwa njia ya sitiari, na mlezi. Twaona picha ya usumbufu mwingi.

Mandhari ya usanii bora ameyaendeleza vizuri huku akituwasilishia viwango viwili vya wasanii, wale wapotofu na wale imara. Mwito wake kwa wasomi, ni wapuuze wasanii wanaotumia lugha chafu au kwa uchafu katika tungo na wale wa kiwango cha chini ambao tungo zao haziridhishi.

Katika mahusiano ya kijamii atupa mandhari ya tabia mbaya zinazodhihirika katika uvunjaji wa nyumba za watu, wahusika wasioshaurika wala kuonyeka, na maasi ya maadili ya kijamii. Mandhari haya nayo yatokea vizuri. Baadhi ya mashairi ambamo yajengeka ni yale ya mashairi msopeko, kipwipwi, na kadhalika.

Mandhari ya kidini nayo yadhihirika kwa uzuri ambapo mahusiano mabaya baina ya binadamu aliyeghafilika na hawaa za ulimwengu na Mola wake yajengwa kwa uzuri na msamiati uliotumiwa hapa ni ule unaofaa. Mshairi awakumbusha waja juu ya fadhila mbalimbali za mwenyezi Mungu na kuwashawishi wayataliki maovu yote na wafuate njia za mungu. Mandhari haya yatokea kwa uzuri katika shairi Tafakuri.

Mahusiano ya wapenzi na unyumba yameendelezwa katika mashairi kama chuchu, sikutaki, si wamwe, moyo, ni kheri mke muole na uke wenza. Yametokea na kupambanuka vizuri, kwa namna inayoaminisha kuwa kuna ukweli wa yaliyomo katika mazingira haya. Wahusika waliotumiwa humo wanafaa. Hata yale wanayoyafanya humo yanafaa na kama hayafai, basi yawezekana katika mazingira hayo.

Mandhari ya unyonyaji yametokea kwa uzuri ambapo 'Nazi' - mhusika wa kisitiari - akubali kunyonywa na bidii yake yapotea bure. Haya ni mandhari ya kiuchumi. Ni mandhari ya wahusika wenye manufaa mengi kupunjwa. Mshairi ashtumu hali hii inayotokea kwa sababu ya ujinga wa mnyonywa. Ni mazingira yaliyosawiriwa vyema.

Kwa muhtasari ni kwamba, msanii ameyajenga mandhari kwa namna ambayo inayafanya kupambanuka kwa uzuri huku yakipokea aina ya wahusika wanaofaa katika kuwasilisha aina ya mawazo anayoyaendeleza. Baadhi ya mandhari ni ya kidhahania,

kwani yanapokea ujumbe na wahusika wa sitiari na mafumbo. Kwa mfano, ametumia wahusika, ng'ombe, punda, kondoo na mbuzi katika mazingira ya malisho ambayo ni ya kimafumbo. Yanakusudiwa kuwa ya utunzi - kwamba yafaa watunzi washirikiane. Kwa hivyo, kwa njia ya mafumbo na sitiari twapambanuliwa aina zingine za mashairi.

## 4.6 PLOTI

katika takriban mashairi yote yaliyomo katika diwani hii yameendelezwa kwa njia ya ploti ya mtiririko au fululizi.

Matukio yameelezwa au kusimuliwa kwa namna ambayo ni ya muwala. Matukio yanashikana kwa njia nzuri.

Mpangilio wa matukio au maelezo watupa dalili za mwanzo, mwili na hitimisho katika kila shairi. Sehemu hizo tatu zilipendekezwa na Aristotle, ambaye alisema kuwa lazima zote ziwepo katika mtindo uliotimia. Ifuatayo ni baadhi ya mifano.

28.1 Pulikizani wapule, shuara nikitamka
Msambe napiga kele, kudhani nina mzuka
Vuani mato muole, miuja iliyotuka
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika

29.7 Umdhanie yulele, yulele kutazinduka
Huwa yu ngezi akele, akele akimulika
Akuonapo u vile, u vile asivyotaka
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika

29.10 Nikomapo sendi mbele, mbele kusikokwendeka
Najinega muambale, nacha yale mapotoka
Mchezea maji male, hazami akaibuka
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika

Mifano hiyo inawakalisha sehemu tatu ambazo ni za mwanzo, mwili na mwisho na maneno yamepangiliwa kwa namna ambayo inaonyesha kuwa sehemu fulani ni mwanzo, ya kati au ya mwisho. Hata hivyo kuna baadhi ya beti ambazo zimetumiwa kuanzishia shairi ambazo hazionyeshi moja kwa moja kuwa ni mianzo.

Sehemu ya mwili ambayo ndiyo yenye maelezo pia yatambulika moja kwa moja na afikapo hatima, atuelekeza kuwa amefanya hivyo. Miisho ya mashairi mengi inadhihirika kwa uwazi kuliko mianzo. Hata hivyo mitindo mbalimbali ya kuanzishia mashairi iliyopo haimaanishi upungufu. Mitindo mingi ni mizuri ili kuondoa uwezekano wa uchoshi wa aina moja ya mtindo.

Kwa mfano katika shairi Tafakari aanza kwa kumwuliza mwanadamu maswali ya alikotoka. Baada ya kumkumbusha alikotoka amwelekeza na kumrejesha kwenye maisha ya tumboni, kuzaliwa vizuri na kwa umbo zuri, kufadhiliwa kwa kunyonya, kukua na kupata umri, kuwa imara kimwili na baada ya fadhila zote hizo, twaona uasi. Katika sehemu hii, mshairi amkumbusha neema na fadhila mbalimbali za kuhusu mwenyezi Mungu. Amshawishi na kumrejesha nyuma kwa wengi ambao walitumia vibaya uhuru aliowapa mungu. Mwishowe ahitimisha kwa wito wa kuachana na dhambi au maisha ya dhunubu.

Kwa ufupi ni kuwa, mwandishi ametumia ploti imara, inayoshikana na kufululiza usimulizi au maelezo toka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho katika mashairi husika.

## 4.7 WAKATI

Nyakati tatu muhimu zabainika katika tungo. Nazo ni uliopita, uliopo na ujao. Hata hivyo kuna kazi zingine ambazo hazina wakati maalum na ambazo zafaa katika nyakati mbalimbali.

Kwa namna msanii anavyoyaendeleza mashairi yake, msomaji hujua moja kwa moja kuwa jambo linalosimuliwa au elezwa limetokea, linaendelea kutokea, ama litatokea. Mara nyingi mambo yaliyopita na yaliyopo husaidia katika kumpa mtu ndoto au njozi ya kutabiria yatakayotokea. Ifuatayo ni mifano ya kuonyesha jinsi nyakati zinavyopambanuka.

68.10 Wataliziba kosale, wapate kukuumbuwa
Ili kusudi wakule, na maovu kutendewa
Mwana wao atawale, ubaki huna satuwa
Ni kheri mke muole, kama wanawali

Mawazo hayo yamewekwa kitabiri na kusimuliwa kama yanayotokea au yaliyotokea japo wakati wake ni ujao. Ifuatayo ni mifano zaidi.

1 54.7 Kipi kisovunda, kwa walimwengu, cha daima?
Pasi na kukonda, kwa walimwengu, yaso wema
Angawa ni Nunda, huja kiwingu, cha nakama

2 55.1 Sili najitowa wazi, wambeja wamenitaka
Na kuwakinza siwezi, wasije wakaudhika
Pale walipobarizi, salimu leo ondoka
Nileje tokoro hizi?

3 48.10 Uitambuwe athari, kuu itakayokufika
Iwapo yako khatri, paovu ikikatika
utaonyesha dhahiri, u kiumbe wa mashaka
Na mateso kuteseka, mwanaadamu fikiri.

Mfano wa kwanza ni wa nyakati zote - za awali, zilizopo na zijazo. Wa pili ni wa wakati huu. Wa tatu pia waangazia matukio ya wakati ujao kwa njia ya kinjozi. Tunahitimisha kuwa, tungo zilizomo humo si za wakati mmoja maalum. Ni tungo za nyakati zote. Wakati umetumiwa kwa namna ambapo wapambanuka vizuri.

## 4.8 TONI

Toni mbalimbali zadhihirika humo, zikiwa ni pamoja na za huruma, masikitiko, na mchanganyiko wao kama ilivyo katika shairi ulezi, Tafakuri, moyo na mengine.

Toni ya uchochezi na kitashtiti yabainika katika shairi Tafakuri ambapo mshairi amchochea mja kutaliki maovu yote na kuanza kufuata njia za Mungu.

Aina nyingine ya toni ni ile ya kukata tamaa ambayo yadhihirika katika shairi malimwengu. Aona kuwa hakuna lolote jema la kutendwa duniani likakubalika na walimwengu. Awaona kama watu ambao hawakubali chochote hata kiwe kizuri vipi.

Toni ya kusimanga yadhihirika katika mashairi kipwipwi, masimango na mengine. Ile dharau na ubeufu kama wa kutapishwa yatokea katika shairi nileje? Toni ya ukataaji na uvunjikaji usiotengenea wa mahusiano ya unyumba yatokea katika shairi sikutaki, moyo na mengine.

Ile ya ridhaa yaangazika katika mke muole, huku ya ushaufu ikitokea katika shairi kujigamba.

Kuna toni ya kujiamini katika baadhi ya mashairi ambako kunatupa sababu yake. Mfano ni katika shairi potole, ambapo msanii aonyesha kujiamini sana katika utunzi.

Toni ya mshangao yatokea katika shairi mpewa sumu hafile, huku ya kutatanisha ikitokea katika ukuni wa koko.

Toni zinazodhihirika zategemea maudhui, mazingira, mpangilio kisintaksia na kisemantiki wa maneno na aina ya maneno yaliyotumiwa. Kwa muhtasari toni hufaa sana katika kusoma au kupata masafa ujumi ya kazi, na ndivyo ilivyopambanuka katika tungo tulizozipitia za mwalimu mbega.

**Tanbihi**

1 Sinonimia - katika kamusi ya Isimu na lugha sinonimia nii uhusiano uliopo baina ya maneno mawili au zaidi ambayo maana zake zinakaribiana sana".

2 Homonimia - katika kamusi hiyo limeelezwa kuwa ni "uhusiano wa leksemu mbili au zaidi katika lugha ambazo huandikwa sawa lakini maana zake ni tofauti.

3 Inayoyaamilisha - Inayoyapa uamili

4 usipuna - limeundwa kurejelea mtaalamu Spooner ambaye wakati fulani aliemegwa na akawa hatofautishi jina lake katika maendelezo ya snooper na spooner

5 Lugha mata - kwa mujibu wa kamusi ya Isimu na lugha ni " lugha ambayo imekufa au haimo katika matumizi tena"

6 Vyazi - neno asilia au zazi - ambalo kwalo kuna ukariri wa baadhi ya vipashio katika tanakali sauti

7 Wekevu - Matumizi ya kiitiksadi ya maneno

8 Ukarapokevu - neno tulililoiunda kwa njia ya muungano wa maneno mawili, kumaanisha kuwa ni kina cha utao, aina ya ukara ambacho kimepokea kina kipoto (tofauti kutoka ukwapi) yaani kina cha ukwapi kilicho tofauti nacho.

9 Tabdilifu - Ni kina cha ukara katika utao ambacho baada ya kupokea kina cha mshororo wa mwisho wa utao, kinaubadilisha kimofolojia. Kwa mfano badala ya kina shi cha ukwapi kunatokea ish.

## SURA YA TANO: TATHMIN NA HITIMISHO

Msanii ametumia fani ambayo si ya kupwaya. Ametumia fani nzuri ambayo kimsingi inasaida sana katika kuwasilisha kwa namna inayoridhisha. Hii inaanzia matumizi mazuri ya lugha katika viwango vyote - vya fonolojia, mofolojia, semantiki, sintaksia na katika muungano wao. Viwango tulivyovitumia katika kuhakikia matumizi ya lugha katika tungo hizi vinaingia katika mojawapo ya miongozo hiyo.

Msamiati uliotumiwa katika diwani zote si mgumu katika kutamkika na kusomeka, japo baadhi ya vipashio vilivyokopwa kama vile "katabtu l' hakiri" kwa maana ya 'Naandika kwa unyonge' ni vigumu kidogo kwa msomaji asiyekielewa kiarabu hata kidogo. Matumizi ya fungu kopwa kama hilo si mabaya, kwani kwa kuzingatia tija ya neolojia, matumizi hayo huongezea lugha katika hazina ya leksia ilizo nazo. Hakutumia vifungu vigumu vya kiarabu kama baadhi ya wasanii kama Ustadh mti-mle walivyofanya.

Viwango kama, vipashio vya msamiati, njia za upanuzi maana katika msamiati, mazingira ambamo msamiati umetumiwa, uangavu na utata wa msamiati, motisha katika matumizi ya msamiati, wizani kimaana, uwezo wa msamiati, asili ya msamiati, uteuzi wa msamiati, aina ya msamiati, minasibisho, tamathali za usemi na vingine vinaingia moja kwa moja katika viwango vya mofolojia, semantiki na sintaksia. Kwa mfano, uhakiki wa vipashio ni sehemu ya mofolojia, upanuzi kisemantiki na wizani kimaana ni sehemu ya semantiki na mpangilio wa msamiati ni sehemu ya sintaksia. Kwa hivyo viwango vyote vinne vimewakilishwa katika uhakiki wa lugha, na ni kwa sababu hiyo twadai kuwa msanii ameitumia lugha kwa namna inayoridhisha. Kamwe hakuutumia uhuru wa kishairi katika kuponda mawasiliano bali katika kuyaimarisha.

Ametumia mitindo mbalimbali ya uwasilishi katika mashairi yenye mitindo kadha kwa njia ambayo pia inaridhisha. Ni aina ya maendelezo ambayo yanakuza fani kwa jumla, kama inavyodhihirika zaidi katika Dafina ya umalenga, kuliko katika Upisho wa umalenga.

Amewaumba wahusika wake pia katika diwani zote mbili kwa namna inayotufanya kuona uamili wao katika tungo. Ni maendelezo mazuri na yanayofaa kisanii.

Katika mandhari, mshairi ametumia mandhari tofautitofauti ikitegemea aina ya ujumbe wa kupitishiwa huku na aina ya wahusika na vitendo vinavyokusudiwa hapo. Hapa pia msanii ametupa mandhari kwa njia imara.

Wakati ambao ni muhimu sana katika kuhusishwa na matukio elezwa ama simuliwa umetumiwa kwa namna ambayo unapambanuka kwa urahisi. Umetumiwa kwa njia ambayo imetuwezesha kupata na kutambua matumizi ya njozi katika tungo.

Ploti nayo imetokea vizuri ambapo maumbo yake ya msago au moja kwa moja au fululizi na ya taharuki yamethibitika katika matumizi. Ni aina ya ploti iliyoyapa mashairi vichwa, miili na hitimisho. Hivyo ni maendelezo timifu kisanii.

Kuna pia madhihiriko ya toni ambayo ni zao la namna uwasilishi unavyofanywa, unahusisha nani, katika mazingira yapi, na katika wakati upi. Ingawa baadhi ya wataalamu kama Murray, wanaiona toni kama zao la mkabala wa msanii kwa kazi au wasomaji, uchunguzi wetu umeiona kama matokeo ya ushirikiano wa viungo vyote vya fani. Hatuwezi kuepuka lugha katika kuelezea fikira zetu. Pia katika kufanya hivyo huenda tukauliza wahusika maswali mahali fulani na wakati fulani. Kwa sababu hii twaona kuwa toni ni matokeo ya ushirikiano wa vipengele hivyo vingine vyote vya fani. Ni muhimu pia kuelewa maudhui katika kuangalia toni inayochipushwa na maendelezo ya kifani. Hili katika ushairi hutokea katika kiwango cha shairi moja. Katika nathari, huenda ikahusu tungo katika ujumla, baadhi ya matukio au sura nzima.

Ni kwa sababu ya matumizi hayo ya fani katika viwango vya lugha, wahusika, mtindo, ploti, wakati, mandhari na toni twasema kuwa msanii ameitumia fani kwa njia inayoridhisha.

Mbali na kiwango hicho, kuna pia umbo changamano lenye mshikamano wa dhati, ambalo limeunganisha viungo vyote vya fani katika diwani hizo. Tukirejelea maelezo yetu kuhusu toni, twaona namna vipengele vyote vinavyoingiliana vizuri katika uamili wao.

Msanii ametumia aina ya fani ambayo itafaa katika nyakati zote. Ni aina ya fani ambayo haitengewi wakati mmoja maalum. Kile tunachokusudia hapa ni kuwa, ni fani ambayo inafaa katika nyakati zote.

Fani iliyotumiwa pia ina uwezo mkubwa wa kumtawala kihemshi msomaji. Hii inategemea namna msanii alivyoitumia lugha, alivyowateua wahusika wake na kuwaumba, aina ya mandhari ambamo amewatumia na mkabala wake kuhusu kazi na wasomaji wake. Kwa mfano katika shairi 'uke wenza', toni ya namna ilivyo vigumu kuyagawa mapenzi kwa usawa yajitokeza. Inagusa hisia za msomaji ambaye ana akilini mwake picha ya wanawake nyumbani wanaogombana bila mwisho kwa sababu ya penzi la mume. Twaoni vizuri jinsi ilivyo vigumu kwa wanaume kupata utulivu hata wajaribu kuwapa kwa usawa, vitu, wakewenza. Pendo haligawiki na hivyo ukewenza una matatizo yake.

Pia tumeona kuwa mshairi ametumia fani yenye mwelekeo mzuri ambao unafungamana na udhibiti wa dhamira alizozilenga msanii. Kwa kututungia shairi 'mtenda jambo Asishe', mshairi alikuwa ana nia ya kutushauri tutende mambo hadi ukamilifu wao ndipo tujue uzuri na ubaya wao. Msamiati alioutumia pamoja na fani kwa jumla inatuelekeza kwenye ufumbatifu wa lengo hilo la msanii.

Mshairi pia ametumia fani kwa namna ambayo inamruhusu mhakiki kuvichanganua na kuvihakiki kivyake vipengele vyake katika kutathmin mchango wa kila kimojawapo, kabla ya kuangalia kimantiki uhusiano baina yao. Ameitumia fani kwa namna ambayo inaruhusu uwezekano huo, na ni kwa sababu hiyo tuliviangalia kila kimojawapo kivyake na wakati mwingine kuangalia uhusiano wao.

Ni kwa sababu hizo mbalimbali twahitimisha kuwa msanii ametumia fani nzuri ambayo imetekeleza uamili wake kwa namna inayodhibiti na kutimiza malengo kuu ya kisanii, na uwasilishi kwa ufundi mkubwa. Maelezo haya ni kwa msingi wa haipothesia na kazi zenyewe.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M.H, (1979) Muyaka: 19th Century swahili popular poetry. K.L.B.,Nairobi.

Akiba, H, (1983), "Ukuzaji na Uendelezaji wa msamiati wa Kiswahili," katika, Tuki, Lugha ya Kiswahili. Makala za semina ya kimataifa ya ya waandishi wa Kiswahili 1. Tuki, Dar-es-saam.

Amana, B, (1982), Malenga wa Vumba. O.U.P, Nairobi

Anne, C, (1976), Introduction to literary stylistics. B.T Batsford Ltd, London.

Bakari, M,(1982) The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects. Tasnifu ya PH.D, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Beckson, K & Ganz, A, (1960), A Readers Guide to Literary Terms. Thames and Hudson, London

Bennet, T.(1979).Formalism and Marxism. methuan and co. Ltd, London.

Besha, M.R, (1975), "Nadharia ya Lugha: Lugha ni nini? Katika, Abdalla, A & Sengo T.S.Y, Mulika Nambari 16. TUKI, Dar-es-salaam

Bloomfield,L,(1935), Language. George Allen & Unwin Ltd London.

Bosha, I, (1993).Taathira za kiarabu katika kiswahili pamoja na kamusi thulathiya (kiswahili-Kiarabu -Kiingereza) Dar-es-salaam University press, Dar-es-salaam.

Chao, A, (1971),"Rai mbalimbali kuhusu ufundishaji mashairi"Katika kiimbila, J.K. (Mha..), Kiswahili V.41/1. TUKI, Dar-es-salaam.

Chatman, S,(Mha..,1971), Literary Style - a Symposium. O.U.P, Oxford.

Chiraghdin,S(1975),"Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili",katika Abdalla, A & Sengo, T.S.Y,(Wah..,) Mulika nambari 7. TUKI, Dar-es-salaam.

Mnyampala,M,(1977), Historia ya Kiswahili. O.U.P, Nairobi.

Cowie, A.P, (Mha..,1991), Oxford Advanced Learners Dictionary. O.U.P, Nairobi.

Davis, R.C. & Finke, L.F, (Wah..,1989).Literary criticism and Theory. Longman, Newyork.

Empson, W,(1930), Seven types of Ambiguity. Penguine Books, Victoria.

Fokkema, D.W & Kunne - Ibsch, E(1978), Theories of literature in the 20th Century. Hurst and Co.,London.

Fowler, R, (1975),"The New Stylistics," Katika, Blackwell, B,(Mha..,) Style and structure in literature. The Pitman press, Bath.

Frankl,P.J.L, (1970), "Maneno ya utaalamu wa sayansi ya lugha; A list of some literary terms - English and swahili", katika kiimbila, J.K.(Mha...)Kiswahili V.40/2.TUKI.Dar-es-salaam.

Gibbe,A.G & Mbughuni, P,(1983), "Maendeleo ya Istilahi za Kiswahili", katika, TUKI, lugha ya kiswahili: Makala za semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kishwahili 1, TUKI, Dar-es-salaam.

Harries, L,(1967)"Style in Swahili", katika Whiteley, W.H, (Mha...) swahili V.37/1, TUK 1, Dar-es-salaam.

________(1969), "Adjuncts in swahili," katika abdulaziz, M.H.,(Mha..), swahili V.39/2 TUKI, Dar-es-salaam.

Hoffman,A,(1975, Research: A handbook for writers and journalist. Midas Books, Hampshire.

Hough, G,(1969),Style and stylistics, Routledge and paul kegan, london.

Johnson, F, (1973),A standard English-Swahili Dictionary, O.U.P,Nairobi.

(1991), A standard swahili - English Dictionary O.U.P, Nairobi.

Kapinga, M.C,(1983), Sarufi Maumbo ya Kiswahili, TUKI, Dar-es-salaam.

karega, M, (1986),"Swahili lexical expansion-prospects and problems," katika, Massamba, D.P.B & Mulokozi, M.M, (Wah..),Kiswahili V.51/1&2, TUKI, Dar-es-salaam.

Kazungu, K,(1982),Deviation and Foregrounging in chosen swahili literary texts, Tasnifu ya M.A, Chuo kikuu cha Nairobi.

Kezilahabi, E, (1973,)"The development of swahili poetry:18th-20th Century,"katika, Temu, C.W & Jaka, R.L.(Wah...) Kiswahili V.42/2 TUKI, Dar-es-salaam.

__________(1976),Ushairi wa shaaban Robert, E.A.L.B, Dar-es-salaam.

__________(1983), "Uchunguzi katika ushairi wa kiswahili ",katika, Fasihi: makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa kiswahili III, TUKI, Dar-es-salaam.

Khan, M.K.,(Mha.., 1984), Mashairi yetu, E.A.P.H,Nairobi.

Kibao,S.A,(1983), "Namna ya Kujifunza, Kuliandika na kulifumbua shairi la Kiswahili", katika, Fasihi:Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa kiswahili III, TUKI, Dar-es-salaam.

Kiimbilia, J.K,(Mha..,1971), Kiwahili V.41/1, TUKI, Dar-es-salaam.

Kitsao, J,(1975), A stylistic approach adopted for the study of written prose texts, Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi.

______(1978),"The writers world," Discussion paper no 101, Chuo kikuu cha Nairobi.

______(1982), An investigation of Themes in swahili literature and an application of stylostatistics to chosen texts, Tasnifu ya PH.D, Chuo kikuu cha Nairobi.

Korg, J, (1959), An Introduction to poetry, Holt, Rinehart & Wilson, Newyork.

Krifka,M,(1985),"Word order and word order charge in swahili,"katika Mulokozi,M,M & Massamba, D.P.B.(Wah...) Kiswahili. V.52/1&2. TUKI, Dar-es-salaam.
Kuhenga, C, (1977) Tamathali za Usemi. E.A.L.B, Nairobi
Lambert, H.E, (1958), Chi-chifundi- a dialect of the sourthern Kenya coast. E.A.S.C, Kampala.
Leech, G, (1969), A linguistic Guide to English poetry. longman, London.
Levin. S.R, (1962), Linguistic structures in poetry. mouton & Co.Ltd, The Hague.
Marealle, I.B,(1978)."Dhana za Mofu,mofimu na Alomofu,"Katika, sengo, T.S.Y & Honero, L.N, (Wah..)Mulika nambari 13. TUKI, Dar-es-salaam.
Masoko, D.L.W. & Mdee, J.S. (Wah.., 1984),"Msamiati wa muda wa fasihi", katika,Mulika nambari 16. TUKI, Dar-es-salaam.
Massamba,D.P.B,(1969), "Kiswahili Fasihi", katika Abdulaziz, M.H, (Mha..)swahili V.39/1 & 2 TUKI, Dar-es-salaam.
__________(1983), "Utunzi wa ushairi wa Kiswahili", katika, Fasihi: Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa kiswahili III, TUKI, Dar-es-salaam.
__________(1988),"Sababu za kubadilika kwa maana za maneno: mifano kutoka kiswahili", katika massamba,D.P.B, & Mlacha,S.A.K,(Wah...), Kiswahili V.55/1 & 2. TUKI, Dar-es-salaam.
__________(Mha..,1990), Kamusi ya Isimu na Lugha. TUKI, Dar-es-salaam.
Mbaabu,I (1992) Sarufi ya Kiswahili. Longman Kenya, Nairobi.
Mbega, H.M, (1975), Upisho wa umalenga. E.A.L.B, Nairobi.
________(1984), Dafina ya umalenga. Longman, Nairobi.
________(1985), Utenzi wa Mfalme Muadilifu. K.L.B. Nairobi.
________(1986), Wasia Bora na Hadithi zake. K.L.B, Nairobi.
Mdee.J.S.(1986).Kiswahili:Muundo na matumizi yake Intercontinental publishers ltd, Nairobi.
______(1986),"Matatizo ya kuunda Istilahi kama yanavyojitokeza katika kiswahili,"katika mulokozi,M.M. & Massamba, D.P.B, (Wah...,) Kiswahili V.53/1 & 2 TUKI, Dar-es-salaam.
Medvedev,P.N et al, (1978), The Formal Method in Literary Scholarship: A critical Intoduction to Sociological poetics The John Hopkins University press, London.
Meussen, A.E,Allen,J.W.T, & Parker, B,(1967),"Notes on swahili prosody", katika , Allen, J.W.T,(Mha..,), Swahili V.37/2 TUKI, Dar-es-salaam.
Mhina,G.A, (1967),"Style in swahili,"katika, Allen J.W.T, (Mha..,) V.37/2. TUKI, Dar-es-salaam.
Mkelle,M.B,(1971),"Change in context and meaning of words,"katika kiimbila, J.K(Mha..).Kiswahili V.41/1. TUKI , Dar-es-salaam.
Mlacha, S.A.K, (1985),"Wahusika katika Riwaya za kiswahili Tanzania",katika, Mdee, J.S & Mbogo,E,(Wah...,) Mulika nambari 17. TUKI, Dar-es-salaam.
Mohammed, M,(1977), Malenga wa Mrima. O.U.P, Nairobi
Mohammed, S.N,(1975).Mtango wa Kiswahili. E.A.P.H, Dar-es-salaam.
Msokile,M,(1993), Misingi ya Uhakiki wa Fasihi. E.A.E.P, Nairobi.

Mulokozi, M.M., & Massamba, D.P.B.(Wah...1985). Kiswahili V.52/1&2 TUKI,Dar-es-salaam.

__________& Kahigi, K.K.,((1979).Kunga za ushairi na diwani yetu. Tanzania publishing House,Dar-es-salaam.

Murray.p.(1978).Literary Criticism. Longman,Newyork.

Mutonya, M,(1991) Maudhui katika Ushairi wa Hassan Mwalimu mbega. Tasnifu ya M.A, Chuo kikuu cha Nairobi

Mwangomango,J,(1970),"Ufundishaji wa Mashairi,"Katika, Kiimbila, J.K. (Mha..,), Kiswahili V.40/2.TUKI.Dar-es-salaam.

Nowottny, W.(1965).The Language Poets use. The Athlone press, London.

Ostrovsky, V, (1967),"Etymological and Phonetic changes among foreign words in kiswahili," katika, Whiteley, W.H, (Mha...)Swahili V.37/1.TUKI. Dar-es-salaam.

Sebeok,T.A,(Mha.., 1960), Style in language , The M.I.T press, Massachusetts.

Senkoro, F.E.M.K,(1982), Fasihi.press and publicity centre, Dar-es-salaam

__________(1988).Ushairi: Nadharia na Tahakiki.Dar-es-salaam University press, Dar-es-salaam.

Shaaban R, (1968), Siku ya watenzi wote. Nelson, Edinburg.

Skelton, R (1978), Poetic Truth. H.E.B, Nairobi.

Spencer, J,(Mha..,1964), Linguistics and style.O.U.P. London.

Stigand,C,(1915), A Grammar of Dialectic Changes in the Kiswahili language. cambridge University press, cambridge.

Syambo,B & Mazrui.A.(1992).Uchambuzi Wa Fasihi. E.A.L.B,Nairobi.

Temu,C,(1984),"Kiswahili Terminology:Principles adopted for the enrichment of Kiswahili language,"Katika,Mulokozi, M.M. & Massamba D.P.B, (Wah....)Kiswahili V.51/1 & 2 TUKI,Dar-es-salaam.

Thompson,D(1959) Reading and Discrimination. Chatto & Windus,London

Todd,L.(1987), An Introduction to Linguistics. Longman, BurntHill.

Topan,F.M,(Mha.., 1975) Uchambuzi wa maandishi ya Kiswahili. O.U.P, Nairobi.

Wallah.W.(1988).Malenga wa ziwa kuu. E.A.E.P,Nairobi.

Widdowson,H.G,(1975) Sylistics and the teaching of literature. Longman, Edinburg

Yambi,J,(1988),"Uundaji wa Istilahi na Usambazaji wake",Katika Massamba D.P.B Mlacha, S.A.K,(Wah..), Kiswahili V.55/ 1 &2 , TUKI Dar-es-salaam.